

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 13 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (MHE. JOSEPH R. SELASINI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Fedha za Mikopo kwa Wajasiriamali**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Ili kujikwamua kiuchumi na kupata mikopo kwa vikundi vya vijana na akina mama, Mheshimiwa Rais, alitoa na kuahidi shilingi bilioni 100 kwa Wananchi wa Tanzania, kwa ajili ya mikopo:-

- (a) Je, ni kiasi gani kimepangwa kuwafikia wananchi wa makundi hayo katika jimbo la Manyovu?
- (b) Je, ni kiasi gani wananchi walipata mwaka uliopita na ni kikundi gani kilipata mgao huo kwenye jimbo la Manyovu?
- (c) Je, ni utaratibu gani unatakiwa kufuatwa ili wananchi wengi zaidi wanufaikie na mkopo huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Disemba mwaka 2011 kupitia mpango wa Rais, wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira jumla ya shilingi bilioni 47.35 zilitolewa katika awamu ya kwanza.

Mnamo tarehe 4 Aprili, 2011 Mheshimiwa Rais, alipofanya ziara katika Wizara ya Kazi na Ajira, aliagiza tathmini ya utekelezaji mpango huo ifanyike. Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa maelezo yake, yuko tayari kutoa shilingi bilioni 100 baada ya kufanyika kwa tathmini ya kina na utaratibu mzuri zaidi kuandaliwa. Matokeo ya tathmini hiyo, yataatuwezesha kujua kiasi cha fedha kitakachopangiwa wananchi na makundi mbalimbali katika Jimbo la Manyovu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka uliopita kutokana na mpango huu, Wilaya ya Kasulu ambayo inajumuisha Jimbo la Manyovu, ilipata mikopo ya shilingi milioni 114.85 kupitia Benki ya *NMB* na *SCCULT*. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wajasiriamali 827 kupitia *SACCOS* za Wanyamu, Umoja, Tumika na Tumaini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu zilizotumika kutoa mikopo kwa wajasiriamali katika awamu iliyopita ni za aina mbili. Benki ya *NMB* na taasisi nyingine zilitoa mikopo moja kwa moja kwa wajasiriamali na benki ya *CRDB* ilitoa mikopo kupitia *SACCOS*. Hivi sasa Serikali inafanya tathmini ya utaratibu huo ili kubaini

mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwa lengo la kuandaa utaratibu mzuri zaidi ili walengwa na wananchi wengi zaidi wanufaika na mikopo itakayotolewa.

Kuhusu taratibu zitakazotumika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge na wananchi, wawe na subira. Utaratibu utatolewa baada ya kukamilika kwa tathminni niliyoitaja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipongeze jibu zuri la Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu mazuri, naomba nilete ombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama, vijana na wazee wa Jimbo la Manyovu, wamenitura baada ya taratibu zako, uwapatie mikopo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ilikuwa ni shukrani. Swali la nyongeza, tubakie huko huko Kigoma, Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilitaka tu kujuua, amesema zinatengwa bilioni 100 kwa ajili ya kusaidia vikundi hivyo vya akina mama na vijana. Lakini sasa ni wakati wa Bajeti, ukienda kwenye *Vote* ya Wizara ya Kazi ama hata *Vote* ambayo yeye anaisimamia ya Uwekezaji; hizi fedha hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, atuambie fedha hizi ambazo zimetengwa kwa ajili ya mifuko ya vijana na akinamama, zitakuja kwenye bajeti ipi? Ni mwaka huu ama ni bajeti nyingine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa kutaka ufanuzi ambao pengine utasaidia wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi, nilieleza kwamba baada ya tathmini na taratibu nzuri kuandaliwa ambazo kwa vyovyote vile tutafanya, Rais ameahidi kutoa shilingi bilioni 100. Sasa zitakapotoka tutajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukienda katika *Vote* fedha hazionekani, ni kweli. Kwanza zile za mwanzo ziko kwenye mzunguko. Na nyingine za nyongeza, basi wakati huo utakapofika, tathmini itakapokuwa tayari na utaratibu mzuri kuandaliwa ili walio wengi wanufaika, basi wakati huo Serikali itajua na kwa vyovyote vile italeta katika Bunge lako Tukufu.

Na. 224

**Upungufu wa Walimu wa Sekondari Kondoa**

**MHE. ZABEIN M. MHITA** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, wameitikia sana mwito wa kujenga shule za Sekondari kutoka 7 mwaka 20005 hadi 32 mwaka 2010 na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza. Pamoja na mafanikio hayo bado kuna tatizo la upungufu mkubwa wa walimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza walimu ili kukidhi upungufu huo na kuwanufaisha wanafunzi kupata elimu bora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, kwa juhudini kubwa ya kuitikia wito wa kushirikiana na Serikali kujenga shule nyingi kutoka shule saba mpaka shule 32 kati ya mwaka 2005 na mwaka 2010. Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa walimu katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji na haswa upungufu wa walimu uliopo katika shule zetu za Kata. Aidha, mpango wa kuzipatia shhule za Kata walimu wenye sifa stahiki ni bayana na Serikali imejipanga kufanya hivyo. Katika mwaka wa masomo 2010/2011 wanafunzi walimu 9,226 waliohitimu mafunzo ya ualimu na walajiriwa, ambapo wa Shahada walikuwa 4,920 na Stashahada walikuwa 4,306. Kati ya walimu hawa, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, ilipangiwa jumla ya walimu 81 ambapo wa Shahada walikuwa 22 na Stashahada walikuwa 59 na wote walipangiwa katika shule za sekondari. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu, Serikali imeongeza udahili wa walimu wanafunzi katika vyuo mbalimbali na kuhamasisha watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuanzisha vyuo vya ualimu. Kwa mwaka 2011/2012 jumla ya walimu wanaotarajiwa kuhitimmo ni 19,031 wa Shahada ni 11,649 na Stashahada ni 7,382. Serikali itaendelea kuwaajiri walimu kwa kadiri watakavyohitimmo na kufaulu na kuwapanga katika shule zetu za sekondari ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudini kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuongeza walimu katika shule za sekondari, bado Wilaya ya Kondoa ina upungufu mkubwa. Naomba nitoe mfano, mwaka jana katika shule zilizofanya vibaya katika mtihani wa kidato cha nne, Jimbo la Kondoa Kaskazini lilikuwa na shule tano, Shule ya Sekondari ya Kikore, Shule ya Sekondari Huruwi, Shule ya Sekondari Thawi, Shule ya Sekondari Changaa na Shule ya Sekondari Kolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zote hizi tano nilizozitaja zilikuwa na walimu wawili wawili tu na hii ndio sababu ambayo ilifanya shule hizi zinafanya vibaya. Sasa ninaiomba Wizara, inapopanga walimu wahitimu katika mwaka 2011/2012 naomba kipaumbele kitolewe katika Wilaya ya Kondoa, ili wanafunzi hawa wanaohitimu elimu ya Sekondari waweze kunufaika na elimu hiyo na kuwapa moyo wananchi waweze kuchangia zaidi katika ujenzi wa shule za sekondari. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zabein Mhita, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Mimi nimeenda Kondoa na kwenye ziara yangu nimeenda pia kwenye Jimbo lake. Kati ya taarifa nzuri nilizozipata ni lazima nianze kwa kumpongeza yeye mwenyewe kwa mchango mzuri mkubwa alioufanya wa kuchangia mabati 11,000 kwa ajili ya kuziwezesha shule zetu zote kule Kondoa Kaskazini, kuezekwa na kuwa katika hali nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jitihada hizo nataka nimhakikishie, kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi; nchi nzima tuna sekondari 4,266 na mwaka huu tunatarajia kuajiri walimu 19,031. Katika hesabu za kawaida tunatarajia angalao kila shule nchini inaweza kupata walimu wasizidi watano. Na hiyo ni pamoja na Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Kwa taarifa nikiwa pale Kondoa, katika Jimbo Kondoa Kaskazini lina mahitaji ya walimu 392 na sasa hivi una walimu 308 una upungufu wa walimu kama 84, jambo ambalo tunaweza tukali-cover na kama ambavyo nimeeleza nilipokuwa ninaunga hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwamba, tunatarajia kuwasambaza walimu kwenye maeneo yote, usambazaji ule ni pamoja na Kondoa Kaskazini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tumekuwa tukisomewa takwimu nyingi za udahili wa wanafunzi, hasa walimu, wanaokwenda kusomea Vyuo Vya Ualimu. Na kwa kuwa, tatizo hili limekuwa sugu katika shule nyingi za sekondari Tanzania nzima na hususan katika Vidato vya V na VI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuingia mikataba na wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu, wa lazima, hasa wale wanaopata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo angalao kufundisha miaka mitano kabla hawajaenda kufundisha katika shule zingine kama wanavyofanya Vyuo Vikuu kwa wanafunzi ambao wanafanya *Masters?*

Kutokana na mikopo ya *SIDA*, *SADC*, wakati ule wanavyolazimishwa kufundisha Vyuo Vikuu miaka mitano ndipo baadaye waamue kuondoka? Ili tuweze kupunguza tatizo hili la ukosefu wa walimu katikia nchi nzima.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili limewahi kujibiwa pia hapa na Naibu Waziri wa Elimu, lakini labda niweze kutosheleza. Kwamba mpango uliopo sasa katika utumishi wa umma kwenye sekta ya elimu; ni kwamba mwalimu anapopata ajira kwa mara ya kwanza ni lazima atumikie miaka miwili kama sehemu ya mkataba. Na kipindi kile cha miaka miwili ni kipindi ambacho mwalimu huyu atatakiwa kuthibitishwa kuwa mwalimu ili apate leseni ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spik,a kwa hiyo sehemu ya mkataba kwanza ni miaka miwili ni lazima atumikie kwenye maeneo yetu. Sasa kwa mkataba ule ingawa umeomba kwa miaka mitano, lakini tayari tuna Sheria ya Utumishi ya miaka miwili kutumikia kwenye vituo vyetu vya ualimu na baada ya hapo sasa tunaweza kuuimarisha utaratibu huo kama ambavyo umeomba. Nashukuru.

Na. 225

#### **Upatikanaji Wa Umeme Mkoa wa Kigoma**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA (K.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA)** aliuliza:-

Mradi wa Umeme wa Malagarasi kupitia Mradi wa *MCC* umesitishwa kutokana na kugundulika kwa vyura kwenye mto huo.

Je, Serikali sasa inawaambia nini Wananchi wa Kigoma kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika ili kuondokana pia na ghamama kubwa ya kutumia jenereta zinzotumia dizeli ambayo hupatikana Kigoma tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhanywa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma, tarehe 29 Juni, 2011. Utekelezaji wa mradi huu ulisitishwa baada ya ripoti ya upembuzi wa kina kuhusu athari za kimazingira ya Septemba 2009, kuainisha kuwepo kwa konokono adimu aina ya

*Golden Snail*, kwenye maporomoko ya mto huo katika eneo la mradi wa Malagarasi II. Aidha hivi sasa kuna upembuzi yakinifu unaofanyika katika eneo jipya la Malagarasi *Stage III*. Kazi hiyo, ya tathmini ya mradi huu kwa sasa bado inaendelea na imeonesha kuwepo kwa uwezo wa kuzalisha umeme mwingi zaidi kuliko ule wa chanzo cha awali ambapo tunawenza kuzalisha *Mega Watt 41*. Mradi huu wa Malagarasi ulikuwa unatarajiwa ukamilike ndani ya kipindi cha miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma pia, unatarajiwa kupata umeme wa uhakika kutoka kwenye Gridi ya Taifa, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa njia ya usafirishaji msongo wa KV 220 kutoka Nyakanazi – Kigoma – Rukwa – Mbeya, ambapo tayari kampuni ya *CMEC* ya China imekubali kujenga mradi huo na taratibu za ufadhili na kukamilika kwa mradi huo zinakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Mkoa wa Kigoma unapata umeme wa jumla ya *Mega Watt* 13.25 kwa mkoa wote. Upatikanaji wa umeme umeongezeka kutoka *Mega Watt 2* zilizokuwa zinapatikana mwaka 2008 hadi kiwango cha sasa cha *Mega Watts* hizo 13.25 kufuatia uwekezaji wa makusudi uliofanywa na Serikali.

Hata hivyo, bado Kigoma inakabiliwa na matatizo ya kufikia malengo ya usambazaji. Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO*, inayafanya kazi matatizo haya pamoa na kuboresha tathmini ya mahitaji ya Kigoma yanayoongezeka kufuatia kupanuka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba pia ya Mheshimiwa Mhonga, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma ilitengewa fedha za *Millenium Challenge Co-operation* kwa ajili hiyo. Tunataka Waziri atuambie, fedha hizi zilipelekwa kwenye mradi mngine upi? Ama zilifanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili. Ni kwa nini sasa Serikali isisikie kilio changu cha siku nyingi kwamba sasa kwa kuwa, mto ule umegundulika una vyura wa ajabu, ni kwa nini isifungue *centre* ya utalii ili Mkoa uingize mapato yatokanayo na utalii? Nataka majibu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Majibu, lile la pili achana nalo, jibu lile la kwanza, achana na mambo ya utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Subrina Sungura, kwa niaba ya Mheshimiwa Muhonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala tumelieleza juzi wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Kafulila, pesa zile kama bilioni 57 ndiyo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya

Malagarasi. Wenye we wafadhili baada ya kuonekana tuna tatizo la wale konokono adimu, pesa zile ziko pale na wao majadiliano yanaelekeza. Kwa sasa hivi kipande kidogo kati ya pesa zile zitaelekezwa katika kuboresha mfumo wa usambazaji ndani ya Kigoma.

Kwa *Mega Watt* hizi 11 usambazaji ule utakwenda kwa maeneo machache labda Kalizi kule na huku chini Mwandiga kwenda mbele kidogo. Lakini vinginevyo bado utaratibu ni ule ule kufikia *megawatt 41* tulenge Malagarasi three, kwa sababu tukiipata ile sasa kwa eneo lote lile megawatt 41 ni nyingi sana kulikua na *megawatt 8* ambazo zina uhakika na hiyo inaonekana upembuzi yakinifu utakamilika taarifa hiyo mwisho wa mwezi wa saba huu au wa nane mwanzo. Kwa hiyo, nakuombeni tuvute subira halafu tuangalie mwelekeo wa mradi huu utakwenda vipi.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona matatizo ya umeme yaliyopo mji wa Kigoma yanafanana sana na yale ya mji wa Tunduru, na kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, Tunduru tumeahidiwa kupata umeme wa *Mnazi Bay*, kufika mji wa Mangaka.

Je, Serikali inatuambia nini sisi wananchi wa Tunduru juu ya kuongeza kasi ya umeme huo kufika Mangaka ili uweze kufika Tunduru haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme wa Tunduru ni kweli linafanana kidogo na suala la Kigoma kwa sababu pale pana majenereta, majenereta ya zamani yamekuwa yanafanya kazi kwa tabu kidogo.

Ahadi tuliyokuwa nayo kwa Mheshimiwa Mturura na wananchi wa Tunduru, ni kwamba pale Tunduru pana namna mbili ya kufikiwa umeme. Awali ilikuwa utoke umeme kutoka Makambako, Songea mpaka Namtumbo, Namtumbo pale twende Tunduru kwa umeme wa *grid*. Lakini nasema mradi huo ni mkubwa na uko mbali, umeme wa karibu zaidi ni huu wa gesi ambao uko mwingu kutoka Mtwara umefika Masasi, mradi wa kutoka Masasi sasa unakwenda Mangaka kwa Mheshimiwa Dunstan Mkapa pana kama kilomita 60 pale.

Tumesema ukishafika Mangaka ni rahisi zaidi kwenda Tunduru kuliko kutokea Namtumbo. Kwa hiyo, ahadi ya Serikali ni kwamba tumewapa kazi *TANESCO*, tukishafika Mangaka, amba ni mradi amba haujamilika na ndiyo ahadi iliyopo sasa hivi tuangalie uwezekano wa kwenda Tunduru kwa sababu ni wepesi zaidi kutoka Mangaka kwenda Tunduru kuliko kutokea Namtumbo amba ni mkoa huo wa Ruvuma, lakini huku ni mkoa wa Mtwara.

Bado Mangaka ni karibu zaidi, kwa hiyo ninaomba niwaambie wananchi wa Tunduru kwamba ahadi ile ipo na ndiyo kazi ile ya wepesi inaonekana itawafikishia umeme wa uhakika zaidi na wa gharama nafuu tutatoka Mangaka kwenda Tunduru.

**NAIBU SPIKA:** Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge kama tulivyokwisha kuwatangazia hapo nyuma kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni alikuwa ameenda Safari. Ningependa kulijulisha Bunge kwamba amerejea na tunaye humu ndani. (*Makofit*)

Kwa hiyo naomba kutambua uwepo wake, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana na pole kwa safari. Sasa namwita Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera.

Na. 226

### **Hitaji la Umeme – Kasulu**

**MHE. AGRIPINA ZAITUNI BUYOGERA** aliuliza:-

Kumekuwepo na kilio cha muda mrefu sana kwa wananchi wa wilaya ya Kasulu kutaka wapatiwe umeme kwani tangu uhuru hawajawahi kupatiwa umeme huo licha ya ahadi nyingi zinazokuwa zikitolewa na Serikali zisizoteklezeka:-

Je, ni lini ahadi ya kuwapatia umeme wananchi wa Kasulu itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nisahta na Madini, napenda kujibu swali la Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uungaji wa umeme katika makao makuu ya wilaya ya Kasulu, ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya kipeleka umeme kwenye makao makuu wilaya ya Kasulu, Kibondo Kigoma, zilizotengenewa jumla ya shilingi bilioni 29.7 kwa ajili ya kununua na kuunganisha jenereta hizo tisa zenye jumla ya uwezo wa MW 11.25 kwa mkoa wa Kigoma kama nilivyosema katika swali la awali. Katika wilaya ya Kasulu kazi hii inatarajiwa kufanywa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Usimikaji wa mitambo miwili ya kufua umeme ambao umefanywa na mkandarasi kutoka Netherlands na kampuni ya M/S Zwart Techniek kwa ufadhili wa Serikali. Kazi ya kusimika mitambo miwili yenye uwezo wa *megawatt 1.25* kila mmoja ilikamilika mwezi Desemba, 2010.

(ii) Ujenzi wa mifumo ya kusambaza umeme yenye urefu 18.5, njia ya msongo ya *kilovott 11* yenye kilomita 56 za njia ya msongo wa volti 400 unaofanywa na kampuni ya *M/S NAMIS CORPORATE LTD.* ya DSM. Kazi iliyokamilika hadi sasa ni

ujenzi wa njia ya msongo wa kV 11, ufungaji wa *transfoma mbili* (2) na usimikaji wa nguzo 262 za msongo wa *volt 400 (low voltage)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii bado inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu, 2011.

**MHE. AGRIPINA ZAITUNI BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kikao kilichopita, Mheshimiwa Waziri wa Nishati, alituahidi wananchi wa Kasulu, kwamba umeme utawaka mwezi wa tatu mwaka huu, 2011,

Mheshimiwa Naibu Spika, haoni kwamba majibu ya Naibu Waziri yanapelekea kutukatisha tamaa wananchi wa Kasulu kwa sababu ahadi hii ya kuwasha umeme wilaya ya Kasulu ni ya muda mrefu?

Kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, na nishukuru kwamba matarajio ya kuwaka umeme makao makuu ya wilaya yako mbioni.

Ninaomba Naibu Waziri anatuambie nini sisi wananchi wa jimbo la Kasulu Vijijini kwamba tutapataje umeme kwa kuwa tayari tuna mradi wa umwagiliaji kijiji cha Tite, ambacho mradi huo una maporomoko makubwa yenye uwezo wa kuzalisha umeme na kusambaza katika vijiji vya Jimbo la Kasulu Vijijini ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Agripina Buyogera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya utekelezaji ya majenereta haya ya Kigoma na Kasulu na yale Kibondo, utekelezaji wa miradi hii ni kweli imechelewa kidogo, lakini nadhani kwenye kikao hiki hiki tumewahi kutoa maelezo kwamba kulikuwa na matatizo kidogo katika upatikanaji wa vifaa. Tatizo lile *TANESCO* amewasiliana na mkandarasi na tumesema tunalifanyia kazi hili kuliharakisha.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge kwanza atambue na nimefurahi kwamba ameshukuru kwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ili kufikia hatua hii tuliyofikia na namwahidi kwamba tunasimamia kwa karibu sana utekelezaji wa miradi hii ikamilike haraka iwezekanavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la maporomoko makubwa kule Tite, ambapo kuna uwezekano pia wa kuwa na mradi wa umwagiliaji, hii ndiyo miradi ambayo imeundiwa *REA*, kwamba tunataka hivi *mini hydro* ambavyo vimezunguka zunguka yuko mmoja kule Nzovwe, Ruvuma na yuko mmoja kule maeneo ya Namtumbo na yupo mwingine Tosamaganga na wapi sijui.

Miradi hii tunahimiza *REA* iwasiliane na wananchi na wataalam wake na wananchi wa maeneo ya pale karibu ili kuangalia uwezakano wa kuzalisha mradi wa umeme wa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimelipokea hili la maporomoko makubwa ya Tite, tutawasilishia *REA* waunganishe katika ile miradi yao ya *min hydro* waangalie kama inaweza kukidhi haja ya kuleta umeme kwa gharama nafuu katika maeneo hayo, ili wananchi wapate nyongeza ya umeme ukiongeza na ile ya jenereta ambayo tayari ipo.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa masuala ya umeme ni kipaumbele kikubwa kwa Waheshimiwa Wabunge wengi nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya atauliza swali la nyongeza la mwisho kwenye eneo hili.

**MHE. JENISTA J. MUHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili la nyongeza. kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu swali Na. 225 muda si mrefu uliopita ametukatisha tena tamaa wananchi wa mkoa wa Ruvuma kwa kutueleza kwamba mradi wa *grid* kutoka Makambako kwenda Songea utachukua muda mrefu.

Kwa kuwa tayari wenzetu wa Umeme Vijiji *REA* wameshafikia hatua nzuri sana za maandalizi ya kutumia umeme wa maporomoko kutoka katika kijiji cha Mahenje, jimbo la Peramiho, tarafa ya Madaba, ili ku-*generate* umeme utakaoingia tena kwenye *grid* ya taifa na kusambazwa katika maeneo ya Songea Vijijini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuhakikishia mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho, kuititia tarafa ya Madaba kwamba mradi ule sasa utaanza kutekelezeka katika Bajeti ya mwaka huu?

**NAIBU SPIKA:** Mradi wa Madaba, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimtoe wasiwas, majibu yangu hayakukusudiwa kukatisha tamaa. Tatizo la Makambako, Songea linaleweka, kwa sababu kwa miaka miwili sasa limekuwa linazungumzwa humu Bungeni ya kwamba tatizo hili lilitokana na mabadiliko katika vipaumbele vya mfadhili wa Sweden.

Tumekwenda tunazungumza naye na tumefikia sehemu nzuri na sasa hivi mchakato wa kumpata mhandisi mshauri umekamilika, kampuni ya *M/S WORK* imeteuliwa kufanya kazi hiyo. inatarajiwa katika kipindi cha wiki hizi za mwanzo za Julai hadi mwishoni makubaliano yale ya kutiliana sahihi yatakamilika.

Mhandisi anatarajiwa kuanza kazi ya ujenzi wa mradi ule wa Makambako Songea mwezi Agosti, 2011 ambapo ataandaa michoro ya njia za umeme na vituo vya kupozea umeme. Baada ya hapo kwa kushirikiana na *TANESCO* atateua mkandarasi atakayefanya kazi ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme, tutafika Songea, umeme utakwenda mpaka Namtumbo utakata kulia, utakwenda mpaka Peramiho, kwa hiyo mpaka Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumhakikishia kwamba mradi huo uko *on truck* na unaendelea vizuri. Lakini hili la Mahanje, hili ni la maporomoko la maji, narejea tena miradi ya *min hydro* tumekubaliana iende *REA* ili ipate utekelezaji. Nitawapelekea *REA*, utekelezaji wa mradi huu na jana kwa bahati nzuri Mheshimiwa Jenista alinizingumzia kuhusu mradi huu na nimetoa maagizo *REA* nikapata majibu ya maandishi leo mchana nitamkabidhi ili ajue utekelezaji wa mradi huu unafikia wapi.

**MHE. MUHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na mpango huo wa kufunga majenereta ya Kasulu na Kibondo, upembuzi yakinifu umeonyesha kwamba Malagarasi, Igamba three tutapata megawati 41.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kupata pesa ili tuanze mradi huo amba ni umeme wa uhakika tunaweza tukapata mkoa mzima na kuwapa mikoa wa jirani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema kwa sasa hivi upembuzi yakinifu ule wa kubaini kama Malagarasi three imekaaje, estimate ya awali ni kwamba zitapatikana megawati 41. Lakini tukishafika hatua hiyo tunarejea tena kutafuta *financial closure* kwa maana tunatafuta pesa za mfadhili.

Tumekubaliana ndani ya Serikali na tumeshalisema hapa Bungeni, kwamba tutakopomaliza upembuzi yakinifu, ikiwa *MSS*, watakwama kuendelea na mradi ule tutatafuta *financing* kwa njia nyingine yoyote ile kwa sababu megawati 41 ni kwa kanda nzima ile ufumbuzi kwa mkoa wa Kigoma wote, maeneo ya Katavi.

Pia kwa maeneo ya Urambo na Kaliua, kwa hiyo ni mradi amba utakidhi mahitaji mengi. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mhonga kwamba Serikali tumedhamiria kwamba mradi huu utatekelezeka.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lilikuwa limeelekezwa kwa Waziri wa Ardhi, na kwa sababu lilikwishapata jibu linalohusu swali hili naomba leo kulisitisha swali hili. (*Makofi*)

Na. 227

**Kufutwa kwa Hati za Mashamba ya Mkonge – Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kufuatia ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza la kufuta Hati za mashamba zaidi ya 10 ya Mkonge yasiyoendelezwa mwaka 2010 Rais wa Tanzania alitoa ahadi ya kuanza kufuta Hati za shamba la mkonge la Kibaranga:-

- (a) Je, Hati ya shamba hilo imefutwa?
- (b) Je, ni lini mashamba ya *Bombuera Estate*, Kwafungo, Lewa, Azimio, Mtapwa na Kihuwi yatafutiwa Hati?
- (c) Kwa nini bodi ya Mkonge bado inaruhusu wawekezaji na baadhi waliogawiwa maeneo ya shamba hilo nje ya utaratibu wakati mkakati wa kufutwa Hati umefika ngazi ya Taifa.

*(Swali tajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, mwenye swali amelisitisha, kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata, la Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

Na. 228

**Tatizo la funza kwenye Matunda**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Tatizo la funza kwenye matunda kama maembe, mapera na kadhalika ni kubwa sana, na inasemekana husababishwa na inzi:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kupambana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tatizo la funza kwenye matunda mengi hapa nchini hususan; maembe, mapera na kadhalika, ni kubwa sana na usambabishwa na funza wanaozalishwa na inzi wajulikanao kitaalam kama *bacterocera invadens*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo hili, vituo vya utafiti vya kilimo vya Tanzania vikishirikiana na Taasisi ya kimataifa ya utafiti wa fiziolojia na ecolojia ya wadudu yaani *International Centre for Insect Physiology and Ecology* au *ICIPE*, wamefanya utafiti wa kina na kujua maumbile, maisha na fiziolojia ya wadudu

waharibifu wa matunda, hususan maembe, mapera, michungwa, miparachichi, ndizi na kadhalika. Aidha, wataalam wetu wamegundua njia za kukabiliana na wadudu hao ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutumia kemikali inayotolewa na mainzi jike kuvutia madume ya nzi hao yaani *pheromone* yaje kushiriki katika tendo la kuzaliana. Kemikali hiyo huwekwa katika ulimbo kwa kiasi kinachowavutia madume wengi ili yanase na hivyo kupunguza sana mazalia ya wadudu hao. Katika mwaka 2010/2011 jumla ya lita 260 za kemikali hiyo zilitumika kwa mafanikio makubwa.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa *TPRAI* na *ICIPE* wamegundua pia manyigu ambayo ni adui wa asili yaani *natural enemy* anayewala mainzi hao aitwaye *Fopius arisanus*. Serikali imewaleta mabuu (au pupa) kwa nyigu huyo 30,000 kutoka *ICIPE* ili wazalishwe kwa wingi na kusambazwa katika nchi kwa ajili ya kuwadhibiti inzi waharibifu wa matunda.

(iii) Wataalam wamegundua kwamba kufanya usafi shambani kwa kuokota maembe yaliodondoka angalau mara moja kwa wiki na kuyafukia kwenye shimo la kina cha futi 3 ili kuzuia kuanguliwa kwa mafunza wa inzi hao pia kuwadhibiti wadudu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafanikio haya Serikali imetoa mafunzo ya namna ya kuwatambua na kuwadhibiti funza waharibifu wa matunda kwa wataalam wa kilimo 116 wakiwemo maafisa kilimo 88, wakaguzi wa mazao 22 na maofisa wa maabara 6. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na shirika la chakula na kilimo la umoja wa mataifa *FAO*, na *ICIPE* imechapisha na kusambaza vipeperushi 6,000, mabango 3,000 na nakala 100 za kijitabu chenye maelezo ya namna ya kuwatambua na kuwadhibiti wadudu hao.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Pamoja na mafanikio ambayo ameyaona naomba niulize swalil hili, kutokana na *data* hizi ambazo zimeahinishwa na Mheshimiwa Waziri inaonekana bado hakuna dhamira ya dhati ya kuondoa hili tatizo kutokana na uhaba wa wataalam na uhaba wa maabara hasa katika mikoa inayozalisha matunda.

Je, Serikali yetu itaanzisha maabara zenyе vifaa vya kisasa na wataalamu wa kutosha katika mikoa na wilaya zinazozalisha matunda kwa wingi? Na hasa katika maeneo ambayo yamegundulika kuwa na tatizo la huyu funza ambaye anaingia kwenye matunda?

Pili, kwa kuchelewa kuwa na Maabara za kisasa na zenyе vifaa vya kutosha inaonekana kwamba katika suala zima la kulinda uzalishaji wa matunda bora na viwango

ni sehemu ya kudumaza kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Je, Serikali ina mkakati gani wa Kilimo Kwanza, imeliangalia hili au tunaangalia uzalishaji wa nafaka tu kama vile Mahindi, Mtama, Mpunga na kadhalika na tumelisahau suala la matunda?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Riziki Omar Juma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwa undani kwamba, tatizo hili siyo la Tanzania peke yake, tatizo hili linazihusu nchi ambazo zinazalisha matunda ya Maembe, Mapera, Maparachichi, Machungwa na kadhalika. Kitu muhimu ni kufanya utafiti na kujua namna ya kupambana na wadudu hawa, siyo kuweka maabara kila mahali. Maabara haiuwi wadudu lakini kinachoua wadudu hawa ni matokeo ya utafiti na namna ya kuutumia ili kupambana na wadudu hawa.

Katika utafiti ambao umefanywa *pheromone* ambayo inawavutia madume kwenda kuzaliana na majike imegunduliwa na inatumika, ikiwekwa kwenye Ulimbo na Ulimbo huu hauhitaji maabara tena ni kuchukua *pheromone* kuweka kwenye Ulimbo na kuitawanya katika maeneo mbalimbali. Utafiti ambao umeanza umefanywa katika Wilaya ya Mkuranga umeonyesha mafanikio mazuri na kazi hii itaendelezwa.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa jinsi ambavyo tumefanya kazi hii na kwa jinsi ambavyo hatua nyingine ya kuwapata Manyigu wanaoweza kupambana na wadudu hawa inavyofanya kazi vizuri. Sina shaka kwamba funza huyu atawenza kuwa *controlled* vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la funza linaloathiri Mapera na Maembe, kuna tatizo kubwa sana sasa hivi katika Jimbo la Kisese Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla na maeneo yote ya walima Pamba kwamba licha ya msimu kufungua tarehe 20/6 mpaka sasa hivi wanunuzi wa Pamba wanasuasua kununua Pamba na tatizo hili limesababisha wananchi kukosa soko la uhakika kwa ajili ya kuuza Pamba yao.

Sasa Serikali inalijua tatizo lakini je inafanya jitihada gani kuhakikisha kuwa wanunuzi wa uhakika wanapatikana ili wananchi wapate soko la uhakika huko Kisese na sehemu nyingine?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la msingi lilikuwa juu ya funza anayekula Maembe, Machungwa na Maparachichi. Naomba Mheshimiwa Mpina atuletee swalii hili kwa njia ya kawaida ili tuweze kumjibu vizuri.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kumwuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi amekubali kuwa tatizo hili linahitaji gharama ya fedha kwa sababu ni kuleta hao madume ambao wanaweza wakasababisha kupunguza kwa inzi lakini pili kemikali ambayo inasadidua kuua.

Kwa sasa Pemba nimeona imeletwa mitego fulani michache sana inawekwa katika miembe na hawa inzi wanaingia ndani ya mitego hiyo. Sasa mimi ninapenda kumwuliza kwamba kuna mkakati gani wa kuomba hata mashirika ya Kimataifa ili kusaidia katika tatizo hili kwa sababu mwisho wa siku litaharibu uchumi wa taifa letu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kwa swali lake la nyongeza.

Ni kweli kwamba tatizo hili ni kubwa, sisi tunashirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa pamoja na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Fiziolojia na Ekolojia ya wadudu katika kupambana na tatizo hili. Aidha, tunashirikiana na nchi jirani za Afrika Mashariki katika utafiti huu na kwa kweli kwa hatua ambayo tumefikia katika utafiti huu nina uhakika kabisa kwamba wadudu hawa tutaweza kuwa-*control* vizuri.

Na. 229

#### **Mkakati wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Katika mukutano uliandaliwa na *WHO* na Wadau wa Afya Duniani, Rais wetu alihudhuria huko Geneva Uswiss, walizungumzia namna ya kutoa taarifa na uwajibikaji.

- (a) Je, nchi yetu ilipata nafasi ya kutoa taarifa yake ya uzoefu na changamoto na mikakati?
- (b) Je, taarifa hiyo ni ipi?
- (c) Je, Tanzania imefaidika vipi na mukutano huu hasa baada ya kutoa taarifa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Martha M. Mlata Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameteuliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza pamoja na Waziri Mkuu wa Canada Mheshimiwa Stephen Harper, kwenye Tume ya Taarifa na Uwajibikaji kwa ajili ya afya ya wanawake na watoto *Commission on Information and Accountability on Women's and Children's Health* katika Tume hii Mheshimiwa Rais amewakilisha nchi zinazoendelea na Tanzania imepata nafasi ya kutoa uzoefu ikizingatia changamoto katika nchi yetu ambayo ni mfano wa nchi zinazoendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo tuliyoweza kuchangia ni kuelezea changamoto katika ukusanyaji wa taarifa na kusisitiza umuhimu wa Tume hii. Kila mdau akikubali mfumo mmoja wa utoaji taarifa kama hatua muhimu katika kuboresha mfumo wa taarifa za afya. Pia umuhimu wa nchi zilizoendelea kuwekeza kwenye kuboresha ukusanyaji wa taarifa kwenye nchi zinazoendelea ulisisitizwa. Aidha, ilisisitizwa kwamba nchi zinazoendelea ndiyo zinachangia takribani 99% ya vifo vitokanavyo na uzazi duniani hivyo ni muhimu kuweka msisitizo kwenye kuwezesha nchi zenye vifo vingi vitokanavyo na uzazi na vya watoto viweze kupiga hatua haraka katika kudhibiti.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano wa kwanza wa Kamisheni ulifanyika Geneva Uswisi Januari, 2011, na wa pili ulifanyika Dar es Salaam, Mei tarehe 1 na 2 mwaka huu 2011. Faida ambayo Tanzania itapata kutokana na Tume hii ni matokeo ya kazi ya Tume. Tume imekamilisha kazi yake na ripoti ya Tume imetoea mapendekezo 10 ambayo yanalenga kuboresha maeneo makuu matatu ambayo ni:-

- Taarifa bora kuwezesha matokeo bora (*better information for better results*).
- Taarifa sahihi kuhusu raslimalifedha (*better tracking of resources*).
- Usimamizi bora zaidi kitaifa kitaifa na kimataifa (*better oversight nationally and globally*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kupewa heshima kubwa kama hiyo, ni heshima yetu sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Rais wetu amekuwa akipewa heshima kubwa sana kwenye mataifa mbalimbali na mikutano mbalimbali na ninaamini kabisa

angependa kuona Tanzania inakuwa ni nchi ya kwanza kuondokana na changizo la 99% ya vifo vya akina Mama kwenye nchi zinazoendelea.

Je, Wizara ina mikakati gani sasa madhubuti ya kuenzi heshima hiyo ambayo Rais wetu amepewa kwa kupunguza vifo hivi au kumaliza kabisa?

Pili, kwa kuwa Tume ilikuwa na mapendekezo 10 ambayo yanashughulikia maeneo makuu matatu lakini mimi nazungumzia kuhusu taarifa sahihi kuhusu raslimali fedha. Kwa kuwa Wizara hii imekuwa ikitegemea sana ....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ungekwenda kwenye swali moja kwa moja ungenisaidia sana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Kwa kuwa Wizara hii imekuwa ikitegemea sana fedha kutoka nje za wafadhili na mara nyingi wafadhili wakati mwingine hawatoi pesa zote. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuziba pengo hilo wafadhili wasipoleta fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru kwa kumpongeza Rais, nimepokea hizo pondezi na nitahakikisha nitamfikishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejipanga vizuri tu katika kuhakikisha kwamba tunamwenzi Rais wetu katika kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akina Mama na watoto.

Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ambayo yako wazi kabisa kwamba Wizara tuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akina Mama na watoto na ndiyo sababu tumehakikisha kwamba kwenye mpango wa MAM kwenye kila *component* na *stage* yake maana yake kwenye Zahanati, kituo cha Afya na kwenye Wilaya tunakuwa na *theatre* ambazo zitasaidia akina Mama wanaopata matatizo ya uzazi ili wasifariki.

Tumehakikisha kwamba tumeboresha mfumo wetu wa chanjo yaani mnyororo baridi kwa ajili ya kutunza *fascine* ndiyo sababu Wizara iumepiga hatua na tukilinganisha na nchi nyingine zinazoendelea 92% ya watoto wanapata chanjo na tumehakikisha kwamba tume *revive MCH 8* ambao wataendeleza zile *clinic* za akina Mama wajawazito ili tuweze kutambua matatizo haraka.

Swali la pili, Mheshimiwa Mlata anataka kujua kwamba tuna mpango gani au mkakati gani wa kuziba mapengo ambayo yatatokana na kwamba kama wafadhili wanaotoa mchango kwenye uzazi wa mpango pamoja na kuboresha afya ya akina Mama wataondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba ndiyo sababu tumefanya *integration* ya huduma za akina Mama na watoto kwenye Zahanati zetu ambazo ziko siku

zote. Vituo vya afya ambavyo viko siku zote pamoja na kuhamasisha mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo yapo hapa nchini *locally* yaendelee kuisaidia Serikali katika kupambana na hili tatizo la vifo vya akina Mama na watoto.

Na. 230

### **Tatizo la Ombaomba Mijini**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Suala la ombaomba limekuwa ni tatizo sugu kwenye miji yetu ya Iringa, Mbeya, Dar es Salaam na kwingineko nchini:-

- (a) Je, Serikali inajua sababu kubwa ya tatizo hili?
- (b) Watoto wadogo wamekuwa wakitumiwa kwenye zoezi la ombaomba na kushihdwa hata kwenda shule. Je, Serikali inasemaje kuhusu suala hilo na Sheria inazungumziaje tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta R. Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Iringa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu nyingi zinazochangia kuwepo kwa ombaomba hapa nchini na baadhi yake ni kama ifuatavyo:
  - Ugumu wa maisha kutokana na umaskini wa kipato.
  - Tabia ya baadhi ya watu kutopenda kufanya kazi yaani uvivu na tamaa ya kujipatia kipato kwa njia ya haraka na nyepesi.
  - Tabia ya baadhi ya watu kutoa kwa ombaomba wakiamini kwamba kwa kufanya hivyo watapata thawabu kwa Mwenyezi Mungu.
  - Mila na Desturi potofu zinazowabagua watu wasiojiweza na wenye ulemavu.
  - Migogoro na kuvunjia kwa ndoa na kudhulumiwa mali za urithi ambako kunasababisha baadhi ya watoto kukimbilia mitaani.
  - Kukosekana kwa Sheria mahsusii inayokataza watu kuwa omnia omnia.
  - Kuwepo kwa vivutio mbalimbali mijini tofauti na vijijini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapinga vikali kitendo cha watoto kutumiwa kuomba omnia ikizingatiwa kuwa ni wajibu wa mzazi au mlezi kuhakikisha kuwa mtoto anapata matunzo, malezi na ulinzi inavyostahili.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 2 ya Mwaka 2009, ni kosa la mzazi au mlezi kumtumia mtoto kama omnia kufanya hivyo kunamkosesha mtoto haki zake za msingi ikiwemo ya kupata Elimu. Sheria inaainisha wazi haki za msingi za mtoto na kupiga marufuku vitendo vyo vyote vinavyosababisha mtoto kukosa haki hizo. Aidha, Sheria hii inaainisha wajibu wa Wazazi, walezi na ndugu wengine katika kumlea na kumtunza mtoto kwa kumpatia mahitaji yake ya msingi kwa kuzingatia uwezo wa mzazi au mlezi huyo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa, Madiwani Viti Maalum katika Manispaa ya Ilala akiwemo Mheshimiwa Ritta Kabati wakati wake walijenga jengo la kuwakusanya watoto wote waliokuwa wanaombomba katika Jiji la Dar es Salaam lakini wazazi walikwenda kuwatoa watoto wale kwa muda wa siku tatu tu yaani waliishi kwa muda wa siku tatu tu. Wakaacha huduma hiyo na jengo hilo na kwa kuwa wazazi hao wanajulikana wanazunguka nao huko Dar es Salaam wakisubiri waombe wao wanachukua pesa walizoomba.

Je, Serikali inawachukulia hatua gani hao wazazi ambao pia wanajulikana?

Kwa kuwa, hata katika Manispaa ya Singida kipo kituo ambacho kilianzishwa na Mzungu ambaye alikuwa anaishi kwa mkataba Tanzania, mkataba ulipoisha aliondoka na tangu alipoondoka hakuna huduma tena anayoituma katika kituo hicho. (*Makofi*)

Kituo hicho sasa hivi kinahangaika na watoto hawana mtu maalum wa kuwashudumia. Kinahudumiwa tu anapotokea msamaria mwema labda Mbunge ama yejote yule.

Je, Serikali inakififikiraje kituo hiki ambacho sasa kimetelekezwa na Mzungu huyo ili watoto hao ambao tayari walishajisalimisha katika kituo hicho waendelee kupata huduma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza naomba nimshukuru kwamba Madiwani wa Viti Maalum walichukua hatua nzuri ya uwajibikaji ndani ya jamii ya kukusanya watoto waliokuwa wanadhalilika nakuomba omnia katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba hatua hiyo ilikuwa nzuri ila naomba kusema kwamba kulikuwa na udhaifu kidogo tu kwamba haikuwekewa msukumo wa Sheria.

Kwa hiyo, walipokusanywa na wazazi wakajitokeza ndiyo ilikuwa nafasi ya wale wazazi sasa wachukuliwe hatua na waambiwe kwamba ni marufuku kuonekana mtaani mkiombaomba na watoto wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi tuna Sheria ya Mtoto na Sheria ya mtoto Kanuni zake zimemalizika. Kwa hiyo, mimi ninaomba sasa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani mkishirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hiyo hatua tena inaweza ikachukuliwa kwa sababu sasa tuna Sheria ya kuweza kuwawajibisha wale wazazi na ninaamini wakiwajibishwa watoto hawatarudi mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Singida ndiyo nimekisikia kwa Mheshimiwa Mbunge na ninashukuru kwamba Mheshimiwa Mbunge kweli anaonekana kwamba anafahamu sana huduma zote za kijamii katika eneo lake. Mimi naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuangalie namna ambavyo Idara yetu ya Ustawi wa Jamii itaingilia kati kuhakikisha kwamba hao watoto wanapata huduma stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Amina Mohammed Mwidau, atauliza swali Na. 231.

Na. 231

### Ahadi za Mheshimiwa Rais - Tanga

**MHE. AMINA M. MWIDAU** aliuliza:-

Katika kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kuufanya Mkoja wa Tanga kuwa mji wa viwanda na kuyarejesha Serikalini na baadaye kuwagawia wananchi mashamba ya Mkonge yaliyotelekezwa na wawekezaji:-

- (a) Je, utaratibu wa kuwagawia wananchi mashamba hayo utaanza rasmi lini?
- (b) Je, ni mkakati gani utatumika kuhakikisha kuwa mji wa Tanga unakuwa mji wa Viwanda zaidi ya ulivyokuwa zamani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mhedhimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina M. Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Tanga imeanza mchakato wa kuyafuutilia mashamba yote ya Mkonge yaliyotelekezwa kwa kushirikiana na Bodi ya Mkonge. Tayari imebainika kwamba mashamba mengi ya Mkonge yamevamiwa kiholela na kutumiwa katika kilimo cha mazao mchanganyiko. Hivyo, suala la kubatilisha hati miliki za mashamba hayo na kuwagawia wananchi kama ilivyo ahadi ya Mheshimiwa Rais, litafanywa baada ya kukamilisha taratibu za kisheria na mfumo mahsusutu utakaotumika kukamilisha azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuufanya mji wa Tanga kuwa wa Viwanda, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Tanga wametenga eneo lenye ukubwa wa hekta 1,363 katika Kata ya Tangasisi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vinavyolenga maeneo maalum kwa mauzo ya nje na maeneo maalum ya kiuchumi (EPZ/SEZ). Eneo hili litawekewa miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme, barabara na mfumo wa majitaka ili kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika viwanda. Aidha, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) limepata eneo jingine lenye ukubwa wa hekta 50 katika eneo la Kange ambalo kwa kushirikiana na wawekezaji wa ndani na nje litaanzisha *Industrial Park* kwa ajili ya miradi mbalimbali. Michoro muhimu ya kuonesha matumizi ya ardhi na mipaka ya viwanja (*Layout Plan na Cadastral Survey*) imeandaliiwa na utaratibu wa kumpata mkandarasi wa kujenga miundombinu ya umeme na maji katika eneo hilo unafanywa. Nia ni kuwavutia wawekezaji na kuhakikisha kuwa uwekezaji huo unaanza kabla ya mwisho wa mwaka 2011.

Halikadhalika Serikali imeanza mchakato wa kujenga bandari mpya pale Mwambani, Tanga ambayo itakuwa kiungo muhimu kwa kuchochea maendeleo ya Viwanda kwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa za viwandani hasa zilizoongezwa thamani kutoka mazao ya kilimo (*Agro Processed Products*) kwenda katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, maendeleo ya viwanda Tanga yatategemea sana bandari yenye uwezo mkubwa kuliko ilivyo sasa, hivyo Bandari ya Mwambani italeta mapinduzi tarajiwu. Kwa sasa Kampuni ya *Scot Wilson* ya UK inafanya ‘*feasibility study*’ kuhusiana na ujenzi wa bandari hiyo.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali iko katika kampeni ya Kilimo Kwanza, hivyo ni muhimu sana kuharakisha taratibu hizo.

(i)Je, Serikali inawaahidi wakazi wa Tanga kuwa ni lini taratibu hizo za kisheria zitakamilika na wao kuweza kugaiwa mashamba hayo?

Je, ni mwaka mmoja, miwili, mitatu, ni lini maana ni bora wawe *specific* ili wananchi waweze kujua?

(ii)Kwa kuwa karakana ya Reli waliorithi kutoka kwa wakoloni ilikuwa mkoani Tanga, na kuhamishiwa Mkoani Kilimanjaro mwaka 1993/1994 kwa sababu ambazo wananchi hawakuzielewa na wananchi wengi wakapoteza ajira?

Je, Serikali haioni kuwa sasa hivi ni wakati mwafaka wa karakana hiyo ya reli kurejeshwa mkoani Tanga kwa kuzingatia kuwa sasa hivi mkoa wa Tanga kuna mikakati mahsus ambayo inataka kuufanya mji wa Tanga kuwa mji wa viwanda kuliko ulivyokuwa hapo awali? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mhedhimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Amina M. Mwidau, la kwanza na la pili ambalo linahusiana na karakana ya reli litajibowi na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taratibu za kisheria ambazo lazima zifuatwe. Kwanza mashamba haya yana Hati Miliki za watu ambao wameyamiliki kwa miaka mingi na hapa katikati yakatelekezwa.

Ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uchaguzi Mkuu ilikuwa ni kuanzisha taratibu za kisheria za kuweza kuyarejesha mashamba hayo. Kwanza Hati zile zibatilishwe, pili yaweze sasa kugaiwa kwa wananchi kwa mfumo na utaratibu ambao utakuwa wazi na utaeleweka kama nilivyooleza katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, narudia jibu langu la msingi kwamba, Mheshimiwa Mbunge avute subira taratibu hizi lazima zifuate mkondo wa sheria na mara zikikamilika kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) itatimiza ahadi yake. (*Makofit*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Amina M. Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli Tanzania lina karakana katika sehemu mbalimbali, siyo Tanga tu kuwa imehamishiwa Moshi, bali kuna karakana zilizokuwepo mbili Tanga, Moshi, mbili Morogoro, mbili Dar es Salaam na Tabora. Kwa kipindi kirefu nyingi za karakana hizi zimekuwa hazifanyikazi pamoja na ile ya Moshi anayoiiongelea Mheshimiwa Mbunge. Zinazofanyakazi ni za Morogoro na Dar es Salaam pekee. Katika mikakati yetu ya kuboresha Shirika la Reli, tunaenda kufufua karakana zote. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tu na hiyo ya Tanga na mimi nina - *declare interest* kwa kuwa ni Mbunge wa Tanga, kama yeye ninataka ifufuke. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuongezea kitu kimoja. Masuala ya viwanda kwa mfano, haya siyo masuala ya Serikali Kuu peke yake, ni masuala ya Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa. Nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge awe anashirikiana nasi kikamilifu katika Halmashauri ya Tanga kuhakikisha kuwa viwanda vinarudi Tanga kwa sababu kazi hiyo tumeifanya na wenzake ambao wako pamoja naye kwenye chama chake nao awashauri kuwa tunapoweka mikakati hiyo watunge mkono kwa sababu Uchaguzi umekwisha na sasa ni wakati wa kujenga Tanga, ni wakati wa kujenga Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Tulitendee haki swal la mwisho, Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda tuko nje kidogo. Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, swal la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Na. 232

### **Ushindani wa Wanariadha wa Tanzania**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Katika miaka ya nyuma mchezo wa riadha uliiletea sifa kubwa nchi yetu kwa wanariadha kama Filbert Bayi, Juma Ikangaa, Selemani Nyambui na wengine kushinda katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa tofauti na sasa ambapo mchezo huu umedorora.

- (a) Je, kwanini wanariadha wa siku hizi hawafanyi vizuri?
- (c) Je, Serikali inatumiae fursa ya kuwa na Rais anayependa michezo katika kuendeleza mchezo wa riadha?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya sababu zinazowafanya wanariadha wa siku hizi kutokufanya vizuri ni pamoja na kutokuwepo kwa misingi imara ya kuendeleza michezo katika jamii zetu na mashulenii, kukosekana kwa vifaa vya mchezo wa riadha, programu ya mashindano ya kitaifa na kukosekana hamasa miongoni mwa wadau wa michezo tofauti na mchezo wa Mpira wa Miguu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kunufaika na kuwa na Rais mpenda michezo kwa njia mbalimbali. Moja ni utekelezaji wa maamuzi muhimu yaliyofanywa na Rais ya kuagiza kurejeshwa kwa michezo ya Shule za Msingi na Sekondari na kufanyika kwa mjadala wa kitaifa kujadili Maendeleo ya Michezo nchini. (*Makofi*)

Mjadala kuhusu Maendeleo ya Michezo nchini umefanyika katika ngazi za Wilaya na Mkoa na kabla ya Bunge hili kwisha utakuwa umefanyika katika ngazi ya Taifa. Mjadala hiyo itatusaidia kupata ufumbuzi wa matatizo yanayohusu Maendeleo ya Michezo nchini ikiwa ni pamoja na mchezo wa Riadha. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini pia niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa wenzetu wa Kenya wanafanya vizuri sana katika mchezo wa riadha na kwa kuwa mazingira ya Kenya na sisi yanafanana sana.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba upo umuhimu wa Serikali pamoja chama cha riadha nchini kwenda Kenya kujifunza na kupata mikakati ambayo wenzetu wanafanya mpaka wakafanikiwa ili na sisi tuweze kufanikiwa? Wakinpendezewa wanihusishe na mimi nitafuatana nao.

(ii) Kwa kuwa katika mashindano ya riadha yaliyofanyika hivi karibuni Tanzania hatukufanya vizuri, tulikuwa watu wa sita (6) jambo ambalo limenisikitisha sana. Lakini kwa kuwa katika Mashindano ya Mpira wa Miguu wa Nchi za Afrika Mashariki na Kati, Tanzania tumefanya vizuri tumepata Kombe la Kagame, kuitia Klabu mahiri *Yanga Sports Club*?

Je, Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali yuko tayari kutoa pongezi kwa klabu ya Yanga kwa kuiondolea aibu Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Swali la msingi lilihusu Riadha, kwa hiyo swali la pili halina haja ya kujibiwa, Mheshimiwa Waziri majibu. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, kama ifuatavyo:-  
Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza naomba niseme kwamba dhamira yetu ni kuwaunganisha wadau tuzungumze kwa kina namna ya kuleta maendeleo, hatujafikia hatua ya kuona kwamba tumeshindwa kupata mawazo na changamoto kutoka ndani mpaka tuombe msaada wa Kenya, tukifika hapo hatutasita kuomba msaada kutoka Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo umesema halina haja sana ya kulijibu niseme tu kwa jumla kwamba ni faraja kubwa sana kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufanya vizuri katika mashindano yaliyomalizika juzi. Timu zetu mbili zimefika fainali, huku Yanga ikitwaa ubingwa, hili ni jambo ambalo Serikali inajivunia, Bunge lazima lijivunie. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. Kipindi chetu cha maswali sasa kimefikia mwisho kwa siku ya leo. Nitoe matangazo halafu baada ya hapo nitakupa nafasi kuhusiana na Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, nianze na matangazo ya wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo amba ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amba ni Watendaji Wakuu wa Wizara. Naomba kumtambulisha Katibu Mkuu, Ndugu Job Masima, ahsante sana na karibu sana Bungeni. (*Makofi*)

Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Iyombe, karibu sana. Naomba kumtambulisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis Mwamunyange, karibu sana Jenerali hapa Dodoma na hapa Bungeni, tunafurahi sana tunapokuona uko pamoja nasi. (*Makofi*)

Ahsante sana makofi hayo ni ya upendo mkubwa na Mheshimiwa Jenerali, karibu Kongwa pia. Ilikuwa ni kambi yake kabla ya enzi hizo. Pia naomba kumtambulisha Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali, Abdurrahman Shimbo, ahsante sana. (*Makofi*)

Naomba kumtambulisha Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Meja Jenerali, Samweli Kitundu. Ahsante sana. Pia tunaye Kamishina wa Sera na Mipango, Ndugu Nyayonga, karibu. (*Makofi*)

Naomba kwa pamoja niwatambulisse Mabrigedia Jenerali wote mliopo, naomba wote msimame, karibuni sana. Naomba niwatambulisse Makamishina na Makamishina Wasaidizi wote mliopo, naomba msimame. Naomba niwatambulisse Makanali wote mliopo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na kwa upande huo wa Wageni wa Mheshimiwa Waziri Hussein Ali Mwinyi, naomba niwatambulisse Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Karibuni sana, Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi, ninyi ni kiungo muhimu sana kwa shughuli kubwa na nyeti inayofanywa na Wizara hii. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao ujumbe wa NSSF kutoka Kenya, umekuja kutembelea Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kujifunza jinsi NSSF ya Tanzania inavyofanyakazi. Ujumbe huu unaongozwa na Afisa Balozi wa Kenya, Tanzania Bwana Patrick Nzusi, Mheshimiwa Balozi. Asante sana. Hawa wanaofuata sijui kama wapo, Meneja Mkuu, Mipango ya Utafiti, NSSF Kenya, Joseph Kamote. Inaelekea timu nzima haipo, yuko Tom Odongo na Rose Meta, Elias Baruti, Jamari Mmari na Andrew Kuyeyana.

Pia tunao wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari, Dar es Salaam Ilala. Wanafunzi kutoka Dar es Salaam, nadhani huenda watakuwa *basement* kule. Ahsante sana hao ndiyo wageni wetu.

Kuhusiana na taarifa za kazi. Mheshimiwa Mwamunyange nimepata vikaratasi vingi hapa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, vinauliza huko jeshini *gender* hakuna? Taratibu jamani. (*Makofi*)

Tangazo, tunaarifiwa kuwa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) litakuwa linaendelea kutoa huduma kwa Waheshimiwa Wabunge kila siku kuanzia Saa 4.00 asubuhi mpaka Saa 7.00 Mchana. Watendaji wa *NSSF* wanapatikana ghorofa ya chini (*ground flow*) jengo la Utawala. Tafadhali kwa yejote anayetaka kujua kuhusu *NSSF* afike hapo ili aweze kuhudumiwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magreth Sitta, anatangaza kikao cha Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ambapo anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wahudhurie katika kikao ambacho kitafanyika leo Saa 7.00 tarehe 13, Mwezi huu Ukumbi Na. 231. Kamati ya Huduma za Jamii, Ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili, tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wenu Mheshimiwa Magreth Sitta. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tangu tuanze session ya Bunge hili la Bajeti, mtaona kwamba tumekuwa hatunaye Katibu wetu wa Bunge mionganini mwetu, amekuwa haonekani. Ninaomba niwatangazie kuwa, Katibu wa Bunge anaugua mguu wake wa kushoto, ambao ulipata uvimbe baada ya safari ndefu ya kwenda Yukon Canada, kwa ajili ya Mkutano wa CPA Februari, 2011. Baada ya kupata uvimbe, mguu uliota lengelenge (*blister*), ambapo alilazimika kwenda hospitali kwa ajili ya matibabu na amekuwa akiendelea na matibabu; bahati mbaya matibabu ya mwanzo, yalimsababishia *allergy* ambayo ndiyo ililetä complication kidogo. Baada ya ushauri wa Madaktari, amebadilishiwa dawa na kwa jinsi hiyo amekuwa kwa muda wote chini ya uangalizi wa Madaktari kwa karibu na kwa hiyo kutohana na matibabu hayo, mguu wake unaendelea kupata nafuu unapona. Kwa sasa ana unafuu kama wa asilimia 80 hivi, kwa hiyo, mara hali yake itakapokuwa imeimarika, tutamwona tena akiwa mionganini mwetu.

Tangazo la mwisho ni kwamba; Mheshimiwa Assumpter Mshama, wengine tunamwita Mchungaji, ameugua tumbo ghafla jana na amelazwa katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, watakaopata nafasi ya kumtembelea, tunakaribishwa kufanya hivyo; na hii inathibitisha maneno niliyoyasema jana kwamba, Waheshimiwa Wabunge, hawana huduma maalum za matibabu kama inavyotaka kutangazwa na baadhi yetu. Wabunge wakiugua, wanapata matibabu katika hospitali zile zile ambazo Wananchi wanapata huduma.

Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012  
Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri; ni kweli Mheshimiwa Hamad Rashid, ultaka mwongozo kabla. Tafadhali endelea.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) na pia ninazingatia Kanuni ya 68(10), kifungu ambacho tayari ulishatoa maamuzi na kwa maana hiyo, nisingependa kurudia maamuzi yako, lakini ninaomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu katika Kambi ya Upinzani...

**NAIBU SPIKA:** Ningeomba uisome kidogo hiyo Kanuni.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Isome kidogo hiyo Kanuni ili twende pamoja wote.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kanuni ya 68 (7), halafu Kanuni ya 68(10) inasema: "Uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho." Sasa ninaomba nitakapotoa maelezo sitogusia hicho kifungu, lakini ndani yake kutakuwa na maneno kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, katika Kambi ya Upinzani au katika Vyama vya Upinzani, tunao Viongozi na Viongozi makini. Tunaye Profesa Lipumba, Maalim Seif Shariff, ambaye ni Katibu Mkuu na pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais. Sisi wengine hapa, tumeongoza Kambi katika Bunge hili kwa uadilifu mkubwa sana. Sasa kwa kauli iliyotoka jana, tulionekana kama Kambi ya Upinzani ni watu wa ovyo ovyo, wanafiki na kadhalika. Ningeomba labda ingeuka kauli ambayo ni sahihi zaidi ili ionekane kwamba, sisi ni watumishi wa watu, tumechaguliwa na watu, tumetoa maamuzi mazito sana mpaka ya kuunda Serikali ya Pamoja ya Kitaifa na tumekuwa Viongozi ndani ya Bunge lako Tukufu. Ningeomba Serikali ije na kauli sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid, ninaomba ukae. Bahati nzuri mwenyewe umeziona Kanuni na umezi-sight hapa; mojawapo ni hii ya 68(10), ambayo umeitaja pia. Inasema: "Uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote kuhusu utaratibu utakuwa ni wa mwisho." Nimeamua jana kuhusu jambo hili, uamuzi wangu ni wa mwisho, kwa hiyo, hatuwezi kuibua tena jambo lile lile.

Mheshimiwa Waziri, ninaomba tuendelee.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili

na kisha kuidhinisha Mapendekezo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uzima na afya njema, kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni katika siku ya leo. Aidha, ninapenda tuungane sote kwa pamoja, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kukutana hapa Bungeni kwa ajili ya shughuli hii muhimu ya Bunge la Bajeti kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili ni Bunge la kwanza la Bajeti tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, nami ninapenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wetu kuongoza Muhula wa Pili wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais. Pia ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais na kisha kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika na hivyo kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke katika Historia ya Bunge hili; ninampongeza sana. Ninapenda vilevile kukupongeza wewe Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Ninapenda pia niwapongeze Mawaziri wenzangu pamoja na Naibu Mawaziri wote, kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Aidha, ninaomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa na wengine kuteuliwa kuwa Wabunge. Sote tunastahili pongezi kuwa Wabunge hasa tukizingatia jinsi Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 ulivyokuwa na mchuano mkali katika hatua zote.

Matumaini yangu ni kuwa, sote kwa pamoja bila kujali itikadi zetu, tutashirikiana na kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha Ulinzi imara wa Taifa na hivyo kuweka mazingira bora na salama kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi zangu kwa Viongozi mbalimbali, ninaomba mahususi kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kwa niaba yangu mwenyewe, kutoa masikitiko yangu makubwa kuhusu tukio la ajali ya milipuko ya mabomu iliyotokea usiku wa tarehe 16 Februari, 2011 katika Kambi ya Jeshi la Wananchi ya Gongolamboto, Dar es Salaam. Ajali hiyo mbaya ilisababisha maafa makubwa, ambapo Watanzania wenzetu wapatao 30 wamepoteza maisha yao na wengine kadhaa wamejeruhiwa wakiwemo waliopoteza viungo na kupata ulemavu. Aidha, Watanzania wenzetu wengine wamepoteza mali zikiwemo nyumba za makazi na majengo ya shughuli mbalimbali. Ninachukua nafasi hii kwa mara nyingine, kutuma rambirambi zangu na kuwapa pole wahanga wote wa ajali

hiyo. Kwa Watanzania waliofariki, ninamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahala pema. (*Amina*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali na Taasisi zake vikiwemo Vyombo vya Dola, Asasi za Kiraia na Watanzania wote kwa ujumla, kwa namna walivyoshughulikia wahanga wa ajali hiyo mbaya. Kufuatia ajali hiyo, Jeshi la Wananchi liliunda Tume kuchunguza na kubaini chanzo chake, kwa lengo la kuchukua tahadhari za kudhibiti matukio kama hayo yasitokee tena katika maeneo mengine katika siku za baadae. Tume imefanya uchunguzi na kuandaa Taarifa. Kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa inayosimamia uendeshaji wa Jeshi la Wananchi, Taarifa hiyo imewasilishwa kwa Amiri Jeshi Mkuu. Hata hivyo, mapendekezo ya Tume hiyo yanayohitaji hatua za haraka, yameanza kufanyiwa kazi, ikiwemo ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhiya mabomu, milipuko na silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi, pole na rambirambi kwa wote waliohusika, ninaomba sasa kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2011/2012. Kwanza, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Makadirio haya. Kipekee, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa ushauri na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Makadirio ninayoyawasilisha leo hapa Bungeni. Wakati wote, Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, juu ya umuhimu wa kulijengea Jeshi la Wananchi uwezo wa kiutendaji ili kuimarisha Ulinzi wa Nchi yetu katika mazingira yetu ya sasa yaliyosheheni changamoto mpya za kiulinzi. Ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali inao wajibu wa kwanza kabisa wa kuhakikisha Uhuru na Usalama wa nchi unalindwa ili kuwezesha ustawi na maendeleo ya Taifa letu kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kutokana na wajibu huo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imepewa jukumu la Ulinzi wa Taifa, yaani kulinda mipaka ya Tanzania ili kuzuia tishio la aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi dhidi ya nchi yetu. Aidha, Wizara hii imepewa majukumu mengine yenye lengo la kusaidia ufanikishaji wa jukumu la Ulinzi wa Taifa yakiwemo yafuatayo:-

(a) Kudumisha amani na usalama na nchi nyingine duniani, hasa nchi majirani na nchi rafiki.

(b) Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kuzuia uporaji wa rasilimali za Taifa, kukabiliana na athari za majanga na inapobidi, kudhibiti vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani na utulivu nchini.

(c) Kuandaa Umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya adui kupitia mafunzo ya Mgambo.

- (d) Kutafiti, kuendeleza na kuzalisha teknolojia ya kijeshi.
- (e) Kuwajenga Vijana wa Kitanzania katika uzalendo, Umoja wa Kitaifa, usawa, nidhamu na ukakamavu na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo nya utekelezaji wa majukumu hayo ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (Jeshi la Wananchi), Jeshi la Kujenga Taifa na Mashirika ya Kijeshi, ambayo kwa sasa ni Mzinga na Nyumbu. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kupitia Sheria ya Ulinzi wa Taifa, inao wajibu wa kusimamia vyombo hivyo katika majukumu hayo. Aidha, kwa niaba ya Serikali, Wizara yangu inao wajibu wa kuhakikisha vyombo hivyo vinawezeshwa katika kutekeleza majukumu hayo kwa kuandaa Mipango na Bajeti ya mahitaji muhimu yafuatayo:-

- (a) Ajira ya wanajeshi wa kutosha, wanaofunzwa, kupatiwa mazoezi na kuendelezwa ipasavyo.
- (b) Mahitaji kwa ajili ya utendaji kijeshi ikiwemo zana na vifaa, matunzo na hifadhi zake.
- (c) Mahitaji kwa ajili ya utafiti, uendelezaji na uzalishaji wa teknolojia ya kijeshi.
- (d) Mahitaji kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu, utoaji wa stahili na huduma muhimu kwa ajili ya wanajeshi.
- (e) Mahitaji kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa.
- (f) Ujenzi wa makazi yaliyo nadhifu na salama na uwekaji wa mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba, jukumu kuu la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kulinda Uhuru na Usalama wa nchi yetu, ninaomba sasa nieleze hali ya Usalama wa mipaka yetu ilivyokuwa katika mwaka 2010/2011, ambayo kimsingi ndiyo inayotoa taswira ya hali ya Usalama wa nchi yetu katika mwaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, kwa ujumla, hali ya Usalama wa mipaka yetu na nchi jirani ilikuwa shwari. Jeshi la Wananchi lililinda ipasavyo mipaka yote ya Tanzania na kuhakikisha Uhuru na Usalama wa nchi yetu. Katika kipindi hicho, hapakuwepo tishio lolote kubwa la kuhatarisha Uhuru na Usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, mwanzoni mwa mwaka 2011 kulikuwepo na matukio kadhaa ya uharamia katika eneo la maji ya Tanzania katika Bahari ya Hindi na kubomolewa kwa

baadhi ya alama za mipaka (*beacons*) katika eneo la mpaka wa Kaskazini mwa nchi yetu. Hali ya Usalama katika mipaka yetu ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpaka wa Bahari ya Hindi vitendo vya kiharamia na utekaji nyara meli vimeendelea kujitokeza. Hata hivyo, katika mwaka huu matukio ya vitendo hivyo yamekuwa yakipungua kutokana na kuwepo udhibiti wa eneo hilo unaofanywa na Jeshi la Wananchi na majeshi ya nchi za kigeni, hususan nchi za Ulaya, Asia na Marekani yaliyoko katika eneo la Ghuba ya Aden. Katika kipindi hiki hadi kufikia Mei, 2011 kumekuwa na matukio kumi na nne (14) ya vitendo vya kiharamia katika eneo letu la Bahari ya Hindi. Katika matukio hayo maharamia wameteka meli zipatazo nne (4) na pia wamejaribu kuziteka meli kumi (10) bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya kiharamia kwenye eneo letu la bahari vimeleta madhara mengi dhidi ya meli zinazoingia na kutoka katika bandari zetu. Mionganoni mwa madhara hayo ni baadhi ya wamiliki wa meli kusitisha utiaji nanga katika bandari zetu na wengine wanalazimika kutumia njia ndefu ili kukwepa vitendo vya uharamia. Aidha, baadhi ya wamiliki wanaomba ulinzi wa Jeshi letu wanapopita katika maji ya Tanzania kwenye Bahari ya Hindi. Pia wamiliki wengine wa meli wanalazimika kutumia makampuni binafsi ya Ulinzi ili kuimarisha usalama wa meli na bidhaa zao. Matokeo ya yote haya ni kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na za bima kwa bidhaa zinazoingizwa na kutolewa kuititia katika bandari za Tanzania. Vilevile makampuni yanayofanya utafiti wa mafuta na gesi asilia katika Ukanda wa Pwani yetu yamelazimika kuomba msaada wa ulinzi kutoka kwa Jeshi letu. Kwa ujumla wadau wa meli za usafirishaji baharini wanalionna eneo letu la bahari kuwa la hatari kwa shughuli zao mbalimbali, jambo linaloathiri Taifa letu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na hali hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa Jeshi letu kiutendaji ili kuweza kudhibiti ipasavyo ulinzi wa eneo letu la bahari na kupambana na maharamia hao pale wanapofanya majoribio hayo. Aidha, kwa kuzingatia kwamba, uharamia ni tishio linalogusa nchi nyingi duniani, Serikali kuititia ngazi mbalimbali, imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama katika eneo la mpaka huu ni shwari. Hata hivyo, kumekuwepo na tatizo la ung'oaji wa alama za mpaka unaofanywa na watu wanaoishi mpakani kwa lengo la kujipatia ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali zikiwemo kilimo, malisho ya mifugo na ujenzi wa makazi. Tatizo hili ni kubwa zaidi katika Wilaya za Tarime na Ranya ambako alama za mpaka zipatazo 19 zimeharibiwa. Mamlaka husika za Serikali zinashughulikia tatizo hili. Hata hivyo, ninawasihi Wananchi hasa wale waishio katika maeneo ya mipaka, kuheshimu na kutunza alama hizo, kwani ni muhimu sana kwa uhai na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali katika mpaka wetu wa Magharibi ni shwari. Hata hivyo, kumekuwepo matukio kadhaa ya ujambazi wa kutumia silaha katika baadhi ya maeneo na yanaaminika kufanywa na raia kutoka nchi jirani wakishirikiana na raia

wenzetu wasio waaminifu. Aidha, kumekuwepo matukio machache ya kijambazi ambapo majambazi kutoka nchi jirani hunyang'anya Wananchi wetu mitumbwi na nyavu zao za uvuvi. Jeshi la Wananchi kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Dola, limeendelea kufanya doria mara kwa mara ndani ya Ziwa Tanganyika ili kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari ingawa tatizo la mpaka katika Ziwa Nyasa halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, NIInapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Wananchi kwa ujumla kwamba, Jeshi letu la Wananchi ni imara na lina uwezo wa kukabili tishio lolote dhidi ya Uhuru na Usalama wa nchi yetu. Wanajeshi wetu ni jasiri, mahodari na wazalendo. Wakati wote wako tayari kulinda mipaka ya nchi yetu, Uhuru na Usalama wa Taifa letu na heshima ya Wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge, bajeti yenyeye jumla ya Shilingi 626,946,612,766.00; ambazo kati yake Shilingi 626,848,617,251.00 ni fedha za Ndani na Shilingi 97,995,515.00 ni fedha za Nje. Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa kuzingatia Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mafungu matatu ya Wizara umeoneshwa katika Jedwali lifuatalo hapa chini:-

Ufuatao ni Mchanganuo wa Bajeti Iliyoidhinishiwa na Bunge kwa Ajili ya Mafungu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Fungu 38 - NGOME; matumizi ya kawaida shilingi 358,214,108,000.00, matumizi ya maendeleo shilingi 18,454,334,000.00, jumla shilingi 376,668,442,000.00. Fungu 39 - JKT; matumizi ya kawaida shilingi 93,922,892,251.00, matumizi ya maendeleo shilingi 12,649,883,000.00, jumla shilingi 106,572,775,251.00. Fungu 57 - Wizara; matumizi ya kawaida shilingi 14,589,633,000.00, matumizi ya maendeleo shilingi 129,115,762,515.00\*, jumla shilingi 143,705,395,515.00. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha matumizi ya kawaida shilingi 466,726,633,251.00; matumizi ya maendeleo shilingi 160,219,979,515.00; na jumla kuu ni shilingi 626,946,612,766.00.

\*Kati ya fedha hizo Shilingi 97,995,515.00 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mpango wa Wizara kwa mwaka 2010/2011 kulingana na bajeti hiyo, yalizingatia shughuli zifuatazo, ambazo kwa ujumla wake zililenga kuimarisha uwezo wa kutekeleza jukumu la Ulinzi wa Taifa:-

(a) Matumizi ya Kawaida:

(i) Kuajiri wanajeshi wapya, kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi, ikiwemo kushiriki katika mazoezi ya pamoja na majeshi ya nchi nyingine.

(ii) Kuendeleza mafunzo ya Ulinzi wa Umma (Mgambo).

- (iii) Kuendesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa kujitolea.
  - (iv) Kugharamia mahitaji muhimu ya umeme, maji, simu, mafuta na vilainisho kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya kimsingi ikiwemo operesheni za kiulinzi na mafunzo.
  - (v) Kutengeneza na kukarabati magari, vifaa, mitambo na zana.
  - (vi) Kutoa huduma muhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT ikiwemo chakula, tiba, sare na usafiri.
  - (vii) Kulipa stahili mbalimbali za wanajeshi, vijana wa JKT na Watumishi wa Umma ikiwemo mishahara, posho za kisheria na likizo.
  - (viii) Kuendeleza shughuli za ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na kiulinzi kupitia ushirikiano baina ya nchi na nchi, ushirikiano wa kikanda na kimataifa.
- (b) Matumizi ya Maendeleo:
- (i) Kuimarisha uwezo wa Jeshi la Wananchi kizana na kivifaa.
  - (ii) Kuboresha shughuli za utafiti, uendelezaji na uzalishaji wa teknolojia ya kijeshi katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu.
  - (iii) Kuboresha Mtandao wa Mawasiliano ya Pekee Jeshini, kupima maeneo ya jeshi na kulipa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi na kurejesha mkopo wa *NSSF* uliotumika katika ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi.
  - (iv) Kukarabati na kukamilisha Miradi ya Ujenzi katika makambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.
  - (v) Kuboresha mazingira ya makazi kwa ujenzi mpya wa majengo na miundombinu pamoja na kukarabati na kumalizia miradi ya ujenzi katika Makambi mbalimbali ya JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2011, fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ni jumla ya Shilingi 598,099,152,773.00, sawa na asilimia 95.40 ya Shilingi 626,946,612,766.00 zilizoidhinishwa na Bunge. Fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya shughuli za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 501,218,237,120.00, sawa na asilimia 107.39 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli hizo. Fedha zilizotolewa zilizidi fedha zilizoidhinishwa kutokana na Mafungu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupatiwa na kuhamishiwa fedha za ziada kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa

majukumu maalum. Aidha, fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya shughuli za Matumizi ya Maendeleo ni Shilingi 96,880,915,653.00, sawa na asilimia 60.47 ya Shilingi 160,219,979,515.00 zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya utolewaji wa fedha iliyoelezwa hapo juu imetoa taswira ya hali ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2010/2011. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, zimetumika katika shughuli zilizopangwa. Hata hivyo, kwa vile katika baadhi ya miezi, fedha hizo zimetolewa pungufu ya mahitaji halisi, utoaji wa baadhi ya stahili na huduma kwa wanajeshi, vijana wa JKT na Watumishi wa Umma ulikuwa chini ya viwango vinavyostahili.

Vile vile, kutokana na fedha zilizotolewa kuwa chini ya mahitaji halisi, ugharimiaji wa mahitaji muhimu kama vile mafuta na vilainisho, umeme, simu na maji kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya kimsingi ulikuwa mgumu, hali iliyosababisha kujengeka kwa mazingira ya kulimbikiza madeni mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa zimetumika katika mradi wa kuimarisha Jeshi la Wananchi kizana na kivifaa. Sehemu nyingine ya fedha zimetumika katika kutekeleza miradi ya uboreshaji wa kiwanda cha Shirika la Mzinga, uboreshaji wa utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi katika Shirika la Nyumbu na kuboresha Mtandao wa Mawasiliano ya Pekee Jeshini. Aidha, kutokana na uchache wa fedha zilizotolewa, shughuli nyingine za maendeleo zilizopangwa hazikukamilika na nyingine hazikutekelezwa kabisa na hivyo kuathiri malipo ya mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu hali ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara wa Mwaka 2010/2011, ninaomba sasa kutoa hali halisi ya utekelezaji ilivyokuwa katika kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shughuli za Utendaji Kijeshi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo na mazoezi kwa wanajeshi kuhusu mbinu za kimapigano ndiyo uhai wa jeshi. Hili ndilo jukumu kuu la kimsingi la Jeshi la Wananchi katika wakati wa amani ili kuwaweka wanajeshi wetu tayari kivita. Kwa hiyo, katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Wananchi limetoa mafunzo kwa wanajeshi ndani na nje ya nchi ili kuboresha taaluma zao. Vyuo vya ndani ya nchi vya fani mbalimbali vilitoa mafunzo kwa wanajeshi kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha, vyuo vya nchi za nje hususan Afrika ya Kusini, Bangladeshi, China, India, Kanada, Marekani, Uingereza, Ujeruman, Zambia, Zimbabwe na nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki za Kenya, Rwanda na Uganda, zimeshiriki kufundisha maafisa na askari katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, mazoezi ya kijeshi katika ngazi ya vikosi yalifanyika kama yalivyopangwa. Mazoezi mengine yaliyofanyika yalilenga kutayarisha vikundi vya Jeshi la Wananchi katika jukumu la Ulinzi wa Amani. Aidha, katika mwaka huo, Jeshi la Wananchi limeendelea kuijandaa kushiriki katika mazoezi ya kijeshi ya ndani na mazoezi ya pamoa na majeshi ya nchi nyingine, hususan

nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mazoezi hayo yatafanyika katika mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

(i) Zoezi *Natural Fire -11* litakaloshirikisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani litafanyika Zanzibar kuanzia tarehe 11 hadi 21 Septemba, 2011.

(ii) Zoezi Ushirikiano Imara litakaloshirikisha Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki litafanyika Nchini Rwanda kuanzia tarehe 17 hadi 28 Oktoba, 2011.

(iii) Zoezi Pomboo (*Exercise Dolphin*) linatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2011 huko Bagamoyo, Tanga, Unguja, Pemba na Mafia. Zoezi hili halitashirikisha majeshi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo juhudhi za kuajiri askari wapya zimekuwa zikiendelea kulingana na uwezo kifedha ili kujaza Ikama na kuziba pengo la maafisa na askari wanaostaafu Jeshi, kuacha kazi kwa sababu mbalimbali pamoja na vifo. Aidha, ili Jeshi liwe na askari wenye nidhamu na walioandaliwa vizuri, askari wapya wanaoandikishwa jeshini ni wale waliopitia JKT ambako hupata maandalizi mazuri ya awali na baadaye kupatiwa mafunzo ya ziada kwenye shule za mafunzo ya awali (*Recruit Training Schools - RTS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera yetu ya Ulinzi wa Taifa inatambua kuwa, Mgambo (*Volunteer Reserves*), ndiyo nguvu kuu ya Jeshi la Akiba la Jeshi la Wananchi wakati linapohitajika. Nguvu hii inaundwa na Watanzania waliopatiwa mafunzo ya mgambo. Aidha, nguvu nyingine ya Jeshi la Akiba inatokana na wanajeshi wastaafu (*Regular Reserve*). Hivyo, katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Wananchi limeendelea kuendesha mafunzo ya Mgambo ya awali ya kujikumbusha (*refresher*) na Uongozi Mdogo kwa Watanzania. Katika mwaka huo, jumla ya wanamgambo 15,485 walihitimu mafunzo ya awali katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara na wanamgambo 79 walifundishwa na kufaulu kozi ya Uongozi Mdogo. Aidha, katika mwaka huo, Zoezi la pamoja la Vikosi vya Mgambo vya Mkoa wa Kigoma (*Exercise Ujasiri 2010*), lilifanyika kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira tuliyomo changamoto mbalimbali za kiulinzi zinazoweza kuathiri Uhuru na Usalama wa nchi yetu zimekuwa zikiongezeka. Kwa hiyo, sanjari na kutoa mafunzo na mazoezi ya kimapiganu kwa wanajeshi wetu, Serikali inatekeleza mipango ya kuimarisha uwezo wa Jeshi letu kizana na kivifa ili kuliweka tayari kivita kukabiliana na changamoto hizo. Hivyo, katika mwaka 2010/2011, Serikali imelipatia Jeshi la Wananchi baadhi ya vifaa na zana muhimu za kivita. Pia, Jeshi limepokea zana na vifaa mbalimbali kutoka Serikali za Nchi rafiki kutokana na ushirikiano wetu mzuri na nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jukumu lake kuu la kulinda mipaka ya nchi yetu, pia Jeshi la Wananchi limeendelea kutekeleza wajibu wake mwingine wa kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na athari za majanga yanayotokea hapa nchini. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Wananchi, kwa kutumia wahandisi medani wake na

kwa msaada wa fedha toka Ofisi ya Waziri Mkuu, limeendela kujenga tuta la kuzuia mafuriko katika eneo la Kilosa Mjini. Jukumu hilo limekuwa likitekelezwa kufuatia mafuriko yaliyoikumba Wilaya ya Kilosa katika mwaka 2010. Ninapenda kuchukua nafasi hii, kulipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri linayoendelea kuifanya kusaidia Mamlaka za Kiraia na Wananchi kwa ujumla katika kukabiliana na athari za majanga yanayotokea hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, stahili ya mishahara kwa wanajeshi na watumishi wa umma, imeendelea kulipwa kwa ukamilifu na kwa wakati kama ilivyokuwa imepangwa. Hata hivyo, stahili nyingine ikiwemo likizo, usafiri kikazi na uhamisho zimetolewa kwa kuzingatia hali halisi ya bajeti. Aidha, kwa kuwa katika baadhi ya miezi fedha zilizotolewa zilikuwa pungufu ya mahitaji halisi, stahili hizi zilitolewa chini ya viwango vinavyostahili na vilivyopangwa kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho zinazoambatana na mishahara ikiwemo posho ya ujuzi na madaraka kwa maafisa na askari ni kwamba, kuanzia mwaka 2010/2011, posho ambazo zilikuwa hazitolewi huko nyuma zimeanza kulipwa na zile zilizokuwa zinalipwa nazo zimeongezwa viwango ikilinganishwa na viwango vya mwaka 1994 vilivyokuwa vinatumika. Aidha, posho ya pango la nyumba kwa wanajeshi wanaopanga nje ya makambi zimeboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, huduma muhimu ya chakula kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutolewa kulingana na uwezo kibajeti. Hata hivyo, kwa kuzingatia hali ya bei halisi ya vyakula katika soko, Serikali inaangalia uwezekano wa kuboresha bajeti kwa ajili ya huduma hii ili kukidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma ya tiba kwa wanajeshi, Jeshi la Wananchi katika mwaka 2010/2011, limeendelea kuimarisha Hospitali zake za Kanda katika maeneo ya Bububu, Kibaha, Mwanza na Tabora, kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kisasa. Aidha, Jeshi limeendelea na ujenzi wa Kituo cha Tiba katika Kambi ya Ally Khamis eneo la Vitongoji Pemba kwa msaada wa Serikali ya Marekani. Pia Jeshi la Wananchi linawasomesha wanajeshi na watumishi wa umma wanaofikia 93 katika kada ya afya kwenye vyuo vya ndani na nje ya nchi. Jeshi la Wananchi linatarajia kujenga Hospitali ya Kanda huko Songea Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la huduma ya tiba, ninafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Jeshi la Wananchi limepokea msaada toka Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumanî wa magari 30 ya wagonjwa (*ambulance*) za kisasa na *Mobile Field Hospital* mbili na kuunda Kombania ya Tiba ya kuhudumia dharura (*Mobile Medical Care Unit*). Ninapenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumanî kwa misaada hiyo na mingine minge ambayo imekuwa ikilipatia Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya usafiri kwa wanajeshi na watumishi wa umma imeendelea kutolewa kwa kutumia magari yaliyopo. Hata hivyo, huduma hii inaathiriwa na hali ya kupanda mara kwa mara kwa bei za mafuta na vilainisho. Kuhusu

usafiri binafsi wa maafisa na askari, baadhi ya makampuni hapa nchini yameonesha nia ya kutaka kukopesha wanajeshi vyombo vya usafiri kwa udhamini wa Serikali. Serikali inafanya kazi mapendekezo hayo. Kwa wanajeshi wenyewe vyombo binafsi na wale waliodhaminiwa kuendesha vyombo vya jeshi, tahadhari imeendelea kutolewa kuzingatia sheria na taratibu katika matumizi ya vyombo hivyo ili kuepuka ajali na madhara mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 gharama za uendeshaji wa mitambo, zana na majukumu ya kimsingi ya mafunzo na operesheni za kiulinzi ziliongezeka sana kutokana na bei ya mafuta kupanda mara kwa mara. Aidha, kwa baadhi ya majukumu hayo, ununuzi wa mafuta uliongezeka kutokana na tatizo la upungufu wa umeme. Ili kuweza kukidhi mahitaji hayo, ililazimu fedha za shughuli nyingine zitumike kugharamia nishati ya mafuta, hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu mengine yaliyopangwa. Aidha, huduma ya maji imeendelea kupatikana na Ankara za maji zimeendelea kulipwa kulingana na uwezo wa bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kiulinzi na kijeshi ni suala linalopewa umuhimu mkubwa ili kusaidia kufikiwa kwa lengo kuu la Serikali yetu la kudumisha usalama na amani duniani. Kwa msingi huo katika mwaka 2010/2011, Serikali imeendeleza na kudumisha ushirikiano katika nyanja ya kijeshi baina ya Tanzania na Nchi ya China, India, Kanada, Jordan, Marekani, Ufaransa, Uingereza, Ujeruman, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki. Aidha, kupitia ushirikiano huo, Tanzania imeendelea kupata misaada mbalimbali ya kuendeleza Jeshi letu ikiwemo nafasi za kozi za ujuzi, Ulinzi wa Amani, mafunzo na mazoezi ya kijeshi kwa maafisa na askari wetu. Aidha, kupitia ushirikiano huo, katika mwaka 2010/2011, Jamhuri ya Watu wa China imetoa msaada wa ujenzi wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (*National Defence College*) Kunduchi, Dar es Salaam na Umoja wa Falme za Kiarabu umeendelea kutoa msaada katika ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (*Command and Staff College*) huko Tengeru, Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ushirikiano kama huo, Nchi ya Marekani imeendelea kutoa nafasi za kozi mbalimbali za kijeshi kwa maafisa na askari wetu. Aidha, imetoa mafunzo kwa Jeshi la Wananchi kwa ajili ya kushiriki kwenye operesheni za kulinda Amani katika Nchi ya Lebanon na Sudan katika Jimbo la Darfur kupitia mpango wa *African Contingent Operation Training Assistance (ACOTA)*. Pia imetoa msaada wa boti mbili za kisasa kwa ajili ya doria katika Mwambao wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Kikanda (*Regional Cooperation*): Ustawi na maendeleo ya Taifa letu yapo salama na yataendelea kuwa salama ikiwa amani na utulivu utakuwepo baina ya nchi yetu na nchi majirani na pia ndani ya nchi hizo. Kwa kuzingatia umuhimu huo, katika mwaka 2010/2011, Serikali imeendelea kuimarisha ushiriki wetu katika ushirikiano wa Kikanda kiulinzi na kijeshi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*). Kupitia ushirikiano katika jumuiya hizo, Jeshi la Wananchi limeshirikiana na majeshi ya nchi hizo katika masuala ya mafunzo na mazoezi ya pamoja ya kijeshi kama nilivyokwishaeleza hapo awali. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na nchi nyingine za

SADC imeendeleza juhudi za uanzishwaji na uendelezaji wa Jeshi la Dharura la SADC (*SADC Standby Force*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Kimataifa (*Multilateral Cooperation*): Katika kuimarisha ushirikiano wa kijeshi kimataifa, Jeshi la Wananchi limeendelea kushiriki katika Operesheni mbalimbali za kulinda Amani duniani zinazoongozwa na Umoja wa Mataifa. Kwa ujumla Jeshi la Wananchi limepeleka walini na waangalizi wa Amani katika misheni (*missions*) tano za kulinda Amani kati ya misheni 15 zinazoongozwa na Umoja wa Mataifa. Nchi ambazo Jeshi la Wananchi limepeleka walini na waangalizi wa Amani ni Darfur huko Sudan, Lebanon, DRC, Ivory Coast na Sudan Kusini. Ushiriki wetu umeifanya Tanzania kushika nafasi ya 20 kwa kutoa askari wengi kwa ajili ya majukumu ya Ulinzi wa Amani Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, umoja wa kitaifa miongoni mwa wananchi wetu ni nguzo muhimu ya Ulinzi wa Taifa letu. Hata hivyo, hivi sasa Taifa letu linakabiliana na changamoto zinazotokana na athari za Utandawazi ambazo kwa kiasi kikubwa zinahatarisha umoja huo. Taifa lisilo na umoja ni dhaifu na linaweka rehani uhuru na usalama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa suala hili, Serikali imendeleza azma ya kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, umoja wa kitaifa, usawa, nidhamu, ukakamavu na ujasiri kwa kuwapatia mafunzo ya JKT. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo kifedha, azma hiyo kwa sasa inatekelezwa kwa kutoa mafunzo hayo kwa vijana wa kujitolea pekee kutoka mikoa yote ya nchi. Hivyo, katika mwaka 2010/2011, vijana 4,752 (4,252 toka Tanzania Bara na 500 toka Zanzibar) wa Operesheni Uzalendo; kati yao wavulana 3,655 na wasichana 1,097, wamehitimu mafunzo ya awali ya JKT. Mafunzo hayo yaliendeshwa katika makambi 6 ya Bulombora, Mafinga, Mgambo, Mlale, Oljoro na Ruvu. Baada ya kuhitimu mafunzo hayo vijana hao wameendelea na mafunzo ya stadi za kazi na uzalishaji mali katika makambi ya Chita, Kanembwa, Makutopora, Maramba, Mbweni, Mgulani, Msange na Rwamkoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, vijana 4,667 (wavulana 3,591 na wasichana 1,076) wa Operesheni Kilimo Kwanza waliojiunga na mafunzo ya JKT mwezi Julai, 2009 walikuwa wanaendelea na awamu ya pili ya mafunzo hayo. Kati ya vijana hao; 1,947 walipata ajira katika taasisi zifuatazo: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vijana 1,050 (wavulana 821 na wasichana 229), Polisi 607 (wavulana 436 na wasichana 171), Ofisi ya Rais 237 (wavulana 211 na wasichana 26), TANAPA 15 (wavulana 12 na wasichana 3), *Barrick Gold Mine* (wavulana 26) na *Tanzam Gold Mine* (wavulana 12). Vijana 2,720 waliobaki waliendelea na mafunzo katika fani za kilimo na ufugaji, useremala, uungaji vyuma, ufundu magari, ufundu umeme na ufundu uashi na kuhitimu mafunzo yao mwezi Juni, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mafunzo ya JKT kwa vijana, wakufunzi wa vijana wameendeleza kimafunzo kwa kuhudhuria kozi za kijeshi za uongozi na ujuzi ikiwemo kozi elekezi kwa wakufunzi 78, kozi ya ukufunzi na uongozi kwa wakufunzi 358 na kozi ya mama mlezi (*matron*) kwa wakufunzi 154.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia utekelezaji wa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza Jeshi la Kujenga, Taifa katika mwaka 2010/2011, limelima ekari 1,625 za kilimo cha mbegu bora kwa matarajio ya kuvuna tani 1,039 za mbegu mbalimbali. Mbegu zitakazovunwa zitauzwa kwa Wakala wa Mbegu (*Agricultural Seed Agency - ASA*) na kampuni binafsi ya *Southern Highlands Seeds Growers* ambao wana mkataba na JKT katika uzalishaji mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji unaendelea katika eneo la ekari 1,000 za zao la mpunga katika Kikosi cha Chita, Wilaya ya Kilombero, kwa kutumia wahandisi wa Wizara. Vilevile matrekta 30 yakiwa na viambato vyake (haro, plau, trela, pampu za umwagiliaji na zana za kupandia), yamenunuliwa na kusambazwa katika vikosi mbalimbali vya JKT kwa ajili ya kuongeza uzalishaji. Aidha, katika kuweka msukumo zaidi wa utekelezaji wa kaulimbiu ya ‘Kilimo Kwanza’, wataalam tisa wako masomoni kuongeza ujuzi katika fani za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azma ya kuendeleza shughuli za viwanda, utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi katika mwaka 2010/2011, Wizara kuitia mashirika yake ya kijeshi imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Mzinga, limeendelea na utekelezaji wa mradi wa kukarabati na kuboresha kiwanda chake cha uzalishaji wa bidhaa za kijeshi. Awamu ya kwanza ya ukarabati imekamilika kwa asilimia 92 na kazi ya usimikaji wa mitambo mipyä unaofanywa kwa kushirikiana na wataalam toka China upo katika hatua za mwisho. Majaribio ya mitambo mipyä iliyosimikwa yanatarajiwa kufanyika hivi karibuni na uzalishaji rasmi uthaanza baada ya kupata fedha za kununulia malighafi. Sanjari na hatua hizo, wataalam toka China wanaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi walioajiriwa hivi karibuni kwa ajili ya kuendesha mitambo hiyo. Aidha, katika juhudhi za kupanua wigo wa mapato, Shirika limeanzisha na kuandikisha kampuni Tanzu ya *Mzinga Holdings Ltd* ambayo kwa mwaka 2011/2012, itaanza na shughuli za ujenzi na ugavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Shirika la Mzinga, kwa niaba ya Jeshi la Wananchi limeendelea kufanya utafiti zana na vifaa vya zamani vilivyopo jeshini ili kuvifanya ukarabati kwa lengo la kuviongezea uwezo wa kutumika katika mazingira ya sasa ya kiulinzi. Kwa kuzingatia kwamba, uwezo wa kununua zana na vifaa vipyä ni mdogo, Serikali itaendelea kuliwezesha Shirika hili kuendeleza utafiti na ubunifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumbu, limetekleza shughuli mbalimbali ikiwemo kukarabati na kununua mitambo ya karakana, kukarabati majengo na miundombinu ya kituo, kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi. Lengo kuu la shughuli hizo ni kulijengea uwezo Shirika ili liwe kituo kinachoongoza cha Utafiti wa Teknolojia za Kijeshi katika Kanda ya Afrika Mashariki (*East Africa Military Technological Research Centre of Excellence*). Malengo mengine

ni kujenga uwezo wa kusanifu teknolojia ya zana za kilimo ili kuchangia katika ufanikishaji wa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, kuimarisha uwezo wa kituo katika uzalishaji wa vipuri na bidhaa nyingine na kufanya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha uhakiki wa ubora wa magari na mitambo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT), iliendelea kutekeleza mradi wa uunganishaji na uuzaji wa matrekta 1,860 yaliyopatikana kwa mkopo kutoka Serikali ya India. Hadi tarehe 3 Julai, 2011 jumla ya matrekta 1,224 yameunganishwa na tayari matrekta 74 yameshauzwa kwa wateja mbalimbali vikiwemo Vikosi vya JKT vilivyouziwa matrekta 30. Aidha, matrekta 501 yamepelekwa katika Kituo cha Kanda ya Kati, Dodoma kwa ajili ya usambazaji katika mikoa jirani. Vituo vingine vya Them - Arusha na Nyegezi - Mwanza vimeshafunguliwa na taratibu za kuvipelekea matrekta hayo zinakamilishwa. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, ninatoa rai kwenu kusaidia kuwalishwa Wananchi wa majimbo yenu kuhusu upatikanaji wa matrekta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, SUMAJKT imeendelea kupata na kutekeleza kandarasi za ujenzi wa majengo kutoka Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Serikali pamoja na Makampuni binafsi. Katika mwaka 2010/2011, SUMAJKT ilipata kandarasi zenye thamani ya Shilingi 43,792,060,414.00 ambazo zinaendelea kutekelezwa. Aidha, kiwanda cha kutengeneza samani cha shirika hilo kilichoko Chang'ombe, Dar es Salaam, kimeendelea kuzalisha samani mbalimbali na kuuza. Pia kiwanda hiki kimeendelea kuwa darasa la elimu ya ufundi wa useremala kwa vijana wa JKT. Vilevile, Kampuni ya Ulinzi ya *SUMAGUARD Co. LTD* ilianzishwa tarehe 1 Februari, 2010 kwa lengo la kufanya kazi za Ulinzi binafsi. Mpaka sasa Kampuni ya *SUMAGUARD* imeajiri vijana zaidi ya 300 waliopitia JKT na inaendelea kupata mikataba mbalimbali ya Ulinzi katika Asasi za Serikali, Asasi Binafsi na Watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalo jukumu la kuhakikisha mazingira bora, nadhifu na yaliyo salama ya makazi katika makambi kwa ajili ya wanajeshi na vijana wa JKT. Hata hivyo, jukumu hili lenye mahitaji makubwa ya fedha, utekelezaji wake unakwamishwa na uwezo mdogo wa Serikali kifedha. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka 2010/2011, shughuli zilizofanyika ni ukamilishaji wa miundombinu katika Chuo cha Ulinzi wa Taifa (*National Defence College*) kilichoko Kunduchi, Dar es Salaam na ukarabati wa nyumba moja ya makazi iliyoko Capri Point, Mwanza. Aidha, katika kuendeleza maandalizi ya kurejesha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, Jeshi la Kujenga Taifa limetekeleza miradi ya ujenzi mpya, ukamilishaji na ukarabati wa majengo katika Makambi ya Bulombora, Makutopora, Maramba, Mbweni, Mgumbo, Mgulani, Mlale, Mlalakuwa, Nachingwea, Ruvu na Rwamkoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisheseleza uwezo wa Serikali kifedha kugharamia upatikanaji wa nyumba kwa ajili ya makazi ya wanajeshi na vijana wa JKT katika makambi kwa sasa ni mdogo. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa Jeshi linakabiliwa na uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi, jambo linalofanya wanajeshi wengi kuishi nje ya makambi. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imefanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kupata mkopo nafuu wa ujenzi wa nyumba za makazi

katika makambi. Ninafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imeridhia kutoa mkopo wenyewe thamani ya Dola za Kimarekani 300, 000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 10,000. Serikali hivi sasa inakamilisha taratibu za upatikanaji wa mkopo huo kuititia Benki ya Exim ya China ili ujenzi wa nyumba uweze kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha Mtandao wa Mawasiliano ya Pekee (*Independent Telecommunication Network - ITN*) ili kuimarisha mawasiliano ndani ya Jeshi la Wananchi. Awamu ya kwanza ya mradi huo ya ukarabati wa miundombinu ili kufufua mfumo wa mawasiliano kwa mwaka 2010/2011, imefanyika katika vikosi vilivyoko katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Morogoro. Lengo la awamu hii ni kuvipatia vikosi mawasiliano ya ndani kwa ndani ya kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuititia Kamati za Mazingira za Taasisi zetu, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira. Katika mwaka 2010/2011, elimu ya uhifadhi wa mazingira imeendelea kutolewa kwa maafisa na askari, vijana wa JKT, Watumishi wa Umma na Wananchi wanaoishi jirani na makambi. Pia mpango wa kudumu wa kupanda miti katika makambi ili kutunza na kuboresha mazingira umeendelea kutekelezwa. Aidha, katika maeneo ya Jeshi, uhifadhi wa misitu unafanyika kwa kuzuia ukataji miti ovyo, uchomaji moto misitu na kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji kwa kufanya doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI yameendelea katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Taasisi zake. Kampeni dhidi ya ugonjwa huu zimeendelea kufanyika katika Vikosi na Kamandi zote za Jeshi la Wananchi kwa kutoa elimu juu ya ugonjwa huo, maambukizi na hatua zote za tahadhari za kujikinga nao. Mkakati wa kampeni hiyo ni pamoja na:-

- (a) Upimaji wa hiari kwa maafisa, askari, vijana wa JKT, watumishi wa umma pamoja na familia za wanajeshi.
- (b) Utoaji wa elimu ya kinga dhidi ya UKIMWI.
- (c) Kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na kufanya suala la UKIMWI kuwa ajenda ya kudumu katika Vikao na Mikutano yote inayofanyika.
- (d) Kamati mbalimbali za ushauri zimeendelea kutekeleza majukumu ya kutoa elimu hiyo.
- (e) Waathirika kupata dawa za kurefusha maisha (*ARV's*) ambazo hutolewa bure kuititia vituo vya *Care and Treatment Centres*, vilivyoko katika Hospitali Kuu za Kanda za Mbeya, Mwanza, Bububu (Zanzibar), Mazao (Morogoro), TMA (Arusha), Mirambo (Tabora), Luhwiko (Ruvuma) na Nyumbu (Pwani). Pia vituo vyote hivyo hutoa huduma kwa wanajamii wanaoishi maeneo ya karibu. Aidha, Watumishi wa Umma

wanaotumia dawa za kurefusha maisha (*ARV's*), wameendelea kupata msaada wa lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kusimamia matumizi bora ya rasilimali za Umma zikiwemo fedha zilizotengwa na Serikali kufanikisha majukumu mbalimbali yaliyopangwa sambamba na usimamizi wa kanuni na taratibu zilizopo. Kwa kudhihirisha umakini katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma katika mwaka 2010/2011, Wizara imepata Hati Safi kutoka kwa Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mahesabu ya Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Ninafurahi kueleza kwamba, huu ni mwaka wa tatu mfululizo Wizara hii inaendelea kupata Hati Safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza dhana ya Utawala Bora na Ushirikishwaji, katika mwaka 2010/2011 Wizara iliveza kuendesha mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi na kuwezesha wafanyakazi wake kushiriki kwenye mashindano ya Mei Mosi, ambapo Timu ya Mpira wa Miguu ilitwaa Kombe. Wizara pia ilishiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2010 huko Mwanza na kupata ushindi wa Pili wa Banda Bora (*Best Pavillion Award*) na mwaka 2011 huko Dar es Salaam na kupata ushindi wa Nne wa Banda Bora pia. Ninapenda kutumia fursa hii, kuwashukuru Wananchi wote walitembelea Mabanda ya Wizara hii na kutoa maoni yao ambayo yamezingatiwa. Aidha, kwa mara nyingine ninaendelea kuwaalika Wananchi kujitokeza kwa wingi kutembelea mabanda yetu kila maonesho ya namna hii yanapofanyika yakiwemo ya Miaka 50 ya Uhuru yatakayofanyika mwezi Desemba, 2011, ili kuona na kupata maelezo kuhusu shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuptitia Kamati za Maadili sehemu za kazi ambazo hufuatilia uadilifu wa maafisa, askari na watumishi wa umma katika maeneo yao ya kazi. Kamati hizi huwakumbusha na kuwasisitiza wafanyakazi kuzingatia taratibu, kanuni na sheria zilizopo. Wizara imekuwa ikiwadhibiti na kuwaadhibu maafisa, askari na watumishi wa umma wasiozingatia kanuni, taratibu na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kutokukidhi kwa ukamilifu mahitaji ya mipango yake ya kila mwaka ya kuendeleza Jeshi letu. Mahitaji ya mipango hiyo, kama ilivyo kwa mipango ya majeshi mengine duniani, ni makubwa ikilinganishwa na uwezo mdogo wa Serikali. Athari ya hali hii ni kuwepo upungufu wa mahitaji muhimu ya kiulinzi ikiwemo zana na vifaa vyta kijeshi, utoaji wa huduma na stahili kwa wanajeshi chini ya viwango vinavyostahili na kushindwa kugharimia kwa ukamilifu na kwa wakati, mahitaji muhimu ikiwemo ya maji, umeme, mafuta na vilainisho. Kwa ujumla hali hii ambayo imeendelea kwa muda mrefu sasa, imekuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kielelezo cha changamoto hii ni Bajeti ya Shilingi 626,946,612,766.00 iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya mafungu yote matatu (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa mwaka 2010/2011, ambayo ni sawa na asilimia 45.10 ya mahitaji halisi ambayo yalikuwa Shilingi 1,389,869,618,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote walioniwezesha kufanikisha kutekeleza jukumu la kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tangu niteuliwe tena kushika wadhifa huu mwezi Novemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonayo juu yangu kwa kunituea tena kuongoza Wizara hii yenye dhamana nzito ya kulinda Uhuru na Usalama wa nchi yetu. Vilevile kwa niaba ya Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, kwa uongozi wake wa hekima na busara kwa suala zima la Ulinzi wa Taifa. Amiri Jeshi Mkuu amekuwa karibu sana kwa kufuatilia na anayo dhamira ya dhati ya kuendeleza Jeshi letu, jambo ambalo linawatia moyo sana maafisa na wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waheshimiwa Mawaziri wote, kwa msaada na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa George Simbachawele, Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole, kwa ushirikiano wenu mnaoendelea kunipatia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kutoa shukrani zangu maalum kwa Waheshimiwa Wabunge, wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Katibu Mkuu Mstaa fu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bwana Andrew S. Nyumayo, kwa utendaji na uongozi mahiri aliouonesha wakati akiwa katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Vilevile shukrani zangu za dhati ninazitoa kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jeneral Davis A. Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi, Luteni Jeneral Abdulrahman A. Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jeneral Samuel N. Kitundu, Makamanda, Maafisa, Askari na Watumishi wa

Umma. Wote ninawashukuru kwa ushirikiano mzuri na ushauri walionipatia na wanaoendelea kunipatia, kuiendesha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake. Aidha, ninampongeza Bwana Job D. Masima, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Engineer Musa I. Iyombe, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Kwahani kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao hapa Bungeni. Ninawashukuru kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Ninawaahidi kwamba, tutashirikiana kuliletea maendeleo Jimbo letu la Kwahani na Taifa kwa ujumla. Shukrani kwa wapiga kura wangu hazitakuwa kamilifu bila pia kukishukuru chama changu cha Mapinduzi, kwa kunipitisha kuwa mgombea na hatimaye kuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani kwa tiketi ya chama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninamshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wafanyakazi walio chini yake, kwa kuchapisha hotuba hii na kuikamilisha kwa wakati. Ninavishukuru pia vyombo vyaya habari hapa nchini kwa kazi nzuri ya kutangaza vyema shughuli zinazofanywa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa mwaka 2011/2012, umelenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya hivi karibuni, hususan Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na 2010/2011. Malengo ya Mpango huo yatazingatia utekelezaji wa shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida:-

- (i) Kuajiri wanajeshi wapya na kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi, ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mazoezi ya pamoja na majeshi ya nchi nyingine na mafunzo ya Ulinzi wa Umma (Mgambo).
- (ii) Kuimarisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wa Kitanzania wa kujitolea.
- (iii) Kugharamia upatikanaji wa mahitaji muhimu ikiwemo umeme, maji, simu, mafuta na vilainisho.
- (iv) Kutengeneza na kukarabati magari, vifaa, mitambo na zana.
- (v) Kutoa huduma muhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT ikiwemo chakula, tiba, sare na usafiri.
- (vi) Kulipa stahili mbalimbali za wanajeshi, vijana wa JKT na Watumishi wa Umma.
- (vii) Kuendeleza shughuli za ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Maendeleo:-

- (i) Kuimarisha Jeshi la Wananchi kizana na kivifaa.
- (ii) Kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Maghala Bora ya Kuhifadhia Silaha za Milipuko.
- (iii) Kukarabati na kukamilisha ujenzi wa majengo na miundombinu katika makambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali katika Hotuba hii kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa kuwa chombo cha kujenga na kudumisha umoja wetu wa kitaifa, hususan kutoa mafunzo ya uzalendo, mshikamano, usawa na ukakamavu kwa vijana wa Kitanzania. Kwa maana hiyo, Serikali bado inayo azma ya kurejesha utaratibu wa mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria ili kuwajenga vijana wasomi wa Kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, ujasiri na umoja wa kitaifa kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM inavyoelekeza. Kurejeshwa au kutorejeshwa utaratibu huo kwa sasa, siyo mjadala tena bali ni kwa namna gani na lini utarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, Serikali imeshaandaa makambi na miundombinu yenyeye uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa mara moja. Lengo lililopo ni kuchukua vijana wote wanaohitimu Kidato cha Sita na kuwapatia mafunzo kwa muda wa miezi sita. Kwa sasa idadi ya vijana hao inakadiriwa kuwa ni 36,000, ambapo ikilinganishwa na uwezo wa makambi itahitajika kuendesha mafunzo hayo kwa awamu mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa suala hili unagusa pia utaratibu wa mwendelezo wa vijana kielimu, hivyo kuhitaji kuandaliwa kwa utaratibu mzuri wa kujiunga na JKT bila kuathiri ratiba ya kujiunga na vyuo mbalimbali. Kwa kuzingatia hilo, upo umuhimu wa kushirikisha wadau wote kufanya maandalizi ya kutosha kabla ya zoezi hili kuanza katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2011/2012, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha jumla ya shilingi 682,315,415,000, ambazo kati yake shilingi 533,396,593,000 zitatumika kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 148,918,822,000 ni Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zimegawanyika katika mafungu matatu kama ifuatavyo:-

Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 415,416,165,000. Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 16,738,584,000.

Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 103,006,880,000, Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo ni 3,162,471,000.

Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 14,973,548,000 na Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 129,017,767,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. ANNA M. ABDALLAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2011/2012 na kuliomba Bunge liyapokee Maoni haya na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inahusisha mafungu matatu: Fungu 38 – Ngome, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa, na Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mara baada ya kuwateua Wajumbe wa Kamati hii mnamo tarehe 8 Februari, 2011, Kamati ilianza kazi ya kufuatilia utekelezaji wa Mpango na majukumu ya Wizara hii kama yalivyoainishwa katika Hati ya Serikali ya Kuanzisha Wizara (*Government Notes*) ya Novemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 21 na 22 Februari, 2011 Kamati ilikutana Mjini Dar es Salaam na kupokea taarifa kuhusu hali ya Jeshi letu nchini na ulinzi wa mipaka yetu. Tarehe 29 na 30 Machi, 2011 Kamati ilikutana tena na kupokea taarifa ya hali ya mipaka yetu na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ili kuisimamia na kuishauri vyema Serikali katika Sekta ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tarehe 8 Aprili, 2011 Kamati ilikutana tena Mjini Dodoma na kufanya kikao cha pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, taarifa zilizowasilishwa kwenye vikao hivyo vinne zinaonesha kuwa hali ya ulinzi wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari na Jeshi letu limeendelea kujipanga kiulinzi. Tarehe 30 Mei, 2011, Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam ili kuipokea na kuijadili taarifa ya Utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuhusu mambo mbalimbali ya utekelezaji katika sekta hii muhimu. Maelezo hayo yalihusu pamoja na mambo mengine, shughuli za Miradi ya Maendeleo, makusanyo ya maduhuli na mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2010/2011. Kutokana na Taarifa hiyo, pamoja na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati, yafuatayo yalibainika:-

Ulinzi na Usalama wa Nchi yetu umeendelea kuwa Ajenda muhimu na kwamba jukumu la kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama limeendelezwa. Taarifa za Serikali zinaonesha kuwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimeendelea kuwezeshwa kifedha na kivifaa ili viweze kumudu majukumu yake kwa ufanisi. Wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama alipokuwa akiagana na Bunge la Tisa, tarehe 16 Julai, 2010 alisema; ninanukuu: “ Nilipokuja kulifungua Bunge letu mwaka 2005, niliahidi kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne itajenga mazingira mazuri ya kazi kwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Kazi hiyo tumeifanya na tunaendeleo nayo.” Mwisho wa kunukuu. Aidha, moja ya vipaumbele kumi na tatu vya Serikali iliyoundwa mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 ni kuhahakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa yenye Umoja, Amani na Usalama na Muungano wetu unaendelea kudumu na kuimarika. Vipaumbele hivyo viliainishwa na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama mbele ya Bunge hili tarehe 18, Novemba, 2010 ambapo Mheshimiwa Rais alifafanua kwa kusema: “Umoja wa Nchi yetu una sura tatu kuu: Kwanza ni mipaka inayotambulisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa salama...” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sura nyingine mbili alizozitaja Mheshimiwa Rais ni Muungano na Wananchi kuwa wamoja, wanaopendana, kushirikiana na kushikamana. Sura hizo tatu za umoja zinasisitiza usalama na uimara wa mipaka ya nchi yetu na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka. Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati kila zilipohitajika, zinaonesha kuwa, hali kwa ujumla ni shwari na mipaka ya Nchi yetu iko salama na kwamba hakuna tishio lolote la kutoka ndani au nje ya Nchi dhidi ya mipaka yetu.

Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudhi za kuliimarisha Jeshi letu. Pongezi mahususi ni kwa Mkuu wa Majeshi, Jenerali Davis Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Abdulrahmani Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Samwel Kitundu, Maafisa na Askari wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofî*)

Majeshi ya Tanzania yameendelea kufanya vizuri katika Ulinzi wa mipaka yetu na operesheni nje ya Nchi.

Wanajeshi wa Tanzania wanashiriki katika ulinzi wa amani katika sehemu mbalimbali ikiwepo pamoja na Lebanon na Darfur. Vilevile, mwaka 2008 Jeshi letu liliongoza kwa ufanisi mkubwa Majeshi ya Nchi za Umoja wa Afrika kukirejesha Kisawa cha Anjuan kilichokuwa kikitawaliwa kwa mabavu na Kiongozi Muasi Kanali Mohamed Bakar katika Umoja wa Jamhuri ya Visiwa vya Comoro. Ufanisi huu umeipatia heshima

kubwa Tanzania na ni moja ya mafanikio kutohana na usimamizi mzuri wa mafunzo ya ukakamavu na uzalendo katika Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini. Kamati inaipongeza Serikali na Wataalamu wake wa masuala ya Ulinzi na Usalama, kuiwezesha Nchi kuheshimika katika sekta hii. (*Makofi*)

Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya 192, ilijojadidiwa mwaka 2002 (*The National Defence Act, Cap. 192, Revised Edition of 2002*) na Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 533 (*The National Services Act, Cap. 533*), zinahitaji marekebisho. Kumbukumbu zinaonesha kuwa, Mheshimiwa Waziri amekuwa akiyahidi Kamati kushughulikia marekebisho hayo tangu Bunge la Tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wakati huo, ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali kuhusu Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ushauri huo ulihusu utaratibu wa kutumia utaalamu wa Maafisa wa Jeshi Wastaafu, kujenga uwezo wa vikosi vyta Uhndisi vyta majeshi yetu na ajira mpya katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuendelea kila mwaka pasipo kuathiriwa na uamuzi wa Serikali wa kupunguza ajira Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati iliishauri Serikali kuhusu mafunzo ya ukakamavu na uzalendo yanayotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, kuendelea kuimarisha majeshi yetu na kulipa madeni mbalimbali ya askari. Ninaomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekuwa siku na sehemu kubwa ya ushauri inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, kuhusu madeni ya askari kwa Mafungu 38 - Ngome na Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeanza kulipa madeni binafsi yasiyokuwa madai ya posho ya likizo. Serikali ilitarajia kuwa hadi mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, madeni yaliyobaki yatakuwa yamelipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Waziri ilieleza namna Serikali inavyoendelea kuimarisha majeshi yetu na kuyajengea utayari wa kuilinda mipaka yetu. Kamati inampongeza Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jinsi anavyoendelea kuliimarisha Jeshi letu na kuliwezesha kumudu majukumu yake kwa ufanisi zaidi tangu alipoingia madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa kwa sasa lina uwezo wa kupokea vijana 20,000 na kwamba, uwezo huo unatosheleza kuchukua vijana wote wanaohitimoo Kidato cha Sita kwa awamu mibili za miezi sita kila moja. Sambamba na hilo, Serikali inaendelea na mchakato wa kuangalia marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa na utaratibu wa utekelezaji wake kwa lengo la kuanza mafunzo hayo kwa namna bora zaidi inayolingana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuzingatia maoni ya Kamati na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wengine kama ulivyotolewa wakati wa kupitia Bajeti

ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu wa kuongeza kasi ya utekelezaji. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Serikali imeahirisha tena mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria na kwamba, inaendelea kufanya maandalizi ya marekebisho ya Sheria na taratibu za utekelezaji wake. Kumbukumbu zinaonesha kuwa, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge la Tisa, ilipofanyiwa Semina kuhusu Sheria hiyo tarehe 11, Julai, 2008, ilishauri marekebisho ya Sheria hiyo. Hadi sasa ni takriban miaka mitatu, mchakato wa kuandaa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na ufuatiliaji wa majukumu ya Wizara uliofanyika kwa kipindi cha Februari hadi Aprili, 2011, Tarehe 30 Mei, 2011, Kamati ilikutana na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kwa Mwaka wa fedha wa 2010/2011. Katika kikao hicho, Kamati ilielezwu jinsi Wizara ilivyotekelza majukumu na malengo yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 pamoja na mwelekeo wa matumizi ya fedha hadi Juni, 2011. Aidha, Kamati ilielezwu mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Mwaka 2010/2011, sanjari na kuelezwu changamoto zilizoikabili Wizara kwa kipindi hicho. Ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa majukumu ya Wizara umefikia hatua kubwa kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati na Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwu kuwa, kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaomba kuidhinishiwa makusanyo ya maduhuli ya kiasi cha shilingi 73,206,000 kwa mafungu yote matatu: Fungu 38 - Ngome, Fungu 39 - JKT na Fungu 57 - Wizaraya Ulinzi na JKT. Aidha, ili kufanikisha azma ya Serikali katika Sekta ya Ulinzi na Usalama, Wizara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 682,999,603,415.00 kwa mafungu yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mpango na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati inaunga mkono hoja. Baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba kutoa maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Katika kutekeleza nia ya Serikali kuendelea kuboresha maslahi ya wanajeshi wetu pamoja na mazingira yao ya kuishi na kufanya kazi, utekelezaji wa jukumu la kulipa madeni binafsi ya askari ufanyike kama inavyostahili.

(ii) Kwa kuwa ni muhimu kuititia na kurekebisha Sheria na taratibu za utekelezaji wa mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria kabla ya kuanza mafunzo hayo, Serikali iongeze kasi ya zoezi hilo. Aidha, kwa kuwa ni muda mrefu tangu Serikali isitishe mafunzo hayo, wakati umefika kuhakikisha kuwa fedha ya kutosha inapatikana kwa ajili hiyo.

(iii) Katika utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Serikali iongeze kasi ya kupitia na kuboresha Sheria ya Ulinzi wa Taifa (*The National Defence Act*) ya mwaka 1966.

(iv) Kwa kuwa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (*The National Defence College*) kimekamilika na ili Chuo hicho kiwe na manufaa yaliyokusudiwa, Serikali iandae mpango kwa ajili ya mafunzo ya Viongozi na Watendaji wa Kitaifa haraka iwezekanavyo.

(v) Kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa lina uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya kilimo, Serikali ilitumie vyema Jeshi hilo katika Mkakati wa Kilimo Kwanza na kuongeza kasi na ufanisi wa malengo ya kuleta mapinduzi katika kilimo, ufugaji na uvuvi.

(vi) Kwa kuzingatia kuwa SUMA JKT inafanya kazi nzuri katika uzalishaji mali, Kamati inatoa pongezi kwa namna shirika hilo linavyofanya kazi na kushauri kuwa, shirika hili liongeze juhudhi ya kujitangaza na kupenya zaidi katika soko. Aidha, Serikali izihimize Taasisi zake kulitumia shirika hili kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha, ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu ili niwasilishe Taarifa na Maoni ya Kamati. Vilevile, katika uteuzi wa Wajumbe wa Kamati, ninakupongeza kwa namna ulivyozingatia uzoefu wa Wajumbe katika Sekta mbalimbali za Utawala, Siasa, Uchumi na Jamii kwa ujumla. Mchanganyiko wa uzoefu wa Wajumbe, umesaidia sana kuiwezesha Kamati kufanikisha jukumu lake muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Ndugu Job D. Masima, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Kamati. Maeleo yao ya kina na ufanuzi wa hoja zilizotolewa kwenye vikao, ulisaidia Kamati kutekeleza ipasavyo wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninamshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mbunge, kwa kunisaidia kuiongoza vyema Kamati. Ninawashukuru pia Wajumbe wengine kwa kazi nzuri, ushirikiano mkubwa na umakini wao wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa heshima na taadhima, ninaomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Capt. Mst. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen Mst. Hassan A. Ngwilizi,

Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura. Aidha, ninamshukuru Ndugu Athuman Hussein, Katibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Ninawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa huduma zilizofanikisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza na kumpongeza sana Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuteuliwa kwenu, pamoja na kazi nzuri mnayoifanya katika kuliendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu, lipokee Taarifa na Maoni haya pamoja na kukubali kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kama yalivyowasilishwa hapa na mtoa hoja muda mfupi uliopoti.

Mshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Abdallah, Msemaji wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Edward Lowassa. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Selasini akimaliza, msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Amina Andrew Clement; ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kunilinda na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge hili nikiwa mzima wa afya, baada ya misukosuko niliyokutana nayo wakati wa mchuano mkali wa kuwania Ubunge katika Jimbo la Rombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mama Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Spika na kuweza kuongoza vyema Bunge hili la Kumi lenye changamoto kubwa kwa kulinganisha na Mabunge yaliyopita. Ninapenda pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Job Ndugai, Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Jimbo la Donge, kwa kumsaidia vyema Spika kuliongoza Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni ya 99(7), ninachukua fursa hii kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kutoa shukrani kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kuniteua kugombea Kiti cha Ubunge Jimbo la Rombo na kushinda kwa kishindo. Ninapenda pia kutoa shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami ninatoa ahadi kwake kuwa, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, ninatumaini mambo yatakuwa mazuri na tutashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ninawashukuru Wananchi wa Jimbo la Rombo, kwa imani yao kubwa kwangu na kunipa kura nyingi na hivyo kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni; nasema ahsanteni sana na ninawaahidi kuwa, tutaendelea kushirikiana kama ambavyo tumekuwa tukifanya kazi kwa kipindi chote hata kabla sijawa Mbunge wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, ninawashukuru Wazazi zangu; Mheshimiwa Roman Selasini Shao, Diwani wa Kata ya Makiidi (CCM), Mama Catherine Matarimo na ndugu zangu wote, kwa malezi na mafundisho mazuri, bila kusahau sala na mawaidha yao ambayo yamenifikisha hapa nilipo. Aidha, ninamshukuru pia Baba yangu wa Kiroho, Paroko wa Parokia ya Pugu Dar es Salaam, Padri Leonardo Amadori na waumini wake wote, kwa sala na ushauri ulionisaidia na unaoendelea kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa, ninawashukuru Mke wangu mpenzi, Digna Peter Kavishe, pamoja na watoto wetu kwa mapenzi, huduma na uvumilivu wao, pamoja na ushauri ambao ninatambua kama vingekosekana, ningekata tamaa mapema katika harakati zangu kisiasa na hivyo safari yangu ya kuja hapa kwa kiwango kikubwa ingekuwa ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania; Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, Jeshi la nchi yoyote, ndiyo alama inayoonekana ya ulinzi wa nchi; hivyo basi, jukumu la JWTZ haliwezi kuchukuliwa na chombo kingine chochote. Kwa sababu hiyo, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kuwa jeshi letu la ulinzi linakuwa la kisasa na lenye nguvu katika nyanja zote. Sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, jambo la msingi ili kulifanya Jeshi letu kuwa la kisasa, ni kuhakikisha kwamba, askari wetu wote wanaishi katika makambi yaliyo katika mazingira bora zaidi kwa kulinganisha na hali halisi ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona sasa ni muda mwafaka kwa Jeshi letu Kitengo cha Navy, kuwa na mkakati maalum wa kufanya doria maeneo ya bahari kuu ili kuhakikisha meli kubwa za uvuvi ambazo zinavua katika eneo la nchi yetu, zinadhibitiwa kwa kiwango cha hali ya juu ili rasilimali zetu zisiendelee kuibiwa huku sisi kama nchi tusikose mapato stahiki. Kwa maana nyingine, tunashauri kuwekwa kikosi

maalum chenye meli na vifaa vyta kisasa ili kukabiliana na meli kubwa za uvuvi zinazovua maji yetu kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu Rasmi za Bunge zinaonesha kwamba, Kambi ya Upinzani, ilikwishatoa ushauri wa kuzifanya mapitio sera na sheria zinazoendesha jeshi letu, kwani zilizopo ni za kizamani na haziendani na kasi ya karne hii ya sayansi na teknolojia. Ili mkakati huo uweze kufanikiwa, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwashirikisha wadau wote wanaohusiana kwa njia moja ama nyingine na ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya nje, Ulinzi na Usalama ni mdau mmojawapo katika kutekeleza azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengi yanayojitokeza kati ya jeshi na Wananchi katika maeneo mbalimbali yanachangiwa na ukweli kwamba, Wananchi hawahusishwi au kushiriki katika mchakato mzima wa utungaji sera na sheria zinazoongoza taasisi hii muhimu kwa ulinzi na usalama wa Wananchi na mali zao. Matatizo hayo ni pamoja na ugomvi mkubwa wa mipaka ya ardhi kati ya Makambi ya Jeshi na Wananchi, katika maeneo mbalimbali, wanajeshi huvamia Vijiji na kuanza kutoa adhabu za kijeshi kwa raia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, kwa njia hii ya utunzi wa sera na sheria za ulinzi zitakazotungwa, zitakuwa zime wahusisha Wananchi kwa kiasi kikubwa na zitasaidia kuondoa migongano isiyokuwa na tija kati ya Jeshi na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matumizi mabaya sana ya vifaa vyta jeshi kwa matumizi ya kisiasa na matumizi binafsi ya wanasiisa, jambo ambalo limeendelea kuongeza gharama kwa jeshi hilo. Mifano iliyo hai ni mwaka juzi zilitolewa taarifa za kuanguka kwa helikopta ya jeshi Mkoani Manyara iliyokuwa imebeba Wazungu waliokuwa kwenye ziara binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni ule wa juzi ambapo ndege ya jeshi ilitumika kumsafirisha Mwenyekiti wa CHADEMA peke yake kwenda Arusha kutekeleza amri ya Mahakama. Tukumbuke Ndege hiyo ilirudi ikiwa na rubani peke yake; jambo hili ni matumizi mabaya sana ya rasilimali za taifa na halikubaliki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaliheshimu sana Jeshi letu na kazi linazozifanya katika mchakato mzima wa kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. Kuna majukumu mbalimbali ambayo kimsingi ni majukumu ya jeshi letu ambayo ni kama yafuatayo:-

- Kulinda mipaka dhidi ya maadui wa nje ya nchi yetu;
- Kusaidiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga;
- Kusaidia kujenga na kudumisha mazingira ya amani na usalama na nchi nyingine duniani, hasa nchi majirani;

- Kuandaa umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya maadui;
- Kutafiti na kuendeleza teknolojia ya kijeshi; na
- Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, nidhamu, sawa na Umoja wa Kitaifa na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi na Biashara ya Uchuuzi; majukumu tajwa hapo juu kwa ujumla yanatekelezwa na Jeshi la Wananchi pamoja na taasisi zilizo chini ya jeshi hilo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa kina ni kwa vipi Jeshi la Wananchi limeingia katika mkataba na nchi ya India kwa minajili ya kukopeshwa matrekta ili Jeshi lienze kufanya biashara ya kuuza matrekta hayo kwa Wananchi na Taasisi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Uchunguzi inayoitwa *Public goods, rents and business in Tanzania*, iliyotolewa na Bwana Brian Cooksey Juni, 2011 inasema kuwa, Serikali imetoa udhamini wa shilingi bilioni 40 kwa SUMA JKT na shirika hilo la Jeshi likaingia Mkataba na Ndugu Jeetu Patel kuingiza matrekta hapa nchini.

Kauli hii ni kubwa mno, kwani Ndugu Jeetu Patel ndiye anayekabiliwa na kesi ya wizi wa mabilioni ya shilingi kutoka Benki Kuu kwenye Akaunti ya Malipo ya Nje (*EPA*) na kesi yake bado inaendelea. Sasa ni kwa vipi tena Jeshi linaingia naye mkataba wa kufanya makubaliano na India kwa udhamini wa fedha za walipa kodi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzani juu ya Jeshi kumtumia mtuhumiwa wa wizi wa fedha za walipa kodi kuingia makubaliano ya kibiashara kwa kutumia udhamini wa fedha za walipa kodi (*Government Guarantee*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Waziri inaonesha kuwa shilingi bilioni 1.123 zilitumika kwa ajili ya utoaji wa matrekta hayo bandarini na hadi sasa matrekta hayo yamewekwa Mwenge - Dar es Salaam na mengine tumeyaona hapo maeneo ya Kisasa - Dodoma.

Swali la kujiuliza; je, ni kweli matrekta haya ni mali ya jeshi au kuna Maafisa wa Jeshi wanafanyabiashara hiyo kwa kutumia jina la Jeshi? Kama ni mali ya Jeshi; Waziri alieleze Bunge hili Jeshi lilitarajia kupata faida kiasi gani baada ya kufanya hiyo biashara ya kuuza matrekta hayo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Jeshi kujiingiza kwenye biashara ambayo siyo jukumu lake, kimsingi, linatutia mashaka makubwa sana kama ni kweli Jeshi letu linatumika kufanya biashara na baadhi ya watu.

Hoja hii inapata nguvu kutoka kwenye Hotuba ya Waziri wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, katika aya ya 24 inayolihusu Shirika la Nyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kunukuu: “Katika mwaka 2009/10, Shirika la Nyumbu limekamilisha kuandaa Mpango Mkakati wake wa muda mrefu, ambao una lengo la kulifanya shirika kuwa kituo maalum cha kuendeleza teknolojia za magari na mitambo ndani na nje ya nchi, pia kufanya utafiti na uzalishaji mdogo mdogo wa bidhaa na vifaa mbalimbali kwa ajili ya Sekta za Ulinzi na Usalama, Kilimo, Viwanda na Usafirishaji.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilitegemea kuwa, Jeshi la Wananchi lingeingia mkataba kwa ajili ya kuiimarisha Taasisi ya Nyumbu ili iweze kuzalisha vifaa mbalimbali vitakavyokuwa vinatoa teknolojia rahisi katika mchakato mzima wa uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Hii sera mpya ilivoletwa na Jeshi na kuhalalishwa na Serikali, yaani Jeshi kujiingiza katika masuala ya biashara ya kichuuzi ya kununua kwa mkopo na kuuza, badala ya Jeshi kuwa taasisi mfano kwa kuvumbua na kusambaza teknolojia katika nyanja mbalimbali za uzalishaji na hivyo kuinua uchumi wa nchi, inatia shaka na doa kwa Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ya Jeshi kutumiwa na baadhi ya wafanyabiashara na matepeli wakishirikiana na baadhi ya Makamanda Wakuu Jeshini, imejidhihirisha wazi katika taarifa iliyotolewa na gazeti la kila siku la “Dira ya Mtanzania” la tarehe 4 - 6 Julai, 2011. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ya kina kuhusiana na taarifa hiyo na ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa Maafisa hao wa Jeshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo ni mwendelezo wa taarifa ambazo zilikwishalalamikiwa na jamii, jinsi ambavyo Ndugu Visran Sileshi alivyokuwa akifanya biashara haramu na baadhi ya Makamanda wa Jeshi na mwisho ilikuwa kwa Jeshi kununua vifaa vibovu kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya kawaida, kuna Wananchi ambao kutokana na utundu wao wa asili, wanatengeneza silaha kama magobore, lakini badala ya Jeshi kuwachukua Wananchi hao na kuwaendeleza, Serikali inawafungulia mashtaka. Hii ni kuwafanya Wananchi wenyewe uwezo wa kubuni na kutengeneza baadhi ya vifaa, kuogopa na hivyo vipaji vyao kupotea kabisa. Hii ni hatari kwa taifa dogo kama la kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka ya *duty free* yalianzishwa maalum kwa ajili ya kuwapatia huduma askari wetu, ambao muda mwangi wanakuwa katika ulinzi wa nchi yetu.

Bidhaa zote zinazouzwa katika maduka haya maalum, zinakuwa zimepata msamaha wa kodi kwa mantiki kuwa msamaha huo uende moja kwa moja kwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka haya baada ya kupata msamaha wa kodi, wanauzu bidhaa hizo kwa bei ambazo ni sawasawa na bidhaa zilizolipiwa ushuru. Aidha, huduma kwa maduka hayo, hutolewa hata kwa watu wasiokusudiwa na kuwaacha walengwa wakiwa hawapati huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia upya suala hili la *duty free shops* ili lifanye kazi kama malengo ya uanzishwaji wake. Sambamba na hilo, ni kuangalia wanaonufaika ni askari wa kada ipi, kwani malalamiko yamekuwa ni mengi kuwa askari wa kada ya chini hawanufaiki kabisa na huduma hii. Tunaomba ufanuzi wa kina kwamba Serikali inapoteza kiasi gani kwa kusamehe ushuru kwa ajili ya mpango huo wa maduka ya kuhudumia askari?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2008/2009, katika aya ya 22 alieleza kuwa Jeshi la Wananchi lilikuwa linafanya utafiti ili kuona uwezekano wa kutumia nishati ya umeme wa mionzi ya jua, mabaki ya chakula na taka za mimea kwa nia ya kupunguza gharama kubwa ya matumizi ya umeme ya Jeshi hilo pamoja na kusambaza katika Vikosi vya Jeshi ambavyo havipati umeme wa gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inalionna hili kuwa ni hatua muhimu sana na ya kupongezwa. Lakini cha ajabu ni kwamba toka muda huo, Serikali haijatoa taarifa ya maendeleo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote majeshi ndiyo yanayotumika kama kitovu cha teknolojia za kisasa na usambaza wa teknolojia hizo kwa matumizi ya nchi kwa ujumla. Ili kutimiza azma hiyo, jeshi hupewa kipaumbele katika kutafuta vijana wadogo kutoka Shule za Awali na Msingi na kuendelea nao katika shule maalum ambazo zinakuwa chini ya uangalizi wao. Hivi ndivyo wanasayansi wanavyopatikana kwa nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jeshi letu halijakuwa na mkakati madhubuti wa kufanya *scouting and recruitment* kwa vijana wadogo ambao watawasomesha kulingana na matakwa yao, Kambi ya Upinzani inasema hayo kutokana na ukweli kwamba wapo vijana ambao wameonyesha vipaji vya hali ya juu katika uvumbuzi wa vifaa mbalimbali kama magari, vipuri vya mashine za kusaga, kutengeneza redio na kufanikiwa kushika baadhi ya mawimbi ya sauti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu lina taasisi mbalimbali zinazojihusisha na utafiti na uzalishaji kama vile Shirika la Nyumbu ambalo linajihusisha na utafiti na uzalishaji wa magari na vifaa vingine vya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha kuwepo kwa utaratibu ambao tunadhani kuwa sio mzuri wa kila kitu ambacho kinakuwa chini ya Jeshi kuwa siri na hivyo kusababisha kutokupata taarifa muhimu ambazo zingetusaidia kuhoji jinsi mashirika yaliyopo chini ya Jeshi yanavyofanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Wizara kama ilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, inaonyesha kuwa katika utekelezaji wa miradi yake ya kuendeleza utafiti, ni Jeshi kukamilisha utafiti wa *power tiller*, kukamilisha utafiti wa gari la nyumbu. Kambi ya Upinzani inauliza hili gari la nyumbu ambalo mwaka 2004 lililetwa hapa katika Viwanja vya Bunge kuwaonyesha Waheshimiwa Wabunge likiwa limekamilika, leo tena tunaambiya bado, kuna nini kinaendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona Jeshi kujifungia wao wenyewe kufanya utafiti wa *power tiller* wakati kuna taasisi nyingine ya Serikali ambayo ni maalum kwa ajili ya kufanya utafiti na usambazaji wa teknolojia ya vifaa vya kilimo kwa ujumla wake na *power tiller* ni mojawapo katika tafiti zinazofanywa na taasisi hiyo, hivyo basi, Jeshi kutokushirikiana na taasisi hiyo kunaweza kusababisha kutengeneza hiyo wanayoiita *power tiller* ni kupoteza muda na raslimali za walipa kodi bure. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa utafiti wowote unaoendelea au utakaoendelea kuhusiana na teknolojia ya kutengeneza vifaa vya kilimo kwa upana wake, ushirikiano na *CARMATEC* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi linasimamia na kumiliki taasisi zifuatazo: *Tanzansino United Pharmaceuticals (T) Ltd, Tanzansino Garments Industry, TATC Nyumbu, Chang'ombe Furniture Ltd, Ndege Beach Hotel, Shirika la Mzinga Meremeta Ltd, Shule za Sekondari, Hospitali na kadhalika.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni haya yote ni makampuni ya kibiashara na tunatarajia kwa kuwa yanafanya biashara, hivyo ni wajibu wake kuweka kumbukumbu za taarifa zake wazi na hivyo kuondoa dhana ya usiri iliyokithiri katika Jeshi la Wananchi. Katika takwimu zote ambazo Bunge hili limekuwa likizipokea toka Wizarani hatujawahi kuletewa taarifa za uendeshaji wa Hoteli ya *Ndege Beach*.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa hoteli hiyo inaendeshwa kibiashara au inafanywa kama sehemu ya viongozi wa kijeshi kupumzikia wao na familia zao tu? Kuendesha hoteli kunahitaji taaluma ya uendeshaji wa mahotel na kama ndiyo hivyo, waajiriwa katika hoteli hiyo wanapatikana kwa mfumo upi? Tukumbuke kuwa mali za jeshi ni mali za walipa kodi na siyo mali binafsi za Maafisa wa Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawo wa bajeti unatolewa jumla jumla tu, kwa mfano inaonyesha kuwa fungu 39, JKT kwa mwaka wa fedha 2010/2011 iliidhinishiwa shilingi bilioni 12.65 lakini limepatiwa shilingi bilioni 3.79 ambayo ni sawa na asilimia 29.9. Hoja ya Kambi ya Upinzani ni kuwa mgawo huu ni kwa ajili ya kuendeleza viwanda vilivyo chini ya JKT ambavyo vinatakiwa kuijendesha kibiashara. Tunaomba jambo hili liangaliwe vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Chang'ombe furniture Ltd* hutengeneza samani za mbao za aina mbalibali kulingana na mahitaji ya mteja. Samani ni pamoja na zile za majumbani, maofisini, mashulen na makanisani. Waheshimiwa Wabunge kupitia vikao mbalimbali wamekuwa wakitoa ushauri mbalimbali kwa Serikali kuhusiana na umuhimu wa Serikali kununua samani za majumbani na maofisini zinazotengenezwa na viwanda vyetu vya ndani badala ya kununua samani hizo toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema kwamba kutokana na mapato yasiyordhisha yanayotokana na makampuni saba ya jeshi kwa fungu 39 na fungu 57 ya shilingi milioni 71.7 tu, wakati fedha zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo kwa mafungu hayo ni shilingi bilioni 132.18, Serikali itoe mgawo kwa kuangalia uwiano uliopo kati ya mapato na uwekezaji wa pesa zinazotengwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hayo kutokana na ukweli kuwa mapato yanayotokana na mashirika hayo hayaoni na matumizi yake, kiasi ambacho kinatengwa na Serikali katika kuendesha mashirika hayo. Bado tuna kumbukumbu ya mambo gani hasa yaliyosababisha Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria kukwama. Hili halikuwa siri, bali ni kutokuwepo kwa nidhamu ya matumizi na usimamizi wa bidhaa zilizokuwa zinazalishwa na taasisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi lina kiwanda cha kutengeneza madawa (*Tanzansino Phamaceuticals Ltd*), lakini hatujawahi kuona kwenye maduka yetu madawa yanayozalishwa na kiwanda hicho. Tanzania imekuwa ikiagiza nje ya nchi maji kuwekea *drip* kwa wagonjwa na akina mama wanaojifungua wakati Jeshi lina kiwanda cha madawa. Hii ni aibu kwa nchi yetu na kwa jeshi letu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi ni madawa ya aina gani yanazalishwa na kiwanda hicho? Jeshi lina mkakati gani kwa madawa yanayozalishwa na kiwanda hicho kuingizwa katika mfumo wetu wa usambazaji wa madawa kwa kuitumia *MSD?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa chombo cha kusimamia (*oversight*) katika utendaji mzima wa makampuni ya kibiashara ya Jeshi ndiyo suala linalosababisha kutokuwepo kwa uwajibikaji na utawala bora jambo ambalo linasababisha kutokuonekana kwa tija kwa yale yote yanayozalishwa na makampuni hayo ya jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usiri ambao unaendelea katika miradi/makampuni ya jeshi umeendelea kuitia hasara nchi hii. Kambi ya Upinzani kwa miaka mitano iliyopita tumekuwa tukihoji umiliki wa Mgodi wa Meremeta na Serikali imeshindwa kutoa majibu sahihi, hatimaye Waziri Mkuu aliamua kulieleza Taifa kuwa Meremeta ni suala la ulinzi na usalama na hivyo ni siri na hakuna mtu mwenye uwezo wa kuhoji tena na mjadala umefungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usiri huu umewaacha wananchi wa Buhemba ambao hadi muda huo bado walikuwa na madai mbalimbali dhidi ya Kampuni hiyo ya Meremeta. Kambi ya Upinzani inasema kuwa Kampuni hii ilikuwa ni ya kibiashara na hivyo bado tuna haki kabisa ya kuendelea kuhoji ubadhirifu wote uliofanywa na baadhi

ya watendaji jeshini kwa mgongo wa kusema kuwa kila jambo ambalo liko chini ya jeshi ni siri na hakuna mamlaka ya kuhoji jinsi linavyoendeshwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema: “*No taxation without representation.*” Kama ilivyotolewa na Katibu Mkuu wa *Inter-Parliamentary Union, Mr. Anders B. John* pamoja na *Mkurugenzi wa Geneva Center for Democratic Control of Armed Forces, Balozi Dr. Theodor Winkler*, kama Bunge linapitisha fedha za walipa kodi kwa matumizi ya Taasisi za Jeshi, ni lazima wawakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge waelewe nini kinafanyika na wawe na mamlaka ya kuhoji matumizi ya fedha hizo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inasema kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni kuwa suala la Meremeta limefungwa na halitakiwi kuhojiwa tena kwa kuwa ni siri ya Jeshi, halina mashiko na ni tetezi dhaifu, kwani kumbukumbu zinaonyesha kuwa kampuni hiyo ya Jeshi ilianzishwa kwa fedha za wananchi, na Wabunge ni wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa mipaka yetu ni jukumu mama la Jeshi letu. Nchi yetu imekuwa imezungukwa na nchi nane, hivyo kuwa na eneo kubwa ambalo linahitaji macho ya Jeshi kwa kipindi chote. Hivi karibuni kumekuwa na kilio na malalamiko makubwa toka kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera na Kigoma kwamba kuna uvamizi unaofanywa na kundi la wahalifu toka nchi jirani za Burundi na Rwanda kwa Wilaya ya Ngara na Karagwe, ambao wananchi wamekuwa wakiporwa mali zao na pia kuingiza makundi makubwa ya mifugo kwenye maeneo ya hifadhi, *DRC* kwa upande wa uvamizi wa wavuvi kwenye ziwa Tanganyika ambao wavuvi wetu wamekuwa wakiporwa mali zao wawapo ziwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kulitumia Jeshi letu kuongeza askari pamoja na vifaa bora vya kufanya kazi hiyo katika maeneo ya mipakani japokuwa kuna vikosi vilivyokaribu na mikapa yetu. Tunasema hayo kutokana na ukweli kwamba kuna vikosi kama vilivyopo Rukwa vya Ikola na Kirando vinakosa vifaa vya kisasa kupambana na majambazi wanaopora zana na mali za wavuvi wetu katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana kwa wanajeshi wetu wanapomaliza utumishi wao kwa nchi, wanabaki wakiwa omboaomba. Jambo hilo linawalazimisha kujingiza katika shughuli ambazo ni za kuhatarisha usalama wa raia na mali zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi limekuwa likiwakopesha askari vyombo vya usafiri, pikipiki na baiskeli askari wengi ambao wanakaa kambini. Lakini kukopeshwa huko hakuwasaidii askari hao wanapomaliza utumishi wao. Tukumbuke kuwa mikopo wanayoipata ya vyombo vya usafiri wanatakiwa kuilipa wakiwa bado kazini. Swali la msingi ni je, wakishamaliza utumishi wao kwa nchi wanaendeshaje maisha yao na familia zao? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka utaratibu maalum kwa askari wetu wa ngazi za chini pindi wamalizapo utumishi wao kuwepo na mpango mahsus kwa ili wasiweze kushawishiwa na yejote kujihusisha na uvunjifu wa sheria za nchi. Sambamba na hilo ni kuwaongezea kipato watumishi hao wa amani ya nchi kutapandisha

kiwango cha pensheni yao ili iweze angalau kuwasaidia pindi wamalizapo utumishi wao kwa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la askari wa kujitolea, walioshiriki katika vita ya Uganda hapo miaka ya 1978/1979 na baadaye kuingizwa katika ajira ya Jeshi. Lakini kwa masikitiko makubwa, askari hao baada ya kustaafu wamekosa mafao yao na sasa wanaishi katika mazingira magumu sana kwani pensheni wanayopata ni kidogo sana kuweza kujikimu wakati wengi wao wamekuwa ni walemvu kutokana na vita hivyo na sasa baadhi yao familia zao zinawanyanyaapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wamekuwa wakipeleka madai yao Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi (Ngome) lakini hawasikilizwi na wanadai kubezwa. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho alitolee kauli suala hili ili wazee hao waliojitlea katika kuilinda nchi yetu nao wapate stahiki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa juhudi kubwa zinazofanywa na Jeshi katika kuinua na kuendeleza michezo. Ni ukweli ulio wazi kwamba wanamichezo kutoka majeshi ndio waliokuwa vinara katika anga za kitaifa hadi kimataifa, mifano ni mingi na kila mmoja analielewa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kulisaidia Jeshi kuimarisha timu zake za michezo yote kwani michezo ni nidhamu, na nidhamu kwa kiwango kikubwa iko kwenye timu zetu za Jeshi, kama tu wachezaji watakuwa ni waajiriwa wa jeshi, na sio wachezaji wa kukodisha jambo ambalo linaharibu sifa nzuri ya nidhamu kwa wachezaji wa Jeshi. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kama Vyuo vya Michezo (*sports academy*) vikiwekwa na kuendelezwa chini ya Jeshi letu, ni dhahiri matunda yake yanaweza kupatikana kwa haraka zaidi na nchi itaweza kuondokana na aibu ya michezo ambayo kwa miaka ya karibuni imekuwa ikitukumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengi sana yanayohusiana na taasisi hii nyeti ya kulinda usalama wa wananchi wote, ila ninaamini haya tuliyosema yatazingatiwa kwa maslahi ya Jeshi letu na wapiganaji wake na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini - Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa ni zamu ya wachangiaji wengine. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Amina Andrew Clement ataanza na atafuatiwa na Mheshimiwa Salim.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili niweze kuchangia.

Kwanza, sina budi kuchukua nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikawa mzima na salama nikasimama hapa Bungeni nikaweza

kuchangia. Pia namwomba Mwenyezi Mungu anijalie nichangie kwa usalama salimini na nitakayoyachangia namwomba ajalie yakubalike, pia yatekelezwe kwa ufanisi. (*Makofi*)

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wana Jimbo la Koani kwa kuweza kunichagua mimi Amina Andrew nikawa Mbunge wao wa Jimbo la Koani. Ahadi yangu kwao iko pale pale, naahidi nitashirikiana nao usiku na mchana kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Koani. Ahadi yangu sana naahidi sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu yote, wanangu, ndugu zangu na baba mpenzi Mzee Andrew Clement kwa kuweza kuniombea dua wakati mgumu wa kipindi cha uchaguzi hadi mwisho nikafanikiwa. (*Makofi*)

Lakini napenda kuchukua nafasi hii adhimu ninayoitoa ndani ya nafasi yangu kumshukuru mume wangu mpendwa, kwa kuweza kunipa faraja nikaweza kukaa ndani ya Bunge hili Tukufu kwa utulivu. (*Makofi*)

Napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, kwa hotuba yake nzuri yenyenye mantiki na iliojaa mambo yote tutakayoyachangia hapa. Lakini naomba zaidi ya mambo ya hayo, nizidi kutoa msisitizo, kuwapongeza Wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi wa Tanzania walio katika makazi hivi sasa na pia waliokuwa wameshastaifu. Nawapongeza kwa jitihada zao za kutulinda sisi Watanzania katika mipaka yetu yote ya nchi yetu pia tukawa tuko katika hali ya utulivu na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwanza kuzungumzia suala la pensheni za Wanajeshi. Wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi waliokuwa wanafanya kazi jana, waliokuwa Jeshini leo, Wastaifu na mlioko leo kazini/madarakani, mjue kesho na nyie mtakuwa wastaifu. Wastaifu hawa wakishapewa barua zao, Wanajeshi kustaifu siyo muda mrefu, tunawaona hali zao zinabadiika mara moja wanakuwa maisha yao yako duni kwa ajili ya pensheni zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri na jopo lake lote la viongozi wawatazame kwa kina Wanajeshi hawa kwa sababu wana kazi ngumu ya kutulinda sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukiwa tumekaa, tunakuwa tuko katika hali ya usalama na utulivu. Nafurahi wanajeshi akili zao zote zinakuwa wanakaa wanafikiria jinsi gani sisi tukae kwenye hali ya usalama. Wanajeshi hawa wanakuwa hawawezi kufanya chochote, maana wakati wakiwa kazini, mwanajeshi kama mwanajeshi hana muda hata kusema nitafute kiwanja nijenge nyumba, hana muda wa kukaa kufanya kitu chochote, ye ye akili yote yote akisikia kitu kidogo kimelia anakimbilia Kambini. Kwa hiyo, naomba wanajeshi waangaliwe kwa kina kwa sababu hata wakiacha kazi bado tunakuwa tunawahitaji. Pindi kikitokea chochote mwanajeshi yule akiwa yuko nyumbani anakuwa yuko mstari wa mbele, akisikia jambo limetokea katika nchi yake hukimbilia kazini na kuja kutulinda. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kwa kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, Wanajeshi awaangalie kwa kina pamoja na Serikali Kuu. Naomba Wanajeshi pensheni

zao zifikiriwe sana, waongezwe pensheni hizo. Pia pensheni zao Wanajeshi wanaapewa kila baada ya miezi sita. Miezi sita ni mingi. Kila mwezi sisi tunapewa mshahara na pia hautukidhi mahitaji yetu sisi Wabunge. Je, mwanajeshi apewe pensheni kila baada ya miezi sita? Naomba muda huu upunguzwe angalau wapewe kwa muda wa miezi miwili na pia pensheni hizi ziwafuate katika Mikoa yao, wasizifuate wao kwa sababu wanapozifuata zile pensheni wanatumia fedha nyingi sana kwa kusafiri na kwenda kuzifuata zile pensheni mwisho wa habari wanakuwa wao hawajabakia na kitu chochote cha kuwakidhi mahitaji yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii tena nielezee sehemu ya maeneo ya jeshi yaliyochukuliwa na wananchi. Kweli Mheshimiwa Waziri, maeneo yenu ya majeshi yamevamiwa na wananchi wetu. Lakini je, nauliza hawa wananchi ni wetu, tayari wameshavamia, wamejiimarisha, wamejenga, wamelima, wamejenga nyumba zao za kudumu: Je, wananchi wetu hawa Watanzania wenzetu tutawapeleka wapi tukiwafukuza? Naomba Jeshi na Waziri na Serikali Kuu, watazame kwa kina suala hili, wananchi wakati walipovamia, Jeshi lilikuwepo na sheria hii hawakuitilia mkazo, waliwaachia. Naomba sana wananchi hawa wafikiriwe, maeneo hasa kwa Zanzibar yapo, naomba Jeshi watafute maeneo mengine waende wakafanye mafunzo yao ya kijeshi. Mafunzo tunakubaliana nayo kwa sababu bila ya mafunzo hawawezi kutulinda, bila ya mafunzo hawawezi kupigana vita, hata mchezo *netball* kama hakufanya mazoezi hawezi kucheza mpira vizuri ukashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani nakumbuka wakati majeshi walikuwa wanasema wanakwenda *manouver*, majeshi wale walikuwa wanaondoka mijini wanakwenda shambani kijijini mbali, hatuwaoni isipokuwa tunawaona tu kwenye magari yamepambwa majani na wao wamejipamba majani kila mahali, hatujui hata wanafanyia wapi hayo mafunzo, hata mizinga hatuisikii. Lakini hivi sasa mko katikati ya vijiji vyetu nataka kusema jambo lililotokea tarehe 8 Julai, 2010 siku ya Ijumaa katika Jimbo langu, kijiji cha Unguja Ukuka Ebona chuma kikubwa sijui ndiyo bomu, sijui ndiyo mzinga umepigwa na majeshi, umeruka umekwenda kwenye nyumba, umepita kwenye dari, umechoma, umeingia mpaka ukumbini pamechomeka chini kimezama: Je, angekuwepo mtu, chuma kile jamani, angebakia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu alikuwa barazani mama mmoja akaanguka, akapata *pressure* akapoteza fahamu, akalazwa hospitali, jana katoka. Naomba sana Wizara ya Ulinzi iangalie sana maeneo yaliyokuwa yako karibu na watu, halafu pia tunafikiria wanajeshi wanapopiga shabaha huwa wanataka zielekee baharini. Jamani katika Kijiji changu mie yanapoelekea mabomu hii mara ya pili hakuna bahari pale, vinaelekea kwenye vijiji vya makazi ya watu. Naomba sana chondechonde leo imevunjika nyumba, mara ya mwanzo ulibomoka mlango, mara ya tatu akija akifa mtu yatakuwa yanazungumzwa mengine. Kusema kweli thawabu, mtu akifa hakuna fidia ya kumlipa, hakuna fidia ya roho. Nyumba mtajenga, ukumbi mtatengeneza, lakini fidia ya roho, hakuna. Nawaombeni tukae tulitazame kwa kina hilo jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hili lililotokea juzi yule mama kapata mshtuko, kapelekwa hospitali, wametumia gari, wamelipa pesa, yule mama kalazwa hospitali,

jamaa zake wameshtuka, wametumia pesa nyingi, wengine pia wamekwenda kumwangalia kutoa pesa ya taxi. Naomba huyu mama alipwe fidia na yule aliyeboomokewa nyumba alipwe fidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa napenda kuelekea kwenye hao Wanajeshi wenye. Katika Jimbo langu, kuna Kambi ya Jeshi, lakini maeneo wanayoishi nyumba zao pamoja na ofisi wanazofanyia kazi ni chakavu mno. Mwanajeshi anatoka kambini, yeze mkubwa wa kambi eti *CEO* akitoka Kambini anaporudi nyumbani watu wote wanamfuata pale, *Wallah* haikidhi, haina viwango hata ya kukaa yeze. Naomba sana nyumba za majeshi zifanyiwe ukarabati, ziangaliwe angalau na wao wakirudi katika kutulinda sisi wakifika pahali wajisikie na mimi nimeonekana na Wizara yangu angalau naishi pazuri. Pia napenda kwenda kwa haraka kengele isinigongee.

Napenda kuelekea upande wa wanajeshi. Kama nilivyosema awali, wanajeshi hawa wakati wakiwa kazini wanakuwa hawana muda wa kukaa pale nyumbani, labda mwanajeshi katoka Zanzibar akishapata kazi anakuwa anapangiwa pengine Mwanza, Musoma kila mahali, hajui viwanja vinatolewa wapi, nilikuwa naliomba Jeshi liwafikirie sana hawa wanajeshi kuwajengea nyumba, halafu wapewe mkopo nafuu wakiwa wanakatwa katika mshahara wao, ili wakati wanapostaifu *at least* wanakuwa na nyumba ya kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kabla kengele haijanigongea, naogopa, nzungumzie kidogo kuhusu wanajeshi wa Jeshi la Wanamaji wa Baharini. Jamani wajeshi wanamaji, kidogo mmewasahau. Bahari ni yetu, bahari ni moja katika maeneo muhimu sana ya nchi yetu, kweli mambo sasa ya kiharamia, ugaidi unakuja sana. Viboti vidogo vidogo jamani vingalawa vinachukuliwa na magaidi, maharamia, watu wanauliwa wakiwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki halali. Naomba jamani Navy, wanaita Jeshi la Wanamaji kwa sababu shughuli zao ziko majini zaidi. Wanatakiwa watulinde, meli kubwa kubwa zinapita ndani ya bahari zetu, zinaharibu mazingira, wanamwaga mafuta machafu, bahari zinachafuka, samaki wanakunyuwa yale mafuta, wanakuwa wale samaki hatari kwa matumizi ya binaadamu. Naomba wanamaji jamani msikae ofisisi, mtafute vifaa vya kuranda ndani ya bahari zetu, mtulinde mpaka ndani ya bahari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kuwatetea wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki ambao Kambi yao iko Buyu. Wananchi hawa maeneo yao yalichukuliwa, majumba yao wanayoishi yamo ndani ya uzio wa Jeshi ambao ulichukuliwa mwisho walikuwa walishajenga, lakini pia waliaidiwa na Mkuu wa Kambi kama watalipwa fidia, mpaka hii leo wenye mashamba hawajalipwa fidia hiyo, wala wale wenye nyumba zao zilizokuwa ndani ya eneo la jeshi hawajalipwa. Naomba walipwe fidia zao ili waende wakatafute viwanja vingine nje ya pale wapate kujenga. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ananisikia, Serikali Kuu inanisikia, wananchi hawa kilio chao ni kikubwa na kiko muda mrefu, naomba nitakapomaliza kama nilivymwomba Mwenyezi Mungu ajalie yakubaliwe yote na hilo likubaliwe na lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena katika Jimbo langu, nasisitiza Kambi ya Ubago chakavu sana, inatajwa kambi nzuri, kubwa lakini majengo yake hayaniridhishi hata mimi Mbunge nikienda pale, Ofisi ya Mkuu wa Kambi, najisikia vibaya kwa sababu iko giza utafikiri tunaingia kwenye handaki. Haidhuru jeshi, lakini ile ofisi haikidhi kiwango cha kuwa ya Mkuu wa Kambi. Hata ninapokwenda na wenzangu naona haya kidogo. Kwa hiyo, naomba katika Kambi zote zitakazotengenezwa, lakini mwanzo ianze Kambi ya Ubago iliyoko katika Jimbo la Koani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Andrew Clement. Nakushukuru sana kwa mchango wako, unalijua jeshi kweli ingawaje hukutuambia unahusiana vipi hasa na yule mama ambaye alipata *shock*. (*Kicheko*)

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana leo kwa kupata fursa hii adhimu ya kuchangia katika Bunge hili. Leo ni mara yangu ya kwanza natoa sauti katika Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, naomba uniruhusu nitoe *Asallam Aleikum*.

Pia naendelea kuwashukuru wanachama wote walionichagua katika Jimbo langu kwa kura nyingi, tumeweza kupata Jimbo vizuri sana la mabadiliko *faster*. Nawashukuru pia viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi kwa kulipitisha jina kwa nguvu zote na hatimaye kushinda kwa kishindo, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchago wangu unagusia katika kuendeleza usalama wa nchi yetu. Baada ya matukio yaliyotokea Mbagala na Gongo la Mboto nina wasiwasi sana na Kambi ya Migombani iliyoko Zanzibar iko katikati ya mji na tunaweza tukapata matatizo kutokana na matukio yaliyotokea katika Kambi hizi nilizozitaja awali. Kwa hiyo, napendekeza ikiwezekana basi tuangalie upya namna ya kuweza kuhamisha Kambi ile ambayo iko katikati ya mji tukaweza kuiweka mbali na sasa hivi ni wakati muafaka kabisa kwa ajili ya hilo. Kwa sababu pale Zanzibar nako kuna matatizo ya kuendeleza Wizara za Zanzibar kwa maana zilipo zinajibana sana, kwa hiyo, eneo lile likipatikana ninaamini kabisa Wizara na Serikali zote tunaweza tukapata mji mpya wa Serikali na Kambi ikasogezwa sehemu ambayo itakuwa muafaka kwa nchi yetu. Naomba hili litazamwe kwa upeo mkubwa sana na tuweze kuweka mazingira yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka nichukue fursa hii pia kuwapongeza wanajeshi wetu kwa kutulinda vizuri sana, kutetea nchi vizuri sana, lakini pia tuna haja ya kutazama hii bajeti ambayo inaletwa kwetu kwa kutaka fedha nyingi sana kwa ajili ya kununulia vitu vyta ulinzi. Mimi nilikuwa napendekeza sana kwamba tuangalie Sheria yetu ya Manunuzi ambayo inatukataza tusinunue vyombo ambavyo vilishatumika.

Katika vyombo vyta Jeshi, mimi naamini kifaru kimoja pengine kinaweza kikafika hata dola milioni tano, lakini leo kuna vifaru viko Ujeruman, Ufaransa, nchi za Ulaya vimekaa vinatolewa siku ya ukombozi tu, baada ya pale havina kazi tena. Naamini vifaru

vile kama tukinunua kwa ajili yetu sisi tutakuwa na vifaa vya kisasa vinavyokwenda na wakati bado, kwa sababu wenzetu wao wako katika kubuni mitambo mipyka kila siku.

Kwa hiyo, hili nafikiri kwa upande wa jeshi litazamwe vizuri sana kuona kwamba tunaweza kupunguza bajeti yetu kwa kiasi gani kwa kununua vifaa ambavyo vina ubora na vizuri vinaweza vikalinda nchi yetu bila ya matatizo yoyote. Naamini pesa zile tutakazozi-save kwa kuititia utaratibu huu, zinaweza zikasaidia sehemu ya afya, sehemu nyingine za elimu, kwa hiyo napendekeza sana haya mambo mawili yatazamwe kwa upeo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea sana kushukuru kupata fursa hii na *inshaallah* tutashirikiana pamoja. Sina zaidi ila ni hayo tu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi kwa kutotoa tamko langu, naunga hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsanteni sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim Hassan Turky. Namwita Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga. Mheshimiwa Yahya Kassim Issa simwoni, Mheshimiwa Lucy Mayenga hayupo pia. Namwita Mheshimiwa Masoud. Anayekuwa hayupo ajue kabisa nafasi hiyo haijirudii tena kwa sababu mjadala huu ni wa leo tu.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nami naungana na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, makamanda wote na wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kusema kwamba Sheria ya Ulinzi wa Taifa ni ya zamani tangu mwaka 1966, imepitwa na wakati. Nimeshuhudia mabadiliko makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia, lakini hadi sasa sheria hii bado haijafanyiwa marekebisho. Mwaka 2008 Waziri alituambia kwamba Kamati imeundwa na ripoti yake ilikamilika, italetwa Bungeni. Miaka mitano sasa hakuna ripoti ambayo imeletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mipaka *beacons* tumekuwa tukipiga kelele mara nyingi. Tumekuwa tukihoji kwamba moja ya kazi ya Jeshi ni kulinda mipaka, lakini mpaka wa Tanzania, Tarime na Migoli Kenya ambapo *beacons* zake ziliondolewa katika vijiji vya Panyako, Ronche na Ikoma hadi leo hatupati ufumbuzi wa aina yoyote. Sambamba na hilo, Tunduma nako Tanzania na Zambia kuna *beacons* zimeondolewa. Lakini sijui Mheshimiwa Waziri akija atuambie kwamba *beacons* hizo ni lini zitawezza kurekebishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye JKT. Serikali imekuwa ikisema mara nyingi kwamba ina dhamira nzuri ya kuchukua vijana JKT ili kuleta maadili mazuri na

uzalendo, lakini mwaka 2010/2011 JKT ilitengewa shilingi bilioni 12.6, mwaka 2011/2012 JKT imetengewa shilingi bilioni 3.1. Serikali inapokuja na maelezo yake ikawaambia Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba maadili yamepungua, uzalendo umepungua lakini kuna upungufu wa shilingi bilioni 9.5. Serikali ina dhamira ya kweli ya kuchukua vijana wa JKT? Serikali iseme wazi kwamba mkakati huu kwa Serikali haupo na umefeli kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nipate ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa wakati wa majumuisho, *National Defensive College* ya Kundushi imekamilika. Chuo hiki kitaanza kazi lini? Je, upande wa pili wa Tanzania, yaani Zanzibar utashirikishwa kiasi gani juu ya vikosi vya *SMZ, KMKM* na wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali za wastaafu ni mbaya sana. Wastaafu wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na hasa wale ambao walishiriki katika vita vya kagera mwaka 1978/1979 ni mbaya kulingana na vyeo vyao walivyokuwa navyo. Utumishi waliotumikia nchi hii, kazi walioifanya na leo hii ukiwaona inasikitisha. Tumekuwa tukizungumza mara nyingi ni kiasi gani Serikali inawatambua hawa, ni kiasi gani Serikali inawathamini hawa, lakini kwa bahati mbaya sana Serikali kila siku imekuwa na maelezo ambayo bado hayaendani sambamba na kupatikana kwa haki zao au kuboresha maisha ya wastaafu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Julai, 2011 tutakuwa na siku ya mashujaa. Taarifa tulioiona kwenye Vyombo vya Habari, sherehe za mashujaa zitakuwepo Mtwara, Naliendele sehemu ambayo tumezika hao mashujaa. Tumeondo mifupa kutoka Msumbiji tukawaenzi pale kwenye ardhi yetu, lakini niiulize Serikali, hivi familia za hao mashujaa inaziangalia vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haipendezi hata kidogo. Muda mwingi wakati wa mashujaa wetu au wastaafu, atakapofariki kutakuwa na risala nzuri la kutoa machozi, kwamba Marehemu alikuwa hodari, shupavu na jasiri, mwaminifu na mtiifu, yeze ni mfano wa kuigwa, Marehemu atakumbukwa, atathaminiwa kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hajathaminiwa akiwa hai, ndiyo mtamthamini ameshakuwa kaburini, ameshazikwa! Hasikii kitu, yeze kule ni Marehemu. Leo tunaonyesha mifupa huko Msumbiji tunakuja kuzika hapa Tanzania kwa heshima, lakini msoma risala anatokwa na machozi kuonyesha kwamba anawathamini. Siyo kweli, hatuwathamini, kwa sababu walipokuwa hai kumbe muda mrefu tuliwatelekeza, hatukuwathamini na hali zao za maisha ni mbaya. Sasa risala ya kusema kwamba atathaminiwa na atakumbukwa kwa kazi nzuri aliyoifanya, jamani hamsaidii kitu kaburini maana yake mnasema mnamthamini. Alishazikwa huko hasikii lolote, watoto wake, familia yake umasikini umewazidi, wao ni wengine? Serikali lini itasikia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisema hapa kwamba Serikali tunasema ni sikuvi, imesikia kilio, basi mimi niliposema juzi, nikasema tafuteni basi hata *tissue* kwa maana kwamba mfikirie fikirie kidogo, Spika akaniambia *tissue* za nini? Zitapotea mara moja! Sasa mara hii sijui tafuteni kitambaa kikubwa hivi mfute machozi, maana

hamwafikirii, familia za wastaa fu, familia za marehemu waliokufa ambao tunakwenda kuadhimisha sherehe hii kuwakumbuka mashujaa wetu Naliendele, Mtwara. Nasema ziangaliwe kwa makini sana, ziko taabani kupita kiasi. Waziri ni msikivu na kwa jinsi alivyotulia pale anavyoniangalia, hee, mambo mazuri kweli leo. Hilo lilikuwa ni la tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yenye mgogoro ya Jeshi la wananchi, yamegusiwa na wengi na hili ni jambo kubwa. Tangu mwaka 2007 ukiangalia taarifa ya utekelezaji wa Serikali kwenye kitabu kile unakuta kwamba Serikali iliahidi itayapima maeneo yenye migogoro ya ardhi na wananchi, itatathmini, itatoa fidia na waliandika kwenye kitabu chao, naomba niwaambie haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Oldonyo Sambu JWTZ - Arusha, *Kunduchi Referal Range* - Dar es Salaam, Bulombola JKT - Kigoma, Buhemba JKT - Mara, Chita JKT - Morogoro, Makutupola JKT - Dodoma, Maramba JKT - Tanga, Mlale JKT - Ruvuma, Rwankoma JKT - Mara, Tunduru TPDF - Ruvuma, Umoja Camp JWTZ - Mtwara, Serikali ituambie sasa kilichoandikwa mwaka 2007 na 2008 kwenye vitabu vyao vya taarifa za utekelezaji wa Serikali. Mliwadanganya wananchi na sisi Wabunge mlitudanganya. Mliahidi kuyapima, kutathmini na kutoa fidia, leo kuna maeneo mengine yamechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii migogoro tungeipunguza. Tuangalie kwa makini sana wananchi wanapolalamika, basi kile kilio chao basi tukisikilize na tukipatie ufumbuzi wa kudumu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atueleze sasa ana mpango gani wa kuyapitia upya, kuyapima, kutathmini na kutoa fidia maeneo haya pamoa na lugha nyingi mara nyingi ambazo tumezizoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wanajeshi yamekuwa yakiendelea kwa kasi, michakato, mipango kabambe, nia ni njema, usikivu wa Serikali tunalipa madeni. Lakini bado yapo yanaendelea na Serikali imeahidi hapa kwamba itayalipa. Lakini ni vyema sisi tuseme tu kwamba ukiangalia bajeti iliyopo na kama kuna kifungu ambacho mtalipa madeni ni jambo jema. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie ni kiasi gani cha fedha kimepangwa kwenye bajeti hii kulipa madeni ya wanajeshi na wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uajiri kwenye jeshi la Wananchi wa Tanzania unalalamikiwa kwenye maeneo mengi na Mikoa mbalimbali, hauko wazi. Taarifa zinapelekwa Mikoani au Wilayani, lakini kunakuwa na malalamiko makubwa. Kwa msingi huo basi, naishauri Serikali iandae mazingira na mikakati yake iliyo mizuri kuangalia ni namna gani ya kutoa elimu kwa wahusika ambao tunakwenda kuwaambia kwamba umefika wakati tuajiri vijana wa aina gani na sifa zao. Tutoe elimu mapema. Watu wanasikia tu kwamba Jeshi linaajiri, lakini hawaelewi utaratibu ulivyo. Kuna malalamiko makubwa na hasa kule Zanzibar ambapo mimi natoka inawezekana ukasikia kwamba jina liliandikwa, lakini baada ya hapo unasikia hakuna taarifa nyingine yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kupata ufanuzi ufuatao: La kwanza, Kiwanda cha Kutengeneza Dawa cha Binadamu Tanzania Siyo ambacho kiliingia ubia na *Whole Group* ya China. Je, kimepata faida kiasi gani kuanzia mwaka 2009 hadi 2010 na hadi Juni mwaka 2012?

La pili, naomba kupata ufanuzi kuhusu kiwanda cha kushona sare za wanajeshi za Kamisuma: Je, kimepata faida gani au hasara kiasi gani kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2010, 2010/2011 Juni?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *Command* ya Navy Kigamboni. *Command* ya Navy Kigamboni imesahauliwa, imekuwa yatima na uharamia unaongezeka. Lakini jamani mafuta mnayotoa ni kidogo sana. Boti tulizonazo zina uwezo kwa kiasi fulani. Lakini je, ni kwa nini muda mrefu mnakuwa mkisuasua kuipatia *Command* ya Navy Kigamboni mafuta ya kutosha kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi na hatimaye baadhi ya boti hizi zinaharibika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na usikivu wako ulivyokuwa mzuri, naomba utakapokuja hapa, na jinsi leo unavyocheka cheka sana nakuona, utoe maelezo ya kina ni kwa nini mnasuasua kutoa mafuta haya kwa *Command Navy Kigamboni?* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa jambo la mwisho dogo ambalo wananchi wamenitura niulize. Katika jambo ambalo kiasi cha miezi nane iliyopita kulikuwa na orodha ambayo ilitakiwa kwa wanajeshi wote walioshiriki vita vya Kagera, wakaorodheshwa katika maeneo mbalimbali, Bara na Visiwani. Lakini hadi leo hakuna maelezo yoyote, mliwatia tamaa kweli kwamba pamoja na kazi ngumu waliyoifanya, basi kuna angalau jambo lolote. Lakini ukimya na usiri uliokuwepo hadi leo ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa awaeleze wale wote waliorodheshwa walioshiriki vita vya Kagera, basi ioneckane kwamba kuna majibu yaliyo mazuri na sahihi. Baada ya maelezo hayo mafupi na jinsi ya utulivu wa Mheshimiwa Waziri, namwamini kwamba atakapokuja hapa kufanya majumuisho, basi nina imani atatoa majibu yaliyo mazuri na ya kufurahisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mie kutoa kidogo maelekezo yangu kwa Wizara hii nyeti. Kwanza tuwashukuru sana wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa nidhamu kubwa na nzuri wanayoionyesha na wanayoendelea nayo hadi leo. Ni askari wa kupigiwa mfano siyo kwa Tanzania tu, lakini hata kwa Afrika. Baada ya kupata taarifa zao wanaposhiriki katika mazoezi ya pamoja ya SADC na sehemu nyingine

wanazopelekwa. Lakini kila kilicho chema lazima kitunzwe. Askari wetu ni binadamu kama sisi.

Jeshi la Wananchi wa Tanzania halina *Trade Union*, walimu wataingia barabarani, madaktari watadai nyongeza, wanafunzi watagoma, lakini kutokana na nidhamu na Sheria za Jeshi au Polisi ni mwiko wao kufanya hayo yanayofanywa na wenzao. Sasa wapi tegemeo lao? Tegemeo ni sisi Wabunge kuwatetea na Serikali kuwapa haki zao. Nzungumzie ajira kwa upande wa Zanzibar. Askari wa Zanzibar wanapokwenda kusailiwa wabakie kusailiwa na kupata vyeti vya kuijunga katika Kambi za kusomea mambo ya kijeshi bila kuja kufanyiwa usaili wa pili upande wa pili wa Bara. (*Makofi*)

Lazima kuwe na *quarter* ya Wazanzibar kama ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, kwa sababu viwango vyao vinaeleweka kwamba ni vya chini kuliko vya wenzenetu. Washindanishwe wao kwa wao wapimwe Zanzibar, wakija huku iwe tayari ajira ni yao. Hilo moja. Hata idadi ya maofisa ambao wanapelekwa Chuo cha Monduli kutoka Zanzibar ni lazima washindanishwe wenyewe kwa wenyewe, Wasishirikishwe Wazanzibar na upande wa pili wa Muungano kwa sababu idadi yao inapungua ya kusomea nafasi ya uofisa katika Chuo cha Monduli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *ration allowance* tumeipigia kelele kubwa sana katika Bunge hili, Sh. 5,000/= ni ndogo. Wanajeshi wanakula, lakini kula ya mwanajeshi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa, wanatakiwa wawe wanakula *calories* maalum kutokana na kazi zao na mazoezi yao. Sasa *diet* ile haiwezi ikapatikana kwa kumtengea Sh. 5,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, kama haiwezekani, kuwe na *supplement budget* ya kumwezesha askari Mwanajeshi au Polisi kuzidishiwa fedha zao kutoka Sh. 5,000/= hadi Sh.10,000/= ili wafikie viwango vya *calories* zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulipwa haki zao kwa likizo na uhamisho ni jambo la lazima. Lama fedha hazipo, wasihamishwe. Kama fedha hazipo, wasipewe likizo. Likizo ni kumpumzisha mtu baada ya kazi ngumu. Unampuzisha aende nyumbani au aende kwa wazazi au aende Mkoa mwingine wakati hana fedha mkononi, anakwenda kupumzika vipi huyu askari? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, likizo zao ziambatane na cheki zao. Kama hakuna cheki, wasipewe likizo wala wasipewe uhamisho. Inasemekana kwamba zimetengwa shilingi bilioni 49 kwa bajeti iliyopita ili malimbikizo ya askari wetu hawa, ya likizo, uhamisho, na wazabuni waweze kupewa kwa wakati. Tunaomba fedha hizi kabla ya tarehe ya 31 ya kufunga Bunge hili askari wetu wa Jeshi la Wananchi wawe wote wameshapewa haki zao za fedha hizi zilizotengwa na kama siyo hivyo, hapakaliki, tutaondoka na Siwa leo, siyo shilingi tena. (*Makofi/Kicheko*)

Kuna nchi moja...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, hairuhusiwi hiyo.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi moja Mbunge aliondoka na Siwa akaenda akakaa nalo Kijijini huko. Siitaji nchi gani, lakini ni hapa hapa Afrika. Ikawa kuna *negotiation* baina ya Serikali na Spika. Kwa hiyo, hapa sasa sisi hatutazuia shilingi, Sanya atatoka na Siwa leo kama askari hawajapewa haki zao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha hizo shilingi bilioni 49 zilizotengwa siyo fedha za kulipia likizo na uhamisho. Lakini kuna fedha za *utilities*, umeme, maji nao walipiwe ili wapate umeme na maji katika maeneo wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni nyumba za kuishi. Katika hiki kitabu leo angalau nimepata afueni kuona kwamba kutakuwa na mkataba au kuna mkataba na Serikali ya China ya mkopo wa ujenzi wa nyumba 10,000 upatao dola milioni 300. Lakini isiwe kwa maneno, tuone kwa vitendo Wachina wanakuja kujenga hizi nyumba. Kwa nidhamu ya askari ni kukaa Kambini. Askari akikaa uraiani ni matatizo, ni gharama hata kwa Serikali. Umtafutie usafiri, hakuna usalama wa kutosha kwake yeye, kwa Kambi na kwa nchi. Askari abakie katika Kambi yake. Kwa hiyo, nyumba za kuishi zitapunguza gharama za usafiri na kuongeza nidhamu kwa jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wamepelekwa kwenda kulinda usalama wa amani kwa mataifa mengine kama vile Darfur, Lebanon. Ninachosisitiza hapa, askari asiondolewe kwanza bila ya kuwa na *life insurance*. La pili, haki zake ambazo anatakiwa azipate akiwa analitumikia Jeshi la Kimataifa ziwe zile zile haki ambazo zina mikataba baina yake na Serikali. *Wana-risk life* yao. Sio rahisi wala fahari kupelekwa Darfur, Lebanon, au kupelekwa mahali pengine *they risk their lives. We have to look after these guys*. Kila mara tukisema sungura ni mdogo, *we never grow up*. Hanenepi, na toka sungura ukimchinja hazidi zaidi ya nusu kilo. Sasa tu-jump kidogo tuwasaide askari wetu. (*Makofi*)

Mimi ninachosema askari waliopelekwa nje kwenda katika ulinzi wa amani haki zao wapewe. Tuwe tunapata ripoti wanaishi vipi huko. Wanakaa chumba watu wangapi? Wawe katika nidhamu ile ile ya kimataifa. Wasije wakatu-*under estimate* kwa sababu jeshi letu linatoka Afrika wakafanyiwa mambo ambayo ni kinyume na taratibu za kimataifa. Lazima tuwalinde na tuwaheshimu. Hii sehemu ya wanajeshi ni wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wanalipwa Sh. 50,000/= kwa mwezi. Hupewa mkupuo wa mshahara wa miezi sita, shilingi laki tatu, ni danganya toto. Hivi unamlipa mtu Sh. 50,000/= kwa mwezi ale siku ngapi? Wanapata Sh. 50,000/= kutokana na ile mishahara ya wastaafu wa zamani ilikuwa ni midogo. Sasa ukifanya *calculation* ya 80% ya mshahara wake ili apate posho yake ndiyo inakuja Sh. 50,000=/. Lazima Serikali sasa iangalie kwamba hivi viwango vimepitwa na wakati hasa ukizingatia na hii *inflation* tuliyokuwa nayo. (*Makofi*)

Leo askari unamlipa Sh. 50,000/=, kama anakula kama inavyotakiwa, kula binadamu ina maana atakula asubuhi, mchana na usiku na kinachobaki usiku akiweke ale asubuhi siku ya pili, hana pesa tena. *What about that twenty nine days zilizobaki katika mwezi? Angalau ku-jump kutoka hapa tuwafanyieni Sh. 150,000/= aweze ku-survive kwa Sh. 5,000/= kila siku. What is fifty thousand? Tujiangalie sisi Wabunge. Kama Mbunge analipwa Sh. 50,000/= hapa kwa siku moja, sikwambii kwa mwezi, una-survive vipi? Hali kama hii: sembe bei gani? Nyama bei gani? Samaki bei gani?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kukutana na askari mstaafu, ananiambia mimi nyama nakula mwaka mara mbili, siku kuu ya Iddi na siku kuu ya Mfungo Tatu. Huyo ambaye amelitumikia Taifa hili hana pa kwenda, hakuna wa kumsaidia.

Sasa mimi ninatoa rai moja, hawa askari wastaafu kwa kila *Zone* zao wapeni mikopo waweze kufanya kazi ndogo ndogo. Askari wastaafu wa Dodoma wapeni haya matrekta mliyoleta waingie Makutopora, wazalishe pale, wazalishe zabibu, wa Morogoro watazalisha mpunga, wa Zanzibar watafutieni boti wavue samaki. Nabii Issa alisema: “Mtu usimpe samaki, mpe mshipi na umfunze kuvua samaki.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata tukiwazidishia posho ikafika laki tatu, bado hatujawafanya kitu. Wako watu wana uwezo, hatuwezi tukasema kwamba hawa watapata ajira mara ya pili katika Serikali yetu kwa sababu umri wao umekwisha. Lakini kuna watu wana uwezo wa kufanya kazi katika Jeshi hili amba ni wastaafu. Tunaweza tukawajengea mazingira askari wale wakafanya, wakaweza hata kujikimu kwa kupata chakula chao cha kila siku. Tuwe na *data base* ya wataalam katika Jeshi ili tuwatumie wanajeshi hawa waweze kuzalisha na kusaidia jamii. (*Makofi*)

Mimi sikatai kwa Wizara hii kuchukua mkopo wa matrekta kutoka India, na mkopo ule umeingiwa mkataba kwa dhamana ya Benki Kuu ya Tanzania na *Exim Bank* ya India, wala hakuna mtu wa kati hapa. Lakini mnautumiaje mkopo huu? Matrekta haya mnayapeleka wapi? Anzeni kuyatumia wenyewe katika maeneo ambayo mnawenza mkazalisha. Wamekopeshwa matrekta ya *40 million dollars* na wakapewa *grace period* ya *five years* wasilipe kitu, *the next fifteen years* wanalipa only 1.5 percent is nothing in business. Nendeni mkaone Jeshi la Jordan, nendeni mkaone Jeshi la *Egypt*, wakati wa amani wanapewa *contract* kubwa kubwa, wanajenga majumba, wanajenga madaraja, wanafanya biashara za kilimo, kwa nini wasifanye wanajeshi? Sisi tuko katika amani. Msikunje mikono! Narejea tena kwamba Tanzania muwe na sifa ya kukopa, lakini muwe na nidhamu ya kulipa, basi, nchi itainuka kiviwanda na katika kilimo. Tukiwa waoga wa kukopa, basi tutabakia wadogo. Ndiyo pale *Bill Gates* alipomwambia Mheshimiwa Rais Kikwete kwamba unapoanza na kidogo unabakia mdogo. *You start with small, you will remain small.* Lakini ukianza na ukubwa unabakia kuwa mkubwa. Kwa hiyo, zidini kukopa lakini muwe na nidhamu ya kulipa. Miaka 15 kulipa kwa dola milioni 40 hata mimi naweza nikazilipa. (*Makofi*)

*If you are serious in business, yes, what is 40 million dollars. Leo Wachina wana fedha hawajui wazipeleke wapi! Wahindi wana fedha hawajui wapeleke wapi! Malaysia*

wana fedha hawajui wapeleke wapi! Sisi tunabakia na umaskini ati tunaogopa kukopa. Kopeni lakini muwe na nidhamu ya kulipa, msiwe waoga wa kukopa. (*Makofi*)

Matrekta haya sasa pelekeni *SACCOS*, wapeni Wabunge, pelekeni JKT, wapeni watu wazalishe ili tuone kwamba jeshi linainuka kiviwanda, Jeshi linainuka kiutendaji ili muweze kukidhi hizi haja ambazo Serikali hazifikii. Mtatoka kwenye Sh. 5,000/= siku zote tutakuwa tunapiga kelele ndani ya Bunge hili Sh. 5,000/= ndogo, itabakia ndogo kwa sababu hatuna mwamko wa kibiashara wa kuinua hii nchi. (*Makofi*)

Sasa wakopeeni bati na saruji kutoka India *very cheap*, wapeni mabati wanajeshi wakope angalau wawe na nyumba. Akiwa na njaa, lakini usiku kasitirika katika kibanda chake. Wapeni viwanja wajenge hawa wanajeshi. Leo wanajeshi wanatangatanga, wengine wanaiza madafu, wengine wanaiza karanga, *why?* Hawa wastaifu ilikuwa walipwe wapumzike kwa sababu wamefanya kazi nzito, lakini hata ukamwona mstaifu anadai kwamba asaidiwe ili akidhi hali ya maisha yake, ujue kwamba mambo yamemfikia shingoni. Lakini mstaifu alitakiwa apumzike. Kama sisi wanasiasa tukipumzika tunapumzika. Kwa nini wao wasipumzike? Kwa nini walimu wasipumzike, kwa nini Polisi wasipumzike? Wale ni binadamu vile vile. Nendeni mkawaone wastaifu *Egypt*, kaone wanajeshi wastaifu Jordan. Ni nchi za kupigiwa mfano. Wanazalisha, wanapata mishahara mizuri, lakini wanajengewa nidhamu ya kuwa na *future* nzuri. Watafutieni viwanja, wapeni mikopo ya bati, wapeni mikopo ya saruji, ili waanze kujijengea. Wajeengeni nyumba za rahisi, na kachukueni makampuni ya nyumba rahisi tumeziona. Yako Malaysia, yako Thailand, yako Bangladesh, yako Pakistan kama zinavyowajengea nchi za Uarabuni na sisi wanaweza kutujengea.

Mheshimiwa Naibu spika, nasisitiza sana na leo mko hapa na Mheshimiwa Waziri yuko hapa, ni lazima tuangalie haya. Kwanza Mheshimiwa Waziri, utuambie hizi milioni 49 kweli zipo na wenyewe watalipwa? Tena watalipwa haraka? Ziwaifikie kwa wakati ili waweze kuondokana na dhiki walizokuvanazo, waondokane na mashaka waliyokuvanayo. Hii Sh. 50,000/= ibakie historia. Tunasema, mwaka huu nitasamehe, lakini mwakani nikiiiona Sh. 50,000/= ndiyo hata kama wastaifu wako 1,000,000 mimi nasema nitaondoka na Siwa katika Bunge hili, ili ijulikane kwamba hawa Wanajeshi wanapewa haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia asubuhi hii katika Wizara yetu muhimu sana, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine, kulipongeza Jeshi letu kwa kazi ambayo wanafanya ya kulinda mipaka ya nchi yetu na kuiepusha na maadui na kuiweka tayari kwamba wakati wowote ambapo tunaweza tukavamiwa, Jeshi letu litakuwa liko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuwapongeza vijana wetu, *in uniforms*, walioko Darfur, walioko Lebanon kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kulinda heshima ya nchi yetu huko waliko. Jambo la msingi na la kusisitiza ni kuhakikisha

kwamba vifaa ambavyo wanajeshi wetu walioko katika *mission* hizi za kulinda amani, vinakuwa ni vifaa ambavyo ni vizuri na vinavyoendana na hadhi ya nchi yetu. Lakini pia nimepata taarifa kwamba kule Darfur, kuanzia mwezi ujao, Naibu Kamanda atakayeongoza Kikosi cha *African Union* kule Darfur atakuwa ni Kamanda kutoka Tanzania. Kwa hiyo, napenda kupongeza sana jambo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Ulinzi kwa hotuba yake nzuri sana. Ameongea vitu vizuri sana na ameonesha ni namna gani ambavyo Kambi ya Upinzani ilivyojipanga na kuweza kuhakikisha kwamba tunaisimamia vizuri Serikali. Lakini pia napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Ulinzi, kwa hotuba yake nzuri na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana tumekuwa tukizungumzia suala la kurejeshwa kwa JKT na Serikali imekuwa ikiahidi kwamba JKT itarudi. Lakini nimeangalia bajeti ambayo imepangwa kwa ajili ya maendeleo, *Vote 39, Development*, zimepangwa takribani shilingi bilioni tatu tu kwa ajili ya JKT. Tunafahamu kwamba ili hao vijana 20,000 waweze kuingia kwenye Makambi, ni lazima Makambi haya yasafishwe, yakarabatiwe, na kadhalika. Siamini kwamba shilingi bilioni tatu zinaweza zikatosha kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, nilikuwa napata wasiwasi kama kuna *commitment* ya dhati ya kuweza kuhakikisha kwamba JKT inarudi na inafanya jinsi ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unavyofahamu mara baada ya JKT kuwa imevunjwa, yaani imesimamishwa mwaka 1994, hapa katikati kumekuwa na vijana wengi sana ambao wanamaliza Kidato cha VI, wanamaliza Vyuo Vikuu na hawaendi JKT. Baadhi ya vijana hao, mimi nikiwemo, tumefanikiwa mpaka kuingia kwenye siasa na kuwa Wabunge, hatujapita JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba na ninatoa rai, nililisema hili mwaka 2006 halijafanyiwa kazi, naomba lirezewe kwamba vijana wote ambao ni viongozi wa kisisasa ambao hawakupita JKT, waandaliwe mafunzo maalum ya JKT kuanzia sasa. Hili lifanywe ndani ya mwaka huu, mara baada ya Bunge la mwezi Novemba, *voluntary*, wasilazimishwe, lakini *voluntary* wale ambao wanataka, mimi nitakuwa tayari, mara baada ya Bunge la mwezi Novemba, wiki nane vijana ambao wana nyadhifa za kisisasa waende JKT. Ni muhimu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kwa sababu ya vijana, Viongozi wa kisisasa wajue historia ya nchi, kuwa na ukakamavu, kujifunza mbinu za kijeshi na kuweza kujua ni mambo yapi ambayo yanapaswa kufanywa kama kiongozi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba hili lifanywe, liandaliwe na ninaamini kwamba itakuwa ni motisha kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ambao hawajakwenda JKT, wakiwaona vijana wanasiwa na magwanda ya JKT wanapiga kwata, *in-take* ijayo, vijana wengi sana

watajitokeza kwenda. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba hili liweze kuchukuliwa kwa uzito wake unavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Defence College*, hili ni jambo ambalo lilichelewa. Nchi kutokuwa na *National Defence College*, ilikuwa ni makosa makubwa.

Kwa hiyo, napenda nishauri kwamba mchakato wa *National Deffence College*, uweze kuharakishwa ili kuhakikisha kwamba watu waweze kujiunga. Nami nilishamwambia Mnadhimu Mkuu wa Jeshi kwamba, nitaomba rasmi katika *in-take* ya mwanzo kabisa *National Deffence College*, kwa ajili ya *Masters of Strategic Studies* niweze ku-join ili niweze kwenda na kujifunza na kuweza kuona ni namna gani ambavyo kama Mtanzania naweza nikailinda nchi yangu kupitia taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkuu wa Upinzani amezungumzia masuala ya *assets* au biashara ambazo Jeshi linafanya. Jambo hili ni jambo la kutilia mkazo sana. Majeshi mengi duniani yanafanya biashara. Mheshimiwa Sanya, ametolea mfano wa Jordan, ametolea mfano wa *Egypt*, yanafanya biashara. *Contracts* kubwa kubwa zote ambazo zinafanya *Egypt* leo, zimeshikwa na Majeshi. Lakini wanakuwa makini sana na aina ya biashara ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tumefanya makosa, tumejikuta tunaliingiza Jeshi letu katika shughuli za kibiashara, *deal* za kibiashara na makampuni *off show*, makampuni ambayo yanakuwa yameundwa kwa ajili ya kufanya wizi. Kumekuwa kuna ripoti nyingi sana, nilikuwa nasoma kitabu hapa cha Nicholous Saxon, *Treasure Islands*, kinazungumzia *off show companies* na namna gani ambavyo zinaiba kutoka Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1997 Jeshi letu liliunda Kampuni ya Meremeta. Kampuni hii ikaungana na kampuni nyingine kutoka Afrika ya Kusini, inaitwa *Trinex*, wakawa na 50%, 50%. Uchunguzi ambao nimeufanya umeonesha kwamba *Trinex* wala siyo Kampuni kwa ajili ya kufanya biashara, ni *Financial Adviser* ambayo kazi yake ni *ku-trot from one African Country to another African Country*, kutengeneza *deals* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarioti hapa, Namibia waliwafukuza *Trinex*. Sisi tukawakumbatia *Trinex*, wakaingia makubaliano na Meremeta. Wakatusabishia mkopo kutoka *NEDCO Trade Services* ya *South Africa*, ambayo ni kampuni tanzu ya *Ned Bank* ya *South Africa*. Mkopo wa \$10,000,000 takribani shilingi bilioni 16 kwa *exchange rate* ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi Meremeta wakashindwa kuzilipa. Baada ya Meremeta kushindwa kuzilipa, Serikali ikalichukua lile deni. Baada ya Serikali kuchukua lile deni, inapofikia wakati wa kulipa, tumeilipa *Ned Bank* ya *South Africa* dola 132,000,000. Tumekopa dola 10,000,000 tumelipa dola 132,000,000. Mheshimiwa Waziri, nitakupa barua ya Serikali ambayo ina-*confirm* huo mkopo kutoka *NEDCO*, ni

barua ambayo ilikuwa inakwenda *Deustche Bank AG* ya London, ambayo ni *Banker* wa *NEDCO Trade Services*, kwa ajili ya mkopo huo wa dola 10,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilifanya uchunguzi wangu binafsi nikawatafuta watu wa *Ned Bank*, kuwaliza, inakuwaje mtukope dola 10,000,000 tuwalipe dola 132,000,000 ambayo ni sawasawa na zaidi ya shilingi bilioni 216? Yaani kwamba, tunakopa shilingi bilioni 16 tunalipa shilingi bilioni 216. Mpaka sasa, hawajatoa hayo majibu. Lakini nitakupatia pia mawasiliano yote ambayo nimefanya na hao watu wa *Ned Bank*, ili uweze kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, rais aliunda Kamati ya Bomanii ambayo ilifanya uchunguzi kuhusiana na Sekta ya Madini. Katika *one of the conclusion* yake kuhusiana na suala la Meremeta walisema, Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya uanzishwaji wa Kampuni za Meremeta na *Tangold*, umiliki wa Serikali katika kampuni hizo na uhalali wa malipo ya dola za Marekani milioni 132, yaliyofanywa na Benki Kuu kwa Benki ya *Ned Bank* ya Afrika ya Kusini. Ripoti hii ilitolewa mwezi Aprili, 2008. Mpaka sasa hakuna uchunguzi ambaa umefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, baada ya kuwa *Treasury Registrer ame-list Tangold* kama sehemu ya Makampuni yanayomilikiwa na Serikali, tukaagiza, tarehe 8 Juni, 2009, nakumbuka tukamwandikia barua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba sasa fanya uchunguzi kuhusu *transaction* iliyotoka Meremeta, Benki Kuu na hawa watu wa *South Africa*. Mpaka sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshindwa kufanya huo uchunguzi kwa sababu amefanya mawasiliano na watu wa *Treasury Registrer*. Hamna lolote ambalo wamelijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tunajua, sisi ni wazalendo, tunajua kwamba kwa njia moja ama nyingine, kuna mambo ambayo Jeshi letu lilifanya ambayo labda hayapaswi kwenda kwenye *Public*. Mambo haya yanaeleweka na tunaelewa. Kuna kipindi hapa *tuli-offer*, basi Serikali iende kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge ika-explain suala hili. Lakini Serikali imekuwa kila siku inaweza jambo hili *under the carpet*. Lakini haliwezi kwisha bila suala hili kufanyiwa uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117, kama sijakosea, baada ya hoja hii kwisha, nitatoa hoja kwamba Bunge liunde Kamati Teule kufanya uchunguzi wa malipo ya dola milioni 132 kutoka Benki Kuu kwenda *Ned Bank* ya *South Africa*, wakati mkopo ambaa tulichukua kutoka Meremeta ulikuwa ni dola milioni 10 peke yake. Wala haitasadidua kusema kwamba jambo hili ni la usalama wa Taifa, haitasadidua kusema kwamba jambo hili ni la ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lisipopatiwa ufumbuzi, litaendelea kupaka matope Jeshi letu. Nasi hatuwezi kukubali Jeshi letu liendelee kupakwa matope, tunataka Jeshi letu liwe ni taasisi safi, taasisi ambayo haihusiki kabisa na ufisadi wa aina yoyote, taasisi ambayo Watanzania watakwenda nayo ikitokea nchi inapata matatizo yoyote. Tumeona nchi mbalimbali kwamba *we want to rely to our army!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba jambo hili liweze kupatiwa ufumbuzi wa mwanzo na wa mwisho. Lifanyiwe uchunguzi, tuone hizo *transactions* zilizofanywa ni kwa ajili gani? Kama kuna mambo ambayo ni kwa maslahi ya umma, Bunge lielezwe. Kama haliwezi kuelezw *in a plainary*, Kamati ya Ulinzi na Usalama ielezwe. Kama Kamati hiyo itakuwa ni kidogo sana, Kamati ya Uongozi ya Bunge, ielezwe. Hatuwezi kuwa miaka mitano tunazungumzia jambo moja, sisi tunasema hivi, Serikali inasema hivi, halipati ufumbuzi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kama nilivyosema, mwishoni kabisa, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, nitaomba Bunge lako liridhie, tuweze kufanya uchunguzi huu. Haiwezekani mabilioni ya fedha hizi za umma zipotee, halafu sisi wawakilishi wa wananchi tukae kimya bila kusema. Kwa hiyo, hayo ndio nilyokuwa napenda kuyazungumza. *JKT* irudi, Wabunge Vijana waingie *JKT* haraka iwezekanavyo. *National Defence College* iwe *fast track* na uchunguzi wa malipo kutoka Benki Kuu, uchunguzi wa dola milioni 132 kwenda *Ned Bank* ya *South Africa* kupitia kampuni yake tanzu ya *NEDCO* ambayo ni *off show company*, imesajiliwa Mauritius, uweze kufanya ili tuweze kulimaliza suala hili kwa kuwa na uchunguzi wa mwanzo na wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto. Nawashukuruni nyote. Maombi ni mengi, muda hautatosha wote kupata nafasi ya kuchangia. Kama tunavyojuua kwa ratiba tuliyonayo, Wizara hii itashughulikiwa leo na tunapaswa kuitendea haki zote leo.

Kwa hiyo, jioni nitawaomba Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Mariam Msabaha, Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Stephen Maselle. Yeyote atakayewahi katika hao, tutapata wastani wa wachangiaji wanne, baadaye Mheshimiwa Waziri na mambo mengine ya ratiba yataendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana, na hasa kwa maombi maalum ya kwenda *JKT* baadhi yetu, zile kalinye kalinye sijui kama mtaziweza! Sisi tulio pita huko tunafahamu mnaongea kitu gani. Ila sasa kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti, tunafikiria tu mkishatoka huko sasa, mkisharudi hapa ndani na buti zenu, kutakuwa salama? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusitisha shughuli za Bunge, hadi saa 11.00 leo jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, nitakayemwita kama hatakuwepo basi tutaendelea na anayefuata. Nilisema tangu asubuhi mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga. Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa!

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa mtu wa mwanzo kwa jioni ya leo, nakushukuru sana. Jeshi ni chombo kikubwa sana katika nchi na ndicho chombo ambacho kinastahiki kuwa na utaratibu mzuri, maadili mema na ndiyo sifa ya Jeshi letu lilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia mambo mengi lakini kama chombo cha Jeshi, chombo hiki haiyumkini kila raia anatakiwa kujua taarifa zake lakini ni vigumu sana. Hata hivyo, tuna wajibu baadhi ya mambo kuweza kuyaelewa, utaratibu wake hususani matatizo ambayo yanatukabili sisi tunaotoka Visiwani. Yako mambo kwa kweli yanatuathiri na kwanza napenda ninukuu kwa sababu katika kitabu hiki kili-base sana upande mmoja wa Muungano, kwa hivyo kwa kweli imenigusa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kunukuu, *Hansard* hii, nasema inatoka Serikalini kwa sababu majibu haya yanatokana na Naibu Waziri, nanukuu:-

*“Ni kuhakikisha kwamba tunaziba mianya yote ya upendeleo na kupata vijana wanaoandaliwa vizuri katika mafunzo ya awali ya Kijeshi. Nimebadili utaratibu wa awali wa kuchukua vijana, hivyo kuanzia Julai, 1, 2008 itaatiri vijana waliopita JKT na JKU”. Mwisho wa kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kunukuu sehemu nyingine:-

*“La kwanza, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba hatuna utaratibu wa kugawa Askari wetu kwa misingi ya huyu atoka Bara na huyu anatoka Tanzania Zanzibar”. Mwisho wa kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar tuna kilio kikubwa sana kuhusu ajira ya Jeshi na kilio hiki kitatufikisha mahali pazito na wenzetu tunajenga imani hata kukuamini hatujui mbele mna mawazo gani. Jeshi vijana wetu wanakuja kupimwa na hapa keshatamka kwamba tutachukua JKU, wanakuja wanapima vijana wetu, wakifika huku vijana wengine wanarejeshwa, wanasema wamefeli lakini walewale waliokujapima ndiyo walewale na huku wanawapima halafu ghafla wanasema kwamba wamefeli, afya yao, watatoa sababu ambazo hazina msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nina taarifa kamili, waliachwa vijana watano, siyo kwamba nasingizia, licha ya kwamba wao viongozi kwa sababu Jeshi letu kwa kweli limemilikiwa upande mmoja tu, Jeshi letu limemilikiwa upande wa Tanzania Bara, kwa Zanzibar kwa kweli hatuna uongozi, hatuna ubavu wa aina yoyote na hapa ndipo mie panaponitia mashaka. Vijana wetu wanapimwa, licha ya wale amba kwa kule

kuna viongozi wanawaita ndugu zao Tabora, Shinyanga, Dar es Salaam au sehemu yoyote nyingine na kuwapa fursa zile na ndugu zetu kukosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka vijana watano waliachwa, nikampigia mhusika akaniambia wao ndiyo wamekosa, ndiyo wamekosa hao. Sikutosheka, nikatafuta boti nikapanda nikaja mpaka Ngome, kufika Ngome namkuta kiongozi ananiambia Mheshimiwa ajira ngumu. Nikamwambia ajira ngumu lakini sitomalizikia hapa wapo wakubwa wako zaidi ya wewe. Nilikaa saa nzima ndiyo kupata jibu walau kwamba vijana wale walete, lakini ilikuwa siyo kwa sababu yoyote ili ilikuwa waweke ndugu zao. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linatuathiri, lazima Jeshi lichukuliwe JKT na JKU, ndiyo *Hansard* inavyosema au kama Serikali inakiuka, inatubadilisha mawazo, inabadili mawazo haya, *Hansard* hii, ituambie leo Serikali, nataka Waziri utujibu hapa, isiwe kisingizio ndugu zetu kuwachukua hapa kwenye JKT halafu mkatubabaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema tumeungana nchi mbili, watoke Zanzibar watoke Bara, hii ni hatari, nasema hii ni hatari Jeshi kutawala upande mmoja wa Muungano, hatari. Tumewaona wenzetu Sudan hapo Kaskazini na Kusini, Kaskazini waliingia Kusini kwa nini? Nchi moja hali hii, sisi tunavuka hapa tunasema Zanzibar, hapa hapakupangwa harusi ya kwamba zimeoana nchi mbili, hakuna nchi iliyoolewa na wala hakuna nchi iliyooa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizi zimekubaliana, tumekubaliana nafasi zote zitoke pande zote, vijana hawa kutokuwa sawa katika Jeshi letu mnaidhalilisha Zanzibar na nakwambieni, hakuna uhakika wa hatma ya Zanzibar, tunapiga kelele hapa Bungeni tu, hapa tunapiga kelele Bunge liko hivi, sasa hivi tunakwenda hivi, hapa vijana wetu mnawaona namna gani wanavyosusia shule, ina maana utaratibu umebadilika hivi sasa kimaisha, keshokutwa watakuja kutuambia hawa, kambi zote wametawala wao, kutoka sehemu moja ya Muungano wanakwambia sasa tunataka Serikali moja, mtafanya nini nyie, mtajikwamua vipi Wanzanzibari? Nasema Wazanzibari tuweni kitu kimoja kwa suala hili, kama tumekubaliana kuungana twende kwa njia ya kimungano. Hiki chombo hiki mimi sikukiamini hata nchi ukasikia juzi Waziri Mkuu kateuliwa lakini unaambiwa kwamba Jeshi lazima likubali na Jeshi likaridhia, je, Jeshi halikukubali ina maana kuna machafuko, sasa huo si utaratibu wa Muungano. Sisi tunasema hapa mnatuona kwamba sijui namna gani, tunasema kama kuna matatizo ya kiuchumi, ya kiutaratibu tukae chini tukubaliane lakini siyo kusema kwamba bila shaka uongozi wote, taratibu zote ziko sehemu moja, hili hatutaki, hatukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo hapa akasema kwamba labda sisi hatukusema bila shaka nchi, hatukudhamiria kwamba watu hawa tunawagawa siyo lengo letu na wala hatuna shabaha hiyo, shabaha yetu tunasema tujue hawa ni Wazanzibari, hawa watatoka Tanzania Bara, wanakaa pamoja, wanakula dempo pamoja, wanafanya shughuli pamoja, pana adui wanakwenda kwa pamoja, tunajua kwamba sasa nchi hii kweli Tanzania, kwa kila upande Askari wametoka. Leo wale pale, wakubwa pale, hebu anyanyue mkono aliyejikuwa katoka Zanzibar, anyanyue mkono aliyetoka Zanzibar, pale watu wameiva wote mabegani, kwani hatuna uwezo? Si kweli sisi tumepindua Serikali, kuna vijana

walikwenda Jeshi, hata kusoma hawakusoma, wakasoma ndani ya Jeshi na walikuwa wapiganaji wazuri Uganda hapo, walikuwa wapiganaji wazuri na wako vijana wenu walikuwa na imani wajipige bunduki na Mzanzibar kaenda kumwambia usijipige tusonge mbele twende utarudi salama, tunawajua mpaka leo wako hai, mnatuambia nini? Mnakwenda kozi mnasoma, kuna kijana mpaka leo yuko hai, kala diploma yake tu kakuta wale wana *Master*. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nakukumbusha kwamba kengele ya kwanza.

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** Nimekubali. Kwa hivyo, tunasema hali kama hii hairidhishi, kwamba Jeshi moja linakaa upande mmoja, leo Mzanzibari anakawa mgeni katika nchi yake! Nenda kambi zote nitolee kiongozi anayetoka Zanzibar, nenda kambi zote kwamba huyu kweli anayeongoza *brigade* hii, ama anaongoza hivi, mbona mnatoa adhabu kiasi kikubwa jamani, siye tumepindua, hatukupata kwa kalamu nchi. Wenzetu kalamu ndiyo iliyokusaidieni, sisi bunduki, mawe, mapanga ndiyo yaliyotusaidia. Hatuwezi kukubali uongozi kama huu, hatuwezi! Sasa nasema tunataka ushirikiano, JKU lazima waje waandikishwe Zanzibar, mnakuja na vifaa vyenu mnawapima, hawa wanafaa tusije sikia kijana anarejeshwa, mje na vifaa kamili, hili tunasisitiza kabisa, mwenendo huu tuhakikishe kwamba ndiyo unaofuatwa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu unapita kati ya Msemaji na Naibu Spika.

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** La mwisho, sasa dakika zangu Mheshimiwa zimepotea kidogo. Hivi sasa kuna utaratibu hasa niliowahi kuzungumza hapa kuhusu suala la Cheju, Cheju watu wamemiliki maeneo miaka 200, kama mapinduzi ni miaka 47 tu lakini kinyume chake sehemu zile zimetisha mipaka na kuonyesha kwamba wananchi sasa hawana haki, hili si suala nzuri. Mabango yale siyo kwamba yamekuja kwa mazungumzo baina ya wanakijiji na Jeshi hakuna, yamekuja kwa sababu wenzetu kwa kweli wakati mwingine wanatuonyesha ubabe sana. Unajua mtu akiwa Jeshi anaona labda yeye ile dunia kaivika yeye, siyo yako, walikuwa wangapi wako chini sasa hivi tunazungumza nao, wako wengine wanaziba mipira ya baiskeli sasa. Hii siyo hali nzuri kama sehemu Jeshi inataka, Jeshi ni letu, wananchi ni wetu, tukutaneni, tukae kitako tuzungumze eneo hili historia yake eneo ilikuwaje. Leo mnakwenda tia mabango tu kama sehemu ya Cheju, kuna miembe ina miaka mia, mapinduzi miaka 47 tu, leo unasema kwamba eneo hili la Jeshi, mimi sikumbuki hali kama hii, tusifanyeni hivi, hali hii italeta mzozo baina ya Wanajeshi na wanakijiji, pale penye matatizo tufuatilie, twendeni pamoja tukashughulikie. Wale wanawakala wao, wenyewe wapo, Wabunge wao wapo, wawakilishi wao wapo, kwa nini tusikae kitako tukazungumza halafu suala hili likajulikana kwamba kweli eneo hili ni la Jeshi au eneo hili la nani, kwa nini hatufanyi hivyo na wako wazee wanakumbuka, kabla ya mapinduzi wapo, kwa nini tusifanyi hivi, tunatumia nguvu tu, maana yake nini? Mimi nasema katika chombo ambacho chenye heshima kwanza Jeshi, najua mimi, niliwahi kupitia siku mbili, tatu. Katika chombo chenye heshima Jeshi, hata uende vipi ni mahali penye amri lakini sasa amri zile zisije mpaka kwenye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema mimi siwezi kuunga mkono mpaka majibu nipate kwamba Jeshi mtachukua JKU na JKT, kama maelezo ya Serikali yalivyosema au mme pangua kauli hii, hili nataka kulijua. Hili nielezwe na kama sikuelezwa hapa Wazanzibari wote nataka tuwe kitu kimoja kwa sababu hili siyo suala langu, hili ni suala la Kitaifa, la kizazi chetu kinachokuja baadaye, tunalinda kizazi chetu kisijepata matatizo hayo na tujue kwamba hawa ni Wazanzibari kweli na hawa ni Watanzania Bara. Hili bila shaka ni dhuluma, niliuliza hapa nikamwambia twende Makutopora, alikataa Waziri hapo, twende Makutopora tukahakikishe, hakukubali, kwa sababu ni kweli dhambi hizi zinafanyika. Kwa hiyo, naomba kabisa na si kuomba, yenye we ni haki yetu, sina haja ya kuomba, tuhakikishe kwamba suala hili linakamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, ahsante sana. (*Makofi*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) nasoma pamoja na Kanuni ya 64(1)(f).

**NAIBU SPIKA:** Zisome.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kanuni ya 68(7) inaeleweka sana, inasema:-

*“Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema nakuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge. Majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye au kadri atakavyoona inafaa”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(f) inasema:-

*“Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au kwa mtu mwingine yeyote”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naongeza (g), *“hatatumia lugha ya kuudhi na inayozalilisha watu wengine”*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge aliye kuwa akizungumza sasa hivi kabla ya mimi kwa mazungumzo yake karibu yote, kwa sehemu kubwa amekuwa akilishawishi Bunge hili, akiomba mshikamano wa Wazanzibari, dhana ya kuomba msimamo mmoja wa

Wazanzibar katika baadhi ya mambo inaashiria kupanda mbegu mbaya sana katika Taasisi kubwa inayoheshima kama hii. (*Makofi*)

Pili, kuonyesha kwamba Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama, yanateuliwa kwa upendeleo na kwamba kuna baadhi ya watu wenye sifa kwa mujibu wa maelezo yake ambao wameachwa kwa sababu tu ya kisingizio kwamba hawa wanatoka sehemu moja ya Muungano. Kauli hii ni kauli mbaya, ni kauli ya kuudhi na kwa kweli inapandikiza mbegu za ubaguzi na katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania hakuna upendeleo, hakuna viti vya dezo, sisi tuliopita kwenye Majeshi kule hakuna kura, ni sifa, haiangalii Wagogo wangapi wameingia, Wasukuma wangapi wameingia, wala Wamasai wangapi, tunaangalia mwenye sifa ya kujiunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema naomba Mwongozo katika maneno ambayo yanaashiria kudhalilisha nafasi za watu wengine, ukizingatia kwamba hata Waziri mwenye dhamana ya Ulinzi ni Mzanzibari, hii inaonyesha wazi kwamba Tanzania haina ubaguzi, kupanda mbegu ya ubaguzi ya u-Tanganyika na u-Zanzibar ni kurudi miaka sijui miaka mingapi nyuma, naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Sendeka, nitatoa Mwongozo wangu baadaye. Nashauri tuendelee na mjadala, ila niihakikishie nyumba hii kwamba Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa ni mwana Muungano na sisi watu wa Dodoma hapa ni shemeji yetu. Kwa hiyo, akipanda u-Zanzibari sijui watoto wale wataenda wapi?

Mheshimiwa Lucy Mayenga atafutiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura. (*Makofi*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi ya kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha leo hii kusimamia hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru akina Mama wa Mkoa wa Shinyanga ambao wao ndio walioniwezesha leo hii kusimamia hapa kwa kunipatia kura nyingi sana za kishindo kikubwa sana. Nasema nashukuru sana tutaendelea kushirikiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, kwa niaba ya akina Mama wa Mkoa wa Shinyanga, nimpe pole Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mama Anne K. Malecela kwa kuuguliwa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa John S. Malecela. Naomba Mwenyezi Mungu amjaalie mume wake huyu afya njema ili aweze kuendelea na juhudzi zote za ujenzi wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi, Mkuu wa Majeshi, Jenerali Davis A. Mwamunyange na kwa kweli kwa

upendeleo maalum kuwapongeza na kuwashukuru Wanajeshi wote ambao wakati sisi tupo hapa ndani ya hili Bunge muda huu, tunaongea kwa amani, tunaongea bila matatizo, ni kwa ajili ya wao huko mipakani walipo ambapo wanafanya kazi usiku na mchana kwa ajili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa yeye ni Amiri Jeshi Mkuu, ni Rais ambaye kwa kweli amejitahidi kwa kiwango kikubwa sana kuhakikisha kwamba Jeshi letu linakuwa ni Jeshi dogo lakini ni la kisasa kwa kuwawezesha kwa njia nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia Jeshi la Wananchi, ni Jeshi la kwetu sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jeshi hili limegawanyika katika makundi manne. Kuna Jeshi la Anga, Jeshi la Majini, Jeshi la Nchi Kavu na JKT. Jeshi la Anga wao kazi yao ni kuangalia kama anga yetu iko salama, Majini huko kuko salama na Nchi Kavu pia nako kuko salama. Wakati Jeshi hili kwa njia yoyote ile wanahangaika kuhakikisha kwamba sisi tupo salama, je, sisi kama wananchi ni nini wajibu wetu kama wananchi na kama Serikali katika kuhakikisha kwamba Jeshi hili tunakuwa nalo vizuri ili hatimaye hata hiyo kazi yake waweze kuifanya vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia haya kwa sababu sitaki kuzungumzia aliyotoka kuzungumzia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu aliyejita lakini ninaomba tuwe na uwajibikaji wa pamoja. Jeshi liwajibike kwetu lakini vilevile na sisi lazima tena hasahaha tukiwa kama viongozi tuwajibike kwa Jeshi. Hatuna budi kuwapa moyo kwani hawa watu wanafanya kazi kubwa, hawa viongozi wanafanya kazi katika mazingira yote, wakati watu wengine wakiwa wamekaa wanakula shushu kama humu ndani kwenye AC wako watu kule porini ambapo wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna *concept* kwa mfano sisi kama wananchi pamoja na Serikali, yapo masuala ambayo yamekuwa yakilalamikiwa sana kuleta migogoro au chuki za kupandikizwa kati ya Jeshi na wananchi. Moja ya suala ambalo limekuwa likzungumzwu sana ni suala la mipaka kwenye baadhi ya maeneo. Utakuta aidha ni wananchi wamevamia eneo la Jeshi au pengine Jeshi wamevamia eneo la wananchi. Hapa nashukuru leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ananisikia, tujitahidi kama Serikali, hawa Watendaji wetu ambao wakati mipaka ya Jeshi ipo, eneo la Jeshi lipo, Watendaji wetu kwenye Halmashauri, Maafisa Mipango Miji wako pale wanaona mtu anavamia, anazungusha kama ni ukuta, anaweka kama ni msingi, anaanza kujenga nyumba mpaka inakamilika, inakamilika nyumba ya kwanza, ya pili na kadhalika mpaka inakuwa ni eneo kabisa la makazi ya watu, wachukuliwe hatua. Mimi nadhani hata na sisi kama Serikali ingawa ni makosa ambayo yanaweza yakawa yalishafanyika huko nyuma, lakini lazima tuangalie tunafanya nini katika kuhakikisha kwamba suala hili linaweza kukamilika ili kuondoa zile tofauti kati ya Jeshi na wananchi ili ugomvi uweze kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile napenda kuzungumzia kwa upande wa Jeshi lenyewe. Sasa hivi nchi yetu ina amani lakini katika kipindi kama hiki ndiyo kipindi ambacho Jeshi kwa kweli linatakiwa kukaza buti. Jeshi linatakiwa katika kipindi hiki waongeze *training*, matishio mengi ambayo yalikuwa huko nyuma ya kwamba adui wa

Tanzania labda ni nchi za jirani kama Kenya, Uganda na nchi nyingine lakini hivi sasa hayapo. Sasa hivi matishio mengi yaliyopo ni matishio ambayo ni mapya kama masuala ya ugaidi, masuala ya uharamia na kadhalika, hayo ndiyo matishio mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi kwa kuwa limekuwa likiendesha *training* zake Msata na maeneo mbalimbali ndani pamoja na nje ya nchi. Naomba hizi *trainings* ziongezeke lakini vilevile zisihusishe mtu mmojammoja kwamba Afisa fulani ndiye anakwenda kufanyiwa *training*, ikiwezekana zisihusishe kama kikosi, brigedia na kadhalika kwa sababu Jeshi linafanya kazi kama timu ya mpira hata mtu mmoja akiwa ni hodari sana wa kucheza mpira lakini hawezikufanikiwa peke yake kama asipokuwa na wenzake. Kwa hiyo, naomba *trainings* za Wanajeshi ziongezewe nguvu na ziwe nyingi zaidi na zaidi kwa sababu sasa hivi tuna amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie JKT. Naipongeza sana JKT imekuwa ni mfano mzuri sana kwani wanatusaidia. Mimi nashangaa hata wale ambao wamekuwa wakisikitika au kushangaa kwa nini JKT wanaingia kwenye kilimo. Tunaposema Kilimo Kwanza siyo sisi tu peke yetu, siyo wananchi peke yetu, ni lazima tutafute na wadau wengine na wadau hawa wanatafutwa kwa sababu na wao pia lazima waonyeshe kwamba wana utayari wa kiwango gani. Sasa kama amezungumza Mheshimiwa Rais kwamba ni Kilimo Kwanza nao wanaona kwamba wana maeneo na kama tunavyojua Wanajeshi ukisema tokeni hapa saa saba usiku wataondoka kwani wana nidhamu ya Kijeshi, wameamua kushirikiana na sisi. Nadhani mtu akikupa mkono anataka kukukamata kama una matatizo na wewe mpe ili muende kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala ambalo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kulizungumzia, ni suala la kurejesha JKT. Mheshimiwa Zitto Kabwe mchana alikuwa anazungumzia kwamba Waheshimiwa Wabunge vijana twende huko, nilikuwa najifikiria naanzae. Nasema hivyo kwa sababu kwa kweli huko JKT, naiomba sana Serikali tujitahidi sanasana hizi pesa tuweze kuzitafuta kwa njia yoyote ile na zipatikane ili vijana wetu warudi JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala mengine huwezi kuyapima kwa *cost benefit analysis* kwamba nimeingiza shilingi milioni 50 basi nitategemea kupata shilingi milioni 100 faida ni shilingi milioni 50, hapana! Masuala kama ya uzalendo, unyenyekevu, ustaarabu, uaminifu na tabia njema za sisi kama vijana kujituma ni masuala ambayo siyo rahisi kuyapima kwamba nimeweka kiasi fulani basi nitaweza kuyapata matokeo yake pengine baada ya mwaka mmoja au miaka miwili. Tunajenga Taifa letu na naomba Serikali tujitahidi sana kuhakikisha kwamba pesa zinapatikana ili hawa vijana wetu waweze kurudi kule. Baadhi ya mambo ambayo yanatokea sasa hivi ni kwa sababu watu hatukupitia JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi tena kwenye ule mfano ambao aliuelezea Mheshimiwa Zitto, tena nitamshukuru sana labda pengine nikienda mimi, yeye Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Kafulila na hata Mheshimiwa Tundu Lissu naye akirudi itakuwa siyo mbaya ili tuweze kufundishwa ni jinsi gani ya kuishi kwenye nchi, ili

tuweze kuwa wazalendo, tuipende nchi yetu, tuweze kuwa waaminifu na hata siku nyingine tukikaa ...(*Kicheko*)

## T A A R I F A

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji aliyekaa kwamba mimi ni Askari, nimekwenda Jeshi la Kujenga Taifa, Operesheni Programu ya Chama mwaka 1989 -1990. Sasa pengine Mheshimiwa Mbunge anafikiri mimi nina umri sawa na wale waliokuwa wanajisema ni vijana, naomba tu apate taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwani taarifa hii imetusaidia sote, naona aliona umekaa kiraiaraia hivi. Mheshimiwa Lucy Mayenga!

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru sana kwa taarifa ya kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu na ninampongeza sana lakini elimu haina mwisho, turudi nyuma kwa sababu pengine inawezekana kaka yangu kuna vitu vingine amevisahau kwani alipita muda mrefu sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuzungumzia kuhusu suala la JKT, suala hili ni la muhimu sana na la msingi sana. Serikali itafute pesa ili vijana waweze kupata mafunzo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala ambayo sisi kama wananchi, nimesema kuna Jeshi la Anga, Jeshi la Maji na kadhalika. Haya majeshi yanahakikisha kwamba sisi tunakuwa salama na tuna amani, wanakaa mipakani huko katika kuhakikisha kwamba tunalindwa ili tuwe salama lakini mimi kuna kitu kimoja ambacho kinaniudhi na kinaniuma kupita kiasi. Kuna mabadiliko ya machafuko na vitisho vya matatizo ya kivita kama nilivyoelezea kwamba miaka ya zamani ilikuwa Tanzania atamuogopa Uganda au Kenya au ataogopa nchi nyingine za jirani lakini sasa hivi nimesema hivi vitisho vitabadijika lakini kitisho kikubwa sana ambacho mimi nakiona ni sisi wanasiwa wenyewe humu ndani. Nasema hivyo kwa sababu siku hizi umezuka na umekuwa kama ni mchezo au kama ni utaratibu au kama ni fasheni, sina maana ya kuzungumzia Vyama vya Upinzani peke yake, mimi nazungumzia Wanasiwa wote tulipo humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ugonjwa unataka kutuingia sisi wanasiwa na ugonjwa huo ni ugonjwa wa kutaka madaraka. Nasema hivyo kwa sababu gani? Sisi wenyewe kama hatutakaa vizuri kama wanasiwa, sisi wenyewe kama hatutakuwa wazalendo kwenye hii nchi, sisi wenyewe kama hatutakuwa watu tunaofikiria leo lakini zaidi tunafikiria vizazi vijavyo, haya Majeshi na huku kuhangaika kwao jinsi

wanavyokesha usiku na mchana hawalali kwa sababu yetu na kwa sababu ya wananchi, hawataweza kufanikiwa ikiwa sisi hatutabdalisha *system* za maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu haiwezekani leo hii mtu ikifika wakati wa uchaguzi, tunaelekea kwenye uchaguzi wa mwaka 2015, leo maneno yanaanza kwamba fulani hafai, fulani sijui hivi, sijui fulani hivi na tumefikia kiwango mpaka cha kuwakosea heshima viongozi wetu wakuu. Sasa hivi katika Tanzania hii Rais ni Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri wake Mkuu ni Mheshimiwa Mizengo Pinda, Makamu wa Rais ni Mheshimiwa Ghalib Bilal, hatutaki mazungumzo mengine zaidi ya hapo, hizi kelele nyingi ambazo zinakuja, mara chokochoko, tunawashawishi wananchi *to turn against the Government*. Mimi leo hii nitasema nataka kugombea kitu fulani au uongozi fulani nimesimama hapa lakini nina watu nyuma yangu. Nitakaposema kikwazo cha kwangu mimi kugombea kuwa, labda nianzie mbali kwenye Ubunge, kikwazo changu ni labda Mheshimiwa Al-Shymaa, watu wote wanaoniunga mimi mkono watasema Al-Shymaa mbaya. Hatuwezi kufika katika utaratibu wa namna hiyo, tutawaingiza wafanyakazi wetu hapa nchini, tutawaingiza vijana hapa nchini kuhakikisha kwamba wanachukia baadhi ya watu kwa sababu ambazo hazina msingi. Lazima tuache hiyo tabia, ni lazima tujue kwamba Mamlaka zote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi imeibuka tena tabia nyingine unakuta mtu yeze amekwenda kuchukua fomu, amegombea Ubunge, amepita amekuwa Mbunge, fomu ile wakati unagombea ilikuwa ni Ubunge na siyo Uwaziri lakini leo hii akija ameshakuwa Mbunge anaanza kusema mimi kwa kweli ninavyoona kwa vile nina *Masters* na *CPA*, nadhani nafanana kuwa kama Waziri wa Fedha. Akiingia ndani ya Bunge hili, asipochaguliwa kuwa Waziri anaona Rais mbaya, Waziri Mkuu mbaya, wameshakuwa watu ambao hawafai na Serikali yote mbaya. Hizo tabia lazima zife kwa sababu tukiendelea nazo tunawajengea nini wale watu wengine ambao wako kule chini? Wewe kama unavyojionaona kwamba ni Waziri kaa tu kama ikiwezekana subiri na mbaya zaidi wanasema kwamba mimi yaani kwa kweli ilikuwa kabisa nipewe Uwaziri lakini bila fulani kwa kweli mimi ilikuwa nipewe kabisa. Hizo tabia ni mbaya na sasa mimi naomba kuwakumbusha kwamba lazima watu waijangalie, *record* zao ndizo zitakazowahukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wewe leo hii unasimama au mimi nasimama nasema kwamba mimi ni Lucy Mayenga, unajifanya msomi lakini *record* yako huko nyuma ikoje? Ulikuwa unafanya kazi lakini mbadhirifu, ilikuwa wewe ukipata shilingi 10,00/= umekula, ulikuwa unafanya mambo ya ajabuajabu, *record* yako mbaya na watu wana *record* za watu. Kwa hiyo, kama imetokea umechaguliwa kuwa Mbunge lakini hukupewa Uwaziri usikae tena kuanza kutafuta kwamba jamani Waziri Mkuu, kwa kweli mimi naona kama vile ilikuwa vibaya...

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Endelea!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuzungumza jambo. Kanuni ya 68 ambayo inatoa fursa, sina Kanuni hapa lakini nakumbuka ...

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba tuokoe muda uendelee moja kwa moja. Inatakiwa unaposima kwa jambo hilo unakuwa umeshajipanga kabisa.

**MHE. MOSES JOSEPH MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 ambayo inatoa fursa kwa Mbunge kuweza kusimamia wakati wowote na kuweza kuomba utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Nakuruhusu uendelee!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji ambaye anaendelea hivi sasa anazungumzia mambo ambayo yako nje ya mada. Leo tunajadili Wizara ya Ulinzi wa nchi yetu, mambo haya ambayo anayazungumza ye ye yalipaswa kuwa kwenye *part caucus*. Kwa hiyo, niombe Mwongozo wako na pengine kama utampa fursa ya kuendelea kuchangia azungumze mambo ambayo yana maslahi kwa Taifa na siyo mambo ya *part caucus* kuja kuyaleta ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Moses Machali, lakini niseme tu kwamba mambo haya tuna mjadala wa Katiba unakuja mbele yetu, watu watayaangalia mambo haya kwa michango ya aina mbalimbali, ziko dawa nyingi za mambo ya aina hii mojawapo ni Mawaziri kutoka nje ya Bunge na kadhalika.

Mheshimiwa Lucy Mayenga, taarifa hiyo umepewa unasemaje?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge ambaye amekaa na ye ye ni mmoja kati ya hao ambao nawazungumza na naikataa taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nachozungumzia ni kwamba Jeshi letu wakati linakaa kupanga mipango ya amani, wakati linakaa kuhakikisha sisi tunakuwa salama lazima na sisi wenye we humu ndani au sisi wenye we kama Viongozi au sisi wenye we kama wananchi tuhakikishe tunakuwa na tabia ambazo zinaendana na masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeishia hapo, naomba wote wenye tabia kama hizo waache, Mamlaka yote inatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Haya jamani, mmeambwa muache. Mheshimiwa Sabreena Sungura, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uhai mpaka leo. Pia napenda kuchukua fursa hii adhimu kuishukuru familia yangu kwa ushirikiano ambao wamenipa na pia napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wanawake, wanaume, wazee na watoto wa Mkoa wa Kigoma kwa ushirikiano ambao wamenipa toka uchaguzi mpaka leo hii. Sina cha kuwalipa ila nawaahidi kwamba hoja zao nitazileta Bungeni, nitazitetea na majibu nitakayopata nitayarudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo. Moja, Wanajeshi wamekuwa wanapata nafasi za kusoma kwa kusuasua na chombo hiki ni chombo nyeti na kama tunavyosema tunataka kuwa na Jeshi la kisasa, Jeshi ambalo litajua sayansi na teknolojia na hiyo itasaidia kupunguza ukubwa wa Jeshi kwa kuwa na Wanajeshi wachache ambao watatumia vifaa vya kisasa zaidi kuweza ku-control nchi yetu. Napenda leo Waziri atueleze kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya Wanajeshi wetu kwenda kujiendeleza? Tunaposema tunataka kuwa na Jeshi la kisasa lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa na *talented military personnel*, hivyo ni lazima tuweke jitihada za makusudi kuhakikisha Wanajeshi wetu wanapata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sasa Wanajeshi hawa wamekuwa wakipata nafasi hizi kwa kusuasua, tangu *intake* ya 14 ya akina Mheshimiwa Sadifa, mpaka leo *intake* ya 25 vijana wengi sana wamekuwa wanaacha Jeshi kwa sababu za kimasomo. Vijana wanaomba kwenda kujiendeleza lakini wanaambiwa watakwenda baada ya miaka mitatu, minne, wa tano na hatimaye wanaamua waachane na shughuli hii na kwenda kujiendeleza na shule kwa sababu wanaona wana sifa za kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye suala la pili, suala la mabomu ya Gongo la Mboto. Napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wale wote waliofikwa na maafa na uharibifu wa mali na nyumba zao. Ilitangazwa kwamba itaundwa Bodi ya Uchunguzi ya ndani ya nchi na Baraza la Umoja wa Mataifa likasema na nchi za nje zishirikishwe na Marekani wakasema na wenyewe watatoa Wanajeshi wao waangalie ni vyanzo gani vilisababisha tatizo hili. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Watanzania wana hamu ya kujuu ni nini hasa kilitokea na sababu ipi ilipelekea milipuko hii ili watu waweze kuchukua tahadhari hapo baadaye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye suala lingine la tatu, suala la makampuni binafsi ya ulinzi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni sheria zipi zinahalalisha makampuni haya binafsi ya ulinzi kuwa yanafunguliwa leo, kesho na kesho kutwa? Ni utaratibu gani unafanyika kwenye udahili? Je, watu hawa wanakula viapo? Je, pindi wanapotaka kuacha kazi, taratibu zinakuwaje? Hili ni suala tete ambalo tunatarajia Mheshimiwa Waziri ajibu la sivyo leo ninashika shilingi katika mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la hii Order inayojulikana kama ‘*Forces Routine Order*’ kwa ndugu zetu Wanajeshi. Wanajeshi wetu wamewekewa *Regulations* kwamba waweze kuwa na familia baada ya miaka sita (6) tangu kuanza kazi. Naona *Regulations* hizi ni kandamizi kwa sababu tunaposema mtu apate familia baada ya miaka sita, kwa zamani *Regulations* hizi nafikiri zilikuwa sawa kwa sababu watu walikuwa wanaingia Jeshini wakiwa vijana wadogo hasa katika miaka 17 au 18, kwa hiyo, *at least* ukimpa hiyo miaka sita mpaka miaka 24 anakuwa bado ni kijana mdogo lakini sasa hivi tunaposema tunataka kuwa na Jeshi la kisasa, vijana wanasoma, watu wanaingia Jeshini wana *PhD, Masters, almost* wanakuwa katika umri wa *thirty's* na kuendelea. Sasa katika *age* hiyo kweli umwambie mtu acae miaka sita (6) ndiyo aoe, hatuoni kama hii ni hatari na tumekuwa tukishuhudia Wanajeshi wetu wanakumbwa na haya maambukizi ya maradhi hatarishi likiwemo gonjwa la UKIMWI na hii ni sababu ambayo inapelekea Wanajeshi wetu waendelee kuangamia. Tunawapa miaka sita (6) lakini wanapojiunga na Jeshi mpaka miaka sita inapofika Wanajeshi hawa unakuta wana watoto wa miaka minne(4) au mitano (5) na wana wanawake wanaishi nao, sasa tunakataa nini na tufanya nini? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi aweze kutwambia je, Serikali iko tayari sasa kupunguza muda huu ama kuuondosha kabisa ili kupelekea Jeshi hili liwe la kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kumalizia na suala la Mikoa yetu ya Magharibi kuhusu ulinzi na usalama. Katika Mkoa wangu wa Kigoma, wavuvi wetu wamekuwa wakitekwa mara kadhaa na wengine wakiuawa, wakinyang’anywa vifaa vya kuvulia na Wanajeshi hawa tunao na wavuvi wamekuwa mara kadhaa hasa katika eneo la Katonga wakichanga fedha za mafuta kwa ajili ya doria na Wanajeshi wanazunguka lakini bado uharamia huu katika Ziwa Tanganyika unaendelea. Sasa tunaomba leo Mheshimiwa Waziri atupe majibu ni lini uharamia huu utakomeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na Ziwa Tanganyika, tunayo mapori ambayo naweza nikayaita mapori hatarishi. Kuna pori linaloanzia Nyakanazi kwenda Kibondo, tuna pori la Malagarasi, tuna pori lingine la Kasandaga na tuna pori la Nyakanazi. Sasa mapori haya kuna majambazi kule yametengeneza Jamhuri yao, yaani unajua kabisa nikipita kwenye eneo hili nimepita Jamhuri ya Majambazi. Watu wanakuwa roho mkononi, ndugu zetu wanadhalilishwa, akina mama wanabakwa, wafanyabiashara wananyang’anywa mali zao, tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini uharamia huu katika mapori haya utakomeshwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu ningependa niishauri Serikali kutokana na mabomu yaliyolipuka Mbagala, kwa kuwa Makambi ya Jeshi yako karibu na wananchi, ni vyema makambi haya basi yangepelekwa kwenye mapori haya hatarishi yaliyoko katika Mikoa hii ya Magharibi ili kuhakikisha kwamba hali ya amani na usalama inakuwa ni njema huko. Maeneo haya na sisi binafsi hata viongozi, hususani tunaotokea Mkoa wa Kigoma, tunapita sana tu kwa kuwa usafiri wa ndege ni wa kusucasua na sisi tunatumia njia hizi, ama mnataka siku ya siku tusikie Mheshimiwa fulani na yeye ameingia katika mkasa huo, mtu kabakwa? Hii itakuwa ni aibu kama nchi tuna uhuru miaka 50, lazima tuweze kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba leo niishie hapo ili na wenzangu nao wapate nafasi ya kuchangia. Nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sabreena Sungura. Kama nilivyosema, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Maryam Msabaha, wengine mtaniwia radhi kwa vile orodha ni ndefu na muda hauko upande wetu. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwanza nimshukuru kabisa Mwenyezi Mungu na mimi kunipa uzima na uhai wa kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na hotuba ya Waziri wa Ulinzi wa upande wa pili (*Upinzani*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme; “Siri ya Mtungi aijuae ni Kata“ leo hii Wazanzibari tukisimama hapa tunatetea vijana wetu, watoto wetu waliotutuma na wanawake waliotupigia kura tuje kuwawakilisha kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano, mnaona kama sisi tunaenda kinyume, lakini hii ni haki yetu kutetea vijana wetu, kutetea upande wa Zanzibar au upande wa Jamhuri ya Muungano kudai haki zetu zote ambazo zinatoka kwenye sekta ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama vijana wengi ambaو wanatoka kwenye sekta ya ajira wanaokuja katika sekta ya Jeshi la Muungano wanakuwa wameshapitia JKU lakini vijana hao wakifika huku huwa wanapimwa afya, pia hili niliwahi kulisema wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na sitapenda kuharibu utamu ambaو kashausema mzee wangu katika Bunge hili, nasema sisi hawa kama vijana wetu, vijana wale wanakuwa wanakata tamaa sana na unakuta wanajiingiza kwenye dawa za kulevyta, vitendo viovu na sisi kama wawakilishi wao ambaو tunakuja katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wanatulaumu sana, wanasema sisi tunakaa huku tunapiga makofi tu, hatuwawakilishi. Leo nasema kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, aniambie kwa kina ni Wazanzibari wangapi walioajiriwa katika sekta hii ya Ulinzi kwa sababu mimi nilivyoangalia kwa macho yangu tu sikuona hata Mzanzibari mmoja wakati wa kujitambulisha hapa, lakini tukisema nyie mnasema sisi tunapenda kuongea, hatupendi kuongea, tunatetea haki za vijana wetu na sekta ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye masuala ya jinsia katika suala zima la Jeshi la Kujenga Taifa. Suala hili la jinsia naona limepigwa teke, halipo kabisa na hata leo ni shahidi kabisa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, mtaona Majenerali waliokuwa wanajitambulisha hapa wote ni Wanaume, hakuna Mwanamke hata mmoja. Tanzania kuna Wanawake wasomi, kuna Wanawake jasiri kabisa, kwa nini Wanawake hawa wasipewe nafasi za juu? Tunasema Wizara hii iangalie kwa kina na sisi Wanawake tunaweza bila hata kuwezeshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kabisa ninasema Serikali ya sasa hivi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ni Serikali ambayo imekomboa wanawake wengi, kwa hiyo kila sekta mwanamke awepo. Nasema hivyo kwa sababu tukiangalia hata Chama changu cha CHADEMA sasa hivi siyo Chama cha Wasomi peke yao, ni Chama ambacho kimechanganyika, kuna wa elimu ya juu na wa elimu ya chini. Kwa hiyo, sasa hivi nasema na hili Jeshi lichanganyike, wawepo ambao wana *degrees*, wawepo ambao wamefika darasa la saba, *form four* kwa sababu wasomi wanapokuwa mahali pamoja ndiyo wanapata kuiba vizuri. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema hilo Jeshi liwe ni la watu wote, lisiwe ni Jeshi la watu wajanjawajanja tu ambao wanajua kucheza na kalamu na hao wa darasa la saba pia wawekwe. Leo hii tunaona Serikali yetu ilikotufikisha kwa sababu inapenda kukumbatia watu ambao ni wasomi ambao wanajua kucheza na kalamu, ndio wanatufikisha huku tuliko sasa hivi. Kwa hiyo, Serikali ya sasa hivi ni kuchanganyika, hili nalisema na Mheshimiwa Waziri hili ulizingatie na ulichukue, hakuna kuajiri wasomi tu, hawa wasomi tumechoka nao sasa hivi, nyie chekeni lakini hii ndiyo *message sent*, mengine nilichangia kwa maandishi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye suala la waathirika wa mabomu ya Mbagala na Gongo la Mboto. Kwa kweli hili ni janga la Kitaifa na siyo Janga la Chama au mtu mmoja mmoja lakini tumekuta misaada ile ambayo ilikuwa inatolewa kwa wale waathirika ambao walikuwa walengwa haikuwfikia na mingine ilitolewa kwa ubaguzi na wengine waliambiwa kwamba nyie ni chama fulani, sisi ni chama fulani kwa hiyo hampati msaada kwa sababu si chama fulani. Mimi naomba yanapotokea masuala kama haya ya majanga ya kitaifa, muangalie linakuwa vipi, kwa hiyo naomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika sekta ya michezo. Tanzania naona kama hii michezo hatujaipa kipaumbele, lakini tuangalie nchi za wenzetu kama Brazil jinsi walivyoiweka mbele michezo. Vijana wengi Tanzania wanapenda kujiajiri katika sekta ya michezo na wana ubunifu mbalimbali lakini vijana hawa tumekuta mara nyingi wanachukuliwa na Kambi za Jeshi, wanaambiwa njooni mjiunge na michezo na baada ya muda fulani mtapata Ajira Jeshini, lakini wakienda kujiunga wakikaa baada ya muda hawapati tena ajira za michezo katika jeshi, hili pia mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la ubaguzi, mimi nitaliita ubaguzi kwa sababu kuna suala kwamba mtoto wa maskini aliyeko kijijini asiyekuwa na umaarufu katika Serikali yetu au asiyekuwa na mkubwa katika Jeshi au sekta ambayo inashughulikia ajira za Jeshi hawezi kupata ajira. Kuna rushwa katika mambo haya, hili lizingatiwe na nililisema sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Haya mambo ya rushwa katika sekta hii ya Jeshi yaondoshwe kwani huku ndiyo kuna UKIMWI, UKIMWI umezidi katika haya mambo kutokana na rushwa ya ngono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya pia yaangaliwe kwa sababu mtoto aliyetoka kijijini, mtoto wa mkulima kama anavyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, anatoka kijijini hajui mtu anakwenda pale, bado kijana yule kama ni mtoto wa kike

kaumbika vizuri, anavutia, anafika ofisini atazungushwa, njoo saa fulani, njoo saa fulani, mpaka ngono zinaendelea kwenye maofisi kwa ajili ya kutafuta ajira. Hili likomeshwe na likemewe, kila mtu apate haki katika Tanzania hii, awe mtoto wa tajiri au maskini wote wapewe haki sawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi nimeyachangia sana kwa maandishi kwa sababu niliona huu muda sitaupata kwani jana pia niliomba kuchangia kwenye sekta ya afya, nikakosa, lakini tuangalie hizi Hospitali za Jeshi, zimekuwa zinasaidia wananchi, basi nazo zipate bajeti ya kutosha, zipelekewe dawa na Serikali ili zipate kusaidia wananchi wengi. Sisi tumeona Bububu wanatusaidia sana kule Zanzibar. Sasa tunaomba nao wapewe bajeti yao ya kutosha kabisa ili wapate kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi bado niwaseme kidogo, inapofika kipindi cha uchaguzi mnakuwa mnagawanywa katika sehemu mbalimbali na mnakuja pia kwenye Kisiwa chetu cha Unguja. Watoto wa Kizanzibari wanapenda kutoka jioni, wamezoea starehe zao, wamezoea kwenda Bwawani, wamezoea kwenda taarabu, wenyewe ni raha juu ya raha nyingine lakini sasa watoto hawa wa Kizanzibari mnakuwa mnawakosesha raha. Naona mambo mengine huku Bara hayapo, kwa sababu mtoto wa Kizanzibari mwenyewe kashafukiza udi wake, kashatia manukato yake lakini sasa anapotoka kwenye sehemu yake ya starehe anakutana na hawa Wanajeshi, kule sisi hatujazoea mambo ya kutishwatishwa, lakini yule mtoto sasa anaanza kutetemeka, mkiona yale mambo mengine yanavutiavutia mnaanza kuwadhalilisha, kwa hiyo, hilo likomeshwe pia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siasa tunazijua wala hatukuzianza jana, tumeanza siku nyingi. Kwa hiyo, mambo ya kuletewa Wanajeshi wengi kipindi cha uchaguzi hatutaki. Haya mambo ya kuletewa Wanajeshi wengi ndani ya Zanzibar ndio yanachangia na UKIMWI kwenye Kisiwa chetu, hatutaki nimesema. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha, hiyo ni kengele ya kwanza. (*Kicheko*)

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hawa Wanajeshi mara nyingi tumeona wakioneshwa kwenye vyombo vya habari katika matukio mbalimbali. Huwa mimi najiuliza siku hizi Kambi za Jeshi labda vyakula hawapelekewi kwa sababu utakuta Wanajeshi sijui wanakuwa na njaa, wanaingia mitaani, wanaanza kupiga vijana mateke, wanafanya fujo, utaona pale walivyofanya fujo na kuchukua vitu vya watu wanaondoka navyo na wengine hata vyombo vya habari pia wamekuwa wakiwaonesha wanashiriki kwenye vitendo vya uhalifu. Hili mliangalie kwa makini, kama Mwanajeshi ufanye kazi yako ya ulinzi usijiingize kwenye vitendo vya uhalifu, ulinde raia wako na ufanye kazi yako ya Jeshi, lakini mambo ya kupiga watu mabuti kwa makusudi hatutaki. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sasa ni la mwisho maana mengi nilichangia kwa manandishi. Mimi nakaa Mpendae, karibu na kwa Spika huko, lakini hawa Wanajeshi

mara nyingi wamekuwa sasa sijui hata niseme vipi kuhusiana na hizi Kambi za Jeshi, kwa kweli hili mliangalie kwa makini sana. Wakati wa jioni wanaweza wakawa wako Kambini, wanatoka nje ya Kambi na wanalewa sana na wanajisahau. Sasa hili tatizo sijui liko wapi, sijui yale maadili ya jeshi yanapotea, sijui wanajisahau na kufikiri na wao ni raia? Ukishavaa ile kombati yako ya Jeshi inatakiwa mtu ubaki kule Jeshini msiwe mnazunguka mitaani, mnafanya fanya fujo na mambo yasiyoendana na maadili ya Jeshi, hili mliangalie kwa makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilishachangia mengi kwa maandishi na naomba mambo yangu ambayo nimechangia kwenye sekta ya Muungano kuhusu ajira za Wazanzibari, leo nipate majibu hapahaha. Kama sikupata majibu kwa kweli nitasimama, japo ni Bunge la mara ya mwanzo, lakini mtuambie na sisi wakisimama Majenerali tuone Wazanzibari na hizi nafasi mchukue kwa uwiano Pemba na Unguja. Sisi tukirudi kule lazima tunaenda kuulizwa, vijana wetu wanaenda huko JKU wakishamaliza wanasema tunaenda kwenye ajira hatuzipati na tukienda huko yaani unakuta vijana wameshajiingiza kwenye mambo mauvo. Tukirudi sisi kama Wazanzibar, nyuso zetu tutaziweka wapi na sisi wametutuma tuje tuwawakilishe au mnataka sisi tunyimwe kura?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya mambo kwa jambo lolote la Muungano sijali kama niko CHADEMA, nitaungana na mwenzangu yoyote wa CCM ambaye atatetea Zanzibar, nitaungana na wa CUF ambaye atatetea Zanzibar, tushikamane tuwe kitu kimoja, maana yake sisi ndio tunajua siri ya Zanzibar ambapo sisi hata watoto wetu walikuwa wakati mwagine wakienda kusoma hawasomi. Sisi Kisiwa kile tunakijua tunavyopata taabu nacho. Kwa hiyo jambo lolote la Zanzibar lazima nitaliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yangu niliyosema hayo mengine mpaka nipate majibu ndio nitaunga hoja mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, huyo ni Mheshimiwa Maryam Msabaha kutoka Mpanda Zanzibar.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ZAINAB R.M. KAWAWA:** Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab, endelea!

**MHE. ZAINAB R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 60(8), hii ni kwa faida yetu wote. Inasema hivi:-

*“Mbunge hatasoma maelezo, isipokuwa, kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake, anaweza kusoma dondo Kutoka kwenye kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia kwenye kumbukumbu alizozianidika”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati msemaji aliyejita alipokuwa akitoa maelezo yake kimuonekano alikuwa akionekana kama vile anasoma.

### **WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. ZAINAB R.M. KAWAWA:** Ndio maana nimesema hii naisema kwa faida ya wote. Kimuonekano alikuwa akionekana kana kwamba anasoma maelezo yake. Hiyo ndiyo hali halisi. Sasa labda kwa vile wenzetu mmezoea kipingapinga hivi, lakini nalisema hili kwa faida yetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzingatie Kanuni na naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab. Nikiri kwamba Kanuni uliyoisoma ni kweli ndivyo inavyosema na kwa faida ya wote ni kweli tunapaswa kuchangia hapa bila kuwa tunasoma moja kwa moja lakini pia niseme kwa hakika sikumuona Mheshimiwa Maryam akisoma moja kwa moja badala yake niliona akichomoa kigongo kimoja baada ya kingine. (*Makofî/Kicheko*)

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze kwa dhati kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Naomba pia nipongeze Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuona umuhimu wa kurudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Nimefarijika kujua kwamba Serikali imeandaa vijana wanaokadiriwa 36,000 kwa ajili ya kuanza mafunzo hayo wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nishauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, turejeshe utaratibu wa Jeshi la kujenga Taifa katika mfumo wa ajira. Hii itaongeza utaifa; itaongeza umoja; itaongeza nidhamu ya kazi na itaongeza uwajibikaji. Hivyo, watu wote wanaomaliza Vyuo kabla ya kuajiriwa Serikalini na hata kwenye sekta binafsi sharti wapitie JKT. Cheti cha JKT kiwe sharti la ajira badala ya *experience* (uzoefu).

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi wa rasilimali Ziwa Tanganyika na athari kwa uchukuzi. Mto Ilongo upande wa DRC, ni chanzo cha Mto Congo unaotoa maji Ziwa Tanganyika. Hivi karibuni Kidhibiti cha Maji (*WEIR*), kuna taarifa kilibomolewa, inahisiwa na mabomu huenda na Askari labda waasi ili kuongeza kasi ya maji kutoka Ziwani. Kina cha maji Ziwani kinawenza kuendelea kushuka na kuathiri usafiri majini kwenye magati ya Lakosa, Kyala, Kaumu, Kabwe, Kagunga, Kipiri na Kasanga upande wa Tanzania. JWTZ na taasisi nyingine zichunguze suala hili ili usafirishaji, ikolojia, samaki na mazao mengine Ziwani visiendelee kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya JKT. Ombi la ujenzi/uanzishwaji wa Kambi Jimboni Igalula ili kupitia Kilimo Kwanza hasa cha mahindi, mpunga na ufugaji, tunalikaribisha Jeshi lije Jimboni na kuchagua moja ya Kata ili Kambi ianzishwe na wananchi pia wapate fursa ya kujifunza kilimo na ufugaji bora na wa kisasa ili kuongeza uchumi na pato la Taifa na Jimbo pia.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kwa vijana wengi wa Mikoani kutopewa kipaumbele wakati wa mchakato wa kuingiza vijana katika Jeshi la kujenga Taifa na JWTZ. Inasemekana kumekuwa na tabia ya urasimu wakati wa usaili na nafasi zinatoka kwa kujuana na wengi wanaopata nafasi ni watoto wa viongozi na wafanyakazi wa Jeshi hilo. Je, ni njia gani zinatumika kuhakikisha vijana kutoka Mikoa mbalimbali na hasa watoto wa Watanzania maskini wanapata fursa ya kutumikia Taifa lao kupitia Jeshi la Ulinzi na kujenga Taifa?

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa na uzima. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa busara na matumaini kwa Watanzania wenye hamu ya utulivu, pamoja na amani katika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii kwa upande wa uwajibikaji wa Majeshi yetu. Majeshi yetu yanatekeleza kazi yao kwa kiwango kizuri, lakini Majeshi hayo yana upungufu wa vitendea kazi kama nyumba za kuishi, nyumba zao ambazo wanaishi hazifanani na kazi wanazofanya ukizingatia majukumu ya kazi zao ni ngumu. Kwa hiyo, wanapaswa baada ya kazi zao wapate mapumziko katika sehemu nzuri lakini kinyume na hayo nyumba wanazoishi wengi wao ni mbaya hususani Kambi ambazo ziko nje ya mji. Je, ni lini Wanajeshi watapatiwa makazi mazuri ili nao waweze kufurahia kazi zao vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi hawa wanaenziwa wakati wakiwa kazini na baada ya kumaliza mkataba wao wa kazi hapo ndipo wanapokosa imani na Jeshi hilo kwa kuanza kusumbuliwa kwa kufuatilia pensheni na ukizingatia wengi wao wanarudi vijijini kuanza maisha mapya. Pensheni hiyo huwa haiwezi kukidhi matumizi ya mstaafu huyo, ukizingatia baadhi yao wamestaafu na ujuzi wao, je, ni hatua gani mmechukua za kuwasaidia wastaafu hao ili isiwe mzigo kwa Taifa letu na kupunguza vitendo vyta ujambazi katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi yanayolituhumu Jeshi kuwa karibu na maeneo ya makazi ya watu hali inayopelekea athari kubwa sana pale inapotokea milipuko ya mabomu kama ilivyotokea Gongolamboto na Mbagala. Changamoto kama hiyo inalikumba pia eneo la Kunduchi – Mtongani katika Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba ili kuepuka madhara, Jeshi limeandaa michoro mipya ya ramani yenye malengo ya kuweka mipaka mipya ya Jeshi

ili ku-accommodate nyumba za wananchi/wakazi wa eneo hilo. Hata hivyo, kumekuwa hakuna taarifa sahihi na wananchi wamekuwa wakisumbuliwa kwa kuwekewa ‘X’ kwenye nyumba zao, ama wakati mwingine wanawaona Wanajeshi wanayazungukia maeneo yao, hivyo kuleta hofu kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa hofu hii, naomba Waziri atoe tamko kuhusiana na mustakabali wa wakazi wa Kunduchi-Mtongani wanaopakana na Jeshi na ni lini Wizara imejiipanga kufanya kikao na wananchi ili kufanya utambuzi wa mipaka mipyä ili wananchi wangu wakae kwa amani na kuweza kufanya shughuli zao za maendeleo kwa utulivu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko toka kwa wastaafu wa Jeshi kutokana na malipo kiduchu wanayolipa baada ya kustaafu. Dhana nzima ya Watumishi wa Jeshi haieleweki baada ya kustaafu ukilinganisha na Mashirika ya Umma. Kiafya hawana mfuko wowote wa afya ya jamii. Mafao yao ni duni sana, hali kadhalika pensheni zao haziwawezeshi kukidhi gharama ya maisha kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha maisha ya wastaafu wa Jeshi, tunaomba Serikali iboreshe pensheni zao kulingana na wakati uliopo kulingana na vyeo vyao. Je, iliwezekanaje kwa Wanadhimu Wakuu wa Jeshi kubadilishwa pensheni zao wakati wamestaafu kulinganishwa kwa vyeo walivyonyavyo Wanadhimu Wakuu wa wakati huu na kuwaacha wastaafu wengine wa ngazi za chini yao? Ni utaratibu upi wa mabadiliko hayo uliotumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya mwisho ni kuhusiana na Jeshi la Akiba (*Reserve Forces*). Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kama Tanzania inalo Jeshi la Akiba na kama lipo linajumuisha makundi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupatiwa ufanuzi, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni nchi ya amani hivyo si mategemeo kuwa Jeshi letu litahusishwa sana na mambo ya kivita. Hivyo basi wakati tunahitaji Jeshi imara la kujihami kwa aina yoyote ya uchokozi, Jeshi letu pia linaweza kutumika kuendeleza taaluma na kuleta mapinduzi ya viwanda. Ushauri wangu ni kuwa Jeshi letu litayarishwe kuwa Jeshi bunifu na tundu ambalo litaweka kwa vitendo uvumbuzi ufanyakao ndani na nje ya nchi hadi liweze kutoa mashine zetu wenywewe za awali (*prototypes*) za magari mapya, *television* mpya, *tractor* mpya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kwa kumpungeza Waziri, Mheshimiwa Hussein Mwinyi pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii muhimu. Nawapungeza Wanajeshi wetu wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda Taifa letu na raia wa nchi hii pamoja na kulinda mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba Kambi ya Makwe Pemba, ni kambi inayotambulika au ikiwa haitambuliki basi ihamishwe maana imesahaulika hata kwenye bajeti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikutajwa. Je, Kambi hii haihitaji kufanyiwa ukarabati? Haihitaji kituo cha tiba, mbona Pemba imetajwa Kambi moja tu ya Ally Khamis Camp?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi za Majeshi yetu sasa hivi ziko karibu na makazi ya watu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa Kambi hizi karibu na makazi ya watu kama vile Mwanyanga na nyinginezo na maafa yameanza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kozi za jeshi zinatolewa, je, zinatolewa kwa uwiano baina ya Bara na Zanzibar ili kuimarisha Muungano? Pia mahojiano (*Interview*) yanapofanyika kwa vijana kule Zanzibar hasa Pemba wakubwa huleta jamaa zao kutoka Bara na hivyo nafasi hizo kuchukuliwa kwa jina la vijana wa Pemba kumbe sio kweli. Namuomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwa umakini mkubwa suala hili.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu (SW) kwa kunijaalia kuwa Mbunge katika Bunge hili Tukufu na pia kwa kunipa afya njema na kunipa ufahamu wa kuchangia bajeti hii japo kwa uchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Khalfan Kikwete kwa uongozi wake wenye nia njema na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze pia Mkuu wa Majeshi yetu, Generali Davis Mwamunyange kwa uongozi wake shupavu wa kuliboresha Jeshi letu ili liendane na mahitaji ya Kijeshi katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Wabunge tuna imani na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Jeshi letu. Kazi ya kuilinda nchi na viongozi wake katika mipaka yote. Pia ushiriki wa Jeshi letu katika kulinda amani kwenye nchi mbalimbali ulimwenguni. Jeshi letu limeiletea sifa nzuri nchi yetu machoni mwa Mataifa mengi duniani kwa kazi yao nzuri na utii kwa viongozi wao. Napenda nichukue nafasi hii kusema ahsanteni sana Wanajeshi wetu, ongezeni bidii msibweteké.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri mengi yanayofanywa na Jeshi letu, kuna upungufu unaohitaji kufanyiwa kazi ili Jeshi letu liendelee kuwa Jeshi la Wananchi. Kuna malalamiko ya ajira za Jeshi kutolewa kwa njia ya udugu, ujamaa au kujuana na hata Chama cha wazazi badala ya sifa za mwombaji. Hili ni tatizo linalohitaji kuangaliwa kwa haraka ili lisipelekee kuharibu sifa nzuri iliyojijengea.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo pia malalamiko ya kutolipwa stahiki zao Wanajeshi wetu waliolilettea sifa Taifa kwa kushiriki na kushinda vita ya Uganda na pia vita ya ukombozi wa Msumbiji. Hili ni tatizo linalouwa morali ya Wanajeshi wetu. Ni lazima liangaliwe vizuri na lipatiwe ufumbuzi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pia malalamiko ya wastaa fu kulipwa pensheni kidogo sana na kucheleweshwa kwa miezi sita (6). Maombi yao ni kuongezwa kwa pensheni zao na walipwe angalau kwa miezi mitatu mitatu ili waweze kuhimili kwa kiasi kidogo ukali wa maisha unaowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linaloendelea kukua katika Jeshi letu ni Wanajeshi kujichukulia sheria mkononi. Inapotokea raia na Wanajeshi kukosana kwa sababu za kawaida tu za kibinadamu au hata mara nyingine kukosana baina ya raia na raia wenzao, badala ya Wanajeshi kuamua ugomvi huo kwa busara au kuwafikisha katika mkondo wa sheria wagomvi hao, Wanajeshi wetu huwa wanawapiga raia hao na hata kuwajeruhi. Tatizo hili linaleta kero, adha na kujenga uhasama baina ya Taasisi hii ya Jeshi na wananchi. Ni vyema sasa Serikali kupitia Wizara hii ya Ulinzi kuweka utaratibu maalum wa kumaliza tatizo hili ili kuwe na mapenzi, mashirikiano na mahusiano mazuri baina ya Wanajeshi na raia, kwani wote ni wananchi wa nchi hiihii moja, Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote ambao kwa namna yoyote ile wametoa michango yao katika kutayarisha hotuba hii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nijikite kutoa mchango wangu katika hotuba hii na nianze kwa kumwomba Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi apokee salamu za pongezi ambazo zinatoka kwa Askari Wanajeshi wenye we hasa wale wa ngazi za chini ambao wamenituma nikuambie kwa dhati ya nyoyo zao, wamefurahishwa sana na hatua ulizozichukua za kuwajali kwa kuwapatia mavazi mazuri ambayo kwa kweli sasa hivi yamewajengea heshima kubwa kwa kuwa popote wanapoonekana basi watu wanawaheshimu na kuwaona wametimia kimavazi kuanzia juu hadi chini yaani kuanzia kofia hadi viatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Askari wetu hawa walipenda upokee pongezi zao ni jinsi ulivyowapangia utaratibu mzuri wa kupanda vyeo. Kwa kweli wameridhika na utaratibu huo wa kila “Senior” ndio apande cheo kwanza. Katika hili wameomba Mheshimiwa Waziri uwe makini kulisimamia ili liende kama lilivyopangwa na wasitokee viongozi wachache wakavuruga utaratibu huu na kuchafua utendaji mzuri na unaotia moyo kwa Wanajeshi wetu hasa Askari wa ngazi ya chini. Pongezi hizi za Mheshimiwa Waziri hazikuja tu burebure bali alizipata baada ya kuwa ni msikivu na mfuutiliaji baada ya sisi Wabunge kutoa kero hizi na kumwomba azifuatilie kwa makini na hasa kwa Askari wa ngazi ya chini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa usikivu na uchukuaji hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie katika suala la ajira. Kuna utaratibu unaotumika katika kuajiri Wanajeshi wetu ambao kwa upande wa Zanzibar bado una matatizo makubwa. Utaratibu wenyewe ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wanatoka wataalam Tanzania Bara kuja Zanzibar kuwapima vijana wetu mbalimbali na mkakati na hali ya juu unawekwa wakati wa uchukuaji vipimo hivyo, lakini ni jambo la ajabu vijana hao wakifika Tanzania Bara wanafanyiwa vipimo upya na wengine kufelishwa na kutakiwa kurudi Zanzibar jambo ambalo linawasababishia usumbufu mkubwa vijana hao. Ni kwa nini vijana wa Zanzibar hupimwa mara mbili? Je, hao wataalam waliowatuma hawana uwezo na kama hawana uwezo kwa nini waliowatuma? Je, kule Zanzibar hakuna wataalam kutoka Jeshini wa kuwapima vijana hao? Kama Jeshi kule Zanzibar halina wataalam basi ni vyema wakaazime Madaktari kutoka hospitali ya Mnazimmoja ili wawapime vijana hao na wakimaliza iwe ndio basi na wasipimwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ninalochangia ni kuhusu suala la wastaifu. Serikali imekuwa ikiwalipa Wanajeshi wastaifu pensheni zao kwa kipindi cha kila baada ya miezi sita. Muda huu ni mrefu na mimi ningeiomba Serikali walipwe angalau kila baada ya miezi mitatu. Sambamba na hilo pensheni hizo ni ndogo mno, ningeiomba Serikali iwaongeze angalau wafikie Shs.100,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mtu msikivu basi nina imani jambo hili atalichukulia hatua za kufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ituambie ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa mipaka ya eneo la Jeshi inatambulika? Hii itasaidia kuepusha ugomvi au migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na raia. Ni vema makazi ya wananchi yawe mbali na eneo la Jeshi. Mbali na kugombea mipaka ni dhahiri kuwa itaepusha pia vifo vitokanavyo na milipuko ya mabomu Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasemaje juu ya kuwalipa wananchi walioharibikiwa kwa kupoteza nyumba zao na mali zao nyingine kutokana na milipuko ya mabomu? Wananchi wanateseka hasa wa eneo la Gongolamboto bado wanaishi kwenye mahema na vilevile mvua inaponyesha ni hatari kwa afya zao kwani magonjwa ya milipuko yanaweza kuwaathiri vibaya na mahema hayana staha kwa maisha ya kawaida ya mwanadamu. Serikali ifanye haraka kujenga nyumba za wahanga hao wa milipuko ya mabomu. Bila kuwasahau wale ambao bado wana malalamiko yao katika eneo la Mbagala ili kila aliyeathirika apate haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumbu ni vema Serikali iwaeleze vya kutosha ili Nyumbu waweze kuijendeleza kiteknolojia ili waweze kutengeneza vifaa na magari yakiwa yenye ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siridhiki na shughuli zinazofanywa na SUMA JKT. Wana miradi mingi lakini karibu yote imezorota kwa sababu ya kutopata pesa za kutosha. Pia Serikali ikiamua kulitumia Jeshi vizuri, tutaokoa fedha nyingi zinazokwenda nje hasa kwenye ununuzi wa samani, kwani tukinunua samani za Jeshi katika shule zetu zote, ofisi za Serikali zote kwa kuanzia tu mapato hayo yatalifanya Shirika hilo la SUMA JKT kuongezeka na watajiendesha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya stahili za Wanajeshi, yapo malalamiko mengi hasa kwa Wanajeshi wasio na vyeo, wanadai pesa nyingi hasa za likizo, matibabu na uhamisho. Vilevile mafao ya wastaafu ni tatizo. Serikali iwatendee haki kwani wao ndio walinzi wa mipaka yetu lakini pia makazi yao hayaridhishi nchi nzima, makazi yao yaboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa mipaka ya Ziwa Tanganyika, bado hali si shwari kwani wizi umekuwa ukiendelea na wavuvi wameendelea kuvamiwa na maharamia ndani ya Ziwa Tanganyika wanaosadikiwa kutoka nchi jirani. Ni vema Serikali ikahakikisha bajeti inatosheleza shughuli nzima ya ulinzi katika Ziwa hilo. Mara nyingi wanashindwa kufanya kazi yao kwa kukosa mafuta ya kuweka kwenye boti zao kwani uhalifu unapotokea wananchi wakiwalalamikia wao hudai hawana mafuta. Hivyo wavuvi wanaendelea kuditidilia kiuchumi wanaponyang'anywa mashine zao na nyavu zao. Naomba Serikali iangalie upya suala la kuongeza bajeti ya Wanajeshi hasa wanaolinda maeneo yote ya mipaka yetu.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mgambo wanafanya kazi kubwa sana hapa nchini lakini inasikitisha kuwa Mgambo hawapo kwenye soko rasmi la ajira. Napendekeza waingizwe kwenye mfumo rasmi wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya posho ya likizo, usafiri na uhamisho kwa wafanyakazi wa Jeshi yalipwe mapema iwezekanavyo. Haiwezekani Serikali kuendelea kuwakopa wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mgogoro mkubwa wa ardhi kati ya wananchi wa Kijiji cha Ikule katika Kata ya Mngeta, Wilayani Kilombero na JKT Chita. JKT wamepora maeneo ya wananchi na wana mgogoro wa muda mrefu, napendekeza Wizara ilifanyie kazi suala hili ili liishe sasa, naomba kauli ya Waziri.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu. Kwanza naishukuru Wizara, Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara. Nawapongeza Wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuilinda nchi yetu na raia wake. Pia nampongeza Rais kutupatia Kituo au kuanzisha Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Wilaya ya Iramba (Singida).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yarudishwe kwa vijana wetu wanaomaliza mafunzo mbalimbali kabla ya kuajiriwa au kuanza kazi. Pamoja na matatizo ya ajira au upungufu wa watumishi mfano sekta za

Walimu, Waganga, mara wamalizapo Chuo Kikuu na Kidato cha Sita, waende Jeshini. Kwa kuanzia mafunzo haya yafanyike hata kwa miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo haya yalikuwa yanamwezesha mhusika kujenga nidhamu ya hali ya juu. Nidhamu imepungua sana kwa wasomi wote. Hawajui historia ya ukombozi wa nchi yetu na Bara zima la Afrika, hawana *critical thinking*, wanashiriki tabia mbovu, madawa ya kulevya n.k

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa kuanza na suala la uwiano wa kijinsia. Hivi Jeshini kwa nini wanawake hawapewi nafasi za juu? Wakati sasa umefika Tanzania tuwe “*gender sensitive*”. Kuwa na Jeshi linaloongozwa na wanaume watupu si jambo jema na halionyeshi picha nzuri kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha ulinzi nchini hususani ujasusi wa kimataifa? Je, Serikali yetu inatumia mbinu gani ili kubaini majasusi wanaoweza kuwa ndani ya nchi yetu? Tatizo la ujasusi wa kimataifa ni tatizo linalogusa dunia nzima. Endapo hatutaweka mikakati madhubuti ya kuzuia ujasusi hakika tutakuwa tunaliweka Taifa letu pabaya. Ni lazima tukumbuke matukio ya ujasusi yaliyowahi kutokea likiwemo lile la kulipuliwa Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam na Nairobi pamoa na lile la Septemba 11 la Marekani. Matukio haya yote yaliathiri nchi yetu kwa njia moja au nyine. Nchi yetu ni lazima iwekeze nguvu nyangi katika kupigana na ujasusi unaoendelea duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kuhusika kikamilifu kwa Serikali katika kupiga vita ujasusi, mimi niko tayari kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kulipongeza na kuyapongeza Majeshi yetu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ulinzi wa Taifa licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa JKT, Jeshi hili ni muhimu sana kwa ujenzi wa Taifa na uzalendo. Hivyo naomba kujua na kupata majibu kwa nini vijana hawaendi kupata mafunzo ya JKT? Pia napenda kujua ni lini Sera ya JKT itapitishwa ili vijana wengi wapate fursa ya kujiunga na JKT ili kuongeza uzalendo kama ilivyokuwa kipindi cha Mwalimu Nyerere?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa JWTZ, napenda kupata majibu kwa maswali yafuatayo. Kwa nini kuna mizunguko ya kuwalipa Askari waliopigana Vita ya Kagera? Pili, napenda kujua juu ya Askari wanaoishi katika mazingira magumu, kwa nini

Wanajeshi wengi bado wanaishi kwenye nyumba za kizamani hasa katika Jimbo langu la Muhamwe, Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kupata ufanuzi juu ya mpango wa Serikali kuhusu mgogoro uliopo kati ya Kambi ya JKT – Kanembwa na wananchi wa Wilaya ya Kibondo hususani kijiji cha Kaziramihunda na kijiji cha Kilemba ambapo wananchi wengi walinyang'anywa maeneo yao baada ya kuanzishwa kwa Kambi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nawapongeza Wanajeshi wa JKT lakini Serikali iongeze kuwaajiri vijana wanaomaliza JKT kuliko kuwarudisha nyumbani baada ya miaka miwili. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa na Jeshi la kisasa litakalotumia teknolojia mpya za kivita ili kupunguza wingi wa wafanyakazi na bajeti kwa ujumla. Nashauri tuwe na *talented military personally* watakaokuwa wavumbuzi na kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu milipuko ya mabomu tuliambiwa imeundwa Kamati ya ndani na ya nje na Baraza la Usalama, Marekani walitoa wataalam wao wafanye uchunguzi je, nini chanzo hicho kilichosababisha, Watanzania wanataka kujuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na makampuni binafsi ya ulinzi wanapata mafunzo mbalimbali, je, Waziri atuambie ni sheria ipi inayoruhusu ufunguaji wa makampuni hayo, udahili unakuwaje na je, wanakula kiapo na wana taratibu gani za kuacha kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Ulinzi pia linakabiliwa na changamoto ya *Order* ya Jeshi ijulikanayo kama *Forces Routine Order* ambayo inawataka Wanajeshi kutooa mpaka wakae miaka sita. Kwa mazingira ya zamani ilikuwa sawa ila kwa sasa Wanajeshi wanaingia na umri mkubwa! Jambo hili linapelekea Wanajeshi wetu kuangamia na janga hili la Ukimwi na maradhi mengine hatarishi. Naomba niishauri Serikali iangalie suala hili kwa kupunguza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Mikoa ya Magharibi ikiwemo Mkoo wa Kigoma, Kagera, Rukwa na Tabora tumekuwa tukisumbuliwa na ukosefu wa amani hasa katika mapori makuu ya Malagalasi, Buselesele - Rusumo, Muleba - Biharamulo na Kibondo - Nyakanazi. Wananchi huko wananyang'anywa mali zao, wanabakwa na udhalilishaji wa hali ya juu. Tunaiomba Serikali iweke makambi katika mapori hayo na tunaomba *escorter* wa magari wawe Wanajeshi na si Polisi kwani Polisi *wame-prove failure*, hebu tujaribu na Jeshi nalo tuone na ikiwezekana iwekwe Kambi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mwambao wa Ziwa Tanganyika, kumekuwa na uovu mkubwa wa kuwaa wavuvi, kunyang'anya vifaa vya uvuvi na wananchi wa Kigoma hususani wavuvi wa Kibirizi na Katonga wamekuwa wakitoa

20,000 kila siku kuchangia ghamara za mafuta ili Wanajeshi wafanye doria, lakini pamoja na hilo bado hali si shwari katika Ziwa hilo, Serikali itafute ufumbuzi wa tatizo hili.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru kwanza kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kupongeza hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kutoa pole kwa JWT kwa majanga makubwa yaliyotokea ya milipuko ya mabomu ya Gongo la Mboto Dar es Salaam, kwani ni pigo kubwa kwa JWT kwa kupotelewa na mali zilizokuwa kwenye Kambi husika iliyolipuka. Pamoja na kupotelewa na uharibifu wa mali na majengo vikiwemo vitendea kazi kupotea, pia natoa pole kwa athari zilizojitokeza kwa wananchi waliokuwa maeneo jirani na Kambi hiyo, ama kupoteza maisha ama kujeruhiwa ikiwemo nyumba za makazi na kadhalika kuharibika. Najua JWT imepata pigo kubwa na kukabiliwa na jukumu la fidia mbalimbali na pia kuhakikisha wanaziba pengo lililobaki wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hasara hizo zilizotokea, pia natoa pole kwa uongozi mzima kwa msukosuko wa maneno mengi na shutuma za hapa na pale toka kwa wananchi na baadhi ya wanasiasa kulaumu bila kuwa na subira. Nachotaka kusema, yaliyopita si ndwele tugange yajayo na kumwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na janga hili tena. Nafarijika kuona kuwa Tanzania si nchi ya kwanza kupatwa na janga hili kwani hata juzi tumesikia Cyprus imepatwa na mkasa kama uliotokea Gongo la Mboto. Hivyo naamini ni ajali kama ajali nyingine tu. Endeleeni na kazi yenu ambayo Watanzania tunawategemea kwa usalama wa nchi yetu na amani. Natambua kazi nzuri na ngumu mnayofanya ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Endeleeni na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi ni chombo kikubwa sana duniani na ndicho kinachoweza kutwaa madaraka toka utawala wowote na wakaongoza Serikali, iwe kwa amani ama kwa mabavu, sasa je, Serikali haiwezi kuweka kanuni au sheria itakayozuia wanasiasa kulikashifu Jeshi letu na kwa maneno makali yenyе kuudhi kwa Jeshi letu, ili wasije wakavuka mipaka na kutufikisha mahali pa kuwatia hasira? Kwani sifurahishwi na maneno ya kutaka wanasiasa waingie hadi chumbani. Mfano Meremeta Serikali inasema ni mambo ya ndani ya Jeshi lakini bado yanang'ang'aniwa tu. Hili na mambo mengine mengi ni mambo ya kuvuka mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze JKT kwa utaratibu mzuri wa kuwapa mafunzo vijana na kisha wanapatiwa nafasi kwenye taasisi zingine za Jeshi kama Polisi, JW, Magereza n.k. Naomba waendelee na waongeze idadi kwani pia hata kwenye makampuni mbalimbali wanawatumia haohao vijana wanaotoka JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa suala la kuunga mkono juhudzi za Kilimo Kwanza, kwanza kwa kutoa mafunzo ya kilimo na pia kuleta trekta za kilimo

na kutoa mkopo kwa wakulima bila kujali anakotoka na mkopo nafuu. Naomba nitoe ushauri tu kuhusu mkopo wa trekta, ni vema JKT wakajiunga na Benki ya *TIB* ili wale wateja watakaotaka mkopo kwao waende *TIB*, wao wamdhulumi kuchukua mkopo kwao, hiyo itarahisisha sana kuweza kupata marejesho sahihi na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuanzisha au kurudisha JKT kwa vijana wanaomaliza elimu ya sekondari kabla ya kwenda Vyuo Vikuu umefikia wapi? Naomba kwa mujibu wa Sheria ya nchi yetu na pia kujenga uzalendo na uadilifu kwa vijana ambaa ndio wategemewa wakubwa, JKT irejeshwe kwani itatusaidia sana. Pia ule mkakati wa kujenga kambi zilizopangwa umefikia wapi ikiwemo ya Ndago?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM NASSORO KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Wenyeviti wa Kamati na viongozi wote wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nachangia hoja hii katika eneo la mazoezi ya Wanajeshi Kambini na mabomu yaliyolipuka Mbagala na Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa faraja kubwa walijotupa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa tatizo la mabomu ya Mbagala na Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, palipo na faraja hapakosi upungufu. Upungufu uliojitekeza Mbagala ni kutohana na udhaifu wa Watendaji na viongozi kwa ujumla kiasi cha kusababisha walioathirika na mabomu kutolipwa fidia zao mpaka leo wakiwemo baadhi ya Waalim wa St. Anthony Secondary School Mbagala. Wananchi wa Mbagala kuna waliofanyiwa vizuri na wengine hawakutendewa haki. Niombe sasa Serikali yangu ya CCM, ni sikivu iangalie wananchi wake kwa jicho la huruma kwani si wao waliofanya makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi katika mabomu ya Gongo la Mboto. Serikali imefanya uamuzi wa busara kuwajengea nyumba waathirika. Naipongeza Serikali yangu kwa busara walijotumia kwa kuwalipa nyumba badala ya fedha, hongereni lakini pia kuna upungufu, kuna wananchi wa Gongo la Mboto walipata madhara hawajalipwa mpaka leo. Sababu hakika wa mawasiliano ya Serikali na walioathirika. Niombe sasa Bunge letu Tukufu kuitia Wizara ya Ulinzi, watoe tamko kwa wale waathirika wenye vielelezo wakaripoti wapi waweze kupata haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije upande wa Jimbo la Temeke ambalo limezungukwa na Kambi za Jeshi ambazo ziko muda mrefu Temeke na Mwenge. Temeke nyumba za wananchi zimejengwa mpaka katika fensi ya Jeshi na Kambi kama ya Twalipo iko jirani na Shule ya Msingi Wailes. Je, Kambi hizi hazina mabomu na kama

yapo Serikali tumejipanga vipi kukabiliana na mtihani huo iwapo utatokea? Niombe sasa Serikali yetu iweke mkazo wa kujikinga kabla ya matukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na Bajeti nzima ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Ahsante sana.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa uwasilishaji mzuri wa Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Maendeleo ya 2025 kuhusu ulinzi na usalama wa nchi yetu inaelekeza kuwa amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao ni mazingira ya msingi na muhimu sana. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu hii imekuwa hazina yetu Watanzania kwa miaka 50 ya Uhuru wa nchi yetu. Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa kuiwezesha nchi hii kuwa na amani na usalama wa raia kwa asilimia kubwa (kuacha maafa ya hapa na pale).

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti nzuri na ya kutosheleza kwa sekta zote, Elimu, Afya, Miundombinu, Viwanda na kadhalika kama hakuna amani, usalama na utulivu, yote ni kazi bure. Tunaomba amani ya nchi yetu ilindwe kwa gharama yoyote. Wanaohatarisha amani na usalama wadhibitiwe kwa nguvu zote. Makundi yoyote yanayoonyesha dalili za kusababisha uvunjifu wa amani siyo tu wadhibitiwe, wapewe onyo kali kwa sababu kurudisha amani iliyovunjika ni kazi kubwa sana na ya miaka mingi sana. Majeshi yetu yasibweteke na usalama uliopo. Pia Serikali iendelee kufufua JKT kwa vijana wetu wanaohitimu shulen. Mafunzo ya mgambo yamedorora katika maeneo ya nchi yetu ikiwepo Mkoa wetu wa Manyara. Kuna utaratibu upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la Wanajeshi kuvamia maeneo ya wananchi/raia kwa mfano, Jeshi la Wananchi, Regiment ya 977 amba walipewa eneo kubwa la *Tanganyika Packers* la ekari 109 kule Arusha, Wanajeshi hao wamekuwa wanavamia na kuweka mabango maeneo ya raia kuwatishia kutoingia kwenye mashamba yao. Matokeo yake wananchi wanashindwa kulima au kuvuna mazao yao. Mwaka jana (2010) imekuwa hivyo, mwaka huu wengi hawakulima kabisa. Miradi ya maendeleo kama ujenzi wa shule na zahanati imekwama. Waziri Mkuu ana taarifa ya mgogoro huu, lakini Serikali imekaa kimya. Wananchi hawa wanaendelea kunyanyasika. Ni kwa nini basi wasipewe maeneo mengine ama kufidiwa mali zao? Mheshimiwa Waziri, naomba majibu ya mgogoro huu kwa niaba ya wananchi wa kata za Moshono, Mangarini na Ndaruma walionitura.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Arusha, Kata ya Mushono, kuna tatizo la Wanajeshi, waliingia katika eneo lile mwaka 2008 na kuweka vibao na kusimamisha shughuli zote za maendeleo ikiwemo ukulima. Mheshimiwa Rais alipokuja wakati wa kampeni mwaka 2010 aliahidi suluhisho lingepatikana mapema. Hadi sasa hivi hakuna suluhisho lolote na wananchi wanateseka sana kwani wamekuwepo katika eneo hilo zaidi ya miaka 50 na hata hivyo kufanya shughuli za kijeshi katika maeneo hayo, italeta usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo.

Nashauri Wizara husika ikishirikiana na Wizara ya Ardhi kukutana na kutatua mgogoro huo na kuwapimia wananchi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara kati ya Wanajeshi na wananchi katika maeneo yao ya kuishi na hili ni kwa sababu ya makazi ya Jeshi au wananchi wanakuwa wakiishi karibu na maeneo yao na hivyo kuleta migogoro kati yao, au Wanajeshi wanapostaa fu hujenga karibu na kambi zao na hivyo baadaye hukorofishana.

Nashauri kuwepo na Sheria ambayo itafanya maeneo yote ya Jeshi nchini yawe mbali na makazi ya watu. Kwa kufanya hivyo, tutaepusha ugomvi pia hata inapotokea milipuko ya aina yoyote basi hawatapata madhara yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa namna ya pekee JKT kwa kazi nzuri wanayofanya na pale panapotokea tatizo wamekuwa mstari wa mbele katika kutatua tatizo hilo mfano, kujenga barabara na majanga mengine. Napendekeza waongezwe mishahara yao ya wastaa fu, walipwe malimbikizo ya madai ya mishahara yao pia kuongezewa fedha kutoka shilingi 5,000 – 10,000, hii ni kutokana na kupanda kwa gharama ya maisha. Pia wapatiwe mikopo na wao ili kuweza kuendesha maisha yao ya kila siku. Makazi ya Wanajeshi pia yaboreshwe na pia kuwe na miradi ambayo itasaidia pato Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, mimi naiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Msemaji wa Upinzani alisema Serikali ilitumia pesa nyangi kumpeleka mtuhumiwa Freeman Mbewe Arusha. Naomba ufanuzi ni gharama kiasi gani ilitumika kugharamia safari hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba kama stahiki kwa Madaktari wanaofanya kazi katika Hospitali za Jeshi. Naomba ufanuzi ni kwa nini Madaktari wanaofanya kazi katika Hospitali za Jeshi hawapati nyumba au posho za nyumba wakiwemo Madaktari wanaofanya kazi pale Lugalo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza vijana wetu wapiganaji waliopo Jeshini na Makamanda wote wa Jeshi letu kwa kazi ya ulinzi wa nchi yetu. Nawapongeza Askari wetu waliopo Darfur na Lebanon kwa kazi nzuri wanayoifanya huko. Wanajenga heshima kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT ni muhimu sana kwa raia na hasa vijana. Hata hivyo, bajeti iliyotengwa kwenye maendeleo kwa ajili ya JKT ni kidogo mno na haileti matumaini hata kidogo. Zimetengwa Tshs.3Bilioni pekee ambazo haziwezi kukarabati Kambi za JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge wengi hivi sasa vijana hawakupitia JKT na hivyo kutokuwa na mafunzo maalum ya kijeshi. Nashauri kuwa mwaka huu kuwe na Programu Maalumu ya Mafunzo ya JKT kwa Viongozi wa Kisiasa (Wabunge) ambao hawakupita JKT. Mimi nipo tayari kijiungu. Ninashauri kuwa mara baada ya Bunge la Mwezi Novemba, kwa miezi miwili (2), Viongozi wa Kisiasa waende JKT. Hii iwe Operesheni Maalum, ifanyike kwa wiki nane (8) mwaka huu. Ni motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Defence College*, ni hatua nzuri sana iliyofikiwa. Ninaunga mkono sana jambo hili. Mimi naomba kuwa kwenye *intake* ya kwanza kabisa katika Chuo hiki, naomba kianze haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Meremeta, sasa iwe ni marufuku kwa Jeshi kuingia ubia na makampuni yaliyosajiliwa *Offshore Companies*, ni chanzo cha ubadhirifu na wizi katika nchi za Kiafrika. Someni kitabu cha *Treasure Islands, Tax Havens and the Man Who Stole the World*, by Nicholas Shaxson. Kitabu kinaonyesha namna nchi za Kiafrika zinavyoibwa kupitia *Offshore Companies*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Meremeta ni moja ya aibu kwa nchi yetu na isirudie tena. Baada ya uchunguzi, mbia wa Meremeta (*Triennex*) ilikuwa ni kampuni iliyoundwa maalum kwa ajili ya kutafuta fedha za miradi. Walifanya hivi huko Namibia (Mradi wa Silicon) na baadaye kufukuzwa huko. Kama *Financial Advise – Triennex* aliiwezesha Meremeta kupata mkopo kupitia *Nedcor Trade Services* ya South Africa (Kampuni tanzu ya Nedbank ya SA pia). Mkopo huu ulikuwa wa \$10m. Meremeta iliposhindwa kulipa, Serikali ikachukua mkopo huu lakini wakati wa kulipa mkopo, Benki Kuu waliilipa NedBank \$132m. Swali ni kwa nini tulipe zaidi ya mara 13 ya mkopo? Kuna riba ya 1300%, hapa ndipo nataka uchunguzi ufanyike kwa nini tumewalipa Nedbank Tshs.216 Bilioni kwa mkopo wa 16 bilioni Tshs? Nedcor imesajiliwa Mauritius, Offshore. Kwa nini Jeshi letu liingie katika *deal* kama hizi? Iundwe Kamati Teule ya Bunge chini ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi ili kupata ukweli wa jambo hili ili kubaini uozo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mtanzania mzalendo najua kama kuna uwezekano wa suala la kununua silaha lakini nataka kujiridhisha kama \$132m zote zilitumika kununua silaha. Naomba *commitment* ya Wizara kwamba itakuwa ni marufuku Jeshi kujihusisha na *Offshore Companies*, iwe marufuku kabisa. Serikali iruhusu uchunguzi wa malipo ya \$132M (Tsh.216bn) kutoka *BOT* kwenda Nedbank.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma za tiba kwa majeshi, Jeshi la Wananchi halangalii hospitali zake na kufanya hospitali hizo kuwa kama magofu ya kizamani, mfano zipo hospitali kama vile ya vitongoji katika Kisiwa cha Pemba Jimbo la Wawi, hospitali hii haina dawa wala huduma

muhimu kwa wanajeshi vile vile wanajeshi ambao wapo Pemba wanapata taabu sana kutokana na kukosa huduma sahihi za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo malalamiko ambayo suala la ajira kwa wanajeshi wapya hauzingatiwi ipasavyo. Kwa mfano, ni kweli wapo watu ambao wanatokea upande wa Tanzania Bara na kuja Tanzania Visiwani kwa ajili ya kuandikisha Jeshi, hii inafanyika chini ya usimamizi wa wale wanajeshi ambao wanavyeo vyta juu katika makambi ya Tanzania na Zanzibar na asili yao ni kutoka Tanzania Bara, hivyo mara nyingi huwaita jamaa na ndugu zao kuja kujiandikisha Visiwani Zanzibar kwa kuwa ndio wasimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 46 ukurasa wa 31 katika kuchangia utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2010/2011 limelima ekari 1,625 za kilimo chenye ubora lakini Jeshi halikuweka mkazo wowote katika Kisiwa cha Pemba na Zanzibar kwa ujumla. Hakuna takwimu yoyote inayooonesha kuwa Zanzibar inahusishwa vipi na chakula kutokana na Kilimo Kwanza. Mimi siamini kwamba utekelezaji wa Kilimo Kwanza Zanzibar unaweza kufanikiwa kwani hakuna nia safi ya utekelezaji wa kweli katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ziwanu, Chake Chake katika mtaa wa Machomane (matrekta) ipo *mess* ya Jeshi ambayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ziwanu na Majimbo yote manne ya Chake Chake, Wawi na Chonga wanaomba *mess* ile ambayo ipo katikati ya makazi ya wananchi iondoshwe mara moja kwa sababu *mess* ile imechangia uchafu, maovu, kinyaa katika jamii ya watu wa Chake Chake. Hivyo kutokana silka, mila na utamaduni wa Zanzibar *mess* ile lazima iondoshwe mara moja. Uchafu wa *mess* hii ni matokeo ya usambazaji wa UKIMWI na maradhi ya kila aina kwa vijana wetu, utumiaji wa dawa za kulevyia na uvutaji wa bangi katika eneo hilo, magoma ya disko wakati watu wapo misikitini imekuwa karaha katika eneo hilo la Matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimuombe Waziri na kumtaka aiondoshe *mess* hii kwani haina faida kwa wananchi wa wilaya nzima ya Chake Chake na badala yake ni hasara kwa jamii ya watu wa Chake Chake iliyotukuka.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kutengeneza/kuunda Jeshi la Kanda maalum litakalohusika na kilimo. Hii ni kwa kuwa wakati nchi haipo katika vita tunatakiwa kuzalisha zaidi chakula ambacho kitakuza uchumi wa Taifa na kuwapatia ajira vijana wengi.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwa kazi nzuri sana anayoifanya na Majeshi ya Ulinzi ya Tanzania kwa kuwalinda Watanzania na uaminifu uliotukuka wa wanajeshi wa Tanzania wamekuwa wa pekee. Tofauti na Polisi na Magereza kwa maoni yangu. Ukikutana na mwanajeshi popote ni mlinzi na msaada kwa kila mtu. Wanayo tabia ya kuigwa ya Utaifa hakika wana maadili ya kutosha. Pamoja na pongezi hizo nina maona yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuwatunze wanajeshi wetu kwa kuwaongeza maslahi ya posho na mshahara na pili, wahakikishiwe namna watakavyomudu maisha kisha utumishi wao lakini kutokana na mazingira yao kuwa hatarishi sana wawekewe bima na ilipwe na Serikali.

Pia wapate au pawepo na huduma za kila wakati za kuwatembelea kwa taasisi zinazoshughulika na ustawi wa jamii kama moja ya namna ya kuepuka magonjwa kama UKIMWI, TB, magonjwa yasababishwayo na pombe kali na mengine kama hayo. Mfano mzuri unaoonyeshwa na askari wetu tuutawanye nchi nzima au katika kila mkoa ikiwezekana au kila Kanda hasa maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rukwa kwa mfano ni mkoa wa pembezoni, itapendeza kuleta Kikosi cha Jeshi la JKT na yapo maeneo ya kuwaweka, mfano iliyokuwa Ruwa JKT na Milundikwa shamba la Taifa. Ni kweli maeneno haya yamekuwa sekondari na zinafanya kazi lakini hakuna kisichowezekana kama nia ipo Serikali inaweza kujenga kwa kuwatumia hawa hawa wanajeshi mahali pengine kwa ajili ya kuwahamisha sekondari zilizopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wilayani Nkasi kuwa kiteule cha Jeshi kinatusaidia sana kulinda usalama wa eneo lote la Mwambao wa Ziwa Tanganyika ambalo limekuwa halina usalama siku nyingi lakini kwa sasa kuko shwari. Naomba kiteule hiki kihudumiwe usafiri wa uhakika na kutuzwa vizuri ikiwa ni mahitaji yote ya kijamii kama maji, umeme na mahusiano mema na jamii inayozunguka na ikiwezekana kipanuliwe kiteule hiki kwa manufaa yao mazuri yaliyoleta utengamano wa usalama katika Ziwa Tanganyika eneo la Wilaya ya Nkasi.

Kuhusu namna tunavyowapata wanajeshi wetu. Nashauri kuwa na uwiano unaozingatia wilaya, mkoa, kanda katika kupata wanajeshi wetu kwa usawa kabisa na lazima tuwe makini na hilo ili tujenge Jeshi ambalo litakuwa limewianisha maeneo na ikiwezekana hata tarafa kwa msingi wa kujenga Jeshi ambalo linatokana na wananchi wote wa Tanzania. Pamekuwa na utaratibu mbaya wa kupata wanajeshi wetu utaratibu huu unaharibiwa na wale wanasaili katika hatua za wilayani na mikoani kwa tabia ya kuwasaili hata vijana ambao hutoka sehemu nyingine kwenda kuchangamkia nafasi mikoa au wilaya nyingine kwa kuwa kuna ndugu zao wanaweza kuwasaidia katika kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu pawepo na jitihada za makusudi kuelimisha, kuhamasisha ule mgawanyo mzuri unaoletwa katika mikoa na wilaya ujazwe na wenyeji/wakazi wa eneo linalohusika kwa nafasi zilitolewa kila mkoa/wilaya. Jeshi litakuwa la wote, letu na halina tishio lolote wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nianze kwa kupongeza jitihada zote zilizofanywa na Wizara hii katika kuandaa hotuba hii.

Napongeza kwa mafanikio yote yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011. Mchango wangu nitauelekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza kwa juhudini kubwa zinazofanywa na Jeshi. Kwa maana ya kipekee niipongeze Kambi ya JKT iliyopo Mkao wa Pwani kusaidia timu ya JKT Ruvu na *Ruvu Shooting* kucheza ligi kuu. Je, ni lini sasa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itasaidia JKT Ruvu hasa katika kuandaa uwanja ambao utatumika katika mechini za ligi ya *Vodacom*, ili kuzisaidia timu hizo na JKT Ruvu katika kupunguza gharama za uendeshaji timu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza shughuli zinazofanywa na Suma JKT, lakini swali langu Taarifa za Mapato na Matumizi zinakaguliwa na nani? Na je, mwaka 2010/2011 imetengeneza faida kiasi gani?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu limetoea mchango mkubwa wa kumuondoa madarakani Kanali Mohamed Bakar katika visiwa vya Comoro. Je, Tanzania kama Jamhuri ya Muungano ambayo imo katika moja za nchi ya AU imetoea mchango gani katika kukamilisha kwamba amani imerejea katika nchi ya Libya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili umoja, amani na mshikamno uendelee kudumu ndani ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni kutozitoa nafasi za Jeshi kutokana na uzawa wa mtu iwe *either* katoka Bara au Visiwani, hata hivyo kuna haja ya kutolewa nafasi za Jeshi kwa kuangalia Muungano nafasi zisitolewe upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wale ambao wameanguka kimaisha baada ya kumaliza vita vya Uganda na wakapoteza viungo na wengine kupata ugonjwa wa akili mpaka leo. Je, Serikali ya Muungano inawasaidiaje watu kama hawa kupitia familia zao. Inafaa iangaliwe kwa kina ukaribu uliopo baina ya Kambi ya Jeshi na wananchi. Suala la wanajeshi kuwa karibu na wananchi ni hatari kwa mfano, ukaribu uliopo baina ya wananchi na kambi ya Jeshi la Gongo la Mboto limeleta janga la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba utafiti utafanyika ili kuikwepesha Tanzania na majanga kama haya.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mungu, muumba wa dunia na vyote vilivyomo ndani ya dunia. Yeye ndiye aliye tuwezesha Wabunge sote kuwepo hapa tukiwa hai na tukiwa wazima. Pia nichukue nafasi hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazungumza kuhusu ajira za Jeshi hili ambazo huhusisha vijana wa pande mbili za Muungano yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Vijana wengi wa Zanzibar wanahamu kubwa ya kujiunga na jeshi lao la ulinzi ili watoe mchango katika Taifa lao. Utamaduni tulio uzoea mara baada ya Muungano nafasi za ajira zikitolewa kwa wingi kwa vijana wa Zanzibar ikiwa ni wahusika wa

Jamhuri ya Muungano. Hizi nafasi za ajira ndani ya Jeshi la Ulinzi kwa upande wa Zanzibar zimekuwa kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar nafasi za uajiri ni kidogo na hazitoshi, vijana wengi sana ambao wanataka kutoa mchango wao kupitia taasisi hii muhimu wanakosa kabisa. Ni wajibu kuangalia upya ajira hii adhimu kwa kila kijana shababi wa Taifa hili hasa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia muingiliano mbaya kati ya kambi za Jeshi letu na makazi ya raia, kambi za Jeshi letu kwa sasa hivi zimechanganyika na makazi ya wananchi jambo ambalo ni hatari sana kwa maisha ya raia. Kutokana na Sheria zetu kutosimamia vizuri wananchi wanajenga ovyo ovyo karibu ama ndani hasa ya kambi pasipo kuchukuliwa hatua zozote. Matokea yake imekuwa kama kawaida tu Jeshi kuchanganyika na raia hasa sehemu za mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivi ni kukiuka miiko ya Jeshi na ni hatari kwa Taifa letu. Athari ya muungiliano wa kambi za jeshi na raia imeonekana ilipotokea milipuko Mbagala na Gongo la Mboto. Watu wamepoteza maisha, wamepoteza viungo vya miili yao pamoja na mali. Matokeo kama haya ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pamoja na hali ngumu ya usalama. Inapasa kufanya juhudzi za makusudi kujenga miundombinu mizuri kutofautisha sehemu za kambi na sehemu za makazi ya wananchi. Tuepushe matatizo makubwa wakati wa majanga ya bahati mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo limo ndani ya jeshi letu ni matatizo ya mipaka kati ya kambi za jeshi na makazi ya raia. Tatizo hili limekuwa kubwa ambalo linajenga uhasama, uadui kati ya raia na jeshi letu ambalo ni jambo la hatari kwa Taifa lolote ambalo hapa mashirikiano baina ya raia na vyombo vya ulinzi. Naomba Serikali izingatie tatizo hili kwa haraka sana ili kujenga maelewano mazuri kati ya raia na vyombo vyetu vya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BRIG. JEN. MST. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia mia hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na uzima leo na kuniwezesha kuchangia hoja hii ambayo ninaiunga mkono. Pia niwashukuru wanangu Evelyn na Joyce ambao wapo na mimi katika shughuli hizi za kazi, wananiyvumulia lakini kwa vile wanajua nipo kazini. Nimshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa maendeleo ya Taifa hili, lakini pia kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Tanzania ni jeshi linalojitoa kwa kuwajibika. Jeshi letu makini linalinda wananchi wa Tanzania japo kwa mishahara na makazi duni. Jeshi la Tanzania japo linawajibika kwa ulinzi wa wananchi, naomba Ulinzi huu usiishie kwa vita tu, hapa ninamaanisha kwamba usalama wa wananchi pia uzingatie kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi za silaha za vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia ulipukaji wa mabomu huko Mbagala na Gongo la Mboto na vifo kadhaa vilitokea, wananchi kadhaa waliumia na wengi kupoteza makazi. Napenda kuwapongeza wale wote waliojitoa kwa hali na mali kwa wahanga wote wa Mbagala na Gongo la Mboto. Pamoja na hayo naiomba Serikali idhibiti hali hiyo ili isitokee tena katika maeneo hayo na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu pia ni vizuri suala la JKT likarudi maana linajenga kujiamini, kujitambua, kuwa na nidhamu kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012. Napenda kupongeza Jeshi la Ulinzi kwa kuimarisha amani na kulinda mipaka yetu; pongezi mahususi naitoa kwa Jeshi kulinda mipaka ya Jimbo la Manyovu ambayo inapakana na nchi ya Burundi. Naomba nijielekeze kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, watu/vijana wa Jimbo la Manyovu (Kasulu) wanaomba kupewa fursa ili nao waweze kuchaguliwa kuijunga na Jeshi letu la Tanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi achukue ombi hilo kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuona umuhimu wa kurudisha JKT kama ilivyombwa na Wabunge wengi baada ya kuona utii wa wananchi kwa nchi umepungua. Naomba Serikali ianze kuwapa mikopo ya muda mrefu ili wanajeshi waweze kujenga nyumba kwani nawaona uraiani wakipanga na kukaa sehemu ambazo haziwastahili. Ninayo imani na Jeshi letu na Wizara nzima katika kulinda mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ajira ndani ya chombo hiki unalalamikiwa na wananchi katika maeneo mengi ya nchi na Taifa letu. Historia inaonesha huko nyuma askari walikuwa wanatoka katika maeneo maalum. Sasa ajira hiyo ipo mikononi mwa askari wenyewe na imetolewa mikononi mwa raia wenyewe. Hivyo familia za askari ndiyo zinazopata ajira hiyo ndani ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Uhuru vijijini ndiko kulikokuwa kunachaguliwa vijana wetu kuijunga na Jeshi/Majeshi yetu. Utaratibu huu urejeshwe tupate askari wanaotokana na wananchi wenyewe na sio askari walioko kambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutotengwa kwa fedha kwa ajili ya kujengwa kwa kambi mpya za JKT hususani Kambi ya JKT Sanjaranda, Itigi kumenisikitisha sana. Kambi za JKT ndizo zinazopika vijana adilifu na wenyewe uzalendo. Kilio hiki kimezidi baada ya vijana wetu wengi hivi sasa kukosa uzalendo na uadilifu kwa nchi yao. Napenda kupata maelezo ya kina ni kwa nini fedha hazikutengwa mwaka 2011/2012?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupata *commitment* kama kweli Kambi ya Sanjaranda itajengwa mwakani? Vijana wetu wengi wamezagaa hawana pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri wa Ulinzi. Naunga mkono hoja kwa sababu ya kazi nzuri sana inayofanywa na Jeshi letu la Ulinzi, nchi yetu ipo shwari. Hali ya Ulinzi na Usalama ni nzuri sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri inayojieleza kwa ufasaha. Tunalipongeza Jeshi hili kwa uzalendo wake katika suala zima la ulinzi na mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukakamavu wa askari wetu unasifika ulimwenguni kote kwa namna ambavyo askari wetu walivyoshiriki na wanavyoshiriki katika kusimamai Uhuru wa wale wote wanaoonewa duniani kote. Jeshi letu limeshiriki katika kuleta Uhuru kwa nchi za Afrika kama Msambiji, Cape Town, Zimbabwe, Namibia na Afrika ya Kusini. Askari wetu wameshirika ukombozi katika Uganda, ukombozi Anjoum. Ulinzi wa amani katika Siera Leon, Lebanon, Dafur, *DRC* na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliongeze uwezo Jeshi letu kwa kulipatia uwezo wa kifedha na vifaa ili kulipatia Jeshi letu uwezo wa utendaji kivita. Ni imani yangu kuwa Jeshi letu litakuwa na mtazamo mahususi kwa kuangalia uwezo wa kijeshi wa nchi majirani zetu, wanavyojilimbikizia silaha. Majirani zetu wanashabaha gani katika kujilimbikizia silaha za kijeshi kwa maana ya nguvu za anga kwa maana ya ndege za vita, jeshi la nchi kavu na jeshi la *Navy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji ni muhimu kwenda na teknolojia za kisasa na vilevile matumizi ya rada zenyet uwezo mkubwa wa kuona umbali mkubwa zaidi kama ilivyo kwa nchi jirani ya Kenya hata nchi ndogo kama Rwanda zina vitu kama hivi vyenye uwezo kuliko wetu, lazima tuone kuna nini kwa wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu (Tanzania) ni nchi kubwa inapaswa kuonyesha kuwa ni Taifa kiongozi katika sekta ya ulinzi ili na wengine waendelee kujifunza kutoka kwetu katika hili kuwa na jeshi lenye uwezo mkubwa wa uzalendo na ustahimilivu kama unavyoonyeshwa na Jeshi letu la kuwa chombo cha kusaidia wananchi wakati wa dharura. Aidha, mikakati yote ya uendelezaji wa Chuo cha Taifa cha Uongozi (*National Defence College*) mkakati wa ukamilishaji wa chuo hiki uanze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ombi langu kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa liimarishe ushirikiano uliopo baina ya JWTZ na vikosi vya SMZ, JKU, KMKM, VOLANTIA ili kupatikana usalama wa uhakika kwa Zanzibar. Wizara kuyafanya matengenezo katika kambi mbalimbali katika sehemu ya Zanzibar ili zilingane na hadhi ya Jeshi letu la Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa Bajeti kutilifanya jeshi letu liweze kutekeleza majukumu yake ya kijeshi katika karne hizi za sayansi na teknolojia. Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuharakisha upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo yanayotumiwa na wanajeshi wetu. Wizara ifikirie kuongoza kima cha gharama za chakula kwa askari, ambacho kitasaidia kuwapatia utulivu askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifikirie kuwapatia magari mapya ya maji katika JWTZ – Zanzibar; katika Bajeti hii Wizara iipatie JWTZ – Zanzibar dawa nydingi ambazo husaidia kuwatibu raia pia katika Hospital za Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uingizwaji wa vijana katika JWTZ – kumekuwa na tabia ya kuwapima mara mbili kwa vijana watokao Zanzibar ili kujiunga na Jeshi hii husababisha usumbufu mkubwa kwa vijana wetu kutoka Zanzibar pale wanafeli katika vipimo vya pili ambavyo hufanyika Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondosha usumbufu huu kwa vijana wetu, naomba Wizara itumie Hospitali ya Jeshi ya Bububu kwa kupimwa vijana hao ili kuondosha usumbufu huo. Pia wale vijana waliotoka Zanzibar ambao wamebahatika kupata nafasi JKT wapewe nafasi za mwanzo katika ajira za JWTZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya Bajeti. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekubali kurejesha Kambi za JKT, naomba nipendekeze Kambi hizo ziwe kama ifuatavyo:-

Hapo awali madhumuni makubwa ya uanzishwa wa Kambi ya JKT yalikuwa ni kutoa mafunzo ya awali ya ulinzi na uchapakazi kwa vijana ili kuwatayarisha kwa maisha yao ya baadaye. Lakini ni dhahiri kuwa kiutendaji madhumuni haya yalivurugwa kwani wale ambao kweli wanahitaji mafunzo ya awali ndio ambao hawakulazimika kushiriki na wale ambao walikuwa na uhakika wa ajira ndio waliolazimika kujiunga. Waliosamehewa ni wale wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne bila kujiunga na chuo chochote. Wakati waliolazimika ni wale waliomaliza kidato cha sita ama wenye elimu ya juu zaidi. Ni wazi basi kuwa mfumo uliotumika haukuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uendeshaji wa programu mbalimbali katika kambi hizo ulilenga zaidi katika kukomoana na kudhalilishana na hivyo matumizi ya akili yalizingatiwa kwa kiwango kidogo. Haishangazi basi kuwa na makambi ambayo kimsingi yalitakiwa yawe na uwezo wa kuzalisha kwa ajili ya kujiendesha na ziada, hatimaye yalionekana kuwa ni yenye kuliingizia Taifa hasara kubwa na kulazimika kusitisha sehemu kubwa ya program zake. Kwa kweli hata mimi nilienda JKU na lilinisaidia sana na sipendi life kwa kasoro hizo nilizo zieleza.

Kwa hiyo, umuhimu wa JKU upo sana ila kinachohitajika ni marekebisho ya msingi. Pia ili kuleta marekebisho yenye tija, napendekeza yafuatayo:-

Kwanza utaratibu wa uendeshaji wa programu kwenye vituo hivi ubadilike ili kuondoa dhana kwa vijana, wazazi na watoa mafunzo kuwa hivyo ni vituo vya mateso kwa vijana wanaomaliza masomo yao. Katika kutekeleza azma hiyo, kwanza kabisa muundo wa awali utabdalishwa na badala ya kujulikana kama Kambi sasa vitaitwa Vituo vya Maandalizi kwa Vijana ili kulitumikia Taifa.

Pia itenganishe kabisa masuala ya uajiri, fursa za masomo na suala la kujiunga na vituo hivyo, vifanywe vituo hivyo kuwa ni huduma muhimu ya miaka miwili katika kutoa mafunzo ya awali ya kijeshi, ukakamavu, kazi za uzalishaji (*Vocationa Training*), Lugha za Kiingereza, huduma za mwanzo (*First Aid*), sanaa mbalimbali, udereva, michezo, pamoja na stadi zinazohusiana na shughuli za uokoaji (*Rescure Operations*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe ruzuku mwanzo wakati wa maandalizi, na mikakati iwekwe kukiwezesha kila kituo kiwe kinajiendesha chenyewe. Serikali iweke vituo katika kila mkoa kwa ajili ya uandikishaji na wale wote ambao wangependa kujiunga na vituo hivi na iwashauri vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne na kukosa nafasi ya kuendelea na masomo katika shule za kawaida na vyuo wajiunge. Iweke utaratibu kuhakikisha kwamba fedha zote zitakazozalishwa na vijana kutokana na miradi mbalimbali ya uzalishaji baada ya kuondoa gharama kwa ajili ya kupewa vijana wakati wa kuhitimu ili ziwasaidie kununulia zana mbalimbali zinazohusiana na stadi walizojifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu Kambi zetu za JKT zitakuwa za kisasa zaidi na kwa utaratibu huu vijana wengi watapata ajira.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi ni chombo muhimu sana katika Taifa letu. Nalipongeza kwa kazi nzuri ambayo Jeshi hilo limekuwa likifanya wakati wote wa amani na wakati wa uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itamke ni vipi wanajeshi wastaa fu watapewa msaada wa kuwasaidia kuweza kumudu maisha pindi wanapokuwa mapumzikoni, nasema hivyo kwani nimeona mimi mwenyewe baadhi ya askari waliostaa fu jinsi wanavyohangaika. Naomba Serikali itoe upendeleo maalum wa namna ya kuwaenzi askari wetu amba walijitolea maisha yao yote kutumikia Taifa. Aidha, napendekeza umri wa kustaafi kwa askari wetu usiwe sawa na watumishi wengine, kutegemeana na ujuzi wao, ingefaa kuangaliwa kwani tunaweza kupoteza watu muhimu ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kurudishwa Jeshi la Kujenga Taifa kuwa liwe ni lazima. Muundo wa Jeshi hilo uwe ni hiyari kwa vijana wa jinsia zote. Kwa sasa hivi hakuna sababu ya kufanya vijana wote kwenda JKT kwa sababu vijana wamehamasika kujiunga na Jeshi bila kulazimishwa. Aidha, kwa hali ya maradhi ya UKIMWI ulivyoenea nchini na duniani, kuwarundika wasomi wote wanaohitimu elimu ya juu kwenye kambi za Jeshi huenda tutawapoteza wasomi wengi na hasa mabinti kulingana na tabia za huko Jeshini, wote tulio pita huko tunafahamu. Waende kwa hiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za JKT muhimu zikatolea kutoka kwa Watanzania wenye sifa; kutoka pande zote za Tanzania na wale watakaonekana wanafaa wachukuliwe kujiunga na JWTZ.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nitamke kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichangie hoja ya matatizo ya mipaka baina ya Jeshi na raia. Nachingwea kuna mgogoro wa mpaka kati ya Kambi ya Majimaji na wananchi wa kijiji cha jirani. Jeshi limechukua ardhi ya kijiji na kuwaathiri raia zaidi ya 65. Hali hii haijaka sawa. Jeshi liachie ardhi ya raia ili utulivu urejee. Aidha, upo mgogoro mwengine kati ya Kambi ya JKT Nachingwea na raia wanaoizunguka Kambi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tafadhali Mheshimiwa Waziri, achukue hatua za kutatua matatizo haya ya migogoro ya mipaka baina ya Jeshi na vijiji vinavyozunguka kambi za Jeshi.

**MHE. ENG. GERSON LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu makambi ya Jeshi karibu na wananchi. Baada ya matukio mawili ya milipuko ya mabomu Gongo la Mboto, nashauri jeshi letu na baada ya ongezeko kubwa la wananchi na hasa Dar es Salaam litafute maeneo ya mbali na makazi na hasa hifadhi ya mabomu na kama ni lazima kuwa hapo basi aina ya silaha ziwe za kisasa zaidi ambazo tahadhari kubwa itakuwa imechukuliwa. Kwa kweli Watanzani watafurahi sana kama hatua za haraka na za uhakika zitachukuliwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, umri wa kustaafu Jeshi kwa wana taaluma ungeendana sawa na watumishi wengine wa umma mfano, wahandisi, madaktari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja ya Bakey, zamani Jeshi walikuwa nayo mengi kwenye *stock*, sasa hivi hawana, nashauri kwenye Bajeti hii muweke ununuzi wa madaraja haya, yatatusaidia kila tukipata maafa.

**MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kwa nini vyeti vinavyotolea na vyuo vya Jeshi mfano, udaktari, ufundi na kadhalika havipewi au kavingizwi kwenye utambuzi wa *TUC*. Vyuo hivi vinatoa elimu ya juu sana na vina uwezo mkubwa.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongea Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa nafasi hiyo. Sina budi kulipongeza jeshi letu kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la JKT vijana wanaotakiwa kuingia kambini suala la muhimu sana kujulikana sifa zao na vigezo vyao. Suala la vijana kuwekwa kambini nirudie kama jambo hili linamfanya kijana wa Tanzania kujua historia ya nchi yake pamoja na ukakamavu. Kufanya hivyo kuelekea kuwa na Taifa imara na lenye nguvu na wenye vijana majasiri na wenye kuweza kulinda Taifa letu.

Pamoja na changamoto nyingi katika Jeshi letu yalioelezwa katika ukurasa wa 41 kuna baadhi ya mambo yanepewa kiapaumbele mfano, suala la vifaa vya kijeshi ni suala muhimu sana sawa na maji, umeme katika makambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Ulinzi imeishauri nini Serikali au inaishauri nini Serikali juu ya umuhimu wa mahitaji muhimu ya Jeshi kukosekana kwake. Suala la vifaa vya kijeshi ni vya lazima katika nchi yetu na sio suala la changamoto kama inavyosomeka katika kitabu cha Bajeti ukurasa wa 41.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Zanzibar tuna maswali tunajiuliza tungependa Waziri atupatie majibu. Wizara ya Ulinzi ni kati ya Wizara za Muungano. Kwa maana hiyo tu basi, kati ya Watanzania wangapi wanaotoka Zanzibar katika Jeshi hilo? Kwa nini vijana wengi wa Zanzibar baada ya kozi za kijeshi hawarudi Zanzibar hupelekwa mikoa ya mbali au mwishoni mwa Tanzania tofauti na vijana wa Bara wachache ndio wanaoletwa Zanzibar kigezo kipi kinatumika katika kuwatawanya vikosini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tujue kwa uwazi na ziwekwe wazi sifa za JKT kujiunga zisiwe siri, kufanya hivyo kutapelekea vijana kuwa na imani na Serikali yao na kuondokana na dhana iliopo sasa kwamba kijana huwezi kupata JKT mpaka ujulikane na wakubwa. Zana hii potofu, Wizara itafute njia ya kuitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo langu kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa warudishe JKT ya zamani na sasa waboreshe kwa kuwapa mafunzo maalumu ya ufundi stadi na ukakamavu. Kufanya hivyo vijana wengi wangeweza kujajiri na wengine kuajiriwa na jeshi lenyewe kama ilivyo hivi sasa. Kufanyika kwa haya ni kupunguza mzigo Serikali Kuu. Pamoja na ajira kwa vijana, Wizara ifungue viwanda vyatia kusindika matunda na viwanda mbalimbali ili kuweza kutumia vijana wa JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Wizara ya Ulinzi kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti. Naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nianze kwa kupongeza kazi nzuri ya Wizara hii na pamoja na kuunga mkono hoja naishauri Serikali katika mambo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa amani ni vyema nguvu kazi ya Jeshi letu ikatumika katika ujenzi wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuongeza nguvu kitengo cha Ufundu cha Jeshi – Nyumbu ili kiongeze uzalishaji na hasa bidhaa na vifaa ikiwa pamoja na magari. Naishauri kuwekeza kwa kiwango cha juu ili eneo hili la ufundi liwe la kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha au kuboresha kitengo cha ujenzi wa barabara ili kiwe kikubwa na chenye uwezo wa Kitaifa kujenga barabara za vijiji na miji midogo. Kwa kufanya hivi Jeshi litatoa mchango wake lakini itapunguza urasimu wa kupata wakandarasi kwa msingi kwamba mkataba wa kufanyakazi utasainiwa kati ya Wizara ya TAMISEMI na Jeshi na kuzihakikishia Halmashauri kujengewa barabara zake katika ubora stahili kwa fedha kinyume na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani kwa kazi nzuri ya Jeshi kwa kuanzia naomba ufundi wa ujenzi wa daraja za chuma uje Rufiji hasa katika maeneo ya Delta ambayo daraja zake hazipitiki na zinapojengwa hazidumu kwa kutokuwa na ubora stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni zito sana kwa Wanajeshi wetu hasa wenye vyeo vya chini, wameshastaifu wengi wao huwa hawana hata pahala pa kulala na kazi maalum za kujivunia kupata kipato kwa siku za baadae. Kwa kuzingatia wengi wao wana nguvu na taaluma na ili wasijihushe na mambo ya kihalifu napendekeza kwanza wapewe mkopo huku wakikatwa mara tu wanapoajiriwa ili waanze kujenga nyumba na makazi yao ya kudumu wakati wao wanakaa kambini.

Pili, kuwadhibiti na kutangatanga kwa kufunguliwa *Cooperative* (Ushirika) na kutumia nguvu zao kwa kuzalisha mali badala ya kuwa *watchman* au waganga na hata wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi maalum natoa kwa mstaafu shujaa Bwana Juma Ali Khamis wa Zanzibar ambaye hana miguu kuanzia kwenye mapaja aliumia na bomu vita vya Kagera. Kwa wenyewe ulemavu, kama ni wachache basi wasaidiwe kwani bado wanategemewa na familia zao. Busara yeche angepatiwa bajaji ya kutembeza wageni ili ajikimu na maisha. Anakaa Saateni, Kambi ya JKU Zanzibar, Mheshimiwa Waziri anamfahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uajiri kuna minong'ono mingi juu ya uajiri kwa wanajeshi JWTZ kuwa namba ya waajiriwa toka Zanzibar ni ndogo. Hili limekuwa kero mionganoni mwa Wazanzibar. Ni busara uajiri ukafikiriwa kutokana na *minimum requirements* (vigezo vya chini) ili malalamiko haya yasiendelee. Vivyo hivyo juu ya upandishwaji wa vyeo. Wengi wanafika hata kuwahesabu watendaji jambo ambalo nadhani linaweza (makamanda) kuleta vuguvugu baya katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mipaka na *beacons* kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyojieleza, matatizo ya *beacons* yamejitokeza hata katika mazungumzo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwelekeo ulivyo na msimamo wa kuungana kiuchumi, kisiasa na kijamii. Jambo hili linaweza kuleta kutofahamiana baina ya nchi zetu. Wazo langu, kipaumbele kitolewe katika kulimaliza tatizo hili la sivyo kero zitazidi kuendelea na mtangamano wa Jumuiya unaweza kuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Jeshi letu jinsi lianvyojitokeza wakati wa maafa na kusitiri waathirika, ila napendekeza Jeshi pamoja na Kitengo cha Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu washirikiane kutoa taaluma za msingi (*basic emergency preparedness and management*) kwa watumishi wa sekta nyingine za Serikali kama inavyofanywa kwenye UKIMWI, ikiwezekana hata katika vyuo na (*simulation events and cases*) zifanywe kuleta umahiri na utayari kwa wananchi ili maafa yasiwe makubwa pindipo janga likitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu na mazoezi ya pamoja ni muhimu kikanda. Ni imani yangu kuwa ulinzi wa pamoja ki-EAC ni imara zaidi kuliko nchi moja. Itakuwa vigumu adui kututeka kama ilivyotokea Afrika Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo, kutokana na ukuaji wa sayansi ya kompyuta na mapigano yake kiutandawazi (*cyber technological war*) ni vema Jeshi likaongeza utaalamu wa ugunduzi wa hatari zinazoweza kutukabili. Ulinzi uwe imara hata katika matumizi ya *twitters* na *facebook* katika kuleta *propaganda* za chini kwa chini zisizo bayana. Hatari hiyo hivi sasa iko bayana kwenye *blogs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa uchimbaji wa *Uranium* utanza, inafaa Jeshi pia litayarische wataalamu wa kugundua na hata kuzima matumizi mabaya kiulinzi katika nyanja zote (uchimbaji, usafirishaji, *storing* na *processing*) itambulike

kuwa sio watu wote wema wako watakaotumia haya kwa njia haramu ya kuangamiza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba yake, nami napenda kuchangia machache katika hotuba hii kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuwa Jeshi la Ulinzi ni muhimu sana katika kuhakikisha usalama wa mipaka ya nchi yetu lakini kumekuwepo na malalamiko makubwa sana hasa kutoka kwa wananchi wanaoishi katika maeneo haya kwa mfano, katika mikoa ya Kagera na Kigoma kumekuwepo na malalamiko ya uvamizi unaofanywa na kundi la wahalifu toka nchi jirani za Burundi na Rwanda kwa wilaya za Ngara na Karagwe ambapo wananchi wamekuwa wakiporwa mali zao. Je, askari wetu wa Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa wanawasaidiaje wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko toka kwa wavuvi katika maziwa yetu kama Ziwa Tanganyika, kuwa wamekuwa wakivamiwa na kuporwa mali zao wawapo ziwani na watu ambao wana silaha za kisasa. Je, wavuvi hawa wa Tanzania wanalindwa vipi na Jeshi letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali ya milipuko ya mabomu Gongo la Mboto Dar es Salaam – katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 3 ameelezea juu ya ajali ya Gongo la Mboto na kuwapa pole wahanga wote na hasa zile familia zilizopoteza baadhi ya wanandugu. Lakini watu wa Gongo la Mboto au wananchi wa Gongo la Mboto hadi leo wapo ambao bado wanaishi kwenye mahema ambayo baadhi yao yameharibika na yanapitisha maji pindi mvua zinaponyesha na wana watoto wadogo. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika juu ya suala hili na Serikali bado inaendelea na upembuzi, mchakato hali ya kuwa wananchi wetu wanateseka, tunatambua kuwa jukumu hili si la Wizara tu bali ni la kushirikisha Wizara tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, urejeshwaji wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, nakubaliana kabisa na wazo la kurudishwa ama kurejeshwa kwa mafunzo ya Jeshi la JKT kwa malengo haya mazuri yaliyoandikwa kwenye hotuba ukurasa wa 47 ambayo ni kudumisha umoja wetu wa Kitaifa, hususani kutoa mafunzo ya uzalendo, mshikamano, usawa na ukakamavu kwa vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba mafunzo haya yaangaliwe pande zote za nchi yetu bila ya kuacha malalamiko kama ilivyo hivi sasa watu wengi wamekuwa wakilalamikia juu ya usaili wa vijana katika Jeshi letu kuwa kuna ubaguzi na hata kupitia katika wilaya zetu bado kuna malalamiko kuwa wazawa wanaachwa na kuchukuliwa watoto wa watumishi ambao wanawaleta kutoka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapongeza wanajeshi wetu wa Jeshi la Ulinzi hapa Tanzania kwa utendaji wao wa kazi ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Pia kujitolea kwa moyo mkunjufu kufanya kazi mara tu inapotoka amri kwa mkuu, hiyo ndiyo hali thabiti ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watu hawa ni muhimu basi sote tuone umuhimu wao wakati wanapokuwa kazini na mara baada tu ya kustaafu, kwani wengi wao wanapata matatizo sana baada ya kustaafu. Mfano, kuna mwanajeshi alipata ugonjwa wa kiharusi na haikupita muda akavamiwa na mahali ambapo alikuwa anatunza kumbukumbu zake ni ndani ya kisanduku chake kidogo. Wezi walibeba kisanduku na yeje akabaki akiwa hana fahamu bado kwa ajili ya ugonjwa. Jalada lilifunguliwa polisi la uvamizi na namba wanayo. Mwanajeshi huyo mstaafu ni mgonjwa mpaka leo na pensheni yake hajawahi kupata hata mara moja na familia yake haijui nini ifanye, mkewe kwa sasa na yeje ni mgonjwa, wote wana hali mbaya. Namuomba Waziri, wawe wanatoa utaratibu wa watu kama hawa nini wafanye, kwani huenda wako wengi na hawajui cha kufanya. Hata kama kipindi cha redio mara mbili kwa mwezi au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara hii iweze kumaliza matatizo yake ya ardhi, kwani kuna matatizo katika baadhi ya maeneo baina ya Jeshi na Wananchi, pia waweke mipaka ya kudumu ili tatizo hili lisijirudie rudie. Jiji la Mwanza katika Wilaya ya Ilemela, kata ya Ilemela mtaa wa Buyombe (kijiji) kuna matatizo makubwa, tunaiomba Wizara ilione hilo. Pia utaratibu wa kuanzia huko wilayani, kwa vijana ambao wanahitaji kujiunga na Jeshi, ni upendeleo mtupu. Jeshi letu hawako sawa sawa, ukifuatilia utamkuta mtoto wa jamaa, ndugu au rafiki. Msikubaliane na watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana wanajeshi wetu kwa kuruhusu wananchi kupata matibabu katika maeneo yao ya hospitali. Imekuwa mkombozi, kwa wananchi na kuwa kimbilio lao. Ni vizuri Bajeti yao iangaliwe kwa mapana yake ili nao waweze kuijendesha, pamoja na watu ambao sio mionganoni mwa familia zao kutibiwa. Mnaonyesha uzalendo mkubwa katika jamii ya Watanzania. Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwanza kabisa kwa kuelezea masikitiko makubwa juu ya unyanyasaji mkubwa unaofanywa na Jeshi la Ulinzi kwa maana ya Wanajeshi wa Kambi ya Nyandoto na hasa wale walio Liande kwenye kijiji cha Ronsolti katika wilaya ya Tarime na cha kufedhehesha zaidi ni pale Waziri wa Ulinzi aliponkuu kuwa Tarime na Rarya vimekithiri kwa uvamizi wa maeneo ya Kambi za Jeshi. Ni matumaini yangu hiki kijiji cha Ronsolti si moja ya waliovamia bali wamevamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ hawana hati yoyote inayoonyesha kuwa walipewa eneo hilo la Ronsolti – Msati kwenye kata ya Nyamisangu katika mamlaka ya mji mdogo wa Tarime. JWTZ walikuja Tarime mwaka 1978 ambapo walikabidhiwa eneo la *Nyandoto Farm* lililokuwa na majengo ya kutosha na hii kambi ipo kando ya Mto Mori yaani ukitoka Tarime Mjini kwenda kwenye Kambi wanawajibika kuvuka Daraja la Mto Mori ambapo mwaka 1979 Mto ulijaa maji. Kutokana na mafuriko ya mvua nyingi na hii ilipelekea wanajeshi kushindwa kupata mahitaji muhimu kutoka upande wa pili (Tarime

Mjini). Hii ilipelekea wanajeshi wa JWTZ kuomba msaada wa hifadhi kwa muda hadi daraja litakapojengwa ndipo warudi kwenye kambi yao rasmi walipopangiwa na Serikali kuishi na ilijulikana kama 28KJ Nyandoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1990 kambi hii ilivunjwa na askari walishindwa 27KJ Makoko pamoja na kambi nyinginezo. Cha kushangaza JWTZ walirudi na kuanza kuwavaa wanakijiji cha Ronsolti kuhama na kuwa wabomoe nyumba zao. Napenda Waziri atueleza ni kwa nini JWTZ imetoa hadi mabango na kuwazuia wanakijiji hawa wasifanye shughuli zozote zile kama kilimo, kukata miti wala kuchimba choo tangu mwaka 2008?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba maelezo kwa hili na lini wanajeshi hawa watahama na kurudi kwenye eneo lao 28KJ. Kwani tarehe 21 Julai, 2010 Mwenyekiti wa kijiji cha Ronsolti (mtaa wa Msati) waliandika barua kwa Serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu na Mkuu wa Majeshi ambapo walijibu kwa barua yeny Kumb. Na. MMJ/1000-0 (*COfs*) ya tarehe 9 Septemba, 2010 kutoka kwa Mkuu wa Majeshi na Kumb. Na. MOJ/MZAIG – 105/Vol./153 kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wakiwaomba wananchi wasiende mahakamani kwa madai malipo na fidia zinashughulikiwa pamoja na michoro kuwa wasiende mahakamani kitu ambacho wananchi hawaafikiani nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba sana Serikali ichukue hatua ya kuwaondoa wanajeshi wale pale ili kuwaondolea madhara ambayo wananchi wanayapata ikiwemo kunyanyaswa kwa kupigwa, kuzuiliwa kufanya shughuli zao za maendeleo, watoto wa kike kubwakwa na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) kwa kazi kubwa sana ambayo imekuwa ikifanya huko Zanzibar. Napendekeza Jeshi hili (JKU) liwe ndilo Jeshi la kusimamia ulinzi na usalama wa nchi badala ya JWTZ kuingilia ulinzi wa Zanzibar.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Matatizo mengi yanayojitokeza kati ya Jeshi na wananchi, wengi wanachukua maeneo ya Jeshi na kujenga makazi yao. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali na Wizara ichukue hatua za kuwahamisha wakazi hao wanaoishi karibu na Kambi za Jeshi. Kama Serikali na Wizara watakuwa makini kuhusu suala hili hata milipuko inayotokea katika Kambi za Jeshi haitawaathiri wananchi kwa sababu watakuwa mbali na maeneo ya Kambi za Jeshi. Tumeona kama vile mabomu yaliyolipuka katika Kambi ya Jeshi Mbagala na Gongo la Mboto yamepoteza maisha ya Watanzania wengi na kusababisha ongezeko la walemavu na watoto yatima. Watoto hawa wamekuwa mzigo kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kuongelea kuhusu misaada inayotolewa na wafadhili mbalimbali kuwasaidia waathirika wa mabomu haikufikia walengwa na vile vile imetolewa kwa ubaguzi kwa itikadi ya vyama vyaya siasa. Tukumbuke kwamba

walioathirika ni Watanzania na Serikali inavyopata janga kama hili la Kitaifa hivyo basi misaada itolewe kwa uwiano bila kujali itikadi ya vyama vyaa siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu ajira katika Jeshi letu la Kujenga Taifa (JKT). Kwa upande wa Zanzibar kumekuwa na malalamiko kuhusu vijana wetu wa Zanzibar wanaomaliza mafunzo ya JKU, wamekuwa wakiomba nafasi za jeshi kwa upande wa Tanzania Bara lakini vijana hawa wamekuwa wakipimwa afya mara mbili mbili na vigezo na nafasi hizo wanakuwa hawazipati. Nafasi hizi zimekuwa zikitolewa pia kwa ubaguzi mkubwa. Vijana wengi wa mikoa ya Pemba na Unguja ambao wazee wao hawana umaarufu wa kujulikana hawapati nafasi hizi na hatimaye zinaishia kwa watu wachache. Naomba Waziri anapokuja kuwasilisha anifahamishe ni kwa nini hili tatizo linakuwa kero kwa vijana wa Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu suala la michezo. Kuna vijana wengi wanavipaji mbalimbali. Tumeona hata nafasi hizi zinatolewa kwa upendeleo kwa upande wa Zanzibar. Vijana wengi kwa upande wa Zanzibar wanajiunga katika timu za Jeshi lakini hawaajiriwi. Serikali iangalie hili pia ni tatizo na ni kero katika Muungano hivyo basi na Wazanzibar nao wapewe haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia pia katika suala zima la kijinsia kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Leo tarehe 13 Julai, 2011 wakati Bunge lako Tukufu linawatambulisha Makanishna na Majenerali hatukumwona mwanamke hata mmoja. Hii inaonyesha dhahiri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) haizingatii kwa upande wa jinsia. Tumeona kuwa wanaume wamekuwa na kipaumbele kuliko wanawake. Naamini kuna wanawake wengi wasomi na kazi za jeshi pia wanaziweza hivyo basi wanawake nao wapewe kipaumbele katika nafasi hizi nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kuhusu suala la wanajeshi wastaafu. Wanajeshi hawa wastaafu wamekuwa wakisumbuka sana wanapokuwa wakifuatilia kuhusu mafao yao. Hawapewi mafao yao kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, Serikali na Wizara ichukue jitihada ihakikishe wanajeshi hawa waliostaafu wanapelekewa mafao yao katika mikoa yao kwa sababu ya gharama ya usafiri. Wengine wanakuwa hawana ile gharama ya kusafiri. Hii itamrahisishia mwanajeshi huyu mstaafu kuchukua mafao yake katika mkoa wake alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika suala la lishe. Lishe imekuwa ni tatizo katika makambi mengi ya jeshi. Wanajeshi hawapewi lishe kama zamani walivyokuwa wakipewa. Serikali iongeze Bajeti katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa sababu wanajeshi wasipopata lishe bora tutajikuta hatuna Jeshi imara na hii itachangia mwanajeshi kuijingiza katika vitendo vyaa uhalifu. Tumeona katika vyombo mbalimbali vyaa habari wakionesha baadhi ya wanajeshi wanavyojiingiza katika uhalifu, hii ni kwa sababu hawapati mahitaji muhimu yatakayoweza kukidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja naomba yaliyo muhimu yazingatiwe.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Hata hivyo nina jambo moja ningependa kufahamu, nazo ni zifi hatua za Serikali kuitia Wizara ya Ulinzi na JKT kwamba Shirika la Mzinga mwaka 1997 wafanyakazi 97 waliopata *redundancy* (kupunguzwa kazini) na wakalipwa mafao yao. Walipinga mafao hayo Mahakamani na Mahakama iliamuru walipwe kwa mafao ambayo Mahakama waliona ni haki kwao. Tangu hapo wamekuwa wanazungushwa bila kulipwa. Ningependa kujua ni nini jitihada ya Serikali kumaliza kazia hii?

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la ajira, Serikali ifanye mabadiliko katika utaratibu wa ajira katika JKT kutokana na utaratibu uliopo sasa kuonekana kupendelea watu wenye ndugu Jeshini au Taasisi za Serikali huku watoto wa wakulima wakipenya kwa mbinde katika mchujo wa kwa ajili askari wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi ni taasisi nyeti sana hivyo tunapaswa kuhakikisha wanaosailiwa na kujiunga wanakuwa na rekodi safi kimaadili. Naomba tusiruhusu wasio na rekodi safi kimaadili na kizalendo kujiunga katika majeshi yetu kwani ni hatari kiusalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utaratibu wa awali wa vijana wanaojiunga Jeshini kama vile kuchunguza rekodi zao kuanzia elimu ya msingi katika ngazi za vijiji, mitaa, kata na hata wilaya urejeshwe ili kupata vijana wenye wito na nidhamu na hii itatoa matukio ya utovu wa nidhamu ulioanza kujitokeza Jeshini siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba mipaka yetu imekuwa salama wakati wote. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu kumekuwa na baadhi ya vitendo vinavyofanywa na baadhi ya askari wasio waaminifu na hivyo kulipaka matope Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya kulipaka tope Jeshi letu vimekua vikitokea mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Jimbo la Kalambo hususani katika maeneo ya kijiji cha Kasanga. Wanajeshi hao wamekuwa ni kero kwa wavuvi kwa kusingiziwa kwamba katika shughuli zao za uvuvi wamekuwa wakiingia eneo la Jeshi na kupigwa na kunyang'anya samaki na kutiwa msukosuko mkubwa na kuachiwa pindi tu wanapotoa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ambalo Jeshi wameweka makazi ya muda ni eneo *strategically* kwa utalii kwani ndilo eneo ambalo wakoloni wa Kijerumani walijenga ngome yao na kuiita *Bismarck* eneo ambalo watalii wanapenda sana kulitembelea maporomoko ya Kalambo. Naishauri Wizara itafute utaratibu wa kuyahamisha makazi haya (*camp*) za wanajeshi ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu na pia kupisha eneo la kitalii na kambi ijengwe eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAJI FREDERICK M. WEREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kumekuwepo na malalamiko ya wazee wetu walilotumikia Jeshi la Mkoloni (*King's African Rifles*) kwamba hawajapata mafao yao yanayopaswa kutolewa na Serikali ya Uingereza. Wazee wengi ambao sasa afya zao zimezorota wanashindwa kufuatilia haki hizo. Uongozi katika ngazi za mikoa na wilaya kila mara wanakumbushia kuhusu haki hizo. Jambo hili linahitaji kushughulikiwa haraka ili kuwaondolea kero wazee wetu na Serikali itoe tamko kuhusu ni nini hasa linasabibisha tatizo hili.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku za karibuni kumekuwa na milipuko ya mabomu kwenye Kambi za Jeshi. Milipuko hii imesababisha vifo na ulemavu na upotevu wa mali za raia wa Tanzania. Matukio yote hayo Wizara imeshindwa kuueleza umma wa Watanzania ni nani alihusika na uzembe huu ambao umegharimu uhai wa Watanzania. Katika majumuisho yako Mheshimiwa Waziri naomba uliambie Bunge hili Tukufu kwa nini usijiuzulu baada ya Wizara yako kushindwa kulinda raia wake badala yake imeua? Iwe kwa bahati mbaya au uzembe! Pia wote waliohusika na tukio hilo wawajibike ikiwa ni pamoja na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni kumezuka tabia ya baadhi ya wasemaji wa Jeshi kuzungumzia masuala ya siasa. Jambo ambalo naamini Jeshi halihusiki na mambo ya siasa. Mfano ni Mnadhimu wa Jeshi alipozungumzia masuala ya siasa na vitisho kwa wanachi wakati wa uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atakapotoa majumuisho alihakikishie Bunge hili kuwa Jeshi halitajiingiza na wala halipaswi kuijingiza kwenye siasa? Nashauri Jeshi letu likajifunze kwa Jeshi la Misri libaki na kazi ya kulinda raia na siasa ibaki kwa wana siasa. Pia ningeshauri Jeshi letu pia lijikite katika shughuli za kilimo cha kisasa, katika maeneo mbalimbali ya Kambi za Jeshi, badala ya kukaa kombini na kusubiri kustaafu hii italiongezea Taifa letu chakula kwa Jeshi letu kujilisha lenyewe.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda nikushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, kwa hotuba yake na utendaji wake wa kazi unaokubalika na jamii.

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo makuu mawili ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, ninapenda kuchangia kuhusu kurudishwa utaratibu wa kuijunga JKT kwa mujibu wa sheria. Tunashuhudia vijana wakikosa uzalendo na hali ya kuipenda nchi yao na hayo ni matokeo ya kuondoa utaratibu wa kuijunga na JKT kwa mujibu wa sheria. Utaratibu huu ulikuwa ukiwafanya vijana kuwa wakakamavu, wenye uvumilivu, wenye nidhamu na pia wenye upendo wa

kuipenda kuitumia nchi yao. Ninayo taarifa kuwa, Serikali ina mpango wa kurudisha utaratibu huu; ninaomba uharakishwe na hasa katika mwaka huu wa fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wastaafu wa jeshi; kwanza, niipongeze Serikali kwa maamuzi yake ya kuongeza muda wa kustaafu. Pamoja na juhudhi hizi za Serikali, kwa ngazi ya *Private* hadi cheo cha Sajenti na kwa asili ya kazi za vyeo hivi, bado wanazalazimika kuweza kufanya shughuli nyingine nje ya Jeshi. Ninaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuwapa ajira nyingine ili wasibaki tu majumbani bila shughuli zozote. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, alitolee maelezo wakati wa majumuisho.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Mtoni imezungukwa na nyumba za raia. Hii ni hatari kwa Jeshi na pia raia ambao wanaishi karibu na Kambi hii. Je, Jeshi linachukua hatua gari? Ama Wananchi waondoshwe au Kambi ifungwe na ikawekwe maeneo ya mbali na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Jeshi ya Bububu ni mpya na ina zana za kisasa kabisa; tatizo lililopo ni kuwa hakuna Madaktari Bingwa wa kutosha. Maradhi yakiwa makubwa kidogo, Hospitali hii inashindwa kutoa huduma. Ninaombwa Wizara ipeleke Madaktari Bingwa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uajiri katika jeshi, kuna malalamiko kuwa nafasi za uajiri katika Jeshi kwa Zanzibar hazitolewi zote. Maafisa wa Jeshi wanaoshughulika na uajiri huzimega na kubakia nafasi chache tu. Vilevile kuna rushwa katika upatikanaji wa kazi, wote wanaojiriwa lazima watoe rushwa kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uchunguzi ufanyike na hatua zichukuliwe.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2011/12. Mchango wangu utajikita kwenye maeneo makubwa ambayo ni utatuzi wa migogoro ya mipaka kati ya Jeshi/Wananchi, malipo ya Pensheni kwa Askari Wastaafu na Makazi ya Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa migogoro mingi ya ardhi hususan mipaka kati ya Jeshi la Wananchi na Wananchi; mfano, Kambi ya Old Shinyanga KJ 82 ina migogoro mikubwa na Wananchi wa maeneo ya Mwawaza, Itogwang'olo, Old Shinyanga yenye pia katika Kambi ya Kizumbi, kuna mgogoro baina ya Wananchi wa Vitongoji vya Lyandu, Busongo na Sehemu ya Mwamashele. Ninaipongeza Serikali na Waziri kwa kukamilisha ripoti ya tume iliyoundwa kutatifi migogoro hiyo. Ninaishauri Serikali kuharakisha kazi ya utatuzi wa migogoro hiyo kwa kulipa fidia kwa Wananchi ambao wanastahili na kuwaondoa ambao hawastahili kuwepo mahali hapo. Tathmini ifanyike haraka ili malipo yaweze kufanya kwa wakati mwafaka ili kuepusha madhara mengi yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo ya pensheni kwa askari wastaafu, posho inayolipwa kwa askari hao kiasi cha Sh. 50,000 kwa mwezi ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya maisha kwa sasa. Ninaishauri Serikali ifikirie kuongeza posho hizi angalau kufikia Sh. 100,000 kwa mwezi ili askari hawa wastaafu waweze kumudu maisha yao. Pili, posho hizi za pensheni zilipwe katika awamu za miezi mitatu badala ya miezi, ambapo ni muda mrefu sana. Haya ni maombi toka kwa baadhi ya askari wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanaishi katika mazingra magumu sana, makazi kwa maana ya nyumba za kuishi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa nyumba za wanajeshi ili kuepusha askari wetu kukaa katika makazi ya raia na kuepusha migogoro ya kimaadili? Ahsante.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa kumekuwepo na hali halisi ya amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Kuwepo kwa hali hii bado hakufanyi maeneo yetu yote kuwa shwari na utulivu. Nchi yetu imekuwa ikiingiliwa na mipaka yetu ni dhahiri muda mwingine hakuna usimamizi wa dhati juu ya hali hii katika majimbo yetu na hususan Jimbo la Biharamulo Magharibi, tumepakana na Hifadhi ya Burigi ambayo sasa imevamiwa na wafugaji haramu toka nchi majirani zetu. Sidhani Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilayani inalifahamu hili na kwa kuwa watu hawa mara nyingi wanapitia katika mikono au mapokeo ya Viongozi Wazito wa Serikali zetu. Ninaiomba Wizara ifanye kazi ya kuwaondosha watu hawa ili tulinde maeneo yetu na tuishi kwa amani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Majimbo yetu kumekuwepo na matukio mengi ya ujambazi mdogo mdogo na kulingana na muundo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Mbunge hahuishwi. Ikumbukwe kuwa, Mbunge ni Mwakilishi wa Wananchi na anawajibika ipasavyo katika nyanja zote ikiwa ni pamoja na suala la ulinzi na usalama wa Wananchi wake. Aidha, ninapendekeza kuwa suala hili lipewe mtazamo chanya; Mbunge awe Mjumbe wa Kamati hii, kwani itaongeza ufanisi na utendaji mzuri wa Kamati hii. Ikumbukwe kuwa, Mwakilishi huyu anapata taarifa nyingi toka kwa Wananchi hawa kwa sababu ya kuwa karibu sana na wapiga kura hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi na ukweli kuwa, kumekuwepo na wimbi kubwa la vijana mitaani na vijiji ambao sasa hawazalishi chochote na hii imetokea mara baada ya kusitisha zoezi la kuwapeleka vijana wengi katika Jeshi letu la Kujenga Taifa. Jeshi hili lilijenga nidhamu kubwa sana kwa vijana hawa na hususan elimu ya ujasiriamali. Leo hii dhana ya kujiajiri imekuwa ndoto, kila kijana anasubiri kupata ajira rasmi; jambo ambalo ni gumu sana. Ninaiomba Wizara izingatie upya suala la JKT, kwani kuitia chombo hiki, tutajenga nidhamu kwa vijana wetu na kuondoa dhana ya kusubiri ajira rasmi na wakati ambao hawana ajira kubaki kuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Ulinzi wa Wananchi liangalie kwa ukaribu mkubwa wanajeshi wastaafu. Kundi hili limefanya kazi kubwa na linastahili kupewa stahili zake vizuri. Leo hii kuna wastaafu ambao wanadai fedha zao za posho, uhamisho na usafiri. Watu hawa sasa wanaishi maisha magumu na hivyo kuilalamikia Serikali hii na kuona kuwa haithamini kazi waliyoifanya. Ninaishauri Serikali ipitie upya madai ya watu hawa ili waweze kujikimu kimaisha kwani wana familia, watoto wanasoma na hata baadhi ya ndugu na jamaa na marafiki kuendelea kuwategemea japo nao hawana kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi za kuijunga na Jeshi zisiwe za upendeleo, zitolewe kwa uwiano sawa katika mikoa yote na jinsia sawa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ya kulinda Taifa letu pamoja na mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/10, Bunge liliridhia kurejeshwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu. Nilitegemea kufikia sasa marekebisho madogo madogo yanayohitajika katika Makambi ya JKT yangekwishakamilika na kuruhusu vijana kuanza mafunzo. Serikali itakubaliana nami kwamba, JKT iliwajengea vijana nidhamu, ushupavu, kujiamini na kadhalika. Ninaishauri Serikali yetu irejeshe JKT haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ninaiomba Serikali Yetu Tukufu Iangalie Namna Ya Kuwatumbia Wanajeshi Wastaafu kwa shughuli mbalimbali za maendeleo baada ya kustaafu kwao hasa wale wa ngazi ya Koplo, *Sergeant* na kadhalika, kwani wanastaafu kisheria wakiwa bado wana nguvu za kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalipongeza Jeshi letu kwa kushiriki katika majanga makubwa yanayolikabili Taifa letu. Sitasahau jinsi walivyowasadidhia Wananchi wa Kilosa /Mpwapwa na kadhalika, kwa kuwajengea madaraja ya muda pale mafuriko yaliposomba madaraja. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwepo matukio ya kulipuka kwa mabomu katika Makambi ya Jeshi la Wananchi kule Gongolamboto na Mbagala na kuua raia wengi wa Tanzania, waliokuwa wanaishi jirani na makambi hayo. Maeneo ya matukio hayo yalivamiwa na raia na kujengwa makazi karibu na makambi ya jeshi. Kwa kuwa sheria hairuhusu makazi ya raia kuwa karibu na Makambi ya Jeshi kwa umbali wa kilomita moja, ninashauri Jeshi liwe makini sasa kutoruhusu maeneo ya Makambi yake kuvamiwa na raia kwa kujenga nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi hulitumikia Taifa kwa uaminifu mkubwa mpaka wanapofikia umri wa kustaafu. Wanajeshi hubeba siri nydingi za Taifa hususan zinazohusu usalama wa Taifa na shughuli za kivita. Ninaishauri Serikali yetu Tukufu iangalie uwezekano wa kuongeza pensheni ya wastaafu wa Jeshi. Kwa sasa kiasi

kinacholipwa kwa maaskari wetu ukilinganisha na kupanda kwa gharama za maisha, kiasi hicho hakitoshelezi mahitaji hata kidogo. Tuwathamini wapiganaji wetu kwa kazi nzuri waliyoifanyi Taifa letu kwa kusimamia amani na utulivu wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kuishukuru kwa Serikali kuwashughulikia Wananchi wanaong'oa alama za mipaka kwa lengo la kujipatia ardhi kwa shughuli mbalimbali za kilimo; ufugaji na kadhalika. Wakiachiwa bila kuadhibiwa, wataendelea kusogeza mipaka ya nchi kama watakavyo. Serikali ikitoa adhabu, itakuwa fundisho kwa Wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuanza kwa kumpongeza Waziri kwa Hotuba nzuri. Ninaipongeza Wizara na Jeshi letu kwa kuendelea kulinda mipaka ya Taifa letu na kudumisha amani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa azma yake ya kurejesha mafunzo ya JKT. Ninawapongeza kwa hatua za maandalizi walizofikia. Kiu ya Watanzania ni kuona JKT inaanza. Watanzania wamechoka kuona vijana wa nchi hii, ambao ndiyo tegemeo la nchi yetu, wanakosa maadili, wanakosa uvumilivu, wanakosa ukakamavu na wanakosa uzalendo. Njia pekee ya kuondoa ulegevu huo ni vijana kupitia mafunzo ya JKT. Je; ni lini hasa JKT itaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitumia muda mwangi na rasilimali za nchi hii kusaidia nchi za Kiafrika kupata uhuru. Alisikika akisema kama jirani yako hayuko huru hata wewe uhuru wako hauko shwari. Tanzania ni sehemu ya Afrika. Je, tunapoona nchi zilizoendelea kama Amerika, Uingereza, Ufaransa kupitia Majeshi ya NATO, wanavamia wanabomoa miundombinu, wanaua raia wasio na hatia; ni nini jukumu letu kama Jeshi la Tanzania? Je, ni kwa kiasi gani tumeisaidia Nchi ya Libya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalishukuru Jeshi letu kwani kwa sasa nchi yetu ni tulivu na salama. Ninatoa tahadhari, Mkao wa Kagera inabidi uangaliwe vizuri. Hawa raia wa kigeni wanaoingia Ngara, Biharamulo, Karagwe na Missenyi kama wahamiaji haramu kutoka Burundi, Rwanda na Uganda, inabidi waangaliwe kwa umakini ikiwezekana wakomeshwe kabisa. Wanaingia kwenye mipaka ya nchi yetu wanajichukulia ardhi, wanaingiza mifugo, wanafanya uporaji na juzi kumetokea mauaji Ngara na Missenyi, Mkoani Kagera. Tulichukulie tatizo hili kiurahisi, kwani wengi wa hawa kwao hakuna hata ardhi ya kutosha, vita vinaweza kuzuka kwa sababu ya kugombea rasilimali. Je, Jeshi limejipangaje kulinda mipaka ya Mkao wa Kagera na kuhakikisha ulinzi na usalama?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mdogo sana, ninaomba Serikali kupitia Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, irejeshe mafunzo ya lazima kwa vijana wanaomaliza masomo ya elimu ya juu kujiunga na JKT kabla ya kupatiwa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua idadi ya wanafunzi imeongezeka sana nchini na uwezo wa Serikali ni mdogo, basi angalau Serikali iwachukue wale wanaojiunga na Vyuo Vikuu pekee, badala ya wale wote wanaomaliza Kidato cha Sita ambao idadi yao ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa maadili kwa vijana wa Vyuo Vikuu na migomo ya mara kwa mara, bila shaka itapungua ama kuondoka kabisa kama utaratibu huu wa mafunzo ya JKT kwa vijana utarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuliweka Jeshi letu vizuri na la kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia, Jeshi letu linapaswa kuwa dogo, lenye vijana walioelimika na lenye silaha za kisasa. Hata hivyo, bado Jeshi letu halijafikia katika hatua hiyo, kutokana na uchumi duni tulionao. Ninaomba Serikali ijpange vizuri kuhakikisha kuwa fedha ya kutosha inatengwa kwa azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu lazima liajiri vijana wenyewe maadili mema na wenyewe imani na mapenzi ya nchi hii ili waweze kuitetea na kuilinda vizuri wakati wa matatizo. Ninaomba pia uajiri ufanywe kwa uadilifu mkubwa, tukitilia maanani sehemu mbili za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar). Zipo tetesi kuwa upande wa Zanzibar wanatolewa Tanzania Bara. Ninaomba Serikali iliangalie vizuri suala hili ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wetu wanaishi uraiani kwa kuwa Kambi za Kijeshi hazina nyumba za kutosha. Aidha, Kambi nyingi za Kijeshi zipo karibu sana na maeneo ya raia. Zipo hatari nyingi kufuatia hali hii. Kwanza, kwa sababu Wanajeshi wetu wengi ni vijana; hivyo, huwepo ugomvi kati yao na vijana wenzao uraiani. Wanapogombana Wanajeshi na Raia, ile tafsiri ya hili ni Jeshi la Wananchi inaondoka.

Matatizo ya mabomu kule Mbagala na Gongolamboto ni janga kubwa kwa Raia waliouawa au kujeruhiwa baada ya mabomu hayo kulipuka. Kwa sababu hizo basi, ninashauri Kambi za Kijeshi zijengwe mbali na maeneo ya raia. Vilevile ni budi zijengwe nyumba za kutosha za askari katika maeneo ya kambi kwa kutumia *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wetu waliopigana katika vita mbalimbali ikiwemo Vita vya Uganda, hawakutendewa haki baada ya kustaafu. Wengi hawakulipwa stahili zao na siku zote wanailalamikia Serikali kuwa wametelekezwa. Hali za wanajeshi hao ni duni sana. Ninaomba Serikali irudie tathmini iliyofanya ili iweze kuwalipa vizuri wapiganaji wetu wa Vita vya Kagera na vingine vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia kuhusu Jeshi na uzalishaji mali. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na amani kwa kipindi kirefu na pia imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba na mito mikubwa inayotiririka mwaka mzima. Ninaishauri Wizara hii kuutumia wakati wa amani katika kuzalisha mazao ya kilimo. Hili litasaidia kulipatia Jeshi chakula cha kutosha na kuuza chakula cha ziada.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa nchi ni jambo muhimu na lisilotakiwa kuwa na ubabaishaji wa aina yoyote ile. Tanzania tunajivunia amani tuliyonayo kutokana na nidhamu ilijojengeka ndani ya Jeshi hili, pamoja na huduma stahili wanazokuwa nazo. Kwa kuwa Jeshi la Wananchi ni pamoja na lile la Kujenga Taifa, Jeshi hili hapo nyuma lilihakikisha kuchukua vijana wote waliomaliza Kidato cha Sita kabla ya kujiunga na elimu ya juu. Zoezi hili liliondolewa miaka ya 90 katikati kwa maelezo kuwa, Serikali haikuwa na uwezo tena wa kuwaweka vijana hawa kambini na kwamba, wamekuwa wengi sana na kadhalika. Kinachosikitisha ni athari zitokanazo na vijana kutopitia katika mafunzo hayo. Hii ni pamoja na vijana kutokuwa na uzalendo, ujasiri na uthubutu, lakini kuwa na uongozi (*leadership skills*). Kwa kuwa Tanzania ina maeneo makubwa ya uzalishaji, ardhi, ambapo wangeweza kulima na hivyo kuzalisha mazao na matunda hasa ikizingatiwa Kilimo Kwanza; ni jambo la kusikitisha kuona Jeshi la Kujenga Taifa (Makutupora), Kambi iliyokuwa maarufu kwa kilimo cha mboga mboga na zabibu sasa hivi ni pori. Tunaitaka Wizara ifanye mpango kuhakikisha wanafunzi wote waliomaliza Kidato cha Sita wanapita Kambi za Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha tena sana kuona pamoja na kuwa Karne ya 21 inayozingatia haki na usawa wa binadamu, bado wanawake hawajapewa kipaumbele. Ninatambua kuwa, Jeshi linahitaji watu wenye afya bora, wakakamavu na wenye elimu toshelezi. Ninaamini wapo wanawake wenye sifa hizi, lakini hawaonekani katika vyeo vya juu kama Majenerali, Mabrigedia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika ninaamini Wizara itaona ni kwa jinsi gani inaweza kuwapatia vyeo wanawake ambao wana uwezo na wamepata mafunzo husika na kufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza Waziri kwa Hotuba yake nzuri, yenye kujali Wananchi wake na kujitahidi kuwalinda kwa kila hali na Mungu atawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa Zanzibar, kuna kilio kikubwa cha wastaa fu kuwa wanapostaa fu hupata shida ya kupata mafao yao na hulazimika kusafiri mara nyingi kwenda Dar es Salaam kufuata mafao yao; kwa hiyo, gharama huwa kubwa na wakati mwingine uwezo wa kwenda na kurudi mara kwa mara huwa haupo; na kwa hiyo huwa vigumu kupata mafao yao kwa wakati mwafaka. Ninaomba Wizara iweke Kanda kwa upande wa Zanzibar ili wafuatilie kule kule na hasa ukizingatia kuwa Benki Kuu ya Tanzania ipo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matukio ya huzuni yaliyotokea Gongolamboto; yale yalishatokea ila ninaomba Wizara iwe makini na kuwe na uangalifu zaidi hususan kwa silaha ambao zimekwishapitwa na wakati au zinazokaribia kumalizika muda wake kuwe na utaratibu maalum wa kuziharibu kabla hazijaleta madhara yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mpango maalum ambao hautazongwa na *element* za siasa, utakaoweka hali za Wananchi kutokuwa na wasiwasi. Nina maana ya kwamba, mipaka baina ya Makambi na maeneo ya raia, ipitiwe upya na ikibidi aidha kambi au maeneo ya raia waondoshwe. Lifanyike hilo kwa ustawi na usalama wa raia na kama sheria zilizopo hazikidhi haja basi zirekebishwe ili ziende na wakati ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kujitekeza. Tukumbuke kukinga ni bora kuliko kutibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pongezi kwa Waziri na Wakuu wa Majeshi yetu, kwa kuandaa Ripoti nzuri ya Bajeti kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina ifanywe katika Kambi zote za Jeshi ili kubaini hali ya ghalna silaha zilizopo na kuchukua hatua stahiki, kuzuia maafa ya raia na askari kama yale ya Mbagala na Gongolamboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lirezeshwe na wanafunzi wote wanaomaliza Kidato cha Sita ama *degree* ya kwanza wapitie ili kuwapa msingi wa utaifa, uzalendo na ukakamavu stahiki.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Wizara ya Ulinzi. Pamoja na hayo, nitoe maoni yangu na ushauri kwa Wizara hii muhimu, kwani ndiyo kazi ya Ubunge Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri kabisa kwamba, kuna ajali, kuna bahati mbaya na kuna majanga. Ninaomba kujikita katika matitizo ya milipuko ya Gongolamboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna kifaa duniani kinachotakiwa kuhifadhiwa kwa uangalifu ni silaha. Ninaponzungumzia silaha nipende kujikita katika mabomu. Mabomu ni silaha nyeti, inayotakiwa kuhifadhiwa na kuangaliwa kwa umakini sana. Nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi kwa kipindi cha miaka mitano na nikaweza kutembelea maghala ambako tunahifadhi silaha zetu ikiwa ni pamoja na mabomu.

Mheshimiwa Naibu Spika; ni vyema Serikali ikaona na ikadhamiria kwa makusudi, kuwa na maghala imara na yenye udhibiti wa kuweza kuhifadhi mabomu na kuweza kuzuia milipuko inayoweza kujitokeza. Jambo la milipuko limejirudia mara mbili na kuwafanya Wananchi waanze kuhoji umakini wa Jeshi letu katika *ku-handle* mabomu haya. Kwa milipuko kujirudia na kupoteza maisha ya Watanzania na mali zao na kuathiri miundombinu na kadhalika, vitendo hivi vimeacha maswali mengi sana yasiyojibika kwenye mioyo ya Watanzania. Watanzania wamejenga woga mkubwa na wanaingwa na hofu na umahiri wa Jeshi lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaisihi Serikali tena kwa unyenyekevu mkubwa, suala hili la *handling* ya silaha zote na hasa mabomu, liangaliwe upya na kwa umakini sana na kuhakikisha milipuko ya mabomu haitokei tena nchini kamwe. Pia ni vyema Serikali ikaangalia upya vyanzo vya milipuko hii ili iweze kuzuia isijitokeze tena na iwe ni mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunapeleka majeshi yetu sehemu mbalimbali Barani Afrika, kwa nia ya kuweka ulinzi na kudumisha usalama katika maeneo ambayo *AU* au *UN* wameamua kudumisha amani. Ninawapongeza Wanajeshi wetu kwa kujitolea mhanga kwa maslahi ya Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi na pungezi hizo, sasa ninapenda kutoa dukuduku langu kwa Serikali kuhusu dhuluma wanazotendewa Wanajeshi hawa na Serikali yetu, kuitia Wizara hii ya Ulinzi. Kwanza, ninapenda ieleweke kwamba, maelezo au malalamiko haya ninayoyatoa si kwa niaba yangu pekee, bali ni malalamiko yanayotoka katika nyoyo za Wanajeshi, wetu ambao kuitia sisi Wabunge wao ndiyo wameweza kutoa sauti hizi; vinginevyo, katika heshima na taratibu za Kijeshi, wasingethubutu kuwaeleza Makamanda wao kwani ndiyo utaratibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutoa mfano halisi kwa Wanajeshi waliopolekwa Darfur, ambapo mfano huo huo ni kwa Wanajeshi walioko sehemu nyingine. Wanajeshi waliopolekwa Darfur wanadhulumiwa au hawapewi haki zifuatazo:-

1. Malimbikizo au chenji yao hawajalipwa wakati Serikali ilipewa fedha na *UN*, ilipewa buti, *combat* na vifaa vya michezo na vyote hawajapata.
2. Posho za kuwaachia familia nyumbani Tanzania hawajalipwa.
3. Pesa za chakula hawajapewa wakati hazina zinatoka kila mwezi. Je, zinakwenda wapi?
4. Pesa za *voucher* kupiga simu hawapewi wakati zimo kwenye Mkataba wa Serikali na *UN*.

5. Pesa za likizo hawapewi kikamilifu wanazopata ni \$ 150 tu, ambapo *UN* wanatoa \$ 650 kwa askari mmoja.
6. Askari wa Tanzania wanaishi chumba kimoja zaidi ya askari watano ambacho wanalipia \$ 800 kwa mwezi.
7. Magari wanayotumia ni *IVECO (Magirus)* ambayo ni mabovu na yanahatarisha usalama wa askari hawa.
8. *UN* wanatoa \$ 5,000 kwa mwezi wakati Jeshi letu au Askari wetu wanalipwa \$ 800 tu. Je, huo siyo uonevu? Je, huo siyo wizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri wa Ulinzi, atupatie marekebisho ya uhakika kwa matatizo hasa yafanyiwe uchunguzi na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira zinatolewa kwa upendeleo na matatizo makubwa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuhitimisha hoja yake, aniletee majibu ya watu walioajiriwa kazi katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita kutoka Jimbo la Mkanyageni ili tuone kama hakuna upendeleo.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tuhuma kubwa juu ya ajira ya Wanajeshi kutoka Jimbo langu la Mkoani lililoko Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Hapo zamani ulipokuwa upimwaji wa Wanajeshi unafanywa na kumalizikia katika Wilaya, walikuwa wanaletwa vijana kutokea maeneo mengine na ni nje ya Kisiwa cha Pemba huchukua nafasi hizo. Kwa wakati huu, upimaji unakamilika pengine huko wanakokwenda hupata mafunzo. Inasemekana katika hali hiyo, vijana wanakosa nafasi hiyo kwa kuambiwa hali zao au afya zao haziruhusu kuajiriwa katika jeshi. Katika hali hiyo, hizo nafasi wanazoondolewa vijana kutoka tuseme Mkoani, huchujuliwa na vijana ambaa hawatoki Mkoani. Serikali inasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri katika hili ni vyema upimaji wa Wanajeshi ukamiliwe katika Wilaya ili upungufu wowote wa idadi ya vijana utakaotokea, uendelee kujazwa na vijana wa Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi waliostaafu kila baada ya miezi sita ndipo wanapopata pensheni yao; muda huo ni mrefu ni vyema iwe baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ukanda wa Bahari ya Hindi, kumezuka maharamia wa Kisomali, ambapo inaonekana wanaambaa katika eneo kubwa katika Bahari ya Hindi. Je, katika kipindi hiki tokea uzuke uharamia Jeshi limewakamata maharamia (*pirates*) na limejipanga vipi kukabiliana na maharamia hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa licha kuwa ni walinzi wa nchi yetu, bali pia wanaweza kuwa ni tegemeo kubwa kwa suala la Kilimo Kwanza. Hapa ni mionganoni mwa mahali ambapo Serikali inaweza kuwekeza katika suala zima la kilimo; ni

vyema Jeshi hili liwezeshwe kiutaalam na kivifaa katika kuendeleza kilimo. Lazima katika hilo, baada ya kuwezeshwa wawekewe mkakati au lengo ambalo watatakiwa walifiki. Haitopendeza baada ya kuwezeshwa ipasavyo, washindwe hata kupata chakula chao. Ninadhani lengo liwe zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukingalia ukurasa wa 20 na 21, kifungu cha 28, imeelezwa uwepo wa mafunzo ya mgambo na jumla ya Wanamgambo 15,485 wamehitimu mafunzo ya awali kwa mikoa 21 Tanzania Bara. Jeshi ni la Muungano; je, Zanzibar hakuna mafunzo ya mgambo yaliyofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu moja inayosababisha kutoanza mafunzo kwa vijana wetu katika Makambi ya JKT kwa mujibu wa sheria ni uwepo wa marekebisho ya sheria inayohusiana na suala hilo. Je, sheria hiyo italetwa lini hapa Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho yanayostahili?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha ombi la Wananchi wa Kongwa, ambao kuititia kwangu wanaomba JWTZ irudishe Kambi ya Jeshi Kongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uongozi wa Wilaya ya Kongwa na Wananchi, wangependa kukabidhi iliyokuwa Kambi ya Mafunzo ya Wapigania Uhuru (sasa Sekondari – tutajenga nyingine), ama tuwape eneo lingine karibu na hapo kwa matumizi ya wependwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii, kutoa machache juu ya Wizara hii. Inashangaza, ajira ya mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa au nafasi yake, mara nyingi huwa adimu sana. Sana sana nafasi hizi hutolewa kulingana na Viongozi waliopo katika vituo husika. Vijana waliopitia mafunzo ya Mgambo, wanaambowiwa watakuwa wanapatiwa nafasi hizi, lakini haiwi hivyo. Kwa mfano, Wilaya ya Masasi watapata lini? Hii ni pamoja na Jeshi la Polisi hali ni hiyo hiyo. Siyo hilo tu, hata vyeti vya Mgambo hutolewa kwa shida na kwa gharama. Ninaomba Serikali na Wizara husika, iangalie hilo na pia haki itendeke ili kila Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji vipate nafasi ya uwakilishi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi hili ni mionganini mwa wapenda rushwa. Watakiwapo kufanya wajibu wao kama kwenye matendo ya uhalifu, wao hujali maslahi kwanza ndipo watekeleze agizo. Mfano mzuri ni pale wanapotakiwa kufuatilia watuhumiwa kwa Jeshi la Polisi. Jeshi hili huwa wanapendelea kushiriki maswala ya siasa. Huwa wanavunja amani kwa kujipendekeza kwa Chama Tawala kwa kuwa-*harass* Wapinzani, kuwabambikizia kesi za uwongo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa manufaa ya umma, ninaiomba Wizara husika iwe na hofu ya Mungu, wakitambua ya kuwa haya yote yanapita na yana mwisho. Wafanye kazi kama masharti ya ajira zao zinavyotaka wafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Wizara hii watumishi wake hawana nyumba nzuri. Hivyo, ninaomba wafikiriwe ili kuondoa hali ya kuchangamana na raia, hali inayowafanya kujenga urafiki na Wananchi jirani na kuwafanya wasitimize wajibu wao ipasavyo pale wanapotakiwa kufanya kazi kwa kuonea haya jirani. Mfano, wahalifu kama ni jirani zake au rafiki watashindwa kutekeleza wajibu wao.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Wizara ya Ulinzi. Awali ya yote, ninampongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda usalama wa nchi yetu katika hali ya nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani za pekee kwa Jeshi la Ulinzi katika maeneo ya Ziwa Tanganyika, kwa kuimarisha ulinzi katika eneo hili kwani Wananchi waliishi katika mazingira magumu sana, kufuatia matukio ya ujambazi yaliyokuwa yakifanyika mara kwa mara na Maharamia kutoka nchi jirani ya Congo (DRC). Mara Jeshi lilipofika maeneo haya, matukio hayo yamedhibitiwa na kwa sasa Wananchi wanaishi kwa raha mustarehe, wakifurahia uhuru na amani ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara iimarishe vitendea kazi vya Jeshi na hasa kuwapatia boti za kisasa kwa ajili ya kufanya doria za mara kwa mara katika Ziwa Tanganyika kwenye Kituo cha Jeshi kilichopo Tarafa ya Karema, Kijiji cha Ikola.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wanaishi katika mazingira magumu hasa nyumba za kuishi hamna. Hivyo, tunaiomba Wizara iwajengee nyumba za kuishi ili kuwapa motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iandae mazingira ya kuboresha afya zao kwa kujenga zahanati za kijeshi katika maeneo wanayofanya kazi ili waweze kupata huduma nzuri ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari linalotumika katika Kituo cha Ikola limechoka, ninaishauri Wizara inunue gari jipya ili waweze kutatua tatizo linalowakabili la matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara ya Wanajeshi na Wananchi wa Ikola, inayojitokeza kwa baadhi ya Wanajeshi kuwapiga Raia pasipokuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaiomba Wizara iwaboreshee Wanajeshi misharaha na marupurupu yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara hii ni muhimu sana, ambayo inatakiwa mambo muhimu yaangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, pia ninawapongeza Mkuu wa Majeshi yetu na Makamanda wote, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kutulinda na kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za usoni, kumekuwa na uvamizi wa kiharamia katika eneo la maji ya Tanzania katika Bahari ya Hindi, ambapo baadhi ya *beacon* zilibomolewa na utekaji nyara meli kuendelea; endeleeni kulinda bahari yetu. Tunawaomba kwa sababu maombi yenu ya fedha ni makubwa na ili tupate pesa zaidi, tusaidieni kwa dhati wavuvi haramu kwenye bahari yetu, tunaambiwa zaidi ya meli 150 huvua ndani ya eneo letu bila idhini, samaki hao kama tungevua wenywewe tungepata fedha nyingi na kuongeza Pato la taifa. Ninajua mkiamua mnawenza; tusaidieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiuliza mara kwa mara kuhusu ndege zaidi ya sita, *Mig 21* zilizopo katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, inaonekana kama vile zimetelekezwa lakini ningependa kujua; kwani ndege hizo mnazianika juani, zinanyeshewa mvua, haziruki zimekaa tu; je, bado zinahitajika au zimekwishapitwa na wakati? Kama bado zinahitajika kwa nini zisifunikwe kwa maturubai ili angalau kupunguza kuingiwa na maji, vumbi na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kubwa la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ni kuhakikisha kuwa, mipaka ya nchi yetu ni salama wakati wote. Mipaka ya nchi yetu ni pamoja na nchi kavu (*Territorial Boundaries*), mito na bahari, anga (*Air Space*) na kadhalika. Katika hili, Jeshi letu limepata mafanikio makubwa na matokeo yake ni amani na utulivu kuwepo nchini kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujangili wa kutumia silaha kali na za kissasa umekithiri mno katika mbuga zetu za wanyamapori kama Serengeti na kwingineko; ninashauri Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Ulinzi wa Tanzania, ambaye pia ni Rais wa Tanzania, ali pe jukumu la ziada JWTZ la kushughulikia majangili katika mbuga zetu hususan Serengeti, Ngorongoro na Selous; Mbuga ambazo pia ni urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni majangili hao waliua Faru aliyeletwa kutoka Afrika Kusini na kukabidhiwa Mheshimiwa Rais huko Serengeti na kuahidi kupewa ulinzi kuliko anaopewa yeye mwenywewe Mheshimiwa Rais.

Vilevile katika siku za hivi karibuni wanyama wetu walikamatwa katika mbuga zetu na kutoroshwa nje ya nchi kwa kutumia ndege ya Jeshi la Kigeni kuititia viwanja vyetu vyaa ndege. Hii ni kashfa na aibu kubwa kwa Taifa. Ninaomba ushauri huu uzingatiwe hata kama uamuzi hautatolewa katika siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu na wajibu wa Wizara kuhakikisha uhuru na usalama wa nchi unalindwa. Kipengele (c), ukurasa wa sita, kuandaa Umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya adui kupitia mafunzo ya Mgambo kwa wakati na kufuatana na mabadiliko na utandawazi. Jeshi la Mgambo wanapomaliza mafunzo wanabadili utaratibu waondoe majambazi au kujiingiza katika masuala ya uhalifu, kwa kuwa maisha ya Watanzania ni duni kutokana na uchumi mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri sasa mafunzo haya yaachwe kwa kuwa ni vigumu kuwadhibiti wenzetu wanaomaliza mafunzo ya Mgambo. Badala ya Mgambo kuwa walinzi wazuri, wanakuwa vijana wanaojihusisha na ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa 2010/11 kwa JKT kwa Miradi ya Maendeleo ni 12.65 bilioni; ni kiwango kidogo sana na hata hivyo, walizopata ni 3.79 bilioni, sawa na 29.9% na huu mgawo ni kwa ajili ya kuendeleza viwanda vivilyo chini ya JKT na vinatakiwa kujidesha kibashara. Ni wazi kabisa JKT hawataweza kujidesha kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mwaka 2011/2012, matumizi ya maendeleo kilipangia bilioni 3.162; ni kiwango kidogo mno, Serikali ijaribu kutafuta namna yoyote kuliwezesha Jeshi hili kwa fedha za kutosha ili waweze kuzalisha katika viwanda hivyo badala ya kuagiza nje ya nchi ili viwanda hivyo viwe vinajitosheleza na kuimarsika. Pia tuwajengee uwezo wa kuwapa fedha nyingi ili waagize vipuri vyta kisasa na kutafuta wataalam toka nchi za nje kama China kuwafundisha kutengeneza *furniture* nzuri. Hilo linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wetu wapewe mikopo ya kilimo ili walime mazao mengi ya chakula na biashara, tuondokane na uagizaji wa chakula nje ya nchi. Watumishi wa Jeshi wote wapatiwe nyumba nzuri za kuishi katika makambi yao, badala ya kuchangamana na Wananchi ili kulinda nidhamu ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya mishahara yaongezwe ili wanapostaa fu wasihangaike, kwa kuwa wao huishi kambini, hivyo kuanza maisha ya uraiani kunawakwaza na kukata tamaa mapema. Jeshi liwe na mpango wa kuwajengea wastaafu wote kwa mkopo nafuu.

**MHE. ABDULSALAAM SHARIA AMER:** Mheshimiwa Naibu Spika, NIaunga mkono hoja. Ninaipongeza Wizara kwa kazi nzuri na ya kujitolea katika ulinzi wa nchi na kuwashudumia Wananchi katika majanga makubwa na madogo. Ninaomba Wizara ifuatilie mipaka ya Kambi ya Jeshi Mikumi na Wananchi wa Mikumi, Kitongoji cha Vikweme, kwani wakazi wengi wa mikumi wanategemea sana kilimo na eneo hilo ndiyo wanalima kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana tena sana, suala hili lifuutiliwe kwa karibu na mimi nipo tayari kushirikiana na Wizara hii ili kuondoa utata uliopo wa mipaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ulinzi wa Taifa ni ya zamani tangu 1966 na dunia imeshuhudia mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia. Ninaishauri Serikali, Kamati iliyoundwa ya kuangalia na kuboresha Sheria hii, iharakishe kuleta mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha Serikali inasuasua juu ya kuchukua vijana kujiunga na JKT, ambapo maadili na uzalendo wa Taifa kwa vijana unapungua. Ninaishauri Serikali iangalie upya namna ya kutafuta fedha kwa JKT ili vijana waendelee kujiunga na JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya Wanajeshi na Raia imekuwa ikitokea maeneo mengi; tatizo ni kwamba, kuna upungufu mkubwa wa makazi na Askari wa JWTZ kuishi uraiani. Ninaishauri Serikali iingie mkataba na mashirika mbalimbali kama NSSF kujenga nyumba za Wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la madeni kwa askari na wazabuni bado ni kubwa na kudhoofisha utendaji na ufanisi kwa askari; ni vyema Serikali ikalipa madeni ya askari na wazabuni kwa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maharamia (*pirates*), linaendelea kudhoofisha usafiri katika Bahari Kuu ya Hindi. Utekaji meli unaongoza ugumu wa maisha kwa Nchi za Afrika Mashariki kutokana na bidhaa kuongezeka ushuru unaotolewa na maharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya maeneo yaliyochukuliwa na JWTZ kwa ulinzi, Wizara iliahidi kuyapima, kutathmini na kutoa fidia. Serikali inasema nini juu ya maeneo yafuatayo; Oldonyo Sambu JWTZ – Arusha; *Kunduchi Rifle Range* – Dar es Salaam; Bulombora JKT – Kigoma; Kiabakar (253) KJ – Mara; Buhemba JKT – Mara; Chita JKT – Morogoro; Makutupora JKT – Dodoma; Maramba JKT – Tanga; Mlale JKT – Ruvuma; Rwankoma – Mara; *Tunduru TPDF* – Ruvuma; na *Umoja Camp* JWTZ – Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wastaafu wa JWTZ na hasa walioshiriki Vita vya Kagera 1978/79, wametelekezwa na Serikali na hali zao ni mbaya sana. Ninaishauri Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Ulinzi, pamoja na Wizara yake, kwa kazi nzuri ya kulinda nchi yetu, lakini pia kwa uwasilishaji wake mzuri wa Bajeti tunayoichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri anipatie maelezo ya kina kuhusu kadhia inayowakuta Wananchi wa Jimboni kwangu Buyu, Shehia ya Chukwani, ambapo kuna Kambi ya Jeshi. Wanajeshi hao wamepimiwa eneo lao baada ya kuwepo mgogoro wa mipaka, matokeo yake baada ya kupimiwa wamepewa na eneo la Wananchi ambao kwa miaka mingi walikuwa wanaishi na kufanya shughuli zao hapo za kutafutia maisha. Eneo waliloongezewa lina mashamba ya asili ya Wananchi, ambao tayari walikuwa wameshajenga nyumba za kuishi, lakini pia kuna vipando (mimea) yao. Waliahidiwa baada ya kufanyiwa tathmini watalipwa, lakini cha kusikitisha mpaka leo hii bado hawajalipwa. Je, Serikali kupitia Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; linawaambia nini Wananchi wa Buyu wanaodai haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi mionganoni mwa Askari wa vyeo vya chini kuhusu *allowance* ya likizo zao, kutopewa fedha za likizo hata kama Wizara hutenga fungu hili. Ninamwomba Waziri kama ni kweli jambo hili lishughulikiwe kwani linaleta usumbufu kwa Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko ya Askari Wastaifu kupewa haki yao kwa muda mrefu, miezi sita, na pesa zenyewe ni kidogo. Hivyo, wanaomba muda huo upunguzwe kwani siku ni nyingi na maisha yamepanda na askari hawa wengi ni wale wanaopokea kiwango cha chini cha mshahara. Hivyo, ninaomba ufanyike utaratibu wa marekebisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko pia ya Wanajensi wa JKT waliopigana vita vya kumwondo Nduli Iddi Amin Dada – Uganda 1978; wanadai mpaka leo hawajalipwa ingawa waliambiwa waorodheshe majina yao kambini, lakini hakuna linalofuata au kuambiwa chochote au ndiyo kusema wameshasahauliwa! Ninaomba Mheshimiwa Waziri awaonee huruma Wanajeshi hawa kiwani waliipa nchi yetu heshima kubwa.

Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi wanajeshi wanalipwa fedha za chakula kwa siku Sh. 5,000/= (Chai 1,000/= chakula cha mchana 2,000/= na chakula cha usiku 2,000/=). Kiasi hiki ni kidogo kwa maisha ya wanajeshi wetu ukilinganisha na bei za bidhaa zilivyopanda. Naomba pesa hii iongezwe angalau ifikie Sh.10,000/= kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za wanajeshi zina hali mbaya sana na zinasikitisha kwani zina uchakavu mkubwa na hata zilizopo hazitoshi kwa wanajeshi wote kuishi kambini. Wanajeshi wanatakiwa kuishi makambini ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi maana kwa hali halisi wanajeshi wapo kazini 24 hours, lolote linapotokea wanatakiwa kuwa mahali pamoja ili kutimiza wajibu wao ipasavyo. Wanajeshi kuishi mitaani haileti *image* nzuri kwa wanajamii wanaowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanajeshi wetu wanatakiwa kushirikiana na majeshi mengine kulinda amani katika nchi zenyе vita vya wenyewe kwa wenyewe kama ilivyo katika mikataba wa *UN* uliosainiwa na nchi yetu, lakini kumekuwa na tatizo la wanajeshi hao kulipwa posho kama inavyooneshwa na *UN*. Posho ya mwezi wanayotakiwa kulipwa ni Dola za Kimarekani 1,028 lakini wamekuwa wakilipwa Dola 823 tu. Je, pesa zinazobaki zinakwenda wapi na ni maelezo gani yanaweza kutolewa juu ya baki hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kozi za kijeshi ni wajibu wa mwajiri kuhakikisha wanajeshi wote wanakwenda kozi, lakini hilo limekuwa halifanyiki kwa kisingizio cha kutokutengwa kwa fedha za kozi na wanajeshi wengine wamekuwa wakikaa miaka kadhaa bila kwenda kozi hizo. Hali hii inaweza kuzungumzwaje? Kama hili halifanyiki wanajeshi watapanda vipi vyeo wakati ni lazima mtu aende kozi fulani ndipo apandishwe cheo chake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwanajeshi anatakiwa kwenda likizo mara moja kwa mwaka kama ilivyo kwa watumishi wengine na hivyo kulipwa stahiki zao za likizo. Kwa nini hilo halifanyiki kwa wanajeshi badala yake wanalipwa mara moja tu baada ya miaka mitatu? Je, wanajeshi nao wameingizwa kwenye mikataba ya Polisi ambao wanakwenda likizo miezi mitatu lakini ni baada ya kukaa miaka mitatu bila kwenda likizo? Likizo na malipo ya likizo ni haki ya mwanajeshi na mtumishi yeoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iliona umuhimu wa kuwaletea wanajeshi huduma za kijamii yakiwepo maduka yenye misamaha ya kodi karibu au katika maeneo wanayoishi na madhumuni ya maduka haya ni kuuza vitu kwa bei nafuu kuliko ile ya mitaani. Kwa nini maduka haya yamekiuka mikataba hiyo na kuuza vitu kwa bei sawa na ya maduka mengine yanayolipa kodi stahiki? Nani amewaruhusu wawekezaji wenye maduka haya kujipangia bei sawasawa na wenzao ambao hawajasamehewa kodi? Mfano, sukari mitaani inauzwa Sh.1800/= na kwenye maduka haya ni Sh.1650/=, tofauti ni Sh.150/= tu. Je, hii ni sawasawa? Bei za vifaa vya *electronics* kama *TV, Radio, Music System, DVD* na kadhalika, vifaa kama Mafriji, majiko, *washing machine* na vifaa vya jikoni, bei zake hazina tofauti na bei za maduka mengine yanayolopia kodi. *TRA* wana habari na hili? Naomba majibu kwa hili, la sivyo yaondolewe maana yanawanyonya Wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wastaifu wamekuwa wakipata taabu sana kupatiwa matibabu katika Hospitali za Jeshi na hivyo kulazimika kulipia matibabu yao. Kama inavyofahamika, mikataba yao ya ajira inasema Mwanajeshi ataendelea kutibiwa bure mpaka atakapokufa, je, akishastaifu ndiyo amekufa? Kwa nini watu hawa ambao wameitumikia nchi yetu kwa uaminifu mkubwa wasiangaliwe kwa kupewa matibabu kama inavyostahili? Kama sheria haziruhusu, basi Wizara iandae Muswada wa wastaifu hawa ili waweze kupewa huduma ya tiba bila kusumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa toka kwa wanajeshi (walio hai bado) waliopigana vita vya Kagera kwamba hawajalipwa stahiki zao kama walivyoahidiwa na Serikali. Wengine wameshakufa na familia zao hazijalipwa

madai hayo mpaka sasa hivi. Wizara inazungumziaje suala hilo kwa madai halali ya wapiganaji wetu walioletea Taifa letu heshima kubwa katika vita hivyo? Naomba nipewe ufanuzi wa hili kwani nina majina kadhaa ya wapiganaji wanaodai pesa zao wa Jimbo la Singida Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio la milipuko ya mabomu limegharimu roho za Watanzania wenzetu wa Mbagala na Gongolamboto, zaidi ya hilo tukio la Gongolamboto limesababisha uharibifu mkubwa wa makazi ya watu. Kwa kuwa Serikali imeshafanya tathmini ya uharibifu huo, kwa nini zoezi la fidia linachukua muda mrefu kiasi hicho? Kwa familia ambazo bado zinalala kwenye maturubai bila usiri waliochanganyika na watoto wadogo, hiyo maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini maghala haya yanaendelea kulipuka mara kwa mara? Ripoti iliyotakiwa kueleza chanzo cha milipuko hii iko wapi mpaka sasa? Ni wajibu wa wananchi kufahamu tatizo ni nini maana ni haki yao kujuwa usalama wao na wa maghala ya kutunzia silaha wanazozinunua kwa kodi zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dokta Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Katibu Mkuu Bwana Job Masima, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Davis Mwamunyange, Maafisa na askari wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kulinda Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jithada zinazofanywa na Wizara ya kufanya Jeshi lijitegemee kwa miaka mingi nimekuwa nikifutilia kwa shauku kubwa maendeleo ya Shirika la Nyumbu. Sababu kubwa ni matumaini kuwa mafanikio ya kutengeneza magari kama walipanga awali ingelisaidia Taifa kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kununua magari kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia. Kwa vile huenda mradi huu hauendelei kwa sababu ya mtaji, nashauri hatua zifuatazo zichukuliwe:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya Maendeleo ya Magari (*Automotive Sector Development Tax*) ambapo kila gari litakaloingizwa nchini litatozwa kodi ya asilimia mbili (2%) ya thamani yake na kupelekwa Nyumbu kwa ajili ya utafiti na kutengeneza magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumbu liruhusiwe kuingia ubia na kampuni yenye uwezo mkubwa kiteknolojia na rasilimali fedha na watu ili kujenga uwezo wa Shirika kutafiti na kutengeneza magari na vifaa vingine vya kivita. Nchi rafiki iliyotusaidia kuanzisha mradi huu ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili pamoja na majukumu mengine limesaidia wananchi kupata uwezo wa kujilinda kwa kuwauzia silaha kwa bei nafuu sana. Nashauri

kuwa ili Watanzania walio nje ya Dar es Salaam na Morogoro, shirika lipanue wigo wa kutoa huduma zake kwa kufungua maduka kwenye Miji Mikuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiagiza chakula toka nje ya nchi wakati Jeshi la Kujenga Taifa lina mashamba makubwa sana huko Ruvu, Oljoro, Chidya, Usangu, Itende, Bulombora, Mgambo, Makutupora na kadhalika. Kama mashamba hayo yangelimwa na kutunzwa kikamilifu yangezalisha chakula cha kutosha Taifa zima na kusafirisha nje. Nashauri kuwa Jeshi lisimamie na kutumia maeneo hayo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichukua mashamba ya wananchi ili kupisha uanzishaji wa Kituo cha Ulinzi wa Anga, Oldonyosambu. Tokea wananchi hao wahamishwe 1984 hadi leo hawajapewa fidia ya ardhi wala mali na matokeo yake hivi sasa hatu wakifiwa hulazimika kwenda kuomba eneo la kuweka kaburi. Naomba Serikali iwafidie wananchi hao ili kuwaepushia adha inayowapata hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie wasaa huu kuzungumzia machache juu ya Jeshi letu. Jeshi ni jeshi, ndiyo maana Mheshimiwa sana Marehemu Baba wa Taifa aliliita kuwa ni Jeshi la Wananchi, hii kweli kabisa liko hapo kuwalinda watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa Jeshi letu linafanya kinyume chake. Je, ni kwa nini Jeshi kila wakati halijitathmini na kuamua kukumbatia mambo yanayolidhalilisha Jeshi na nchi. Mfano mzuri, ni Jeshi kujitosa kufanya biashara na wahujumu uchumi kama Jeetu Patel (*EPA*) waliowahujumu wananchi. Hii inaonyesha kuwa kuna masuala ya siasa yanaingizwa. Wanajeshi wetu ni watiifu na kwa asili (*nature*) ya kazi zao, viapo vinawazuia kubishia wakuu wao wanapowashushia amri. Bunge lako Tukufu lifanye juhudhi ya kuwasadia wanajeshi wetu dhidi ya viongozi mafisadi watakaojipenyeza kuwatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nichangie njia bora ya kuwatumia Wanajeshi wa Jeshi la Kujenga Taifa, wale wataalam wapangiwe kazi zinazolingana na utaalam wao kwenda kulisaidia Taifa kutokana na sehemu zile ambazo zina tatizo kwa wafanyakazi mfano elimu, wakafundishe, walimu ni wengi, Madaktari pia Mainjinia na kadhalika mwaka hata zaidi wanakuwa jeshini wakiisaidia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze tu kwani ukiondoa hitilafu chache chache, Wanajeshi wa Tanzania wana nidhamu ya hali ya juu bali wanachafuliwa na baadhi ya wanasiasa wanaoingia kuwatumia vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie upya matumizi ya ardhi katika eneo la Kiluvya ambapo kuna Kambi ya Jeshi.

Watoto wengi wa Kijiji cha Tondoroni wanakosa fursa ya elimu kwa sababu wanatakiwa kuhama eneo hilo. Naiomba Serikali ibadilishe matumizi ya eneo hilo kwa kuhamisha Kambi ya Jeshi na kuwabakiza wananchi wa Kijiji cha Mloganzila, Tondoroni, Kiluvya A na B wabaki katika eneo hilo na pia eneo hilo litengwe kwa matumizi mengine ya idara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ipange mpango wa ujenzi wa nyumba za mkopo kwa Wanajeshi kipaumbele kikiwa ni Wanajeshi wa kada ya chini. Pia kuboresha mishahara na mafao ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha Kambi za Jeshi kwa kuwa na mazingira ya kisasa zaidi ili kuongeza ari ya wanajeshi wetu wawapo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo cha JKT kiboreshweli kiwe chanzo cha uchumi cha Taifa hili kwa kuongeza ufundi na hivyo kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na majengo ili uchumi uendelee kubaki ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha kutosha katika bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kama ilivyoainisha katika Fungu 57.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara hii nyeti kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu. Pamoja na pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na jeshi letu natoa ushauri juu ya suala la mahusiano. Kambi zetu za jeshi zimekumbwa na tatizo la ongezeko la mahusiano yasiyordhisha kati yake na wananchi au vijiji vinavyozizunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano halisi ni Kambi ya Jeshi Kaboya, Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera, utawala wa jeshi umekuwa ukibadili mipaka ya jeshi bila kuwahuisha majirani zake (vijiji) kama taratibu za ujirani mwema na ardhi zinavyoolekeza. Kambi ya Kaboya imeweka vizingi na kuzuia mito ya asili ambayo miaka nenda rudi wananchi wamekuwa wakichota maji. Hali hii inachafua mahusiano ya chombo hiki ambacho kwa Mkoa wa Kagera kina sifa nzuri ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Jeshi Kaboya inazo nyaraka ambazo zinaonyesha mipaka yake. Kimsingi hili ni eneo la mashamba ya mzungu lililochukuliwa na Serikali. Kuanzia hatua hiyo Serikali inabidi kuweka wazi eneo lipi ni lake na sehemu gani ni ya vijiji. Kwa masikitiko nimepokea taarifa ambapo wapiganaji wetu wameshikana mashati na wananchi wakigombea miti au mazao kwenye maeneo. Hii siyo stahili ya Jeshi la Wananchi. Tunategemea katika bajeti hii suala hili lipitiwe na zaidi Kambi ya Kaboya irejeshe utaratibu wake wa zamani wa kushirikiana na wananchi katika michezo. Mimi kama Mbunge niko tayari kusimamia jukumu hili.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi za uajiri wa Jeshi Zanzibar zinakuwa finyu kwa Zanzibar. Kwanza usaili wake hata ukifaulu bado unakuwa huna tamaa ya uajiri hadi nafasi ya usaili wa pili itoke Tanzania

Bara ndio utakuwa umefanikiwa. Je, wakati Tanzania Visiwani umekubalika viyi ushindwe kuajiriwa. Nafasi zote za Zanzibar zinakwenda wapi, kwa nini zisirejee tena Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumegundua kwamba nafasi hii huwa ni kiini macho kuja Zanzibar na tayari zinakuwa zimetengewa vijana wa Tanzania Bara, si ya vijana wa Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanajeshi wanapostaafu kazi na kupewa kiinua mgongo chake tayari tumemjengea umaskini kwani tatizo la maisha linaanza kumkumba, anakuwa hana maisha mema, hana uhai, anakuwa kimaisha amechoka. Kimtazamo hawezi kukubalika katika jamii. Tayari tunawafanya wawe majambazi kwani hafanyi kusudi ila anatafuta maisha, kwani wastaaafu hao tayari wana uzoefu wa silaha na wanajua kuitumia. Ili kuwasaidia itabidi tuwaenzi katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali kufanya utafiti wa kambi zao zilizoko mitaani hasa Zanzibar zipo katika hali tata kwani kambi hizo zina silaha nzito. Tumuombe Mungu asaidie isitokee tatizo la mlipuko. Usalama wa Mzanzibari uko wapi? Hata hakuna elimu ya tahadhari iliyotolewa kama elimu ya kujihami na kinga yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara kuliangalia suala hilo na kulipatia tahadhari ya maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na JKT kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake pia kwa uwezo mkubwa wa namna anavyosimamia Wizara hii nyeti kwa ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu hali ya mipaka ya nchi yetu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri katika hotuba yake kwamba pamekuwepo na tatizo la kuvunjwa alama za mipaka mfano, mpaka wa Kaskazini yaani Wilaya za Tarime, Rarya kitu ambacho kinaweza kupoteza uhalisia unaoonesha mipaka yetu na nchi jirani na pengine kupelekea utata wa mpaka, naishauri Serikali kuhakikisha kwamba alama zote za mipaka zinalindwa ipasavyo. Pia nashauri tuwe na ufumbuzi wa kudumu kuhusu mpaka wa Kusini katika Ziwa Nyasa. Ni muhimu kuwa na mpaka wa kueleweka katika eneo hili wakati tuna mahusiano mazuri na nchi ya Malawi. Viongozi wetu wakuu yaani Mheshimiwa Rais wetu Dokta Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya watu wa Malawi Dokta Bingwa Mutharika. Wakati huu ni muafaka kwa sababu ya mahusiano mazuri ya viongozi wetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na hasa ya matumizi ya maendeleo. Jeshi letu linapaswa kununua zana za kisasa ili kuweza kulinda uhuru na usalama wa maisha yetu. Katika siku za hivi karibuni nchi yetu

imeshudia kuwepo kwa milipuko katika makambi ya majeshi yetu hasa kambi ya Mbagala na Gongolamboto. Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba hata makambi mengine yanayohifadhi milipuko yana zana ambazo zinaweza kulipuka kwa sababu milipuko hiyo ni chakavu (*expired*) na hivyo inatakiwa kuharibiwa. Mfano kambi ya ulinzi wa Anga Welezo na Ubago kule Zanzibar zina milipuko ambayo inahitaji kuteketezwa ili kuweza kuhifadhi na kulinda maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu mafunzo ya vijana katika Jeshi la kujenga Taifa. Naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kurejesha mafunzo hayo. Hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hasa vijana wanaropoka sana kwa sababu hawajawahi kupata mafunzo yoyote ya nidhamu, uzalendo na mapenzi kwa nchi yetu. Nashauri Waheshimiwa Wabunge hasa vijana wapate mafunzo mafupi katika JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi letu kwa miradi ya maendeleo ambayo linaisimamia. Kwa vile Jeshi ni taasisi yenyenye nidhamu, nashauri utendaji wake katika miradi linayoisimamia iwe ya kuigwa. Jeshi liweke kumbukumbu zake kwa uwazi kabisa na watendaji wanaopangiwa kusimamia miradi hii wawe waadilifu sana. Pindi wakifanya tabia za wizi, nashauri wapewe adhabu kali ili kutoa funzo kwa wengine wenye tabia kama hiyo. Jeshi liwe kioo cha utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Jeshi liwe na mkakati madhubuti wa kuwasaidia wanajeshi wote wastaafuli ili kwa vile walijitolea maisha yao kuilinda nchi yetu, waendelee kufaidi matunda ya jasho lao baada ya kustaafu hadi Mungu atakapowaita kutoka dunia hii na kuwaingiza kwenye pepo yake. Naomba sana Wizara ianzishe taasisi maalum ya kuwatunza na kuwaenzi wanajeshi wetu mara wanapostaafu. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na maelezo mahsus kuhusu pendekezo hili. Haikubaliki kwa wanajeshi wetu walijitolea muhanga maisha yao, baada ya kustaafu waanze kuishi maisha dhalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa na nzuri ya ulinzi wa Taifa letu pia jitihada za Wizara yako kusaidia wananchi pia wanapopata majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ruangwa lililoko Mkoani Lindi linapakana na Wilaya ya Masasi, Mkoani twara likitenganishwa na Mto mkubwa uitwao Mto Lukuledi. Wananchi wa Jimbo la Ruangwa wanapata huduma ya kiafya hospitali ya Ndanda, Mkoani Mtwara kwa kuvuka Mto huo wa Lukuledi ambao kwa sasa kwa nguvu za wananchi wamejenga daraja la miti ambalo kila ifikapo masika daraja hilo huzolewa na maji. Kutokana na uwezo mdogo wa mapato ya Halmashauri tumeshindwa kupata fedha za kujenga daraja la saruji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata msaada wa kupata madaraja ya vyuma ambayo yameng'olewa kwenye eneo la Nanganga ambako daraja jipya limejengwa ili kuokoa maisha na usumbufu wa kujenga kila mwaka msimu wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri anayoifanya. Napenda pia kutoa pongezi kwa Katibu wa Wizara na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kubwa kwa Mkuu wa Majeshi, Jenerali Davis Mwamunyange; Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Abdulrahmani Shimbo pamoja na Maofisa wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Kujenga Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi na shukrani za pekee ni kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa jinsi anavyoendelea kuimarisha na kulipa nguvu Jeshi letu. Ni kweli wanajeshi wanafanya kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa raia au wananchi ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, kutokana na kazi nzuri wanayoifanya Serikali yetu inabidi iwaangalie zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka yetu imezidi kuwa imara. Lakini, naomba Waziri Dokta Mwinyi na Wizara yake waangalie zaidi na kuboresha Wizara. Kwa mfano, mpakani mwa Tanzania na Malawi, upande wa Malawi kuna walinzi masaa yote, hii sivyo ilivyo upande wa pili wa nchi yetu. Kwa hiyo, naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Wanajeshi na Vikosi vya Kujenga Taifa yaboreshwe zaidi. Jambo zuri na kubwa wanaloofanya ni kutekeleza kilimo kwanza. Nikiwa Mbunge wa Mkoa wa Morogoro, natoa pongezi kwa vikosi vyetu vya Morogoro wanavyojituma katika kilimo kwanza. Kikosi cha Mzinga Morogoro, walizalisha mbegu za kilimo cha miembe. Pia Mkuu wa Kikosi hiki Kanali Charles Mzanila kwa kazi nzuri anayofanya. Wanajeshi wote kwa vikosi vyote wanapaswa kuwa kama yeye (*Creative*). Ameweka kitega uchumi, ujasiriamali, kuna ukumbi mzuri wa jeshi ambao sherehe zote za Morogoro Mjini zinafanyika Mzinga. Watu wa namna hii wanapaswa kupewa motisha. Mzinga wanaingizia Jeshi kipato, kwa hiyo, Ofisa huyo na maafisa wenzake wafikiriwe kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Jeshi la Kujenga Taifa wanafanya kazi nzuri. Mlale JKT – Songea, Ruvuma, Mkuu wa kambi anafanya kazi nzuri sana. Kambi hii wamejikita katika kilimo kwanza, wanazalisha mbegu za mahindi. Naomba wapeni vifaa zaidi vya kilimo ili waweze kuzalisha mbegu zaidi. Mbegu hizi zitatumika au zinatumika Mkoani Ruvuma, ukiwa Mkoa wa Kilimo. Kwa sababu kijana huyu anafanya kazi nzuri na yeye apewe motisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanaomaliza darasa la saba, hawapati nafasi ya kuendelea na kidato cha kwanza. Kwa hiyo, vijana hawa waangaliwe, wengi wajiunge na JKT. Hivyo, vigezo vyta kijiungu na JKT kama urefu na *cutting point* (28) *Division IV* viangaliwe zaidi kusudi vijana wengi waingie JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa na timu yake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongozi pia ziende kwa Mkuu wa kikosi cha Mzinga, Morogoro kwa kazi nzuri ambayo hata wananchi wa kawaida wanaiona, ni ubunifu sana, amebadilisha mandhari ya mzinga kwa kujenga ukumbi wa kisasa ambao unatumika na Morogoro kwa shughuli zao mbalimbali (sherehe na mikutano), pia amefanya mambo mazuri ya kilimo kwanza. Katika kilimo wanafanya vizuri, uungwana mtu akifanya vizuri apongezwe na akiharibu akosolewe, Kanali Charles Muzanila anastahili pongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Serikali katika taasisi nyingi zinazotoa huduma kwa jeshi letu kama vile umeme na maji inaonekana jeshi letu wanadaiwa sana, hususan Mtwara, mamlaka ya Maji safi *MTUWASA* wanadaiwa deni kubwa la umeme ambapo wangeweza kulilipa kama Jeshi la Wananchi wangelilipa deni lao kwa *TANESCO*. Mamlaka ya maji ilinusurika kukata huduma ya maji kwa wakazi wa Mtwara kama isingekuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kutangaza hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Wambura kuhusu deni hilo. Serikali ihakikishe madeni haya yanalipwa kwa watoa huduma na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mchakato wa uteuzi wa vijana wa kijiungu na Jeshi, malalamiko mengi yanatolewa na wananchi kwa vijana wanaodahiliwa kwenda kijiungu na Jeshi la kujenga Taifa wanachukuliwa kwa upendeleo, wengi ni ndugu wa Wakuu wa Idara katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya au Wakuu wa Wilaya wenyewe na hata wale waliopitia JKT wanaoteuliwa kupatiwa mafunzo ya ziada kwenye shule za Mafunzo (*RTS*) kuwa nafasi zinazotolewa kwa upendeleo, nashauri Wizara ipange namna ambayo itaondoa hisia za upendeleo kwa jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maisha ya wanajeshi baada ya kustaafu inaonekana hawana maisha mazuri kwa maana ya mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wangu ni kwamba ni vema sasa Wizara ikaandaa mafunzo ya kuwawezesha wanajeshi wetu namna ya kuishi baada ya kustaafu, wapewe mafunzo ya kujitambua kwamba baada ya maisha ya kijeshi wanatakiwa kijiandaa kwenda kuishi katika jamii, wawe wanajiandaa kwa kuwa na nyumba, ujenzi wa nyumba wanaweza wakahamasishwa wakiwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mishahara midogo siyo hoja, mbona Walimu na Wauguzi wana mishahara midogo na wanajiandaa kwa makazi bado wakiwa kazini?

Athari ya kusubiri mpaka wastaafu inawafanya kutumia sehemu kubwa ya mafao yao kujenga nyumba na mara nyingi hawamalizi. Mafunzo pia yalenge kwenye *financial management* kwamba waelekezwe namna ya wao wenyewe wajue namna ya kutumia vizuri kila wanachopata inaonekana wengi ni walevi siamini kama wanakuwa wana athari za kimaisha “frustrated” wanahitaji elimu ya maisha tu.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la kujenga Taifa limejikuta lipo katikati ya makazi ya watu ambapo si stahiki yake. Tunaitaka Serikali kuliangalia hilo na kuhamisha jeshi katikati ya miji na makazi ya watu. Kwa kuwa viwanja vinatolewa na Serikali na jeshi pia ni la Serikali yetu kuna uwezekano wa kuwahamisha au kulihamisha jeshi mji unapokua ili kuondoa mikinzano kati ya jeshi na wananchi. Mfano Zanzibar kambi zote za jeshi zipo mijini na kila ndani ya kilomita saba kutoka mjini kuna kambi kama vile Migombani, Nyuki, Mwera na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na mkakati maalum wa kuwawezesha wastaafu kuwapatia mafao na pia wale wote waliokufa kazini kuenziwa familia zao na kuondokana na matatizo ya kimaisha. Pia Bima ya Afya kwa wastaafu wa jeshi na hata kwa familia zao baada ya kustaafuli ili kuwaenzi kwa vitendo wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iboreshe makazi ya wanajeshi wetu kwani makazi yao ni machakavu na hayaridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu heshima katika maeneo ya Jeshini. Inapendeza kuona kuwa katika eneo ama kambi ya jeshi kusiwe na njia ya kupita kama ilivyo, kwani kwa sasa katikati ya kambi ya jeshi kuna njia ya kupita raia wa kawaida. Tunataka kambi iwe kama kambi na ihodhiwe na jeshi tu bila kuingiliwa na shughuli za kimaisha za watu kama vile barabara, wananchi wa kawaida kukatiza au kupita ndani ya eneo la jeshi bila ya shughuli mahususi. Jeshi likiwa nje ya mji hakuna raia atakayepitapita ndani ya eneo la jeshi bila shughuli au sababu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar katika kambi iliyopo nyuki ni kero kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo kwa kuwa ipo jirani na hosteli za SOS, hivyo huwa ni kero kwa wanafunzi na wakazi wengine wa jirani na hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Pemba eneo la Meccy lililopo Wawi Matrekta ambapo wanajeshi huwa ni sehemu yao ya starehe na pia kuwakera wakazi wa maeneo hayo kwa kutumia vibaya eneo hilo kwani kila balaa hupatikana hapo kama vile ulevi, ukahaba na tabia mbovu zinazopatikana katika eneo hilo. Tunaitaka Serikali na kushirikiana na Wizara yako kuliangalia hili na kulifanyia kazi ili kulinda na kuenzi tamaduni na heshima za wakazi (wazanzibari).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na milipuko ya mabomu katika maeneo ya Gongolamboto na Mbagala kulikopelekea wananchi wengi kupoteza maisha na wengine makazi. Ambapo hadi leo kuna wahanga wanaishi kwenye mahema bila ya kujuu mwelekeo wa maisha yao na uhakika wa maisha yao ya kila siku. Tunaitaka Serikali

kukamilisha zoezi la kuwapatia hifadhi ya makazi na pia kuwawezesha ili kujiedeleza katika maisha yao na kuwa na uhakika wa maisha yao ya kila siku.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri pamoja na uongozi wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba nzuri na yenye kueleweka, lakini kubwa zaidi hotuba ambayo inaendana na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu unaendana na mambo mawili ndani ya Jeshi la Ulinzi ambayo ni ajira na mwenendo mzima wa Uongozi ndani ya JWTZ

Mheshimiwa Naibu Spika, katika JWTZ hakuna uwiano wa ajira kati ya nchi mbili hizi zilizoungana. Sura ya jeshi hili linadhahirisha wazi kwamba liko upande mmoja wa Muungano yaani Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18/06/2008, Naibu Waziri alisema napenda kunukuu: "Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba hatuna utaratibu wa kugawa askari wetu kwa misingi ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli kama hii ndiyo inayosababisha Zanzibar kukosa haki yao. Hii inamaanisha hata maana ya Muungano vijana hawaelewi. Kwa muundo huu Zanzibar haina maslahi ya Muungano ndani ya chombo hiki. Idadi ya vijana Bara waliojiunga na Jeshi la kujenga Taifa mwaka 2009 – 2010 ni 4,297 wa Operesheni Uadilifu na 4,400 wa Operesheni Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya vijana hawa ndiyo wale baadhi yao wanajiunga na JWTZ. Kwa idadi kama hii kama hapakuwa na mgawano Mzanzibari atakuwa na nafasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe hiyo hiyo 18/06/2008 Naibu Waziri alisema, naomba kunukuu: "Mheshimiwa Mwenyekiti ili kuhakikisha kwamba, tunaziba mianya yote ya upendeleo na kupata vijana wanaoandaliwa vizuri katika mafunzo ya awali ya kijeshi, JWTZ limebadili utaratibu wa awali wa kuchukua vijana. Hivyo kuanzia Julai Mosi 2005, JWTZ litaajiri vijana waliopita JKU na JKT." Mwisho wa kunukuuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni kauli zinazoonyesha udanganyifu mara haangalii sehemu anayotoka, mara anaelekea kutoka JKT na JKU. Wazanzibari tunasema Jeshi litoke Zanzibar mbali na Tanzania Bara, mbali kwa idadi inayokubalika ili Wazanzibari wapate haki zao, tumechoka na madhila yalijotawala ndani ya Jeshi. Pia hatutaki nafasi za Zanzibar kuingizwa vijana kutoka Bara kwa kutumia ujamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wote wa Jeshi umetawala upande mmoja wa Muungano. Hii ni hatari kwa Zanzibar hakuna kambi hata moja kiongozi kutoka Zanzibar. Hivyo, wenzetu mna siri gani? Huu sio utawala bora lazima nafasi tugawane.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pia nawapongeza wanajeshi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naomba kuchangia ni kuhusu mabomu ya Gongolamboto. Ajali hiyo mbaya ilisababisha maafa makubwa ambapo Watanzania wenzetu wamepoteza maisha yao na wengine kadhaa wamejeruhiwa wakiwemo waliopoteza viungo na kupata ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kushughulikia nyumba za wakazi wa eneo lile kwa haraka, kwa kuwa wanaishi maisha ya tabu sana kwa kuishi kwa majirani, yale mahema yamechoka kwa mvua. Nasema hayo kwa kuwa mimi ni shuhuda wa haya maafa, ni mkazi wa Gongolamboto na nilitembelea maeneo yote yaliyoathirika, mpaka kambini nilikwenda kutoa pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wale waliopata ulemavu wasaidiwe kwa namna ya pekee kwa kuwa ulemavu walioupata utawaathiri kwa kiasi kikubwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha atuambie idadi ya waliopata ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwapongeza wanajeshi wanaolinda amani huko Darfur na Lebanon kwa kazi nzuri wanayoifanya, kikubwa ni kwamba waangaliwe hali zao kwa kina kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri na wataalam wake wote kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta hapa Bungeni. Waziri wa Wizara hii alitoa kauli hapa Bungeni baada ya kutokea milipuko ya mabomu Mbagala kwamba ripoti/taarifa ya uchunguzi wa tukio lile italetwa hapa Bungeni ili Wabunge waweze kuiona. Leo ni miaka miwili ripoti imeshatoka inafanywa siri. Kwa nini wawakilishi wa wananchi wanafichwa ripoti muhimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejifunza nini kutokana na matukio mawili makubwa ya milipuko ya mabomu ya Mbagala na Gongolamboto yaliyopoteza mamia ya Watanzania wasio na hatia na wengine kupata ulemavu wa maisha? Wapo wananchi ambao bado wanaishi jirani/karibu na kambi za Jeshi maeneo mbalimbali hapa nchini Serikali ieleteze Bunge, kuna mipango gani ya kuhakikisha wananchi hao hawatapata madhara ya kulipukiwa na mabomu tena? Kwa kuwa mabomu hayatoi taarifa, wala Jeshi halijui lini yatalipuka, Wizara hii imekwendaa mikakati gani ya dhati kuepusha majanga haya yanayotokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walioathirika kwa mabomu bado wako kwenye mahema wakitaabika kwa juu na mvua, wamekuwa kama wakimbizi ndani ya nchi yao. *This is unfair!* Serikali itawatoa lini kwenye tabu wanayopata? Lini watajengewa nyumba waweze kuleta familia zao kama wengine? Misaada inayotolewa kwa wahanga wa mabomu na iliyokwishatolewa mamilioni ya fedha na vifaa mbalimbali kwa upendeleo. Malalamiko yanatolewa kila leo, vyakula vinavyotolewa havifiki kama

vilivyopangwa, viongozi wanaogawa misaada ile wanapunguza kwa kujinufaisha wao, mifuko ya sembe inafunguliwa kama ni kilo 50 wanatoa kilo 20 wanapeleka kwa mlengwa kilo 30. Lakini wanalazimishwa kusaini kilo 50 kamili. Huu ni wizi wa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha misaada ile inawanufaisha walengwa? Kwa kuwa wahanga wamekuwa wanalamikia viongozi wanaotafuna misaada yao. Je ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wahusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa ni pongezi kwa Jeshi au Wanajeshi wetu kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kulinda nchi yetu, mipaka yetu na ndani ya nchi. Tunaathirika na kuenzi utendaji wao na tunaiomba Serikali ijali na kuangalia maslahi yao kwa ujumla wake kuanzia mishahara, makazi, marupurupu, posho zao na familia zao pia.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni moja kati ya vyombo vikuu vya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Chombo hiki cha Jeshi la Wananchi Tanzania kiliunganishwa kwa lengo na madhumuni ya kuwalinda Watanzania wa Bara na Visiwani. Jeshi la Wananchi Tanzania ni la Watanzania wote na linawajibu wa kusimamia haki za pande zote. Kutokana na umuhimu wa chombo hiki cha Jeshi la Wananchi tokea kuasiwi kwake kama chombo cha Muungano ni Wazanzibar wangapi wamepewa dhamana za juu katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania ukiachia nafasi ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akiwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wetu ambao mwaka 1979 walishiriki katika vita vya Uganda, baada ya vita vile walilipwa nini baada ya ile ahsante waliyopewa na baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. Wale ambao walirudi vilema walilipwa nini? Wale ambao walifariki familia zao zilifikiriwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna waathirika wa vita vya Uganda au matokeo mengine yoyote ambayo yalinasibika na matokeo ya ulinzi wa nchi yetu waathirika hao ni lazima waangaliwe na wapewe malipo ambayo yatawasaidia wasiwe omboomba kana kwamba walikuwa na laana ya kulitumikia Taifa hili.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kushukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Naomba nielekeze mchango wangu upande wa Miundombinu ya kazi za Maaskari wetu wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) na hasa wale wa kambi ya Potoa, kambi ambayo ipo katika Jimbo langu la Mkwajuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati nilipata bahati ya kutembelea kambi hii na mionganoni mwa matatizo walionieleza ni ukosefu wa sehemu ya kuridhisha ya kufanya kazi zao. Hii ni kutokana na kuwa majengo ya Ofisi zao ni mabovu sana, yanavujisha wakati wa mvua kiasi cha kuwafanya washindwe kutekeleza majukumu yao ya kazi na hata wakati mwingine kutumia vifaa mbalimbali kama vidoo vya *plastic* kuzuia maji yanayoingia ndani yasisambae na kuathiri baadhi ya vifaa vilivyo sambaa kwenye sakafu

vilowane. Hivyo, namwomba Waziri atafute muda maalum ili afuatane nami twende kwenye kambi hii ili ajionee mwenyewe hali ngumu waliyonayo askari wetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ni lile linalohusiana na Pensheni ya Maaskari wetu wastaaafu, ni suala ambalo linazungumzwa na kila mmoja wetu kwa kuwa ni suala linalomsikitisha kila mmoja wetu. Pensheni wanayopewa askari wastaaafu ni ndogo mno hailingani kabisa na jinsi ya uzito wa kazi yao waliyokuwa wakiifanya wakati wa Utumishi wao Jeshini. Sio tu kwamba Pensheni hiyo ni ndogo lakini pia muda inayotolewa unakuwa ni mrefu mno. Kipindi cha miazezi sita kulipa Pensheni askari aliystaaafu ni kipindi kikubwa mno na hasa kwa mtu ambaye maisha yake yamelenga katika kutegemea Pensheni hiyo. Hivyo, ningeomba Serikali kujaribu kufikiria upya suala la kuongeza kima cha Pensheni kwa Askari wetu hawa, aidha, kupunguza muda wa utoaji wa Pensheni hiyo angala badala ya kuwa ni kila baada ya miezi sita basi iwe ni baada ya miezi miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika kuchangia suala la *Uniform* (sare) wanazovaa Maaskari wetu. Kama sikosei zamani kulikuwa na Sheria ambayo ilikuwa imeweka udhibiti wa uvaaji wa sare hizo. Hivi sasa inaonekana kwamba ni jambo la kawaida kumkuta raia wa kawaida asiyekuwa Askari kavaa sare ya Jeshi na huku akitembea barabarani bila ya kuwa na wasiwasi wowote wa kutiwa nguvuni na vyombo vya dola. Hii ni hatari kwa Taifa letu kuona kwamba sare za Maaskari wetu kuwa sasa ndio *fashion* kwa vijana wa mitaani, hii ina maana ya kuukaribisha uhalifu ndani ya nchi utakaochukua sura ya kufanywa na vikosi vya Jeshi letu la Ulinzi jambo ambalo litapelekea Jeshi letu kutoaminika mbele ya macho ya wananchi na si tu kutoaminika bali pia kutoheshimika. Hivyo, naiomba Serikali kuchukua hatua makusudi za kuweka Sheria itakayokataza uvaaji wa *uniform* za askari kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu katika changamoto za hapa na pale kwa kulimudu kama mwanamke shupavu. Hongera sana wanawake tunaweza. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni na kuchangia kwa uchache. Natoa shukrani kwa viongozi wangu wa Chama cha Wananchi (*CUF*), kwa kunitua kuwa mwakilishi wa Mkoa wa Dodoma (Mbunge wa Viti Maalum Kondo).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri ya kulinda amani na utulivu kuliko nchi nyininge za jirani. Jeshi letu pamoja na ukakamavu inayoonyesha naunga mkono hoja hii ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012, kwa mafungu yote matatu (73,206,000.00). Kama ilivyo Fungu (38), Ngome (39), JKT (57), Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kuwa sekta ya Ulinzi na Usalama, Wizara inahitaji matumizi ya jumla Sh. 682,999,603,224/= kwa mafungu yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Jeshi letu la kulinda mipaka inabidi juhudzi za ziada zichukuliwe, zaidi kwenye kulinda mipaka yetu kwani bado tuna wimbi linalojitokeza la kupokea wakimbizi ambao si waadilifu husababisha kuingiza silaha kinyemela na kuichafua nchi yetu kwa ujambazi pia angalizo liwepo kwa Jeshi tokea wanapojiunga na mafunzo haya kwani baadhi yao hujihusisha na vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza wizi wa ujambazi hauanzi hivi hivi tu ila kuanzia utotoni hadi ukubwani na kuwa jambazi. Ningependa kuona jeshi hili kuwa la kisasa, wanajeshi wajengewe nyumba, wanapostaafu walipwe mafao yao mapema ili waweze kulea familia zao wakiwa na nguvu na wale waliopoteza maisha watoto wao au familia zao zitunzwe na ziendelezwu kitaaluma katika masomo ili kuwapa hamasa vijana wengi kupenda kuijunga na Jeshi na hivyo kufanya ushindani katika ajira ya Jeshi na kufanya Jeshi lipate vijana bora na wenye uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la michezo Jeshini ni muhimu ili kujenga afya, burudani na mazingira ya urafiki mionganini mwa wanajeshi wetu. Michezo ikiendelezwu Jeshini ni fursa nyingine kupata ushindi wa Kimataifa katika michezo na kuliletea Taifa sifa kubwa. Jambo hili litapelekea kuwa na Jeshi zuri na la kisasa ambalo litakuwa na uwezo sawa na majeshi ya nchi nyingine au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri. Nianze kwa suala la makazi ya Wanajeshi, ni kipindi kirefu nyumba za kambi ambazo wanaishi Wanajeshi hao ni mbovu sana na hazijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu, mfano Kambi ya Mtoni, Kambi ya Mwanyanya, nyumba zao zote mbovu. Hivyo, nashauri nyumba hizo zifanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malipo ya wafanyakazi wa ulinzi ni kipindi kirefu kuna wafanyakazi ambao wanakwenda safari za kikazi, lakini posho zao huwa hawalipwi vile vile wafanyakazi wengine huwa wanakwenda mafunzioni (*course*), imebainika kwamba mfanyakazi huyo hujilipia mwenyewe gharama za safari na akimaliza mafunzo pesa zake huwa halipwi au hata kucheleweshwa malipo haya, vile vile malipo kwa wastaafu wanachelewa kulipwa. Nashauri Wizara iandae mpango maalum wa kupita kila kambi kutafuta wale Askari ambao wanadai malipo mbalimbali ili kuchukua hatua ya kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uajiri, imekuwa ni utaratibu wa Kijeshi kuwaajiri vijana kila baada ya muda, lakini hata hivyo kwa upande wa uajiri wa vijana kutoka Zanzibar wanapofika Tanzania Bara, kupimwa na kuambiwa hawafai, hawana vigezo, wakati kijana huyo ametumia gharama kubwa na akirejeshwa hata nauli ya kurudia anakuwa hana. Hivyo, nashauri vijana wote kutoka Zanzibar wapimwe Afya zao huko huko Zanzibar kuitia Hospitali kubwa ya Bububu na kama hakuna Daktari, Wizara ipeleke Daktari mwenye dhamana akaifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya Jeshi ya Mwanyanya kambi hii kwa muda mrefu imekuwa haina maji kwa matumizi ya Wanajeshi hao, hivyo nashauri kambi ipatiwe huduma ya maji. Pia kambi hii iko katikati ya vijiji na iko wazi sana na haina uzio, hivyo, nashauri kambi hii izungushe uzio au ukuta ili angalau kambi hiyo iwe na heshima ya kuitwa kambi. Aidha, nashauri kambi hii ipatiwe huduma ya usafiri wa gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bima ya Afya ya Wanajeshi. Lengo na madhumuni ya Bima hii ni kumwezesha Mwanajeshi huyo kupata huduma ya Afya bila ya matatizo, lakini kumekuwa na malalamiko kuwa, huduma inayopatikana katika Hospitali zilizotengwa ni huduma finyu na makato ya mwisho wa mwezi ni makato makubwa sana kuliko huduma anayopata mhusika huyo. Nashauri suala hili liangaliwe kwa kina na lifanyiwe marekebisho ya haraka, hususan kwa wanajeshi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Ofisi ya Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Ulinzi ni Wizara ya Muungano na imekuwa na Makao Makuu yake Dar es Salaam na mwananchi au kiongozi anapotaka kufuatalia masuala mbalimbali hasa anayetoka Zanzibar inakuwa ni vigumu mpaka apande Ndege au Boti ndio afike. Hivyo, nashauri Wizara kupitia Serikali Kuu ianzishe Ofisi ya Wizara ya Ulinzi kwa upande wa Zanzibar na si vibaya akawekwa Naibu Katibu Mkuu kwa upande wa Wizara hiyo huko Zanzibar na hii itaondoa usumbufu wa ufuataliji kwa masuala ya Wizara (*management*) kiutawala yatakuwa rahisi na itaondoa kabisa usumbufu.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi ni chombo muhimu sana ndani ya nchi yetu na kwa kuwa pia ni chombo cha Muungano, tungetegemea kwamba, wakati wa kuajiri jeshi lingetangaza na kuzingatia Muungano wetu kati ya Bara na Zanzibar. Basi wangezigawa nafasi na kwa zile za Zanzibar yafanyike kwa vijana wa Zanzibar peke yao na wala wasichanganywe na wale wa Bara. Kitendo cha kuwafanya usaili wa pamoja, hii inaleta dhana kwamba vijana watokao Zanzibar wanafelishwa kwa makusudi kabisa kwa kisingizio cha kukosa sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa za kuajiri vijana ni kuwa na elimu ya *Form IV*, lakini kwa vijana watokao Tanganyika, hata wale wa Darasa la Saba (VII) wanachukuliwa na wanaonekana kwamba wana sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani wanajeshi katika miaka 1977, nafasi za kozi kwa maafisa (*Officer cadet*) zilikuwa zikigaiwa, na Zanzibar ilikuwa na nafasi zake ambapo ilikuwa ni lazima nafasi hizo zizajwe na Wazanzibar wenyewe. Hii ilikuwa na dhana kwamba nafasi za juu ndani ya Jeshi ziwe na uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili sasa halipo na tatizo limethihirika kwamba hivi sasa katika chombo hiki cha Muungano sura iliopo ni kwamba nafasi za juu kuanzia Mkuu wa Majeshi hadi wanadhimu ndani ya chombo hiki hakuna Mzanzibar hata mmoja, jambo ambalo mimi naomba Waziri atuambie: Je, hakuna Mzanzibar ambaye anasifa ya kuwa katika nafasi hizi za juu Jeshini?

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani maafisa walipokuwa wanamaliza mafunzo yao, walikuwa na kiapo cha utii kwa Serikali ya Muungano pamoja na viongozi wake, lakini pia utii kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na viongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la kiapo cha utii kwa maofisa hawa ni kwa Serikali ya Muungano tu na hawana jukumu la utii kwa viongozi wa Zanzibar. Hii ni kuidhalilisha Zanzibar na viongozi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi hawa baada ya vita ile waliahidiwa kwamba pamoja na ahsante waliyopewa na Mwalimu Nyerere, lakini walipewa ahadi ya kulipwa pesa za vitani, lakini hadi leo hii wapo ambao hawajalipwa fedha hizo. Naishauri Serikali kwanza ijali kazi kubwa iliyofanywa na wanajeshi hawa na kwamba ili kuonesha kujali kazi hiyo waliyoifanya, basi iwalipe fedha hizo wale wote ambao bado hawajalipwa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna tatizo kwamba hatujali umuhimu wa fani, ujuzi au utaalalm alionao mfanyakazi. Ifikapo muda wa kustaaafu kisheria, mstaafu huyo bila kujali sifa aliyonayo, Serikali inaona watu hawa hakuna haja ya kuwafikiria tena, na huwa tunasubiri wakati wa dharura ndipo tunaulizana, tutafanyaje. Naishauri Serikali kwamba watu wa namna hii kwa umuhimu wao, basi ni vyema iendelee kuwa nao kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu hawa bado wanastahili kuishi kama watu wengine. Hivyo basi, suala la kuwalipa pensheni wastaafu kwa miezi sita, hili siyo jambo zuri. Naomba niishauri Serikali iwalipe wastaafu hawa kila mwezi badala ya miezi sita, lakini pia pensheni hizi ziendane na ongezeko la viwango vilivyopo vya mishahara kwa wafanyakazi ili na wao waweze kujikongoja kufuatana na mwenendo wa hali ya maisha hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. ALPHAXARD KANGI NDEGE LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau niweze kuchangia hotuba hii kwa maandishi.

Kwanza, nalipongeza jeshi letu kwa kazi nzuri ya kuendelea kulinda mipaka ya nchi yetu na hivyo kudumisha ulinzi na usalama kwa nchi yetu. Pia napongeza Jeshi letu kuendelea kufanya na kushiriki mazoezi ya kivita ndani ya EAC ikiwa ni pamoja na kushiriki kuleta amani kule visiwa vya Comoro na Darfur.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu linazo changamoto nyingi ambazo ni pamoja na uduni katika utaalalm wa kuhifadhi zana za kivita hususan mabomu kama ilivyodhahirika katika makambi ya Mbagala na Gongolamboto na kusababisha vifo na ucharibifu wa mali. Je, Wizara inahakikishaje kwamba tatizo hili halitoki tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wananchi waliopata hasara ya mali na uharibifu wa nyumba huko Gongolamboto bado hawajafidiwa, sasa nataka kujua tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi walio wengi wanapostaafu wanakuwa hawana nyumba za kuishi kutokana na udogo wa mishahara yao kushindwa kuwajengea uwezo wa kujenga nyumba. Je, Wizara haioni haja na umuhimu wa kuanzisha mfuko maalum wa kuwapatia mkopo wa ujenzi wa nyumba na kuwasidia kupata viwanja kwa urahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la wanajeshi kuwabugudhi raia na kuwanyanya ikiwa ni pamoja na kuwapiga na kuwajeruhi. Aidha, jeshi limekuwa na tabia ya kuvamia ardhi ya wananchi maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Naomba nizungumzie uvamizi wa ardhi uliofanywa na JWTZ mwaka juzi, 2009 katika Kijiji cha Bunere kwa kuchukua mlima Chitafubhu zaidi ya ekari 30 ambapo kuna mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo liko katikati ya Kijiji hicho na limekuwa eneo la kufanyia mazoezi ya kivita ambapo mazoezi yamefanyika mara mbili. Mazoezi haya kufanyika katikati ya kijiji, yamekuwa yakisababisha hofu kubwa mionganoni mwa wananchi wa vijiji vyote vilivyoko jirani na kijiji cha Bunere.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uvamizi huo wa ardhi ya wananchi, Jeshi limeweka mabango kuzunguka eneo vamizi yanayosomeka: “HATARI – HILI NI ENEO LA JESHI HAIRUHUSIWI RAIA YEYOTE KUINGIA ENEO HILI – AMRI.” Mabango haya pia yameendelea kuwatia hofu wananchi na hivyo kusababisha jeshi hilo kuchukiwa na wananchi hao. Naomba Waziri anipe maelezo ya kina na tamko ambalo Jeshi litatakiwa kuachia eneo hilo kwani ni kinyume na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kusema hayo, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie hoja zangu na kuzitolea maelezo ya kina, ama sivyo itaniwia vigumu kuitisha bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumize mambo matatu. La kwanza ni tatizo la mabomu ya Mbagala na Gongolamboto yaliyopoteza maisha ya Watanzania wengi wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu haiko makini na hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu, kwani tatizo lilipotokea mara ya kwanza tulisema bahati mbaya, lakini jambo hili lilipojirudia tena, hii ni aibu kwa Taifa letu kwa jambo lile lile kujirudia

ambalo limepoteza tena uhai wa Watanzania. Naishauri Serikali kutokukubali jambo hili likajirudia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nilipenda kuchangia na kushauri Wizara irudishe haraka JKT – Jeshi la Kujenga Taifa. Umuhimu wa JKT unaonekana hapa nchini mpaka imesababisha vijana wengi kukosa nidhamu jambo ambalo ni bayaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya kuboresha nidhamu, pia ni muhimu sana kwa kuongeza ajira kwa vijana wetu, kwani huwa wanapata mafunzo ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya kazi za maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nilipenda kuchangia kuhusu Makambi yaliyokuwa JKT - mfano Mafinga, hayatumiki ipasavyo na tukiendelea kuacha hivi hivi, yatakuja kuwa magofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mipango mizuri na hotuba nzuri. Nalipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri ambayo linafanya ya kuhakikisha mipaka yetu ni salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri JKT ipanuliwe na uandikishaji upanuliwe/uongozwe kwa kuwa vijana wetu wengi wanashauku ya kujiunga. Jeshi hili linawasaadida vijana kuwa wakakamavu na pia kuamsha utaifa wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwa dhati kwamba suala la makazi liangaliwe, wapiganaji wajengewe nyumba zinazofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri hili liangaliwe kwani wapiganaji wanastaafu wangali na afya nzuri na bila kuzeeka hata kidogo.

**MHE. LUHAGA JOELSON MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza kuwa ni lini mafao ya Mzee Shiwa Shigela mkazi wa Kijiji cha Mwabusahi Jimbo la Kisese aliyeshiriki Vita Kuu ya Pili ya Dunia yatalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge vijana ambaao tulikuta utaratibu wa mafunzo ya JKT umefutwa tutapataje fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo kuanzia sasa na kwamba tujenge uzalendo na umoja wa Kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri mpango wa Serikali wa kuwapa mafunzo ya JKT, vijana wote wanaohitimu Kidato cha Sita, Serikali itakubaliana nami kuwa kutokana na idadi kubwa na ongozeko la vijana nchini na ili kufikia malengo ya kuwajenga vijana wasomi wa kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, ujasiri na umoja wa kitaifa ni muda muafaka sasa wa kuzifanya shule zote za sekondari toka kidato cha I – IV kuwa za Kijeshi? Yaani zitoe mafunzo ya JKT.

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi yake nzuri inayofanya kwa kulinda nchi yetu, watu wake na mali zake. Naiomba Serikali ijitahidi kuangalia na kuongezea Wizara hii uwezo kwa mahitaji muhimu yote ili Jeshi letu liendelee kufanya kazi yake vizuri kwa kuwa hakuna ufanisi wa jambo lolote bila kuwepo kwa usalama na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi yake ya uingizaji wa matrektakaribisha nchini kupidia Shirika la Uzalishaji mali JKT (SUMA JKT) kwa nia ya kuendeleza jitihada za Serikali kwa kauli mbiu ya “Kilimo Kwanza”.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara itoe ushauri kwa Serikali kupunguza bei ya matrekta ili wananchi waweze kunufaika kuhamasika na kuweza kununua matrekta hayo. Kwani uwezo wa wananchi ni mdogo, matrekta yasipopunguzwa bei ipo hatari ya matrekta hayo kuendelea kulundikana na baadaye kuharibika kwa kukaa muda mrefu bila kufanya kazi na hatimaye Serikali kupata hasara kubwa, hivyo bei ya matrekta ipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wetu wanapomaliza utumishi wao kwa nchi, waenziwe kwa kuwaongezea mafao yao na kupewa kwa mtiririko wa kuwafanya wasiwe omibaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iongeze kasi ya idadi ya vijana wetu wanapomaliza Kidato cha Sita kuingia JKT, wapitie mafunzo ya JKT ili kupata mafunzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujifunza uzalendo wa nchi yetu, maadili ya Mtanzania na historia ya nchi yetu, kabla ya kupata uhuru na baada ya kupata uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake ya bajeti kwa umahiri mkubwa. Hata hivyo niwape pole kwa bajeti ndogo ambayo haifikii malengo. Tunategemea uadilifu wa Wizara na Jeshi utajibana kwa hicho kiwango cha fedha kilichopatikana kuteketeza kazi iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dhamira thabiti ya Serikali kurejesha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, napenda kuishauri Serikali iandae vema makada ambao watakuja kufundisha vijana hawa katika masuala ya uzalendo na kujitolea. Taifa letu sasa linakabiliwa na changamoto za mmomonyoko wa maadili, kukosekana kwa uadilifu katika utumishi wa umma, tabia za udanganyifu katika mitihani, uvivu, madawa ya kulevyu, kukosekana kwa tabia ya kujitolea kwa ajili ya jamii na tabia ya utegemezi katika jamii (ombaomba). Mahali pa mafunzo kama JKT licha ya kufundisha ukakamavu na ujasiri, ni mahali muafaka kwa kufundishia maadili ya Taifa letu. Kwa kuwa mafunzo haya yatatorewa katika umri wa vijana, sina shaka yataeleweka vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kutokana na tatizo la upungufu wa ajira kwa vijana wengi nchini JKT inaweza kutumika vema kuwa mahali pa kujenga tabia ya

ubunifu na utalaam wa ujasiria mali kwa vijana wetu, hususan wale wasio na mpango wa maendeleo ya elimu ya juu. Hivyo ushirikishaji wa taasisi kama vile *SIDO* na *VETA* ni muhimu sana katika hili. Vikosi vyetu vya JKT vinaweza kuwa maeneo ya umahiri katika fani za kilimo, ujenzi, ufundi na biashara, iwapo vitatumwa vyema kiasi cha kuzalisha mapato makubwa na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana mpango wa ujenzi wa makazi ya maaskari wetu wa JWTZ na JKT. Licha ya kuwatia motisha askari wetu, lakini pia itaondoa nafasi ya siri za majeshi yetu kwenda kwa raia kwa urahisi iwapo wataendelea kuishi katika makazi ya raia. Ni muhimu mpango huu uanze haraka mara baada ya kukamilisha mikataba. Naomba sasa ukandarasi wa ujenzi wa nyumba hizo ufanywe na jeshi lenyewe kupitia SUMA ili lijiongezee mapato. Lakini pia kwa sababu huwa wanafanya kazi yao kwa umahiri, uadilifu na kwa wakati, naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie kuwa tenda ya ujenzi huu utafanywa na kikosi chake cha SUMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa hotuba yake aliyoiwasilisha mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Mwinyi kwa kuendelea kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kumteua kuongoza hii Wizara nyeti ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kuchangia hoja hii, mchango wangu utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio dhahiri kuwa Jeshi la Tanzania limejitahidi kwa kiasi kikubwa kulinda mipaka ya nchi yetu. Hii inadhihirisha wazi kwani tangu mwaka 1978 ambapo Iddi Amin Dada wa Uganda alipovamia nchi yetu, hakuna nchi yoyote ambayo imejaribu tena kuivamia mipaka ya nchi yetu. Hii ni sifa kubwa kwa jeshi letu. Ombi langu kwa wanajeshi wa Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwa waendelee kuwa na moyo wa uzalendo, upendo, umoja na mshikamano ili wahakikishe kuwa mipaka ya nchi yetu haichezewi wala kuvamiwa na nchi yoyote ile hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT katika nchi yetu yalisisitiza upendo, uzalendo, maadili, umoja, mshikamano pamoja na uzalishaji mali. Kwa ujumla, mafunzo haya yalijengeka katika misingi mikuu ya kumwandaa raia wa Tanzania kuwa na ari ya kuipenda nchi yake pamoja na umuhimu wa kuienzi siasa ya ujamaa na kujitegemea katika nchi yetu. Kwa ufupi, mafunzo ya JKT yalimfanya raia wa Tanzania kuwa mzalendo wa dhati wa nchi yake pamoja na kujitegemea yeeye mwenyewe kwani alijua umuhimu wa uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi, napenda kuishauri Serikali ihakikishe kuwa inarudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Mafunzo haya yakirudishwa, nchi itakuwa na uhakika kuwa inajenga vijana na raia wake katika misingi ya upendo, uzalendo, umoja na mshikamano. Hivyo mafunzo haya yatajenga Taifa lenye uelekeo wa

maadili na siyo kama ilivyo sasa ambapo kijana anahitim Kidato cha Nne, Kidato cha Sita, Vyuo au hata Vyuo Vikuu pasipo kupata mafunzo yoyote yale ya uzalendo, uzalishaji mali na hata namna ya kuipigania nchi kwa dhati, Kijana kama huyu akipata nafasi katika utumishi wa umma; ndiye huendeleza migomo na usaliti kwani hana maadili yoyote ya uongozi na uzalendo.

Pia kwa kurejesha mafunzo ya JKT katika nchi yetu, nina uhakika wa dhati kuwa shughuli ya uzalishaji mali hasa mazao ya chakula itaongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Vijana wetu watakaojiunga na JKT watasadid sana juu ya uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo kuokoa fedha nyingi zinatotumika kununulia chakula kwa ajili ya uhifadhi katika maghala ya Taifa. Pia ifahamike wazi kuwa kurejesha mafunzo ya JKT katika nchi yetu, kutasadid kujenga ukakamavu kwa vijana wa kitanzania. Hali ya ukakamavu itasadid kwa kiasi kikubwa kuimarisha afya za Watanzania. Magonjwa nyemelezi yanayotokana na uzembe hasa shinikizo la damu (*Pressure*), kisukari na kadhalika, naamin yatapungua kwa kiasi kikubwa ikiwa vijana wetu watajiunga katika mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT yafundishwe katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni. Ikiwezekana Serikali yetu ijitahidi ili kuhakikisha kuwa Vyuo vya Mafunzo hayo viwe porini mbali kabisa na makazi ya wananchi. Hii itasidia kupima imani ya vijana wetu. Pia nadharia mbalimbali zinazohusu mashujaa waliojitoa mhanga kuzipigania nchi zao hata kumwaga damu zifundishwe. Mafunzo haya yalenge zaidi kumfanya kijana aipende nchi yake na pia ajue stadi za maisha kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali yetu ihakikishe kuwa inahamisha Kambi zote za kijeshi zilizopo mijini na sehemu nyinginezo zenye makazi ya watu. Kambi hizo zipelekwe porini au mbali na makazi ya watu. Hali hii itasadia kuondoa wasiwasi uliojengeka mionganoni mwa Watanzania wanaokaa karibu na Kambi hizo. Wasiwasi wao mkubwa ni juu milipuko ya mabomu kama ilivyowahi kujitokesa katika Kambi zetu za Mbagala na Gongolamboto. Hili jambo litiliwe msisitizo na Waziri ahakikishe kuwa analifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo. Lengo lake la kuhamisha hizo Kambi ni zuri ili kuwafanya wananchi wetu waondokane na maisha ya wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo, ufugaji, useremala, ushonaji, upambaji na kadhalika ni kazi ambazo zinaweza kuiletea nchi yetu fedha au kupunguza matumizi ya fedha za uendeshaji wa shughuli hizo. Hivyo basi, naishauri Serikali yetu ihakikishe kuwa kila mwanajeshi licha ya kuwa na jukumu la kulinda mipaka ya nchi yetu, pia awe na shughuli maalum ya kuliingizia Taifa kipato. Shughuli hiyo maalum iwe ni uzalishaji mali, mathalan kazi ya kupanda, kumwagilia na kuitunza miti katika nchi yetu ifanywe na jeshi ili kuokoa fedha ambazo Serikali huzitumia katika kazi hii. Shughuli ya kilimo hususan mazao ya chakula itapunguzia Taifa mzigo wa kununua mazao ya chakula na kuwalisha wanajeshi wanaokaa kambini. Tuzame katika fikra zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili naomba liangaliwe kwa jicho la kiyakinifu. Tatizo hili linaleta mahusiano mabaya baina ya wananchi wanaozunguka Kambi hizo pamoja na wanajeshi wanaoishi katika Kambi hizo. Jambo la kusikitisha na kushangaza ni kuwa baadhi ya maeneo kama vile Nyandoto na Ronsoti katika Wilaya ya Tarime yamechukuliwa kwa nguvu na jeshi bila ridhaa ya wananchi. Izingatiwe kuwa maeneo hayo mawili bado Kambi za Jeshi hazijajengwa lakini wananchi walionyang'anya maeneo hayo kwa nguvu na jeshi wamekwama kuendesha shughuli za uzalishaji na hata kuwazuia kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, inataka busara na hekima nyingi kuhakikisha kuwa tunaomba migogoro isiyokuwa ya lazima katika jamii zetu kati ya wanajeshi na raia wanaoishi karibu na Kambi za Jeshi. Binafsi, nataka Waziri leo atoe kauli ya uhakika kuhusu mgogoro uliopo baina ya wakazi wa Nyandoto na Ronsoti Wilayani Tarime na jeshi ambalo lilichukua maeneo hayo kwa nguvu. Je, ni kwanini maeneo hayo yasirudishwe kwa wananchi? Je, ni haki jeshi kuvamia makazi ya watu na kujinyakulia ardhi kwa nguvu? Nahitaji majibu ya uhakika, leo hii mgogoro huu uishe. Kauli ya Serikali ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijitahidi sana kuboresha makazi ya wanajeshi. Naomba nyumba za wanajeshi ziboreshwani na kukarabatiwa. Pia Serikali ihakikishe kuwa inajenga nyumba za kutosha kwa ajili ya makazi ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya pensheni, posho, motisha kwa wanajeshi wastaifu, Jambo hili ni muhimu sana lizingatiwe na kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. Kwanza kabisa, wanajeshi wanapostaifu hasa wale wa vyeo vya chini huwachukua muda mrefu kupata pensheni (viinua mgongo vyao). Pili, kuna dhana kuwa wanajeshi wa *KAR* wa enzi za Mkoloni (Muingereza) hupewa motisha na pensheni kila mwezi. Je, madai ya dhana hii ni kweli? Naomba ufanuzi kuhusu dhana hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naweka msisitizo kuhusu suala la mgogoro wa ardhi Nyandoto na Ronsoti Vs Wanajeshi lipewe jibu la kisayansi lenye utoshelevu.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama - Generali Davis Mwamunyange pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye lengo la kuongoza tija katika kuendesha Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa jeshi letu linafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha nchi yetu inadumisha amani na usalama, hivyo kabla sijaanza kuchangia, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono bajeti hii na niwatakie utekelezaji wenye mafanikio kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Kambi ya Jeshi Wilayani Manyoni. Nina matumaini kuwa hali ya ulinzi katika misitu yetu ya hifadhi itaimarika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uamuzi huu wa kujenga Kambi hii ya jeshi ni wa muda mrefu na wananchi walishapata taarifa, namwomba Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi atueleze wananchi wa Singida hususan Wilaya ya Manyoni kuwa zimetengwa fedha kiasi gani kupitia bajeti hii ili ujenzi wa kambi hii ya Jeshi uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuwapeleka vijana wengi katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa muda wa mwaka mmoja, vijana wanatoka kila Wilaya na kila Mkoa kitendo kinachowaweka vijana kuwa wakakamavu na tayari kulitumikia Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwa utaratibu wa kuwafundisha vijana wetu kazi ya ulinzi kisha wanaajiriwa wachache na wengi wao wanarudi kijijini, ni kweli usiojificha kuwa tunataka kufuga majambazi. Kwani wengi wao hutarajia kupata ajira Serikalini, lakini inakuwa kinyume cha matarajio yao. Ni vyema sana Serikali iwe inawapeleka vijana wachache ambao wakihitimu wote wapate ajira Serikalini. Ninasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutaarifu Serikali kuwa yapo malalamiko kutoka kwa wanajeshi pale wanapopelekwa kufanya kazi nje ya vituo vyao vya kazi wakiwa na viongozi wao ambao wao hulipwa posho lakini wanajeshi wa chini huwa hawalipwi. Ninaombwa Serikali izingatie kuwa wanajeshi hawa wengi wao wanafamilia, hivyo huziacha familia katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitahadharisha Serikali kuwa utaratibu wa wanajeshi kukaa uraiani siyo mzuri, kwani ni rahisi sana kupata vishawishi na kufanya vitendo vya uhalifu au hata kutoa siri za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali kujenga nyumba nyingi za wanajeshi kuendelea na nidhamu ya jeshi pamoja na kutunza siri za nchi yetu. Pia itawapunguzia gharama za kupanga uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa utaratibu wake mzuri wa kuwapandisha wanajeshi wetu vyeo pale inapobidi. Kwa kuwa wanajeshi wote hupenda kupandishwa vyeo, basi ni vyema utaratibu huu uwe na uwiano mzuri kwa kuangalia elimu, utumishi uliotukuka kwa kuangalia jinsia, pia mfano tumeuona leo Watendaji Wakuu waliotambulishwa na Naibu Spika ni wanaume karibu wote. Ni muhimu sana wanawake nao wakawepo katika ngazi za juu za uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi wa Kidato cha Sita kwenda JKT miezi sita kwa mujibu wa sheria, naipongesa sana Serikali kwa uamuzi wake. Ni ukweli usiojificha kuwa uamuzi huu ni wa busara sana kwani utawajenga vijana wetu kinidhamu, kiulinzi pamoja na maadili mema kwa jamii na ndani ya majukumu yao pale

wanapopata ajira au kujajiri. Naomba uamuzi huu uanze mara moja ikiwezekana kuanzia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile zipo taarifa kutoka kwa wanajeshi kuwa hata wao wapo ambao wanaidai Serikali posho mbalimbali ambazo huchukua muda mrefu kulipwa. Naomba kwamba, kwa kuwa ni haki ya kila mwanajeshi kulipwa stahili zake mfano posho za uhamisho, posho za safari na kadhalika, ni vyema wawe wanalipwa kwa wakati ili kuwaongeza ari ya kazi endapo Serikali haina fedha, basi ni vyema uhamisho usitolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa angalizo kwa Serikali kuwa kuna wakati sare za jeshi huonekana zinavaliwa na raia wa kawaida na ukiuliza unajibiwa zinapatikana kwenye mitumba. Naomba suala hili lidhibitiwe. Vile vile inasemekana hata silaha hutumiwa pia kwenye maeneo ya uhalifu uraiani. Naomba Serikali iweke ulinzi mkali wa silaha na risasi ili zisitumie katika uhalifu kwani ni kudhalilisha Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kurudia tena kuwa naunga mkono hoja nikiwa na matumaini makubwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakati akitoa ufanuzi wa hoja za Wabunge atanijibu. Mungu ibariki Tanzania, Mungu libariki Jeshi letu la Tanzania, Amen.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni pongezi kwa Wizara na wapiganaji wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mchango wangu ni katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu wanaomaliza vyuo ni lazima wapitie JKT ili pamoja na mambo mengine tudumishe uzalendo na umoja wa Taifa. Hili litekelezwe haraka. Jambo hili limechukua muda mrefu sana, ni vyema tumalize sasa wakati wa amani kwa sababu linaathiri pia uwekezaji katika mwambao wa ziwa upande wa Tanzania hasa kwa Wilaya ya Mbanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza sana vituo vyetu vya Mzinga na Nyumbu kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuendeleza teknolojia. Ni hamu yangu kuona Nyumbu wanatengeneza gari itakayotumiwa na Rais ajaye 2015 katika sherehe za kuapishwa kwake 2015. Lazima tuthubutu! Vituo hivi vinaweza kutoa mchango mkubwa kwa kuendeleza teknolojia vijijini ili kupukuchua mahindi, alizeti na umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza pia hospitali ya Lugalo kwa huduma nzuri. Namtakia Mheshimiwa Waziri, Mkuu wa Majeshi na wapiganaji wote wawe na mafaniko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELAH JASMINE KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kurudisha matakwa ya vijana

kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, ni imani yangu kwamba, vijana hawa wataongeza tija kwani watasaidia katika uzalishaji wa chakula na kukuza uchumi. Ningeshauri Serikali iende mbali zaidi, kwa kuwafundisha stadi mbalimbali za ufundi ili pindi wanaporejea uraiani wawe na utaalamu fulani. Itakuwa ni vyema pia kwa kuwa vijana hawa walizalisha na kulipatia Taifa kipato, basi itafaa wapewe vitendea kazi bure vya kufanya kazi zao mbalimbali. Nasema bure/kubadilishana (*exchange*) kwani walishatoa nguvu kazi yao kwa kufanya hizi. Hiyo itasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, na wakati huo huo kuchangia katika uchumi na hivyo kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kwa niaba ya wanawake wa Dar es Salaam ambao wamekuwa wakilalamikia mchakato mzima wa kuajiri katika JKT. Uajiri umekuwa ukichukua muda mrefu na wanaokosa wamekuwa hawapatiwi taarifa ili kufahamu hatima ya maombi ya ajira au usaili walioufanya JKT. Hivyo ninapendekeza wawe wanaarifiwa ili kuwa na uwazi na kuweka rekodi sawa.

Katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2011/2012, imeelezwa kwamba SUMA JKT iliagiza matrekta 1,860 na kwamba matrekta 74 tu ndiyo ambayo yameuzwa kwa wateja mbalimbali. Kwa kweli, hili ni tatizo. Hivi inashindikanaje kuuza matrekta haya? Vile vile, tunafahamu zipo Kambi mbalimbali ambazo wanaweza kununua ili kuyatumia kulimia na baadaye kuzalisha chakula. Sambamba na hili, ni kwa nini pia Magereza mbalimbali wasipatiwe au kuuziwa matrekta hayo ili wazalishe kwa ajili ya chakula kwa wafungwa, na kuuza cha ziada?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wabunge pia wamepatiwa fomu za maombi ya kukopeshwa matrekta haya, hata hivyo, riba ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. WILLIAM AUGUSTAD MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukupongeza wewe binafsi na Wizara yako kwa kazi nzuri ya ulinzi wa nchi yetu. Naomba nichangie au nishauri katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi yanayotolewa na wanajeshi wa vyeo vya chini kwamba wanapokwenda likizo hunyimwa fedha zao za likizo. Kama hili ni kweli, nashauri litafutiwe ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma Karakana ya Nyumbu ilisifika sana katika fani ya ufundi na utaalalm wa magari pamoja na mitambo mingine ambapo jamii ilinufaika sana na matokeo ya kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba: Je, nini sasa kifanyike pale kwa manufaa ya jeshi na wananchi kiujumla? Aidha, kama ni kweli kwamba sasa lengo ni kujenga uwezo wa shirika ili liwe kituo kinachoongoza cha

utafiti wa teknolojia za kijeshi katika kanda ya Afrika ya Mashariki: Kwa nini hili halijitafsiri katika bajeti iliyopo?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na pia napenda nimpongeze Waziri wa Ulinzi pamoja na Mkuu wa Majeshi kwa kulinda mipaka yetu vizuri. Nchi yetu ina amani na bado iendelee kuwa na amani ya kudumu.

Mheshimiwa Waziri, napenda nikutaarifu kuwa askari wetu wa jeshi wanapenda sana kuchukua sheria mikonono mwao. Nasema haya kwa ushahidi. Mimi natoka katika Jimbo la Wawi ambalo lina Kambi kubwa ya Jeshi. Wakati fulani Itokea kuna timu za mpira walicheza, ikatokea wachezaji kupigana, basi wanajeshi waliingilia kati, waliwapiga mpaka wengine walipoteza fahamu. Kwa kweli hali hii haipendezi na inaleta chuku kati ya wanajeshi na raia. Naomba jambo hili likomeshwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nielezee matatizo wanayoyapata wanajeshi wastaafu. Wanapata taabu sana hasa pale wanapocheleweshewa haki zao za kustaafu. Naomba uandaliwe utaratibu ili huu ucheleweshaji usitokee tena. Wastaafu hawa wanalipwa pensheni yao kila baada ya miezi sita. Hili ni tatizo kubwa, angalau wangeliipwa kila baada ya miezi mitatu. Maisha yao ni magumu, pensheni yao ni pesa ndogo sana haikidhi maisha yao. Naomba Serikali iangalie upya malipo haya kwani wastaafu hawa wanadhalilika sana, na huku tukizingatia kuwa hawa kwa mujibu wa kiapo chao ni askari wa akiba.

**MHE. JOYCE JOHN MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi linapaswa kutumika kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa kutumia taaluma mbalimbali walizonazo wapiganaji wetu katika kipindi hiki ambacho nchi iko katika amani na salama badala ya wapiganaji hao kuachwa kukaa kambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya wapiganaji ambao hutumia taaluma zao kuhudumia jamii kama vile Madaktari wanaofanya katika Hospitali za Jeshi mfano Lugalo na Makongo Dar es Salaam na wamekuwa wakifanya vizuri sana. Lakini bado haitoshi kwani idadi kubwa ya wanajeshi ambao wana taaluma wanakaa tu makambini. Ni kweli kuna baadhi ya wapiganaji ambao hutumia taaluma zao kuhudumia jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kazi zote za kitaalamu zinazofanywa na jeshi kuwa na ubora na kutekelezwa kwa kipindi kifupi kwa gherama nafuu kulinganisha na zinazofanywa na kampuni nyingine kuwa na ubora na kutekelezwa kwa kipindi kifupi na kwa gherama nafuu kulingana na zinazofanywa na makampuni au watu binafsi, na mifano mingi tu ipo kama walivyosaidia katika suala la ujenzi wa miundombinu ya reli na madaraja yaliyoharibiwa na mafuriko mkoani Morogoro (Kilosa), daraja la Chalinze, bomba la maji Ruvu na ujenzi wao huwa unadumu kwa kipindi kirefu. Lakini bado wapiganaji hao hawapewi upendeleo maalum katika tenda za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike wakati sasa Serikali itoe kazi zote zinazohusiana na ujenzi wa nyumba zake na taasisi zote za umma kwa JKT kwa kuwa tayari tunayo

mifano hai inayodhihirisha wana uwezo kama walivyofanya katika ujenzi wa mabweni katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Tengeru ambapo licha ya kukamilisha kazi ndani ya kipindi kifupi na kwa gharama nafuu, lakini pia walitoa msaada wa kuchimba kisima cha maji kwa jamii ya chuo hicho bila kudai gharama za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la ujirani na mahusiano mema kati ya Jeshi na wananchi. Umefika wakati sasa kitengo cha uhusiano jeshini kiende mbele zaidi katika kutekeleza majukumu yake kwa kuunganisha wananchi na jeshi lao ili kuondoa matukio ya makabiliano ya raia na askari yanayosababishwa na sababu ndogo ndogo zinazoweza kutatuliwa kwa majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi liwe hakika lipo kwa ajili ya wananchi kama linavyoitwa na isitokee matukio ya askari kudaiwa kuvamia mitaani na kuadhibu wananchi eti kulipiza kisasi cha mwenzao/wenzao kukosewa na raia matokeo yake wanaumiza raia na kusababisha vifo wakati mwingine. Naomba tujenge jamii inayomaliza tofauti zake kwa majadiliano badala ya makabiliano. Askari akikosewa na raia atumie njia sahihi kisheria kudai haki yake badala ya kujichukulia sheria mkononi ya kutembeza mkong'oto kwa raia. Tukio hili limeshatokea Mkoani Arusha Wilaya ya Arusha mjini Kata ya Moshono (Kijenge) mwanzoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi litumike kuzalisha chakula katika Taifa, vijana wa JKT watumike kuzalisha chakula cha kutosha kulisha Taifa kama ilivyowahi kufanyika zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utalihakikishia Taifa letu chakula cha ziada na itaondoa tatizo la njaa kama tunavyoshuhudia nchini sasa. JKT wana uwezo wa kuzalisha kwa sababu wana nguvu kazi na utaalam katika sekta nyingi ikiwemo useremala, kilio na kadhalika na ndio maana hata mabanda yao yamekuwa yakiongoza kwa ubora katika maonyesho mbalimbali ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanaojiunga na jeshi kwa kujitolea ambao hawajafanikiwa kupata ajira ya kudumu ndani ya JKT kwenyewe, naamini wakipewa mafunzo ya kutoka katika Sekta ya Kilimo wanaweza kutumika kutekeleza mpango wa Serikali wa Kilimo Kwanza pale wanaporejea katika jamii. Hii itafanya Sera ya Kilimo Kwanza ifanyike kimatendo zaidi na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mkuu wa JKT, na wapiganaji wote kwa kazi kubwa ya kuilinda nchi yetu na kuhakikisha kuwa nchi iko salama. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuliwezesha jeshi kuunda majukumu yake kwa kulipatia Jeshi Sh. 598,099,152,733.30 sawa na asilimia 95.40 tofauti na Wizara nyingine ambazo zilipatiwa fedha kidogo kwa ajili ya mpango wake wa

mwaka 2010/2011. Vile vile kutoa Sh. 501,218,327,120.00 sawa na asilimia 107.39 ya fedha iliyoidhinishwa. Huu ni ushahidi kuwa Serikali inataka jeshi lake lifanye kazi kwa ufanisi. Hata hivyo, matumizi ya maendeleo yalifikia asilimia 60.47, hivyo naiomba Serikali mwaka huu wa fedha, fedha za maendeleo zitolewe kwa kiasi kikubwa ili kukamilisha miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kurudisha mafunzo ya JKT kwa wanafunzi wanaomaliza *Form VI* kwa muda wa miezi sita. Sikusikia kuhusu wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu kwani nao ni muhimu waende JKT baada ya kumaliza Vyuo Vikuu. Nasisitiza suala hili lipewe umuhimu na liharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza pia kuboresha nyumba na makazi ya wanajeshi ili wafanye kazi kwa utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa ya kulinda nchi yetu na mipaka yake, jeshi lina nafasi nzuri ya kushiriki katika michezo. Nazipongeza timu zote za jeshi kwa mafanikio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa majeshi yetu yagawane michezo ili ijkite zaidi na michezo husika na hivyo kufanya vizuri zaidi kwa mfano, Jeshi la Ulinzi – mchezo wa ngumi, Jeshi la JKT – mchezo wa netiboli, Jeshi la Polisi – Mpira wa miguu, Jeshi la Magereza – mpira wa mikono, Uhamiaji – *basket ball*. Utaratibu huu utasaidia kuboresha viwango vya michezo husika kuliko kujihusisha na michezo yote.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Wizara na Jeshi kwa kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, na sifa nzuri ambazo jeshi letu linazo, lakini sifa hizo zinapunguzwa na baadhi ya askari wasio na maadili. Baadhi ya askari hao hujihusisha na kupiga raia kwa visingizio mbalimbali, mfano vitendo vya ujambazi na kdhalika. Nashauri ili kulinda heshima kubwa kwa jeshi letu, basi wale wote watakaobainika na vitendo vya utovu wa nidhamu na kwenda kinyume na maadili ya kijeshi na maadili ya kitanzania, basi hao wafukuzwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, milipuko ya mabomu iliyotokea Gongolamboto na kupoteza maisha ya watu na kusababisha hasara kubwa kwa mali za watu, ni moja ya matukio mabaya yanayolipaka matope jeshi letu. Ni kweli ajali haina kinga. Hata hivyo, bado uangalifu zaidi unatakiwa ili kulinda maisha (uhai) na mali za raia. Aidha, katika milipuko hiyo, Serikali (Jeshi) ilipata hasara kubwa kwani vifaa vingi vya kijeshi ambavyo viligharimu pesa nyingi (kodi za wananchi) viliharibika vibaya.

Nashauri Wizara na Jeshi vihakikishe kwamba zinachukuliwa hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba matukio mabaya kama hilo hayatokei tena. Nataka pia kujua: Je, fidia kwa waathirika wote imefanyika? Gharama zote ni kiasi gani? Ili kuondoa malalamiko kuhusu hilo ni vizuri zoezi la fidia lifanyike kwa haraka na uwazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha tena mpango wa mafunzo ya JKT. Hata hivyo, nashauri yafuatayo: vijana wote wanaopitia JKT na kuhitimu mafunzo yao wapatiwe ajira au shughuli zitakazowafanya wawe na kazi za kufanya. Nafurahi hilo linafanyika kwa sehemu kubwa. Itakuwa hatari kama vijana hao watapata mafunzo halafu wakaachwa hivyo hivyo. Nashauri pia vijana wanaomaliza Kidato cha Sita waanze mapema inavyowezekana kupitia mafunzo ya JKT. Ni dhahiri kabisa kwamba vijana wengi ambao leo wanamaliza Kidato cha Sita au cha Nne na kwenda vyuoni moja kwa moja na kupata ajira wanakosa uzalendo, utanzania halisi, wanakosa pia ukakamavu, jambo ambalo linawafanya baadhi yao wakiwepo baadhi ya Wabunge kukosa maadili mazuri ambayo naamini wangepitia mafunzo hayo wangeyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana SUMA JKT kwa kazi nzuri sana wanazoendelea kufanya hususan katika Sekta za Ujenzi na Kilimo. Naomba nishauri kwamba katika miradi ya ujenzi, jeshi lijitahidi kuwa na vifaa vya kutosha pamoja na wataalam zaidi, Wahandisi na *Technicians* ili kuboresha kazi za ujenzi.

Kuhusu Kilimo Kwanza, nashauri bei za matrekta zipunguzwe kama alivyoshauri Waziri Mkuu alipotembelea maonyesha ya Saba Saba – Dar es Salaam. Ni dhahiri kwamba bei ya sasa za karibu shilingi milioni 46 ni kubwa sana. Bei hizo zitafanya Watanzania wengi (wakulima) washindwe kununua matrekta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ili liwe na sura ya kitanzania nashauri ajira zinazofanyika ndani ya Jeshi la Wananchi na JKT ziwe na sura ya Utanzania. Ajira zizingatie vijana kutoka maeneo yote ya nchi yetu. Nashauri pia hatua za awali za kuwapata vijana hawa kuanzia Wilayani zisiwe na upendeleo. Aidha, vijana wanaomba ajira hizi wasihamishwe kutoka Wilaya moja hadi nyingine kwa misingi ya kupatiwa nafasi, kwa kufanya hivyo vijana wengine kwenye Wilaya hizo watakosa nafasi. Vitendo vya rushwa pia viepukwe katika suala zima la ajira, vinginevyo vijana kutoka familia masikini watakosa ajira hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ambayo ina amani na usalama wa kutosha. Hii inatokana na kuwa na utawala bora na uongozi bora. Nchi yoyote duniani inakuwa na sifa kubwa kama ina usalama wa kutosha. Napenda kutoa shukrani kubwa kwa Mkuu wa Majeshi wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi wa Tanzania kwa umakini na ubora katika kuimarisha jeshi letu la Tanzania. Kila kitu kizuri hakikosi kuwa na changamoto. Hili ni suala la kawaida kwa kila jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambazo zinakabili Jeshi letu ni kushuka kwa kiwango cha ujuzi wa kijeshi kwa mfano kutumia silaha kubwa za kivita kama zile zinazotumika na mataifa makubwa kama vile silaha zinazotumiwa na Marekani,

Ufaransa, Urusi na nchi nyingine zilizoendelea; Jeshi kukosa vijana wasomi wanaojitolea kujunga na Jeshi la kujenga Taifa na ukosefu wa majengo kwa wanajeshi, wanajeshi wengine wamepanga nyumba mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ichukue jukumu la kusomesha vijana wengi katika masuala ya kijeshi ikizingatia teknolojia inakua kila siku. Pia ijenge majengo kwa ajili ya vijana wetu wanajeshi ili wakae katika nyumba za jeshi siyo kupanga mitaani. Nashauri pia vijana wanajeshi waongezewe motisha kifedha ili vijana wengi waweze kuipenda kazi ya jeshi na kuwa na shule maalum ya kijeshi ambayo itachukua kuanzia vijana wadogo, yaani Shule ya Msingi mpaka Chuo ngazi ya Diploma katika mafunzo ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kupongeza tena kwa kazi nzuri inayofanywa na Amiri Jeshi Mkuu, Rais - Dkt. Jakaya Kikwete kwa kuimarisha na kuhakikisha uhuru na usalama wa nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hatua hiyo, sasa Waheshimiwa Wabunge naomba mniruhusu nimwite Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa apitie michango ya Waheshimiwa Wabunge na kujibu hoja zetu ili tuendelee na taratibu nyingine.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa katika muda huu ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana mke wangu Mariam na watoto wangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika kipindi chote ambacho niko katika majukumu ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji ni wengi mno na kwa maana hiyo sitoweza kuwajibu wote hapa ndani kwa muda niliokuwa nao. Nitajitahidi kadri nitakavyoweza kupitia hoja zote zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliochangia kwa maandishi ni 110 wakati waliochangia kwa kuzungumza ni tisa (9). Naomba niwatambue, nianze na wale waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo. Mheshimiwa Amina Andrew Clement; Mheshimiwa Salim Turkey; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim; Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto; Mheshimiwa Yahya Kassim Issa; Mheshimiwa Lucy Mayenga; Mheshimiwa Sabreen Sungura na Mheshimiwa Mariam Msabaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao. Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar; Mheshimiwa Jerome Bwanausi; Mheshimiwa Stephen Masele; Mheshimiwa Salim Hemed Khamis;

Mheshimiwa Susan Lyimo; Mheshimiwa Juma Nkamia; Mheshimiwa Benardetha Mushashu; Mheshimiwa Felister Bura; Mheshimiwa Antony Mbassa; Mheshimiwa Said Mussa Zubeir; Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela; Mheshimiwa Mohamed Mnyaa; Mheshimiwa Ali Khamis Seif; Mheshimiwa Job Ndugai; Mheshimiwa Clara Mwatuka; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso; Mheshimiwa Richard Ndassa; Mheshimiwa Kaika Telele; Mheshimiwa Rose Kamili; Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu; Mheshimiwa Hamad Ali Hamad; Mheshimiwa Alphaxard Lugola; Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa; Mheshimiwa Eustace Katagira; Mheshimiwa Luhaga Mpina; Mheshimiwa Ignas Malocha; Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani; Mheshimiwa Nyambari Nyangwine; Mheshimiwa Diana Chilolo; Mheshimiwa Angella Kairuki; Mheshimiwa Gaudence Kayombo; Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Joyce John Mukya; Mheshimiwa Josephat Kandege; Mheshimiwa Juma Njwayo; Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli; Mheshimiwa Rosweeter Kasikila; Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee; Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo; Mheshimiwa Subira Khamis Mgali; Mheshimiwa Brig. Gen. Hassani Ngwilizi; Mheshimiwa Salum Barwany; Mheshimiwa Albert Ntabaliba; Mheshimiwa John Lwanji; Mheshimiwa Jasson Rweikiza; Mheshimiwa Amina Mwidau; Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu; Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge; Mheshimiwa Mohamed Missanga; Mheshimiwa Godfrey Zambi; Mheshimiwa Mendrad Kigola; Mheshimiwa Augustino Mrema; Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba; Mheshimiwa Ester Bulaya; Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh; Mheshimiwa Halima Mdee; Mheshimiwa Omar Rashid Nundu na Mheshimiwa Riziki Omar Juma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis; Mheshimiwa Ali Juma Haji; Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya; Mheshimiwa Regia Mtema; Mheshimiwa Salome Mwambu; Mheshimiwa Leticia Nyerere; Mheshimiwa Felix Mkosamali; Mheshimiwa Sabreena Sungura; Mheshimiwa Martha Mlata; Mheshimiwa Mariam Kisangi; Mheshimiwa Martha Umbulla; Mheshimiwa Namelock Sokoine; Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda; Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto; Mheshimiwa Christowaja Mtinda; Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye; Mheshimiwa Naomi Kaihula; Mheshimiwa Selemani Jafo; Mheshimiwa Charles Mwijage; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar; Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba; Mheshimiwa Kassim Majaliwa; Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma; Mheshimiwa Agness Hokororo na Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa; Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir; Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa; Mheshimiwa Magdalena Sakaya; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo; Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy; Mheshimiwa Moza Abeid Said; Mheshimiwa Joyce John Mukya; Mheshimiwa Mathias Chikawe; Mheshimiwa Vicent Nyerere; Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko; Mheshimiwa Meshack Opulukwa; Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid;

Mheshimiwa Juma Sururu Juma; Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali; Mheshimiwa David Silinde; Mheshimiwa Desderius Mipata; Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Abdallah Juma Sadalla na Mheshimiwa Frederick Mwita Werema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niwatambue kipekee wachangiaji kupitia Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Waziri Kivuli wa Ulinzi, Mheshimiwa Selasini. Naomba nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri na nataka tukubaliane kwamba karibu Wabunge wote waliochangia wanaienzi kazi nzuri inayofanywa na Majeshi yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru na niipongeze Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maelezo mazuri waliyotoa hapa mbele na kwa kutupa moyo wa kuifanya kazi yetu vizuri zaidi. Naomba nianze kujibu hoja za Kamati hiyo, kwanza kulikuwa kuna hoja ya kulipa madeni ya Wanajeshi na madeni ya wazabuni na kadhalika. Katika hili, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imesikia kilio cha Askari, Wabunge waliokuwa wakitetea na Wizara yetu kwa kutoa fedha za kulipa madeni yote yaliyohakikiwa chini ya Wizara ya Ulinzi. Tumepewa na Hazina shilingi bilioni 58.9 kulipia madeni yote yaliyokuwa ya Askari kwa binafsi yao, wazabuni pamoja na madeni ya maji, umeme, simu na kadhalika. Kwa hiyo tatizo hili sugu la muda mrefu kwa sasa limemalizwa kabisa. Napenda niwashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili, ambalo limechangiwa na Wabunge wengi nalo ni uanzishwaji au urejeshwaji wa JKT kwa mujibu wa sheria. Niseme tu kwamba Serikali imejipanga vyema na katika hotuba yangu mtaona kwamba sasa JKT inao uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja. Hiyo ni hatua nzuri, ni hatua ambayo itatuwezesha kuchukua vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita endapo tutafanya waingie katika mafunzo haya kwa awamu mbili. Kwa taarifa au takwimu tulizokuwa nazo ni kwamba wahitimu wa Kidato cha Sita nchini mwetu kwa sasa ni 36,000. Kwa hivyo kama wataingia JKT kwa awamu mbili ya miezi sita, sita tutaweza kuwaingiza wote na tunakusudia kuanza utaratibu huo katika mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu limevuta hisia za watu wengi humu ndani na sisi kama Serikali tunatambua fika umuhimu wa kurudisha tena mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria. Jambo hilo litafanyika, naomba niwaondoe hofu, maandalizi yanaelekea kuwa mazuri, kilichobaki ni kuhakikisha tu kwamba mitaala ya Vyuo Vikuu, maana wanapoanza hawa kwa miezi sita (6) isije ikaonekana kwamba wale wanaoingia miezi sita (6) ya pili wakakosa kuanza mafunzo ya Vyuo Vikuu kwa wakati. Kwa hiyo, tutashauriana na wenzetu wa Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba hili sio tatizo ili mwakani tuenze mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu iliyotolewa na Kamati ilikuwa ni kupitia upya Sheria ya Ulinzi wa Taifa yaani *National Defence Act* ya mwaka 1966. Tunakiri kwamba sheria hii ya mwaka 1966 mambo mengi yamepitwa na wakati, ni lazima tufanye mabadiliko hayo sasa ili kuweza kuendana na wakati tuliokuwa nao. Taarifa

niliyokuwa nayo ni kwamba taratibu za kuhuisha sheria hii zimekamilika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishapelekewa mabadiliko hayo na taarifa alizotupa ni kwamba Sheria hii sasa itafikishwa kwenye Bunge lako Tukufu mwezi Novemba kwa ajili ya kuihuisha Sheria ya Ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya *National Defence College* kuanza kwake na kutumika kwa Wanajeshi pamoja na wananchi kwa ujumla. Chuo cha Ulinzi cha Taifa kimeshakamilika na kwa sasa unafanywa utaratibu wa mafunzo ya Wakufunzi. Hatua hii ikikamilika na mafunzo kuanza rasmi, Viongozi, Watendaji, Watendaji Waandamizi Serikalini na Wanasiasa watajumuishwa kupata mafunzo hapo. Kinachofanyika kwa sasa ni kuaandaa mitaala na vilevile wanatafutwa Wahadhiri. Wahadhiri watatokana na Wanajeshi wenyewe, watatokana na Wakufunzi kutoka Vyuo Vikuu, watatokana vilevile na watu wenye taaluma mbalimbali wakiwemo Wachumi, Mabalozi, Wataalamu wa Mazingira na kadhalika. Lengo ni kuhakikisha kwamba mitaala inaanndaliwa vyema ili kinapoanza basi kiweze kukidhi mahitaji tuliyokuwa nayo. Naomba niwashukuru kwa kipekee Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kusaidia katika maandalizi ya mitaala ya chuo hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyine ilikuwa ni JKT kujikita na kuwa mfano katika Sera ya Kilimo Kwanza. Tunakubaliana na Kamati na sisi tunaona umuhimu upo wa kuhakikisha kwamba JKT kuwa mfano katika jambo hili na kinachokwaza sasa hivi ni bajeti finyu ya JKT. Kwa hivyo, tutaendelea kuomba fedha ziongezwe mwaka hadi mwaka ili JKT waweze kuboresha zana za kutekeleza Sera ya Kilimo Kwanza kwa kuzalisha mbegu bora kwa kuanzisha ufugaji wa kisasa na kadhalika. Haya yote yatawezekana endapo bajeti itakuwa inakidhi kuanza shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kutokana na hotuba ya Kamati lilikuwa ni SUMA kujitangaza. Kwanza tunapokea pongezi zilizotolewa na Kamati kwa SUMA na wameitaka SUMA wajitangaze zaidi na sisi tunasema hilo tunalipokea na tutahakikisha kwamba SUMA wanajitangaza ili waweze kuuza zaidi bidhaa ambazo wanazitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie katika hoja zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwanza alitaka tuhakikishe kwamba Askari wote wanakaa Kambini. Hiyo ndiyo azma ya Serikali. Wanajeshi kukaa kambini kunasaidia mambo mengi sana. Kwanza wanakuwa tayari wanapohitajika wakati wowote, lakini pili tunadhibiti nidhamu zao wakiwa kwenye makambi. Serikali imekuwa ikifanya ukarabati wa baadhi ya makambi kutokana na fedha tunazotengewa mwaka hadi mwaka. Jambo hili limeonekana na uzito kwa sababu fedha zenyewe hazikidhi mahitaji lakini hata hivyo taarifa njema niliyokuwa nayo ni kwamba maombi ya Serikali ya Tanzania kwa *Exim Bank* ya China kujengewa nyumba 10,000 yamepata kibali cha *Exim Bank* China, kwa hivyo tuna mategemeo makubwa sasa kwamba mkataba huo utakaposainiwa tutawenza kupata nyumba 10,000 katika makambi na hakutokuwa na sababu kwa nini Wanajeshi wote wasirudi makambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, lilikuwa ni kuhusu Kamandi ya Navy kupewa uwezo wa kufanya doria katika eneo la Bahari Kuu. Hii ni azma yetu, tunatambua fika

kwamba maeneo ya *Exclusive Economic Zone* watu wanavua, wanamwaga takataka za sumu, wanafanya kila aina ya matatizo huko na laiti kama uwezo wetu ungekuwa unatosha tungefanya doria za mara kwa mara. Kwa sasa uwezo wetu bado ni mdogo, lakini Serikali inajizatiti katika kuhakikisha kwamba tunapata melivita ambazo zitawenza kufika katika maeneo hayo ili pamoja na kudhibiti uharamia tuweze kulinda raslimali zetu katika *EEZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuitwa kwa Sera na Sheria zinazoongoza Jeshi letu, kama nilivyosema awali jambo hili limefanyiwa kazi na litaletwa Bungeni kwa ajili ya kuhuisha Sheria ya Ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi mabaya ya vifaa vya Kijeshi kwa ajili ya kisiasa na matumizi binafsi. Katika hili, nataka niseme kwamba hoja iliyotolewa kwamba Wanajeshi au Jeshi linatumia zana na vyombo vya usafiri bila ya kuwa na matumizi maalum, si sahihi. Naomba hili niliweke sawasawa. Kwanza itambulike kwamba vyombo mnavyoviona kwa mfano ndege au helikopta na kadhalika ni lazima viwe vinafanya mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani uwe na vifaru vimepaki mpaka wakati wa vita lazima vifanye mazoezi, mizinga lazima ifanye mazoezi na ndege halikadhalika. Kwa hiyo, inapokuwa ndege hizi mnaziona zinaruka kutoka sehemu moja kwenda nyingine wala si matumizi mabaya, ni utaratibu mzuri uliowekwa na Jeshi katika kuhakikisha kwamba marubani wale wanapata usoefu na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati ilipotokea kwamba kuna maombi maalum kutoka Jeshi la Polisi, kwamba, waweze kutumia ndege ya Jeshi kumpeleka Mheshimiwa Mbobe kule Arusha hatukuona tatizo kwa sababu kwanza vyombo hivi vya ulinzi na usalama ni vyombo ambavyo vinashirikiana. Leo ikitokea majanga ya aina yoyote sisi tunahitaji Helikopta ya Polisi, tutaomba tuchukue twende na wao wanapokuwa na jambo, wanapohitaji ndege ya Jeshi, watatuomba na tutawapa wafanyie hiyo kazi. Kwa hiyo, nadhani Kambi ya Upinzani ingetupongeza kwamba tumehakikisha Kiongozi wao amesafirishwa kwa njia nzuri badala ya kutulaumu kwa jambo hilo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maduka ya *duty free* Jeshini. Tunatambua kwamba wanajeshi wengi wanalamika kwamba bado maduka mengi kati ya haya hayakidhi haja kwa sababu bei zinazotolewa sio pungufu kama inavyotakiwa na aina ya bidhaa sizo zinazotakiwa. Yapo machache yanayotoa huduma nzuri na sasa hivi tumeunda Kamati ya kuitia upya utaratibu wa *duty free shops* zote ili hatimaye tutengeneze utaratibu bora zaidi utakaotoa unafuu kwa wanajeshi kama ilivyokusudiwa. Jambo hilo limeshafikia hatua nzuri, nasubiri kupokea taarifa ya Kamati hiyo ili tufanye maamuzi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja hii ya kutumia wafanyabiashara matapeli kama ilivyoandikwa katika Gazeti la Dira kuhusu SUMA JKT kuingia mkataba na mfanyabiashara aliyetajwa. Naomba niweke rekodi sawasawa. Si sahihi kwamba SUMA JKT wameingia mkataba na mfanyabiashara yejote. Mkopo wa matrekta ulianzishwa

kutokana na Serikali ya India kukubali kuikopesha Tanzania kwa masharti nafuu na Serikali ya Tanzania imekuwa ikichukua mikopo hiyo na wa matrekta ulikuwa wa kwanza na baada ya hapo tumeingia mkataba mwingine wa kununua magari ya Jeshi na tutaendelea kuchukua hivi karibuni, Mheshimiwa Mwandsoya amepata mkopo kwa ajili ya maji, Dar es Salaam. Tutaendelea kuchukua mikopo hii. Waliongibia mkataba huu ni Serikali, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ndiyo iliyosaini na *Exim Bank* ya India kuhusu mkopo wa matrekta. *Exim Bank* ya India baadaye Serikali na ni Wizara ya Fedha ikasaini mkataba na SUMA JKT kama ndiyo watekelezaji na hatimaye SUMA JKT ikaingia mkataba na kampuni inayoitwa *Escorts of India* ambao ndiyo wazalishaji wa matrekta haya. Kwa hiyo, hakuna ukweli hata kidogo kwamba SUMA JKT imeingia mkataba na mfanyabiashara, aliyemtaja Mheshimiwa Selasini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kuhusu viwanda ambavyo viko chini ya SUMA JKT. Kuna *TANZASINO*, kuna KAMISUMA na kadhalika. Ni kweli na nikiri kwamba sio mashirika yote au viwanda vyote hivi vinafanya vizuri. Vingi kati ya viwanda hivi bado havijafanya vizuri kama tunavyotaka. Kwa mfano, hiki kiwanda cha *TANZASINO* kinachozalisha dawa, si kwamba hakijawahi kuzalisha wala si kwamba hakijawahi kuuza dawa zake. Walikuwa wanazalisha dawa za *paracetamol ib-profen, metronidazol, diclophenac* na walikuwa wanauzu mpaka *MSD* kuingia katika Zahanati za Serikali. Walikuwa wanauzu kwa watu binafsi, Majeshi pamoja na Magereza. Kwa hiyo, hii kazi ilifanyika lakini kutokana na mtaji mdogo waliokuwa nao wawekezaji, wabia wetu, kiwanda hiki kwa sasa kimefungwa na kwa hiyo, tunaangalia kupata wabia wenye uwezo zaidi ili kuweza kuzalisha dawa kupitia SUMA JKT. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ya suala la viwanda vingine kama KAMISUMA *garments* na chenyewe vile vile kimefungwa, mbia wetu hakuwa mzuri kwa sababu kwanza viwanda hivi ni vya ubia, halafu viwanda hivi sehemu kubwa vinaongozwa na wabia wenzetu kwa sababu wao ni *majority shareholders*. Tumeona kuna udhaifu katika wabia hao, kwa hiyo, tumeamua sasa kutafuta wabia ambao ni bora zaidi ambao tutahakikisha wanazalisha bidhaa kwa manufaa ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maelezo hayo ambayo yalitolewa na Kambi ya Upinzani, sasa naomba niingie katika hoja za jumla na kama nilivyo sema awali sidhani kama nitaweza kuzimaliza zote lakini naomba niende kwa kadri muda utakavyoniruhusu. Kuhusu suala la pendekezo la Serikali kuangalia uwezekano wa kuwapa ajira nydingine askari wanapostaa fu. Tunatambua na nilijibu swali hapa kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, ni kweli wapo askari wanaostaa fu wakiwa na umri mdogo kutokana na kanuni zao za kustaafu. Lakini ni kweli vile vile Jeshi limeongeza muda wa kustaafu kwa miaka mitatu kwa kada zote. Kwa hiyo, natambua sasa muda umepita yaani umri wa kustaafu umeongezeka lakini bado wapo wanaostaa fu wakiwa na nguvu na wanawenza wakaendelea kufanya kazi. Tunashauri, kwamba Jeshi likiwhitaji baadhi ya wataalam hawa huwa linawachukua kwa mkataba lakini si rahisi kuwa-*absorb* wote katika Jeshi. Kwa hiyo, tunashauri Taasisi za Serikali, Makampuni Binafsi, Mashirika ya Umma na waajiri wengine wote waendelee kuwatumia wataalam hawa ambao wana usoefu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za likizo. Kama nilivyosema madeni yote yamelipwa, fedha za likizo si hoja tena katika Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya mipaka. Migogoro ya mipaka nitatizo kubwa sana na Wabunge wengi mliochangia mmeliona lipo tatizo hili la msingi kabisa na nakubaliana na ninyi kwamba ipo haja ya kulifanyia kazi ya ziada kuweza kuondoa matatizo haya. Matatizo ya migogoro yanatokana na mambo matatu makuu. Kwanza, yako maeneo ya Jeshi yaliyovamiwa, hakuna ubishi, maeneo ya Jeshi wakati zamani jeshi likichukua maeneo makubwa sana mbali kabisa na wananchi. Lakini kutokana na matatizo ya ardhi tuliyokuwa nayo wananchi wamekuwa wakiendelea kuingia maeneo ambayo yanamilikiwa na Jeshi. Baya zaidi Maafisa wa Mipango Miji katika sehemu nyingi wameendelea kupima maeneo ya Jeshi au yaliyokuwa karibu na Jeshi bila kulishirikisha Jeshi. Kwa hiyo, hili limekuwa tatizo kubwa katika maeneo mengi. Tatizo la pili, ni baadhi ya maeneo yaliyokuwa yanamilikiwa na watu Jeshi akayaomba na akayachukua lakini yalishindwa kulipia fidia.

Kwa hiyo, tunatambua na kuna watu ambao wako katika maeneo haya wana haki na inabidi walipwe fidia lakini mpaka sasa hawajalipwa fidia kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini jambo hili linafanyiwa kazi kwa nguvu ili tuweze kupata fedha kuwalipa wananchi hao. Sura ya tatu ni pale ambapo wananchi walitoa maeneo kwa Jeshi wao wenyewe. Baadhi ya vijiji vilitoa maeneo kwa Jeshi. Leo kwa sababu ya matatizo ya ardhi wanayataka yale maeneo wao wenyewe wakidai kwamba hawakuyatoa ambapo natambua kwamba maeneo hayo yapo vile vile. Sasa nini tunafanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeunda Kamati imetembelea na ninayo ripoti yao, imeangalia sehemu zote, wametushauri wapi pa kulipa fidia, wapi Jeshi libadilishe mipaka ili kutoa nafasi kwa wale walioko, kubaki na kadhalika. Kwa hiyo, nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge wote mliuliza kuhusu migogoro ya ardhi, naweza nisiweze kujibu moja baada ya nyingine. Lakini nataka niwahakikishieni kwamba suala hili linafanyiwa kazi na Wizara yangu itatoa taarifa baada ya kukamilisha kupidia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati tulioiunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya msingi ilikuwa ni kuhusu pensheni kwa wastaafu wa Jeshi. Tunakiri kwamba pensheni wanayolipwa wastaafu wa Jeshi ya shilingi 50,000/- ni ndogo kwa wakati tulionao, bahati mbaya sana pensheni hii inawagusa wale waliostaafu zamani kwa sababu pensheni inakokotolewa kutokana na mishahara ndiyo maana wanapata viwango vidogo na kabla haijaongezwa wengine walikuwa wanapata chini ya shilingi 50,000/- ndiyo ikaongezwa mpaka kufikia shilingi 50,000/- Wanaostaafu kwa sasa kwa sababu mishahara yao ni mizuri kwa kipindi hiki kilichopita, hawana tatizo hili, pensheni zao ni nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, lipo suala la msingi la kuangalia upya wale waliostaafu zamani ili tuone tunawasaidiaje kupandisha pensheni zao. Hili suala tunalifanyia kazi, kama mnavyotambua, linahusu bajeti, nalazimika kushauriana na Wizara ya Fedha kabla hatujalipeleka Serikalini kwa maamuzi ya pamoja kwa sababu linahusu wastaafu wengi mno na pesa wanayoipata tunakiri ni kidogo sana. Kwa hiyo,

linahitaji kufanyiwa kazi na nataka niahidi kwamba tutalifanya kazi. Isipokuwa hili tatizo la utoaji wa hizi fedha wapo Waheshimiwa Wabunge wanaosema kwamba, kutoa kwa miezi sita si sawasawa. Nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba fedha hizi zinatolewa mwanzo, hazitolewi baada ya miezi sita, zinatolewa Januari na fedha zile zinakuwa ni za Januari mpaka Juni. Halafu zinatolewa tena Julai mpaka Desemba na tumefanya hivyo kwa makusudi kwa sababu ni kidogo, unapomwambia mtu aje kuchukua 50,000/= kila mwezi gharama za usafiri zinakuwa kubwa, usumbufu unakuwa mkubwa. Kuna watu walilalamika sana Wizara ya Fedha ikabadilisha, ikatoa pensheni ya miezi miwili miwili, malalamiko yakaanza upya wakidai kwamba sisi kwa sababu fedha ni ndogo wengine tunakopa, mnapotulipa miezi miwili tunashindwa kulipa madeni yetu, ni bora vilevile miezi sita. Sasa nataka niseme kwamba, kwa kuwa fedha hizi zipo na hazina utata, bado ni uamuzi wa wastaa fu wenyewe kusema wanataka walipwe vipi na tutakuwa tayari kutimiza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malalamiko ya askari waliopigana vita Uganda. Niseme tu kwamba, hakuna malipo maalum ya askari waliopigana vita Uganda. Malipo yaliyokuwepo ni ya kawaida. Wale ambaao wamestaafu wanalipwa pensheni zao kama nilivyosema tunatambua ni ndogo kwa sababu ni muda mrefu umepita na wale ambaao wamepata ulemavu wanalipwa posho ya ulemavu. Kwa hiyo, si sahihi kwamba, waliambiwa wajirodheshe kwa sababu kuna fedha maalum wanahitaji kulipwa, hiyo nadhani ilikuwa ni taarifa ambazo si sahihi na kwa maana hiyo hata kuna baadhi waliwahi kusema kwamba Serikali ya Tanzania inaidai Serikali ya Uganda na Serikali ya Uganda ikilipa fedha hizo watapewa watu hao waliopigana vita bado taarifa hizo si sahihi. Ninachowea kusema ni kwamba, tutaendelea kurekebisha pensheni ili tuweze kuwaongeza kiwango wanachopata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu milipuko ya mabomu Gongo la Mboto, yamechangiwa na Waheshimiwa wengi hapa. Nataka kusema mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mabaraza ya uchunguzi yamefanya kazi yake, kama mlivyosema kuna mabaraza mawili. Kuna timu kutoka Marekani kufanya uchunguzi, ilifanya uchunguzi na kuwasilisha ripoti yake na Baraza la Uchunguzi lililoundwa na Mkuu wa Majeshi, limefanya uchunguzi na limewasilisha ripoti yake. Taratibu za kupitia ripoti hizo zinaendelea na bila shaka Serikali itatoa uamuzi wa mambo gani ya kufanya baada ya hapo. Ninachowea kusema ni kwamba, Makao Makuu ya Jeshi yameshaanza kuchukua hatua ambazo zimetolewa kama mapendekezo kutokana na ripoti hizo na ripoti hizo zimegawanywa katika muda wa aina tatu. Muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Muda mfupi ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Ukaguzi utakuwa unafanywa katika maghala mara kwa mara kuliko ilivyokuwa awali kuhakikisha kwamba ukaguzi unafanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, yale mabomu yote yaliyokwisha muda wako yataketezwa kuhakikisha kwamba tatizo likitokea hayatupi athari kubwa kama ilivyotokea. Huo ni muda mfupi, muda wa kati. Muda wa kati ni kuendeleza fani ya hawa wataalam wa mabomu kuweza kuwasomesha kwa wingi zaidi ili waweze kutusaidia. Lakini vilevile tutafanya ukarabati wa maghala yanayohifadhi milipuko hiyo. Hatua za

muda mrefu ni kujenga maghala mapya na kama mtakavyoona tumeweka fedha kiasi katika bajeti hii ya kuanza kujenga maghala mapya yenye *standard* zinazotakiwa. Maghala yatakayojengwa kwa zege (*concrete*) sio matofali ya kawaida. Yajengwe kwa zege yanakuwa *underground* ambayo yatatoa usalama zaidi kwa kuhifadhi milipuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za wanajeshi za makazi na ofisi zao kama nilivyoeleza, nimetoa ufanuzi kwamba tunategemea kupata mkopo na hiyo hali itaweza kurekebishwa. Kuhusu vyeti vya waliohitimu mgambo kutolewa baada ya kumaliza mafunzo ya Mgambu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania huendesha mafunzo ya Mgambu katika ngazi mbalimbali na baada ya mafunzo vyeti hutolewa. Mpaka sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeshatoa vyeti 51,536 kwa Wanamgambo mbalimbali waliohitimu mafunzo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvamizi wa maharamia katika eneo la maji yetu, tunaweza kusema kama nilivyoonyesha katika Hotuba yangu hili ni tatizo kubwa na kama nilivyo sema kumetokea matukio 14 ambayo kwa kweli ni matukio mengi. Leo katika nchi yetu ghamra za uteletaji wa mizigo zimepanda, bei za bidhaa zimepanda, *insurance* za makampuni ya meli zimepanda na wale wanaotafuta na gesi kuna athari kubwa kwa sababu wanatumia fedha nyingi kuwekeza wanataka wahakikishiwe usalama wao. Kwa hiyo, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunapata meli na zenyewe pia tuna mpango wa muda mfupi na muda mrefu. Ukitoa *order* ya meli mpya leo utaipata baada ya miaka minne. Serikali inafanya hilo kuweza kupata meli mpya lakini vile vile tutaweza kutafuta kuititia washirika wetu wa maendeleo kupata meli ambazo zitawenza kutumika katika muda huu tulionao kuweza kuzuia majanga haya. (Makofu)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza bei za matrekta yanayozalishwa na JKT. Hili linafanyiwa kazi na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba bei za matrekta yale zitapungua kwa sababu Serikali imeona haja ya kuhakikisha kwamba zile ghamra nyingine zinabebwa na Serikali ili tuweze kupunguza bei ya matrekta, wananchi wengi waweze kupata matrekta haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi kujichukulia Sheria mkononi kwa kuwapiga raia, hili ambalo amemalizia kusema sasa hivi Mheshimiwa aliyezungumza mwisho kabisa hapa, ni kwamba, kwa ujumla wanajeshi wa Jeshi la Wananchi na JKT wengi nidhamu zao ziko sawasawa, lakini hatuwezi kukataa katika kila taasisi, wapo watu wachache ambao wanakwenda kinyume na taratibu. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, nataka nimshukuru Mkuu wa Majeshi katika hili, kila inapotokea taarifa za wanajeshi kujichukulia sheria mkononi hatua zimekuwa zikichukuliwa. Tunachotaka sisi ni kwamba, tupate taarifa, wanapochukua sheria mkononi kwa kuwapiga raia hatua za kinidhamu zinachukuliwa dhidi yao. Kwa hiyo, katika hili Mbunge naomba nikusihii kwamba, wanajeshi kama wanafanya makosa kama unavyosema tupatia taarifa na nakuhakikishia taratibu za kisheria zitafuata na watachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Kunduchi kuwekwa alama ya X, hili ni la Mheshimiwa Halima Mdee. Vikao vimefanyika baina ya Wizara ya Ulinzi na

JKT na Manispaa ya Kinondoni, baadaye suala hili limefikishwa kwenye Halmashauri Kuu ya ya Majeshi ya Ulinzi, Kamati iliyohusisha pande zote iliteuliwa kwa kupitia suala zima na kutoa mapendelekezo yafuatayo:-

Kwanza kupima upya na kuwaachia wananchi waliongia wawe nje ya kambi ya RTS. Hili ni pamoja na makaburi, kwa maana hiyo, Jeshi limekubali kwamba mipaka itabadilishwa ili kuwaacha wananchi waliopo waendelee kubaki pale. Lakini baada ya kubadilisha mpaka huo kwa wale walioko bado ndani ya kambi uthamini utafanyika na Manispaa ya Kinondoni itafanya utaratibu wa Serikali kulipa fidia lakini lazima waondoke kwa sababu sasa watakuwa ndani ya Kambi. Kwa hiyo, ninachowenza kusema hapa ni kwamba, kama nilivyosema awali kila eneo lenye mgogoro litafanyiwa taratibu kama hizi, aidha kuwalipa fidia wananchi au kubadilisha mipaka ili waweze kubaki hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wabunge vijana ambao walikosa utaratibu wa kupita JKT sasa wapewe fursa ya kupitia JKT, limesemwa hapa. Nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, hilo ni wazo zuri, Mkuu wa JKT amelikubali na utaratibu utaandaliwa. Utaratibu utaandaliwa kwa mafunzo ya wiki nane kwa kila anayetaka aende akapate mafunzo haya ya uongozi kupitia JKT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Serikali kuanzisha Mfuko Maalum wa kuwapatia mkopo wa ujenzi wa nyumba na kuwasaidia kupata viwanja Wanajeshi. Hili tunatambua na hatua zimeanza kuchukuliwa. Tumeomba Manispaa, tumeanza na Dar es Salaam, Manispaa za Dar es Salaam zitupatie viwanja ili tuweze kujenga nyumba za gharama nafuu ili tuwakopeshe Wanajeshi na wakatwe kutoka kwenye mishahara yao. Kinachotafutwa sasa hivi ni wawekezaji wa kujenga nyumba hizo kwa gharama nafuu na vile vile tukishaingia mikataba nao, basi Wanajeshi watakuwa wanakatwa fedha kutokana na mishahara yao kuwalipia ili wanaposttaafu kila mtu awe angalau ana nyumba ya kuishi, ikiwemo Zanzibar bila shaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malalamiko ya vijana wengi wa Mikoani kutopewa kipaumbele wakati wa mchakato wa kuingiza vijana katika Jeshi la Kujenga Taifa. Utaratibu, JKT siyo inayochagua vijana wa kwenda kuijunga kule kwenye makambi. JKT inatoa nafasi hizo kupitia Mikoa, kila Mkoa unapewa nafasi maalum na kila Mkoa unatakiwa upeleke nafasi hizo kwenye Wilaya zake na hatimaye majina yanaletwa Makao Makuu ili wapangiwe katika Kambi mbalimbali za JKT. Kwa hiyo, si kweli kwamba JKT ndiyo wanaobagua kwamba nani apewe nafasi na nani asipewe. Ukweli ni kwamba nafasi hizo, maamuzi hayo yanaamuliwa kutoka kwenye Wilaya zetu, kutoka kwenye Mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ajira, hususan ajira katika Jeshi kwa Wazanzibari limesemwa kwa uchungu hapa. Nataka nilitolee maelezo ya kitakwimu, mwaka 2008 ajira ya Wazanzibari Jeshini, wavulana walijiriwa 507, wasichana 65, jumla 572; mwaka 2009, wavulana 428, wasichana 73, jumla 501; mwaka 2010, wavulana 22, msichana 1, jumla 23; mwaka 2011, wavulana 256, wasichana 13, jumla 209. Kwa hiyo jumla kwa miaka hii niliyoitaja kuanzia 2008 mpaka sasa kutoka Zanzibar

walioajiriwa ni 2,035. Kwa bahati mbaya, hapa sina takwimu za Bara. Nitawapeni taarifa nkipata takwimu halisi. Sasa hivi siwezi kutoa takwimu hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwiano wa kijinsia Jeshini: Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamechangia kwamba Jeshi letu halina uwiano wa kijinsia. Napenda kusema yafuatayo:- Hili ni vyeo pamoja na jinsia yenyewe. Utaratibu wa kupanda vyeo Jeshini una taratibu zake, taratibu hizo ni pamoja na kwenda kozi, muda wa kukaa na cheo kimoja na nidhamu aliyonayo mhusika. Hata hivyo, JWTZ inafuata haki katika upandishaji wa vyeo. Katika Afrika, Tanzania ndiyo yenyewe Meja Jenerali wa kike wa kwanza, naye ni Meja Jenerali Zawadi Madawili. Pia, kuna Brigedia Jenerali, Grace Mwakipunda na Brigedia Jenerali, Ruth Kingazi na Makanali wapo wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ikumbukwe kuwa wanawake kuingia Jeshini ni hatua iliyofuata baadaye baada ya kuanzisha Jeshi mwanzo hawakuwepo Jeshini kulingana na mazingira yaliyokuwepo wakati huo. Kwa sababu walichelewa kuanza kuingia Jeshini, bila shaka idadi yao itakuwa ndogo na wengi vyeo vyao havitakuwa vile vya juu kabisa. Lakini ukweli ni kwamba ukiangalia majeshi mengine katika Kanda yetu, Mabrigedia Jenerali wako katika Jeshi letu zaidi kuliko kwingine na vyeo vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilizungumze moja hili la hawa Wazee waliopigana Vita vya Pili vya Dunia. Tanzania *Legion* ni Chama cha Wazee waliopigana Vita vya Pili vya Dunia na kuna Taasisi kule Uingereza iliyoona ni bora kuwasaidia na wakawa wanachangisha fedha na wanazileta kuwasaidia wenzao katika hizi nchi zinazoendelea. Kwa bahati mbaya sana kukatokea migogoro ya uongozi ndani ya Tanzania *Legion*. Matokeo yake ile taasisi ya Uingereza ikasitisha kutoa fedha zile na kwa maana hiyo ndiyo maana sasa hivi wanalamika kwamba hawapati fedha hizo, Wizara yangu ikaliingilia kati suala hili. Tunachofanya sasa ni kuhakikisha kwamba tunawakusanya, kwanza tunawatambua kila sehemu walipo, baadaye tunawataka wafanye uchaguzi kuchagua uongozi wao ili tuwaambie Ubalozi wa Uingereza kwamba sasa uongozi uko timamu na wanaweza kuendelea kuwapa fedha hizo ili ziwafikie walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Wazee wengi kati ya hawa umri wao sasa umekwenda sana, wana matatizo mengi, tunatambua. Lakini, bila ya kuwa na uongozi huo, Waingereza hawako tayari kuendelea kutoa fedha hizo. Jambo hili linafanyiwa kazi, tumeunda Tume ambayo inazunguka na wamekwishaleta taarifa ya idadi, wamewatambua hawa wazee. Tutawasaidia kufanya uchaguzi ili hatimaye waweze kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa njibu maeneo ya Mheshimiwa Amina Andrew Clement kuhusu suala lake maalum la kwamba, kuna nyumba imeangukiwa na kitu kilichotokea kwenye Kambi ya Jeshi. Nataka nimhakikishie kwamba hili jambo tutalifanya uchunguzi na ikithibitika kwamba, hayo yametokea kama anavyosema

Mheshimiwa Mbunge, taratibu zitafuata za kumlipa mhusika. Pia kwa maeneo yanayochukuliwa na Jeshi, taratibu zitafuata za kulipa fidia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salim Turky yeye alitaka kambi zihamishwe kutoka kwenye miji. Napenda nirudie tena katika eneo hili, niliwahi kusema wakati najibu swali hapa. Kambi hizi hazijawekwa mradi tu zikae pale zilipo, zimebekwa kwa madhumuni maalum ya kistratejia. Kwa maana hiyo, unaposema kambi zihamishwe mijini, nadhani tutahamisha zote maana leo kambi ngapi ambazo hazipo mjini? Wakati wanaanza, kambi hizi zilikuwa mbali. Leo kwa sababu ya uhaba wa ardhi, watu wamekaribia mno. Kwa maana hiyo, hatuwezi kuondoa kambi hizi mijini, badala yake kama nilivyosema wakati najibu swali, kwa maeneo kama Mbagala na Gongolamboto tutaondoa maghala ya milipuko katika maeneo yale. Lakini, kambi zitaendelea kubaki pale kwa kazi nyiningine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Manunuzi iangaliwe ili kutoa nafasi kwa Jeshi kupata vifaa vilivyotumika. Suala hili Serikali imeliangalia na tunalifanyia kazi kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba wenzetu wote wa nchi jirani tunazopakananazo wanunua vifaa vilivyotumika kwa ajili ya majeshi yao kwa sababu zana za kivita ni zana zenyenye gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Mayenga, nakubaliana naye kwamba Sheria ya Ulinzi wa Taifa imepitwa na wakati, JKT imetengewa fedha ndogo za maendeleo, shilingi bilioni tatu. Hili tunalitambua, lakini, kama tulivyosema, miaka ya nyuma wamekuwa wakitengewa kiwango ambacho wameweza kukarabati makambi yao hadi sasa wana uwezo wa kuchukua vijana 20,000 na hizi bilioni tatu ni kwa ajili ya kufanya ukarabati mdogo mdogo ili hatimaye mwaka ujao wa fedha tupate fedha za bajeti zitakazokidhi kuanzisha mafunzo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Defence College (NDC)* kitaanza kama nilivyosema na maslahi ya wastaa fu yataboreshwa kama tulivyozungumza hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maeneo ambayo alichangia Mheshimiwa Sanya ambayo ni ajira, alisema kwamba, Zanzibar wapate *quarter* na hata kozi za kwenda uofisa *cadet* ziwe kwa *quarter*. Hili kama nilivyo iliju, Mheshimiwa Sanya ndivyo ilivyo, kuna nafasi maalum zinazotolewa kwa pande zote za Muungano ili hatimaye tuweze kuwa na Jeshi ambalo lina watu kutoka pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumza kwamba, kiwango cha *ration* kiongezwe. Hili linafanyiwa kazi na nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba *ration* imeangaliwa na tutaweza kuongeza posho hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile alichangia kuhusu madeni. Hayo yalishalipwa na kuhusu kuwawekea maslahi kwa ujumla ya wastaa fu; kama nilivyosema, tunatambua fika kwamba fedha wanazopewa wastaa fu hususan waliostaafu zamani ni chache na kwa maana hiyo Serikali italifanyia kazi jambo hili ili kuweza kuboresha hizo pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Sabreena Sungura kwamba, fedha kiasi gani zimetengwa kwa mafunzo, nitaomba tu apitie kwenye vitabu vyetu vile vya *OC*, utaona kwenye *Vote 38* kuna fedha za mafunzo, utaona kwenye *Vote 39* kuna fedha za mafunzo. Kwa hiyo, fedha hizo zipo. Kukidhi na kutokidhi haja ni suala lingine ambalo linategemea uwezo wa kibajeti, lakini fedha zimetengwa kwa ajili ya mafunzo. Lakini Mheshimiwa Mbunge nadhani mafunzo anayozungumzia ni tofauti. Wako vijana ambao wanajiunga na Jeshi, wakiingia tu kwenye Jeshi, wanataka waende kusoma vyuo vikuu, waende kusoma kwenye *college* walipiwe na Jeshi. Sasa, tunachowenza kusema ni kwamba, utaratibu ulioko Jeshini, vijana hao lazima waende kwa zamu. Haiwezekani ukawalipia wote wanaotaka kwenda kusoma, haiwezekani. Kwanza, utawaondoa wote Jeshini kwa sababu wengi wao wanataka kusoma, lakini pia uwezo wa Jeshi kuwasomesha wote haupo, lakini ukiangalia fedha za mafunzo zipo kwa mafunzo aina mbalimbali, siyo hao tu wanaokwenda vyuoni, lakini na mafunzo yale ya kawaida katika kila Kikosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabomu ya Gongolamboto na taarifa ya uchunguzi kama nilivyosema ni kwamba taarifa za uchunguzi zimekwishawasilishwa kwa mamlaka husika na zitafanyiwa kazi kuititia Serikali na hatimaye kutolewa uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makampuni binafsi ya ulinzi, sheria gani inaruhusu! Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba vibali vya makampuni ya ulinzi havitolewi na Wizara yangu. Vibali vya makampuni ya ulinzi vinatolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, nakuumba Mheshimiwa Mbunge usije ukashika shilingi kwangu wakati hili halinihu. Maana ultishia kushika shilingi kama sitokupa majibu hapa. Hili halihusiki na Wizara ya Ulinzi, ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na bila shaka wana vigezo vyao ambavyo unaweza ukapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hii *Regulation* ya wanaoingia Jeshini kutoruhusiwa kuoa au kuolewa kwa muda aliotaja Mheshimiwa Mbunge, ni sahihi kwa sababu mara zote Jeshi lazima liwe lina watu ambao wako tayari wakati wote. Huwezi ukawa na Jeshi la watu wote wameoa au wameolewa, ule utendaji kijeshi utaathirika. Lakini, rai yako uliyotoa tutaipokea na itaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nilishawahi kuambiwa na Viongozi wa Jeshi kwamba suala hili linafanyiwa kazi hususan kwa sababu utaratibu wa ajira umebadilika Jeshini, badala ya kuchukua kutoka mitaani, sasa wanachukua vijana kutoka JKT ambapo pale JKT wamekwishapitia miaka miwili. Kwa hiyo, ipo kila sababu ya kupunguza ule muda ambao wakishaingia Jeshini, wakishaajiriwa, kupunguza ule muda kwa sababu walishakaa JKT. Kwa hiyo, hili linatazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wavuvi kushambuliwa katika Ziwa Tanganyika na katika mipaka ile tuliyonayo na nchi tunazopakana nazo. Nililisema katika hotuba yangu kwamba Jeshi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vimekuwa vikifanya doria katika maeneo haya ya mpakani, iwe mipakani kule Kagera, iwe katika Maziwa yetu, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, limekuwa likifanya doria za

mara kwa mara kuweza kuhakikisha kwamba kwa sababu tunatambua hata katika hotuba yangu ya bajeti yapo maelezo mle kwamba kumetokea matukio ya uhalifu, uharamia, uhalifu wa kutumia silaha. Kwa hiyo, Jeshi linatambua hali hiyo na operesheni maalum zinafanyika ili kuweza kudhibiti vitendo hivyo. Tutaendelea kuongeza viwango vya bajeti ili kuweza kufanya doria hizo ziwe mara kwa mara zaidi ili kuondoa tatizo linalokabili wananchi wetu katika maziwa na mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani maswali ya Mheshimiwa Mariam Msabaha kwa kiwango kikubwa nimeyajibu. Lakini kuhusu hili suala la kwamba Jeshi sasa pia lichukue vijana wa darasa la saba, kwa kule Zanzibar vijana wa *form two*. Hili Mheshimiwa Mbunge, si kwamba halipo, lipo, lakini kwa vigezo maalum. Inapotokea kuna nafasi za ajira kwa mfano madereva au nafasi za ajira kwa mfano, watumishi wale wenye aina fulani ya ujuzi (stadi maalum), tunachukua. Wapo vijana wa darasa la saba wanaochukuliwa, wako vijana kutoka Zanzibar wa *form two* wanaochukuliwa, lakini wawe na stadi fulani, isiwe darasa la saba peke yake. Kwa maana hiyo, ni kwamba, hili jambo si geni, linafanyika na tutaendelea kuwapa stadi wale ambao wameingia JKT, wakakosa ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama, wakitoka pale anakuwa na stadi fulani ili hatimaye wakienda nje waweze kujiajiri wao wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala moja ambalo limenigusa sana ambalo Mheshimiwa alilisema ni kwamba, waathirika wa mabomu ya Gongolamboto bado wanapata tabu na kwamba hawajalipwa fidia na kadhalika. Wakati najibu swali hapa nilisema kwamba SUMA-JKT imepewa jukumu la kujenga zile nyumba. Kiwanja wamepewa, wako katika utaratibu wa kuanza ujenzi. Serikali ya Mkoa wa Dar es salaam inasimamia suala hili na ni kwamba, tunawahakikishia jambo hilo litafanyika na wale wote ambao wako kwenye mahema pale wataweza kupewa hizo nyumba zitakapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa hili la kusema misaada inatolewa kwa itikadi za kisiasa, naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge hata kidogo. Hakuna misaada uliotolewa Gongolamboto kwa itikadi za kisiasa. Misaada yote ilikuwa inaratibiwa na Kamati ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na uongozi wa Mkoa wa Dar es salaam. Waliohusika wote kwa taarifa tulizonazo ni kwamba, walikuwa wanapata misaada hii na hakuna aliyekuwa anaulizwa chama chake au dini yake au jinsia yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa kwenye ajira za Jeshi liangaliwe kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Nataka niseme tu kwamba, ajira zinapotoka, kwa kuwa wanaotaka ajira ni wengi mno, bila shaka wako wengi watakaokosa. Kwa hiyo, ni rahisi kwa wale wanaokosa kuanza kulalamika kwamba labda wametakiwa rushwa au vitu kama hivyo. Nitatoa mfano, wakati tunatafuta nafasi ya vijana kwa ajili ya udereva, nafasi 200 zilitangazwa, waliojitokeza ni zaidi ya vijana 5000. Haiwezekani vijana hao wote wakapata hizo ajira. Lakini, kama upo ushahidi wa rushwa, basi namwombwa Mheshimiwa Mbunge anipatie na namhakikishia litafanyiwa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la Wanajeshi kutishia raia wakati wa uchaguzi Zanzibar na kushiriki katika uhalifu, katika hili, naomba niseme kwamba matamko kama haya wakati mwingine yanahitaji kuwa na ushahidi wa dhati kabisa. Ni matamko ambayo yanagusa hisia, ni matamko ambayo kama huna ushahidi, ni jambo ambalo utawafanya walinzi wetu wa amani hawa kujisikia vibaya, kwa sababu wao wanafanya kazi ya ulinzi wa nchi yetu usiku na mchana wakitegemea kwamba Watanzania wataenzi kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, inapotokea kwamba matamshi kama haya yanatolewa, namwomba Mheshimiwa Mbunge, sisemi kwamba haiwezekani kuwa yametokea, ninachosema ni kwamba, kama kuna ushahidi, basi tupatие ushahidi huo. Ninachosema ni kwamba, Jeshi kuliko taasisi nyingine yoyote ndiyo taasisi inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Yanapotokea matatizo yoyote katika Jeshi, hatua za kisheria zinachukuliwa mara moja. Kwa hiyo, ninachoomba tu ni kwamba, haya maelezo anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge ni vema yathibitishwe kwa maelezo ambayo yatakidhi haja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimalizie kuhitimisha hoja kama nilivyosema awali kwamba, siyo rahisi kuweza kujibu hoja zote. Kuhusu suala zima la uanzishwaji wa Kambi za JKT katika Wilaya mbalimbali. Wapo Wabunge wengi sana wangependa tuanzishe Kambi za JKT katika Wilaya zao, kimsingi jambo hili limekubalika na Serikali inayo azma ya kuanzisha kila Wilaya Kambi moja ya Jeshi la Kujenga Taifa na hii itakuwa ina maana zaidi pale ambapo tutakuwa tumeanza kuchukua vijana kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu vijana hao ni wengi na watahitaji maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu swal la Mbunge wa Singida, Jimbo la Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Lwanji ambalo amekuwa akilizungumza mara nyingi sana kwangu na humu Bungeni, nataka nimhakikishie kwamba watalaam wa JKT walishatembelea Mkoa wa Singida na kufanya tathmini yao, mchakato wa kuanzisha kambi hiyo unaendelea kwa kutegemea hali ya fedha itakavyokuwa. Lengo la Serikali ni kuwa na Kambi za JKT katika kila Wilaya. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, endapo tutapata fedha kwa bahati mbaya sana mwaka huu wa fedha kama mtakavyoona katika kitabu cha maendeleo, JKT wamepata fedha bilioni tatu ambayo haikidhi kuanzisha kambi mpya yoyote, lakin tutakamilisha Kambi ambazo zimeshatangulia ili mwakani tuweke bajeti itakayoweza kukidhi uanzishwaji wa kambi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa mara nyingine tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na kwa kulispongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri wanayoifanya na naungana nao kuwapongeza Wanajeshi kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutulinda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbushwa tu kwamba, naomba nimirambue Mheshimiwa Modestus Kilifi kwamba naye alichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri kwa majibu mazuri uliyoyatoa na sasa Wabunge naomba tuendelee, Katibu kwa hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### FUNGU 38 - JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA

Kif. 1001 - *Defence Force Headquaters'*  
Command.....Sh. 396,260,814,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu kwamba, hapa siyo mshahara wa Waziri ila kuna mshahara wa *CDF* hapa lakini wenyewe huwa haukamatwi, tunakamata mshahara wa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema utaratibu wetu ni ule ule, tunaongea mara moja tunaendelea, naomba tuwe *specific*.

**MHE. SUZAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, nipo *Subvote 1001*, kifungu kidogo cha 220400, *Medical Supplies and Services*, kifungu hiki kinaonesha kwamba hakikupata fedha kabisa wakati mwaka jana kilipata shilingi bilioni moja. Naomba kujuu hawa wanajeshi wetu hawatibowi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili la matibabu limehamishwa kwa maana kwamba limetengewa kasma ya peke yake, ukurasa wa 189, *Military Hospitals*, *Subvote 1010*, imetengwa shilingi 2.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fungu hilo ndiyo lita-cover matibabu kwa ajili ya Wanajeshi wote.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, *Subvote 1001, item 221700, food supplies and Services*, kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kiwango cha fedha za chakula ni kile kile, wanajeshi wanaongezeka na gharama za chakula zinaongezeka, Waziri atueleze, kwa nini *figure* hii haibadiliki au wanajeshi hawaongezeki?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ni kwa ajili ya *rational allowances* na huwa zinatolewa na kama nilivyosema Serikali inalifanya kazi ili iweze kuongeza kiwango cha *rational allowance*. Isipokuwa kwa kujibu swalii lake ni kwamba, ikama ya Jeshi kuna

watu ambao wanastaafu, kuna watu ambao wanaacha kazi, kuna watu ambao wanafariki, kwa hiyo, mpaka sasa hivi ajira zote mpya zinaziba huo upungufu unaotokea.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi wa kasma 221200, inayohusu *Communication and Information*, ufanuzi ninaouhitaji unahusu mafungu ambayo yametengwa kwa ajili ya Mawasiliano ya Kijeshi, nafikiri. Ukiangalia mwaka 2009/2010 fungu hilo lilipewa bilioni 1.4 mwaka jana 2010/2011, fungu lilipewa bilioni 1.2 na mwaka huu 2011/2012, pendekezo limetengewa shilingi milioni 878. Nashindwa kuelewa kwa nini mahitaji ya mawasiliano ambayo napenda kuamini ni jambo muhimu sana katika masuala ya kijeshi, kwa nini hili fungu limekuwa linapungua kama nilivyoonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki niende mbele sana lakini nimeangalia vile vile katika hizo *command* mbalimbali za Jeshi letu hali ni ile ile kwamba fungu la mawasiliano limekuwa linashuka tangu mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu. Naomba ufanuzi katika hilo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba ieleweke kwamba *communication and information* tunayoizungumzia hapa siyo mawasiliano yale ya kijeshi ni tofauti, hii ni haya mawasiliano ya kawaida ya kiofisi yaani *internet and email connection, post and telegraph wireless, telephone, telex, advertising na telephone charges* na vitu kama hivyo vya kiofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu inayofanya fungu hili lipungue ni la kibajeti tu, kwa sababu *OC* ya Ngome kwa mwaka huu imepungua kwa asilimia nane kutokana na ufinyu wa bajeti na kwa mtazamo wao kwa vipaumbele vyao wameamua kupunguza baadhi ya mafungu kwa kadri walivyoona inafaa.

**MWENYEKIDI:** Lakini pia mkongo wa Taifa unapunguza matumizi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ndogo ya 270800, *Current Grant to non Financial Public Units*, ambapo ndiyo Jeshi kwa zile taasisi ambazo inafanyanazo kazi, huwa inapeleka *grants* ama *subsides* na vitu kama hivyo, wakati nachangia hapa nilielezea kwa kirefu sana suala zima la Meremeta na wakati Waziri pamoja na kujibu masuala mengine yote hakuligusa kabisa suala hili na naamini kabisa kwamba suala hili sasa ni lazima lifikie mwisho kama jinsi ambavyo nilivyolieza, hatuwezi kuwa ni Taifa ambalo tunarudia jambo moja kila siku, kwa hiyo, naomba Waziri atoe maelezo na niseme kabisa kwamba, iwapo maelezo ya Waziri hayatanitosheleza nitaomba kuondoa shilingi katika kasma hii, ili iende ikiwa nusu, lakini kama akinitosheleza na vile vile nilishalieza Bunge lako Tukufu kwamba nitatumia kanuni 117(2) (a) kwa ajili ya kutaka Kamati Teule ya Bunge iundwe kwa ajili ya kuchunguza kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 216 ambacho tuliilipa *NedBank* ya Afrika ya Kusini kwa ajili ya suala hili la Meremeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya Waziri ili jambo hili tuweze kulifikisha mwisho.

**MWENYEKITU:** Kabla ya kumuita Waziri nikufahamishe tu kwamba kwa lile suala la pili, kama una nia ya kuleta hoja utaratibu wake unafahamika wa kikanuni, namna ya kuwasilisha hoja kwa Katibu na kadhalika, *otherwise* tunaendelea na suala la kwanza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nikiri kwamba sikumuelewa Mheshimiwa Zitto vizuri katika hoja yake. Kama hoja yake ni kwamba fungu hili ni fedha za nini, jibu ni kwamba, fungu hili ni fedha ambazo zinalipwa katika Vyama vya Michezo vya Majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni *Grant to non Financial Public Union*, yaani Jeshi linatengewa fedha kulipa ada wanaposhiriki katika michezo ya majeshi kwa mfano na hapa hizi fedha zote zilizopo hapa zinakwenda katika ushiriki wa Jeshi katika michezo ya Majeshi (BAMATA). Kwa hiyo, sioni vinahusiana vipi na swali lake lile lingine.

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Zitto ali-declare *interest* mapema akasema kwamba hajafika Jeshi bado. Kwa sababu ni nje ya pale, tunaendelea.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *commitment* ya Serikali kwa kuwa Waziri amekiri kwamba Tume yake imeshampa ripoti ya migogoro ya mipaka kati ya Jeshi la Wananchi na wananchi.

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Maselle unaji-address wapi?

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *subvote* 1001, ninahitaji *commitment* ya Serikali kwamba...

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Maselle nina hakika hujajipanga vizuri, hebu naomba ujipange vizuri halafu labda tutawenza mbele ya safari.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1007 - *Land Force Command*.....Sh. 8,327,061,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1008 - *Air Defence Command*.....Sh. 6,210,402,000/=

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Naomba ufanuzi kwenye *Command* hii ya anga, kwenye *item* 220800, *training*

*domestic*, Waziri anieleze pamoja na mambo mbalimbali ya masomo ya mafunzo ambayo yameainishwa na matatizo ambayo tunayo, kwa nini kuna upungufu mkubwa wa shilingi milioni sita.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali ni kwamba, *training domestic* ni fedha ambazo zinatumika katika kutoa mafunzo kwa wanajeshi wa *command* hiyo na kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, wao wenye we wamejipanga kupunguza baadhi ya maeneo kadri wanavyoona inafaa. Kwa hiyo, kama hoja ni kwamba kwa nini inapungua. Jibu ni kwamba, ni kwa sababu tu bajeti waliyopata kwa ujumla wake ni ndogo, kwa hiyo, wameona ni wapi wabane wao wenye we.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na hilo linajibu maswali yote mengine yatakayofanana na hili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1009 - *Navy Command*.....Sh. 2,511,237,000/=

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Nataka nipate ufanuzi kwenye kipengele kidogo cha 210100 cha *basic salaries pensionable post*, kinaonekana hakijatengewa fedha kabisa. Nataka ufanuzi kutoka kwa Waziri, kwa nini hapa hakuna mishahara, lakini wakati huo huo tunaona kwamba kuna posho huku chini. Nataka kupata ufanuzi kuhusiana na hilo. Nashukuru.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mishahara za *Command* zote sasa zimewekwa Makao Makuu ya Jeshi. Kwa hiyo, ukiangalia *Navy*, *Air Force*, *Land Force* utakuta hamna mishahara lakini ukiangalia Makao Makuu ya Jeshi utakuta mishahara imeongezeka.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea hii inayoitwa *Command* ya *Navy*, kwanza niseme kwamba, tunapata matatizo ya kijamii kwa sababu ya randama, sasa tutakuwa tunafikiria tu kwamba, labda hiki ni kitu gani, hatuna uhakika kwa sababu hatuna randama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* 220600, kuna *clothing, bedding, footwear and services*, nafikiri kwamba ni sare za wanajeshi kwa ujumla. Kama hivyo ndivyo, nauliza upungufu huu mkubwa unamaanisha nini, ni kwamba hatutaki wanajeshi wetu wavae sare katika mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Maswali ya Bajeti ndogo Mheshimiwa Waziri amekwishatoa ufanuzi wa kutosha na nikawaomba kwamba maswali ya Bajeti ndogo hebu nadhani majibu yale yanatosha.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nevy* ni moja ya eneo muhimu sana la Jeshi. Swali ambalo Mheshimiwa ameuliza ambalo lilikuwa swali langu la kwamba *Nevy* kwa upande wa *clothing, bedding, footway services* shilingi laki nane haielezeki wala huwezi kusema kwamba una Bajeti ndogo kuwapa wanajeshi wako viatu, una Bajeti ndogo kuwapa wanajeshi wako mashuka, una Bajeti ndogo kuwapa wanajeshi wako huduma zinazostahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Zitto naomba ukae chini. Nimeshalitolea uamuzi kabla kwa hiyo, kulirudia tena na kulinyanya ni kupima tu mamlaka ya Mwenyekiti kama anajua kuendesha kiti chake. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1010 – *Military Hospitals*..... Shs. 2,106,651,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 39 – JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT)**

Kifungu 1001 - *The National Service Force*..... Shs. 103,006,880,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 37 – WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1001 - *Administration and General*..... Shs. 12,943,751,000

**MWENYEKITI:** Sidhani kama tutaweza kuwafikia wote kwa sababu muda wetu ni mdogo sana. Naomba twende moja kwa moja kwa kifupi ili tupate majibu ya haraka.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kweli wala sina tatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ila tu kwa ajili ya kuweka mambo sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1997 wafanyakazi wanaokaribia 90 hivi waliokuwa wanafanya kazi kwenye Shirika la Mzinga Morogoro wakiwemo na wapigakura wangu wa Tandahimba walipata *redundancy* walipokuwa wanaandalialiwa malipo yao (stahili) ya kurudi nyumbani na mambo mengine hawakuridhika nayo kwa sababu stahili zile zilionekana kuwa ni ndogo na wakaamua kwenda Mahakama. Mahakama iliamua kwa kadri inavyoona stahiki hizo kuwa ni stahili zinazofaa kwa mujibu wa Mahakama.

Baada ya hapo Serikali kupitia Wizara hii na labda niseme kupitia Shirika la Mzinga, haijawalipa malipo yale yanayotokana na maamuzi ya Mahakama badala yake imekuwa kila wakati wanaambiwa subiri Bajeti, jambo hili linachosha na ni kero. Ningombaa kupata maelezo ya Waziri anamaliza lini jambo hili. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Juma Njwayo kama ifuatavyo; lazima nikiri kwamba suala hili halijaletwala kwangu rasmi na hawa wafanyakazi wenyewe malalamiko hayo. Ninazo taarifa kwamba kulikuwa kuna kesi juu ya jambo hili na ninazo taarifa kwamba kuna hukumu iliyotolewa na kwamba wanaokosana sasa hivi ni kati ya Wakili wa wale waliofungua mashtaka baada ya kusema kwamba fedha zilitolewa na Wakili yule hakuzifikisha kwao. Kwa hiyo, ninachomuomba Mheshimiwa Njwayo ni kwamba pengine ingekuwa vema wahusika au kupitia kwako wewe mwenyewe mkaniletea hiyo kesi ili tuitazame upya na kama kweli kuna suala Wizara yangu kuhusika na malipo basi niweze kulifanyia kazi. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia sana suala la Dafur na askari wetu kule ambao wamejitolea roho zao kwa kulinda Bara la Afrika. Lakini manyanyaso na matatizo waliyonayo kwamba wananyimwa, wanalala askari watano chumba kimoja kodi yao dola 800. Fedha za likizo katika dola 650 wanalipwa 150, mshahara katika dola 5000 wanalipwa dola 800. Sasa wanashindwa na magari ya *IVECO* yaliyopelekwa yana hali mbaya, mabovu yanahatarisha maisha yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu tufafanulie. Moja tu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Ni mawili kwa mujibu wa Kanuni.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti anasema moja tu Mheshimiwa Mnyaa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuleta malalamiko katika Wizara ya Ulinzi, unafahamika. Kama mwajeshi anahisi anaonewa kwa aina yoyote ile utaratibu ni kwanza kupeleka malalamiko yake kwa Mkuu wa Majeshi na endapo hatakuwa amepata maelezo yanayokidhi anavyotaka basi anayo kila sababu ya kukata rufaa kwa Waziri. Sasa hayo unaniambia Mheshimiwa Mnyaa, mimi sijawahi kuyasikia hayajanifikia malalamiko haya. Sasa ningekushauri tu uwaarifu wahusika wafuate basi utaratibu huo ili unifikie rasmi niweze kuchukua hatua. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimechangia kwa maandishi kwa hiyo, naomba kujua Wanajeshi wa Jeshi JWTZ wataondoka lini kwenye Kijiji cha Ronsolti, ambacho kipo katika Kata ya Nyamisangula, ukizingatia kwamba baadhi ya Wanajeshi hawa amba walikuwa ni wenye familia baada ya kuwa

wamepata madhara ya mvua kunyesha na mafuriko kule Tarime wakaomba wanajeshi wenye familia wapewe hifadhi kwenye Kijiji cha Ronsolti kwa muda kwa sababu mawasiliano yalikatika kati ya Kambi ya Nyandoto ya Kikosi namba 28KJ na Mjini Tarime, kupata mahitaji yao na viongozi wa kijiji kile wakawapa hifadhi ya kwa muda na mpaka sasa daraja limeshajengwa lakini cha ajabu wanajeshi hawataki kuondoka badala yake wanadai kumiliki kile kipande cha ardhi na kwa kipindi kile walipewa ni kati ya ekari moja au mbili.

Kwa hiyo, napenda nipate maelezo kwa hilo kwa sababu viongozi wa kijiji wameshachukua hatua mbalimbali na wameshamwandikia hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkuu wa Majeshi akawajibu kwamba wasiende Mahakamani wanafanya jitihada...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naamini umeeleweka.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Naomba kutoa shilingi kama sitaridhika na majibu ya Waziri na naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni namba 103.

**MWENYEKITI:** Mmechelewa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Esther Matiko swali lake kama ifuatavyo:-

Nilisema wakati najibu hoja kwamba matatizo ya mipaka/ardhi kati ya wananchi na Jeshi katika nchi yetu yapo maeneo mengi. Nimeseme vilevile kwamba Wizara yangu iliunda Kamati ya kwenda kupitia migogoro hiyo ili hatimaye walete taarifa kwetu na tuweze kuchukua hatua. Sasa nilieleza kwamba Kamati imekamilisha kazi yake wameshaleta Wizarani kinachosubiriwa ni kwamba tukae katika kikao chetu cha juu pale Wizarani ili tuweze kuchukua hatua kwa majibu wa mapendekezo ya Kamati hiyo. (*Makofi*)

Ninachomuomba Mheshimiwa Mbunge na suala siyo la kwake peke yake pamoja na Mheshimiwa Nyangwine kwamba kwa mujibu wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo, tutachukua hatua na kama nilivyosema yapo baadhi ya maeneo ambayo jeshi watakubali kubadilisha mipaka, yapo baadhi ya maeneo ambayo jeshi watalazimika kulipa fidia. Sasa kujibu sasa hivi hapa itakuwa vigumu kwa sababu bado kikao chetu hakijakaa ili kupitia mapendekezo ya Kamati iliyofanya kazi hiyo. (*Makofi*)

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi mbali na mambo mengine ikiwa ni pamoja na mambo mengine ikiwa ni pamoja na kuuliza ni gharama kiasi gani kilitumika katika kuchukua helikopta na kumpeleka Mheshimiwa Freeman Mboge kwenye kesi yake. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amejibu ingawa sijaridhika na majibu yale. Niliuliza pia lipo tatizo kwa madaktari ambao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda jielekeze katika jambo moja kwa moja. Sasa lile uliloliongea au hili linalokuja.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Linalokuja.

**MWENYEKITI:** Basi ungekwenda moja kwa moja.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba wako madaktari ambao siyo wanajeshi wako *titled* kupata nyumba au kulipiwa fedha kwa ajili ya pango la nyumba lakini wamekuwa hawapewi nyumba au fedha hiyo. Sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba je, ni kitu gani kinachokwamisha suala hili kwa madaktari hawa ambao wameajiriwa katika hospitali za jeshi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba suala hilo nililiona na kwa bahati mbaya tu kwa kukosa muda sikuweza kulijibu lakini ukweli ni kwamba kila mwanajeshi mwenye stahili ya kupata nyumba aidha, anapata nyumba au anapewa fedha za kwenda kukodi. Kama Mheshimiwa Mbunge anamtambua mtu ambaye haya yote mawili hayapati anifikishie jina hilo nitachukua hatua.(*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua kutokana na kauli ya Serikali ya tarehe 18 Juni, 2008 kuhusu kuchukua vijana kutoka JKU hapa mazungumzo mengi yalikwenda kutokana na JKT tunataka kujua vijana kutoka JKU kuna msimamo gani kuhusu kauli hii bado ipo au mmeifuta?

**MWENYEKITI:** Kabla ya kumruhusu Mheshimiwa Waziri, kwa mamlaka niliyopewa inabidi niongeze muda wa nusu saa ili angalau tuweze kupata Wabunge wengi zaidi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo; kauli haijafutwa inapotokea nafasi za ajira wanachukuliwa vijana kutoka JKT na vijana kutoka JKU. (*Makofi*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la mgambo. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sera ya Taifa ya ulinzi inatambua uwepo wa mgambo kama jeshi la akiba. Lakini mgambo hawa wanaishi bila mfumo rasmi wa kupata maslahi yao. Wanapata posho zao kwa kutegemea ajira za muda zitokee labda wamachinga wamekaa barabarani wao wanakwenda kuwatimua ndipo wanapopata mahitaji yao. Labda wananchi wanaambiwa wachangishe michango wanakwenda kukusanya michango kinguvu halafu wanapata posho kuitia michango ya wananchi. Sasa nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, haoni sasa umefika wakati wa mgambo Tanzania kuingia kwenye mfumo rasmi wa ajira?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Regia Mtema kama ifuatavyo; ni kweli kwamba mgambo ni jeshi la akiba, lakini majeshi ya akiba ni mengi si mgambo peke yake, kuna wastaa fu wote wa jeshi, kuna vijana wa JKT na kadhalika. Si rahisi kwa Jeshi la Ulinzi au kwa Wizara ya Ulinzi kulipa kundi lote hilo. Tunachosema mara zote ni kwamba suala la mgambo kwa kiwango kikubwa linashirikishwa na Halmashauri za Wilaya husika. Ndio maana hata mafunzo ya mgambo utaratibu wake unapitia Wilayani. Kwa hiyo, mimi ningetoa rai kwamba hizi mamlaka za Serikali za Mitaa zingeangalia utaratibu wa kuwaajiri hawa endapo wanahitaji askari wa kutoa huduma chini ya Halmashauri zinazohusika. (*Makofî*)

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu kimaandishi nilikuwa nimeomba ufanuzi juu ya kujenga Shirika la Nyumbu kuwa ni kituo kikubwa kinachoongoza cha utafiti na teknolojia kijeshi katika Kanda hii ya Afrika. Sasa nikitazama katika Bajeti hilo halijitambulishi kwamba Bajeti ina *address* maelezo hayo. Sasa naomba Waziri anipatie maelezo juu ya kile kilichoelezwa kwamba wanafanya kituo ambacho ni imara katika *East Africa* kwa ajili ya utafiti na mbinu za kijeshi. Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mgimwa kama ifuatavyo; ni kweli kwamba ushirikiano wa Afrika Mashariki umekiteua Kituo hiki kuwa *Centre of Excellency* katika teknolojia ya kijeshi. Lakini ni ukweli vile vile kwamba Bajeti ni finyu na haitoshi. Lakini nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba katika *strategic plan* ya shirika wana mipango yao wenye we ya kufanya mambo yatakayoweza kuwazalishia mapato ili waweze kuendeleza kituo hicho. Sisi kama Wizara ya Ulinzi tutafanya kila tunaloweza katika Bajeti ijayo kuweza kuwaombea ili angalau waweze kupata fedha za kukiendeleza kituo hicho. Lakini si kwa sababu hatuoni umuhimu wake bali ni kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti tu. (*Makofî*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba nijikite kwenye suala la usalama wa mipaka Mheshimiwa Waziri ametuambia usalama wa mipaka yetu upo shwari, lakini sasa hivi hapa Tanzania kuna biashara ya usafirishaji watu inaendelea yaani *human trafficking* ambayo inapigwa vita Kimataifa sehemu zote na tumeshuhudia mara nyingi ripoti za kukamatwa Wasomali, raia wa kigeni kutoka Somalia ndani ya mipaka yetu, Wasomali wametapakaa kutoka Tarakea mpaka Kyela, Mbeya mpaka sehemu nyingine tunasikia kwamba wanahifadhiwa na Wenyevevi wa Vijiiji. Sasa historia ya sehemu ambao hawa watu wanatoka kule Somalia kuna historia ya mambo ya kigaidi kama *Al-Shabab* na vitu kama hivyo, sasa tuna uhakika gani katika hawa Wasomali wanao *infiltrate* katika nchi yetu hatuingiliwi na *vi-element* vya hawa watu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbilinyi kama ifuatavyo; kwanza nimueleze kwamba kazi hiyo ya kudhibiti waingiaji haramu inafanywa kwa ushirikiano na vyombo vyote vya dola. Jeshi la Wananchi kwenye mipaka lakini Uhamiaji, Usalama wa Taifa na

kadhalika na bila shaka hao anaowazungumzia Mheshimiwa Mbilinyi ni wale ambao tayari wamekamatwa, kwa hivyo, vyombo vyetu vimefanya kazi inayotakiwa. Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba vyombo hivi nya ulinzi na usalama vitaendelea kufanya majukumu yake kuhakikisha kwamba hatupati watu ambao wanaweza wakaleta masuala ya ugaidi katika nchi yetu. (*Makof*)

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa swali langu Mheshimiwa Waziri ameshalieleza nya kutosha lakini nataka nimpe kwamba katika suala la eneo la Mlonganzira pale na Tondoroni vijana wanakosa kazi kutohana na suala zima la mgogoro wa mipaka, naomba japo kuwa umefanya harakati la kuhakikisha tatizo hilo unalitatu, lakini naomba eneo la Kiluvya pale liwe kama kipaumbele cha kwanza katika mpango mkakati katika utekelezaji wa tatizo hili, ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wakati akitoa majibu yake alisema mchakato wa kuwapata vijana wanaojiunga na jeshi letu unaanza *level* ya Wilaya na Mikoa, lakini kumekuwa na malalamiko makubwa kwamba wanaopewa *priority* ni vijana ambao ni watoto wa maafisa wa jeshi au marafiki na ndugu wanaofanya kazi katika jeshi lakini wale watoto wa wakulima wanaotoka vijijini na kwetu kule Mara na Mikoa mingine wamekuwa wakikosa nafasi lakini malalamiko yamekwenda mbele zaidi kwamba hata wale wachache wanaobahatika kupata wakienda kwenye mafunzo wamekuwa wakiwekewa vikwazo na kutafutiwa sababu ndogo tu na kufukuzwa, lakini wale watoto wa viongozi na watoto wa maafisa wamekuwa wakilindwa hata kama hawana uwezo, nilikuwa nataka ufanuzi na *commitement* ya Waziri je, yuko tayari kuchunguza hilo ili haki itendeke kwa mujibu wa sheria na vijana wa Tanzania wote waweze kupata nafasi na kuwe kuna uwiano wa Kitaifa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya kama hilo lipo watakaofaidika wengi si kwamba ni Mara?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo; kwanza niseme tu kwamba utaratibu wa uteuzi wa vijana wa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa unafanywa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na za Mikoa kwa hivyo bila shaka mimi sioni wanajeshi, hao wanajeshi wanaingiaje hapa? Kwa sababu katika Kamati zile mwanajeshi pekee labda ni yule mshauri wa mgambo, lakini waliobakia ni viongozi wa Kiserikali.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba hakuna ushahidi wa kuthibitisha hilo isipokuwa niseme tu kwamba hili la pili ni kwamba wanapofika kule kambini wanaondolewa bila sababu za msingi, sijawahi kuona malalamiko hayo rasmi, napenda Mheshimiwa Mbunge kama anayo anifikishie tutayafanyia kazi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa mujibu wa Kanuni ya 24 ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika kiapo cha utii yamebeba maneno ya uaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kuilinda, kuifadhi na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sasa Ibara ya 33 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ndogo ya pili inasema Rais atakuwa MKuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

Sasa katika masuala ya ulinzi ukienda kwenye nyongeza ya kwanza ya orodha ya mambo ya Muungano namba 3 ulinzi na usalama maana yake ni ulinzi na usalama ipo kwenye mambo ya Muungano. Sasa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 123 inamtamka Rais wa Zanzibar kama Kamanda Mkuu wa vikosi na idara maalum za Zanzibar na mwenye mamlaka ya mwisho na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachotaka kwa maslahi ya Taifa kama atakavyoona inafaa. Sasa kwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni suala la Muungano na ni mionganini mwa mambo yaliyoko kwenye orodha ya Muungano, sasa kwa kuwa Amri Jeshi Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kuwa tena na vyombo vingine hivi ambavyo navyo vinashughulika na masuala ya usalama na ambayo yamepewaa mamlaka na marekebisho ya kumi ya Zanzibar, yanayokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ambayo inatamkwa bayana kwamba sheria ile itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi inakinzana kwa mujibu wa Ibara ya 64(3) na 64(5) itakuwa ni batili na itatenguka kwa kadri itakavyokiuka, sasa kwa sababu mgongano huu upo na Amiri Jeshi ni mmoja, je, Waziri anatuambiaje katika hili la mgongano kati ya mamlaka hizi na ubatili na kutenguka kwake ili tuweze kuwa na Amiri Jeshi Mkuu mmoja.

**MWENYEKITI:** Hili sijui kama lilikuwa la Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Ole-Sendeka kama ifuatavyo; Amiri Jeshi Mkuu ni mmoja, hawapo wawili na ndiyo maana Jeshi la Ulinzi liko pande zote mbili na Jeshi la Polisi lipo pande zote mbili, viongozi ni hawa hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar inachoanzisha ni idara maalum na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar idara maalum hizo anaruhusiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuzianzisha na ndicho alichofanya mpaka sasa hivi hakuna mgongano huo unaosema. Kwa sababu idara maalum mfano chuo cha mafunzo asingeanzisha Rais wa Zanzibar kusingekuwa na maana yake chombo cha mafunzo ni sawa Magereza ambayo sio sehemu ya Muungano, kwa hiyo, mimi nadhani mpaka sasa hivi maeneo ya kiulinzi kwa maana ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya Muungano hakuna muingiliano wowote na mpaka sasa hivi kazi zinafanyika sawa sawa. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. katika mchango wangu Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri ya jeshi letu, niliomba nipate ufanuzi jinsi ambavyo mlipuko wa mabomu kule Mbagala na Gongo la Mboto ulitoa uhai wa watu, ukaharibu mali na wengine kuwa vilema na wakapata ulemavu, niliomba Mheshimiwa Waziri katika maelezo yako imeonesha kwamba jeshi limekuwa *reactive* badala ya kuwa *proactive* kwa sababu umeeleza kwamba kuna maandalizi na mmeomba watu kutoka nje ili waweze kusaidia, lakini katika maelezo yangu kwamba pamoja na uharibifu uliotokea, hakuna mtu aliywajibika. Nimeomba ungetoa maelezo na

ufafanuzi wa kina kwa nini mwenyewe hukuwajibika ili kuleta utawala bora kuonyesha kwamba jeshi lina nidhamu watu wanapokosea kwa uzembe au kwa bahati mbaya wanatoa mfano katika Taifa letu. Ningemueleza kidogo Mheshimiwa Mchungaji ni wakati gani Waziri anatakiwa kuijuzulu maana haiwezekani ikawa kila linapotoka tukio Waziri anajiu zulu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kama ifuatavyo; labda ningemueleza kidogo Mheshimiwa Mchungaji ni wakati gani Waziri anatakiwa kuijuzulu maana haiwezekani ikawa kila linapotoka tukio Waziri anajiu zulu. (*Makofi*)

Waziri anatakiwa kuijuzulu endapo itathibitika kwamba mamlaka zilizokuwa chini ya utawala wake zimevunja sheria, kanuni au taratibu. Sasa leo inapotoka ajali huwezi kusema watu wajiu zulu, kinachotakiwa ni kwamba uchunguzi wa kina ufanyike na mambo haya ya ajali ya milipuko wala sio mara ya kwanza kutokea katika nchi yetu, inatoka kila mara juzi tu tumesikia Cyprus milipuko hiyo imetoka, yanatoka hayo. Ninachosema ni kwamba hoja hapa iliyokuwepo ni kwamba lazima ithibitike kwamba kuna uzembe uliofanyika kabla hamjataka watu wajiu zulu. (*Makofi*)

**MWENYEKITU:** Ahsante sana, Mchungaji Msigwa hukuungwa mkono kwa hiyo tunaendelea.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kongwa tulikuwa na Kambi ya wapigania Uhuru Kusini mwa Afrika, wapigania Uhuru kutoka Msumbiji, Namibia, *South Africa* na maeneo mengine na baada ya wapigania Uhuru hawa kuondoka, kambi hili limetelekezwa na ni mara nyingi wananchi wa Dodoma tumeomba kwamba ile kambi ifufuliwe na iweze kutumika na hatujaomba mara moja na Waziri amesema kwamba kwa sababu Wabunge wengi wameomba kwamba makambi ya jeshi yafunguliwe katika Wilaya zao na atafanya hivyo, lakini hii sio kambi mpya, ni kambi ya zamani, yenyе kumbukumbu nzuri kwa wapigania Uhuru, ninaomba kujua kwamba kambi hii itafufuliwa lini ili ianze kazi. Ahsante.

**MWENYEKITU:** Swali muhimu kweli hili, ufanuzi wale askari wanaokataliwa Musoma waje Kongwa, Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Bura kama ifuatavyo; ni kweli kwamba nimesema tutajitahidi kuanzisha makambi ya JKT kila Wilaya, lakini kwa maeneo ambayo tayari yana makambi kama hayo, yatapewa kipaumbele kwa sababu gharama zake ni pungufu. Kwa hiyo, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu wa fedha hatuvezi kwa sababu Bajeti tuliyokuwa nayo ni ndogo sana, lakini tutakopoanza utaratibu huo, basi kambi hiyo ya Kongwa itapewa kipaumbele.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo katika mipaka katika Bahari ya Hindi, tumeshaona kwamba uharamia na utekaji nyara meli na uvuvi haramu wa kutumia mabomu katika Bahari ya Hindi hasa inayogusa pwani ya Mtwara na

Lindi tuliahidiwa kwamba tutapewa *speed boat* miaka mitano iliyopita, nataka kupata ufanuzi kuhusu suala hili, ni lini tutapewa zile *speed boat*?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mikidadi kama ifuatavyo; ni kweli kwamba yapo mahitaji ya doria katika mwambao wa nchi yetu, kwa bahati mbaya sana uwezo wa kuweza maana mwambao wa nchi yetu ni sehemu ambayo ina urefu mkubwa sana, si rahisi kuweka *speed boat* maeneo mengi kwa sababu ya uwezo wa Kibajeti, lakini hatua zinachukuliwa za kuweza kupata angalau chache, lakini wakati huo huo tunaendelea kuwaomba washirika wetu wa maendeleo ambao wameonesha nia ya kutusaidia na endapo tutafanikiwa kwa hilo basi bila shaka mwambao huo wa Mtwara na Lindi utazingatiwa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niitupie lawama Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Nne, naomba Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri, mwaka 2000/2005 hii ilikuwa ni Awamu ya Tatu, nilikuwa Kamati ya Ulinzi, Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Ulinzi alikuwa Mheshimiwa John Samuel Malecela na ndipo nilipokutana nae hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ulinzi alikuwa ni Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, matumizi ya fedha za jeshi zote zilikuwa zinaletwa ndani ya Kamati ya Ulinzi, kwa sababu si sahihi matumizi yote ya jeshi wakinunua bunduki, vifaru, pisto yaletwe humu ndani, kwa sababu tutakuwa tunatoa sura ya jeshi letu, udhaifu wake na ukakamavu wake na si sahihi. Kwa hiyo, mambo yote yanayohusu pesa za MEREMETA na nini tulikuwa tunaletewa kwenye Kamati ya Ulinzi, lakini awamu hii ya nne nafikiri Serikali hajafanya hivyo.

Naomba Mheshimiwa Waziri hili ulione kwamba ni kosa linalofanya watu wengi wafikirie kuna matatizo huko, naomba ujibu hili uone unalichukuaje wewe kwa sababu hili jambo lazima liwe siri, matumizi ya manunuzi yanayofanyika kule kwenye jeshi ndugu zangu Wabunge hatuwezi kuyaleta kwenye *public* na ulimwengu wote ukajua, itakuwa sio Taifa tena, lakini Serikali inawajibika na inalazimika kupeleka ndani ya Kamati ya Nje na Usalama. Mheshimiwa Waziri hebu toa ufanuzi katika hili. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kama ifuatavyo; nakubaliana nae mia kwa mia si busara hata kidogo kuja kuzungumzia matumizi ya jeshi letu hadharani, ni vyema tukaendeleza utaratibu huo wa kuzungumza masuala haya kwenye Kamati na mimi nakubaliana na wewe na ndivyo ilivyo kwa sasa tunapeleka taarifa zetu kwenye Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama isipokuwa tu hili la MEREMETA sikulizungumza huko kwa sababu Waziri Mkuu alishalisema hili suala. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi siwajibiki tena kulieleza hili suala, lakini ninachoweza kusema ni kwamba kama taarifa hiyo ilitolewa wakati huo bila shaka ipo na tutaweza kufanya hivyo tena kwa wale watakaopenda lakini kwenye Kamati. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakusudia kutoa shilingi kwa jambo ambalo nitaomba Waziri alitolee ufanuzi. Hii nasimama ni mara karibia ya nne, nimekuwa Mbunge miaka mitano, leo ni mara ya nne ninasimama kuhusu tatizo la wavuvi wa Kigoma wanavyouawa kwenye Ziwa Tanganyika. Naomba Waziri leo atuambie hivi wale watu wa Kigoma nao tunawaambiaje, kila siku tutashughulikia, lakini mpaka leo hata wiki moja iliyopita wavuvi wa Katonga wameuawa, wamenyanganya mashine 68, hivi kweli Wakongo hawa tumewashindwa kuwasimamia?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Serukamba kama ifuatavyo; nimesema hati kwenye hotuba yangu kwamba bado yapo maeneo katika mipaka yetu ikiwemo Ziwa Tanganyika ambayo kunatokea matokeo ya uhalifu, wakati mwingine wa kutumia silaha, kuwapora wavuvi na wengine hupoteza maisha. Jeshi la Wananchi wa Tanzania linachofanya ni kufanya doria za mara kwa mara ili kuweza kuzuia athari hizo zisitokee. Kwa bahati mbaya sana ni kwa sababu huwezi kufanya doria zile kila siku na wenywewe labda wanategea kipindi kile wakiona kwamba hakuna doria ndiyo wanafanya uhalifu huo. Ninachowea kumuhakikishia Mheshimiwa Serukamba ni kwamba tutaendeleza juhudhi, tutaweka Bajeti zaidi kwa ajili ya kuongeza idadi ya doria hizo na nimuhakikishie vilevile kwamba mimi binafsi nitakwenda katika maeneo hayo ili tuone ni jinsi gani tutaweza kuongeza zaidi nguvu ya kulinda maeneo ya Ziwa Tanganyika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Serukamba hukupata mtu wa kukuunga mkono katika kutoa shilingi. (*Kicheko*)

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi natoa shilingi na naomba wote mniunge mkono Upande wa Upinzani. (*Makofi*)

Mimi nilivyokuwa nauliza swalilangu kuhusu upande wa Zanzibar na Pemba kipindi cha uchaguzi kuwa majeshi wanakuja kule na wanatufanya vitendo vya uhalifu yaani vitendo vibaya, eeh! Kuna vitendo wanavyotufanya.

Mheshimiwa Waziri ameniambia nitoe ushahidi na jambo ambalo nazungumza, mimi nina uhakika kabisa na tunavyokuja kutoa hoja zetu au tunachagia Wizara, tumeshapata kero za wananchi, kwa hiyo, mimi natoa shilingi na naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

**MENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Waziri kama una ufanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenyanya ili nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuunga mkono hoja yangu. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu mimi linafanana na suala la Mheshimiwa Serukamba katika Wilaya ya Tarime, kuna vijiji vya Mangucha, Kihonga, Masanga na Vyang'ora huwa vinavamiwa mara nyingi sana na watu kutoka Kenya na hususani wanakuja kuchukua mifugo ya wafugaji na mara nyingi sana huwapiga risasi wakazi wa vijiji hivyo vya Tarime. Naomba kauli ya Serikali ni lini matatizo hayo yatakoma.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJANGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Nyangwine kama ifuatavyo:-

Bado narudia kusisitiza kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kuwa linatambua kwamba matukio hayo yapo, tutaendelea kuongeza idadi za doria katika mipaka hiyo. Tutaendelea kujitahidi kuweka Bajeti ya ziada ili kutoa nafasi ya wanajeshi ambao wako kule kuweza kutimiza majukumu yao ya kuhakikisha kwamba mipaka yetu inakuwa salama zaidi kuliko ilivyo sasa na hii ni kwa mipaka yote ikiwemo maziwa yetu ya Tanganyika na Victoria pamoja na sehemu zetu za mipaka na nchi za jirani.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, wakati nimechangia kwa maandishi nilikuwa nimeelezea mgogoro wa muda mrefu sana baina ya wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi wa Kata za Moshono, Nduruma na Mlangarini kule Arusha na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshalitolea ufanuzi wa ujumla, lakini kwa kuwa hili linagusa maisha ya kila siku ya wananchi, kwa kuwa wanajeshi wameweka mabango kwenye mashamba ya raia kusema kwamba hakuna mtu anaruhusiwa kuingia katika eneo hilo matokeo hawakuweza kuvuna hata mazao yao na wengine hata mwaka huu hawakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hili niendelee kulileta hapa kwa kuwa linagusa maisha ya kila siku na maamuzi au maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanaweza yakachukua muda mrefu na wananchi wakiendelea kuteseka kwa ajili hawana mahitaji yao ya kila siku kwa sababu wanategemea mashamba. Sasa naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJANGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Martha Umbulla kama ifuatavyo:-

Mabango hayo yamewekwa kwa sababu ya kutoa tahadhari ya wananchi kutojenga majengo ya kudumu au kulima mazao ya kudumu katika maeneo hayo. Lakini kama wapo wananchi ambao wamelima mazao ya muda mfupi hakuna sababu kwa nini wasiruhusiwe kuvuna. Tutatoa agizo hilo kwamba waruhusiwe kuvuna mazao yao lakini masuala ya kuendelea kukaa hapo yatategemea sana maamuzi yetu baada ya kuipitia taarifa ya Kamati niliyoisema. (*Makofi*)

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swal langu la nyumba iliyoangukiwa kitu kizito alisema suala hili litafanyiwa uchunguzi. Napenda kumuahikikishia Mheshimiwa Waziri kuwa nyumba ile tayari imeshafanyiwa matengenezo ya kuridhisha. Lakini naomba

uchunguzi wake zaidi uelekee kwa yule mama, afya yake imepata mgogoro wakati wa tukio kwa sababu yule mama ile nyumba hahusiani nayo hata kidogo.

**MWENYEKITI:** Yule mama aliyepata ka-shock, Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJANGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo tutalitekeleza.

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho kwa jioni hii ufanuzi wa mwisho, Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, Waziri alipokuwa akitoa ufanuzi wa malipo ya wazee wetu ambao walipigana vita ya dunia yaani mafao yao alisema kwamba wanatambua na uongozi utachaguliwa ili fedha zilizopo ziweze kutawanywa kwa wazee hao.

Sasa ninaomba kumuuliza tu kwamba ni lini sasa hatua hizo zote zitakamilika ili wazee hawa waweze kupewa fedha zao akiwemo Mzee Shiwa Shigela asikie mwananchi wangu huyu mzee, asikie moja kwa moja huko aliko kwamba hizi fedha zake atazipata lini. Zaidi tunashukuru Mkuu wa Majeshi kutukubalia sisi Wabunge vijana kwenda kwenye mafunzo ya JKT na mimi naomba zile fomu ziwashishwe ili Desemba/Januari tuhudhuria mafunzo hayo. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ufanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJANGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, siwezi kutoa tarehe maalum au muda maalum kwa sababu baada ya kukamilika kwa kukusanya takwimu za wazee hawa kinachotakiwa na kinachofuata pale ni wapate uongozi. Kwa sababu wale *Commonwealth Ex-Service League* ambao wanatoa fedha hizo wanasema hawawezi wakatoa hizo fedha pasipo na uongozi madhubuti. Ukikamilika mchakato wa kukamilisha uongozi tutawaambia Ubalozi wa Uingereza wawaambie hao wahisani wao watoe hizo fedha ili ziweze kugawiwa.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nikueleze tu na Bunge lako ni kwamba tayari kuna fedha ambazo zipo Ubalozi wa Uingereza pamoja na kwamba ni kidogo mno. Lakini zinasubiri kukamilika kwa mchakato wa kupata uongozi wa *Tanzania Legion*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyezekiti. Kufuatana na muda tulionao waliokuwa wamesimama katika fungu hili ni 35, kati yao 21 wamepata nafasi ya

kuzungumza, 14 hawakupata nafasi ya kuzungumza kwa sababu ya muda. Ningombwa kuwaomba radhi tuvumiliane wakati mwengine. Kwa hiyo, sasa tunaingia katika utaratibu wa *guillotine*. Katibu.

### **FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA**

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Shs. 12,943,751,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....	Shs. 218,111,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Shs. 399,045,000
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Shs. 170,132,000
Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Shs. 60,696,000
Kifungu 1006 - <i>Legal Service Unit</i> .....	Shs. 52,300,000
Kifungu 1007 - <i>Information, Edu. and Comm.</i> .....	Shs. 123,167,000
Kifungu 1008 - <i>Military Tender Board Unit</i> .....	Shs. 104,183,000
Kifungu 1009 - <i>Independent Telecommunication Network</i> .....	Shs. 174,857,000
Kifungu 2001 - <i>Industries, Construction and Agriculture</i> .....	Shs. 569,705,000
Kifungu 2002 - <i>Military Research and Dev.</i> .....	Shs. 148,600,000

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MPANGO WA MAENDELEO**

### **FUNGU 38 - JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA**

Kifungu 1001 - <i>Defense Forces Headquarters, Command</i> .....	Shs. 16,738,584,000
--	---------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 39 - JESHI LA KUJENGA TAIFA JKT**

Kifungu 1001 - <i>The National Service Force</i> .....	Shs. 3,162,471,000
--	--------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Shs. 0
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Shs. 70,000,000

Kifungu 1009 - *Independent Telecommunication Network*.....Shs. 0  
Kifungu 2001 - *Industries, Construction and Agriculture*.....Shs. 150,000,000  
Kifungu 2002 - *Military Research and Dev.*.....Shs. 128,797,767,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, taarifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Ulinzi na Kujenga Taifa kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naomba kukupongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Ndugu Job Masima, viongozi wote wa Majeshi yetu kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiendelea kuifanya.

Waheshimiwa Wabunge, wameonyesha imani kubwa sana kwenu katika namna ambavyo mnatekeleza wajibu wenu. Tunaamini kabisa kwamba mtaendelea kufanya kazi nzuri kwa mwaka ujao wa fedha.

Kwa jinsi hiyo sasa nitumie nafasi hii kushughulikia Mwongozo ambaa ulikuwa umeombwa mwanzo na Mheshimiwa Ole-Sendeka kuhusiana na uchangiaji uliofanywa hapo kabla na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Mwongozo ninaoutoa ni kwamba nilipowasikiliza hawa wawili kwa kweli wote wala hawakinzani. Kila mmoja alikuwa na msisitizo tu tofauti ila lengo lao ni moja la kujenga umoja wetu Watanzania wote, wote walikuwa wanasisitiza suala la kwamba jeshi letu liundwe na wanajeshi ambao wanatoka katika pembe zote za nchi yetu kwa sura yake, kwa maana ya Wilaya zote, Mikoa yote na pande zote mbili za Muungano wetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi niwashukuru wote wawili kwamba walitusaidia kutuweka sawa kwa kweli. Nimeona kuna mtu amenyanyuka. Ni nini?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2)(a) ambayo naomba kuisoma. Baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa na kuamuliwa, Mbunge ye yote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii anaweza kusimama mahala pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule.

Naomba kutoa taarifa ya mdomo kwamba nakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule ya Bunge kuchunguza malipo ambayo yamefanywa na Serikali kutoka Benki Kuu ya jumla ya shilingi bilioni 216 kwenda *Ned Bank South Africa* kwa mkopo wa shilingi bilioni 16 ambao Kampuni ya MEREMETA iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa uliuchukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto kwa kusoma ile Kanuni ya 117(2)(a) ndiyo ameisoma. Sasa na mimi nisome ya (b) hiyo hiyo 117. Mbunge ambaye anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule atawasilisha taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli kama ulivyoainishwa chini ya Kanuni ya 30(iv). (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba uzingatie ushauri huo niliousoma kwa kuwasilisha kwa Katibu ili utaratibu uweze kufuatwa. Kwa maelezo hayo kwa kuwa muda wetu wa shughuli za leo, Mheshimiwa Tundu Lissu ungekaa kwa sababu muda wetu niliokuwa nimeomba wa nusu saa niliopewa na mamlaka na kanuni umekwisha. Kwa hiyo, sina mamlaka tena ya kuongeza muda zaidi ulivyo na saa yetu inashuhudia. (*Makofi*)

Ninaomba kuwashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa kwa siku ya leo na shughuli zote zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika na muda wetu kwa kweli umeisha. Kwa jinsi hiyo naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 2.16 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 14 Julai, 2011 saa tatu asubuhi*)